

RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

**Kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za
Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka
ulioishia Juni 30, 2012**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Barabara ya Samora, S.L.P. 9080, Dar es Salaam.
Simu ya Upopo: "Ukaguzi", Simu: 255(022)2115157/8, Tarakishi: 255(022)2117527,
Barua pepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali taja

Kumb. CFA.27/249/01

Tarehe 28/3/2013

Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 9120,
DAR ES SALAAM.

**Yah: Kuwasilisha Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi
Mkuu wa Hesabu za Serikali Juu ya Taarifa za Fedha za
Mamlaka ya Serikali za Mitaa Kwa Mwaka wa Fedha Ulolioishia
Juni 30, 2012**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) na kifungu cha 48 cha Sheria ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000), pamoja na kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ninayo heshima na taadhma kuwasilisha ripoti kuu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulolioishia tarehe 30 juni, 2012 kwa taarifa yako na hatua za utekelezaji. Nimetoa mapendekezo ambayo kama yatakelezwu, yanaweza kutumika ili kupunguza dosari zilizojitokeza na kurekebisha sababu zilizopelekea kutokea kwa mambo yaliyoripotiwa katika taarifa hii.

Nawasilisha,

Ludovick S. L. Utouh

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Yaliyomo

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali.....	xix
Dira ya Ofisi	xix
Lengo la Ofisi	xix
TAFSIRI/VIFUPISHO	xix
Dibaji.....	xxii
Shukrani	xxix
Muhtasari wa Mambo Muhimu katika Taarifa ya Ukaguzi.....	xxviii
SURA YA KWANZA	1
1.0 UTANGULIZI WA MAMBO YA JUMLA	1
1.1 Mamlaka na Madhumuni ya Ukaguzi	1
1.1.1 Mamlaka ya kufanya Ukaguzi	1
1.2 Viwango na taratibu zinazotumika kutoa taarifa	5
1.3 Idadi ya Halmashauri zinazokaguliwa na mpangilio wa Ofisi ya ya Taifa ya Ukaguzi.....	8
1.4 Majukumu ya kisheria ya Mamlaka za Serikali za mitaa katika kuandaa Taarifa za Fedha	10
1.5 Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha	11
SURA YA PILI	15
2.0 MAANA, AINA, VIGEZO NA MWELEKEO WA HATI ZA UKAGUZI.....	15
2.1 Hati za Ukaguzi	15
2.2 Maana ya Hati za Ukaguzi	15
2.3 Aina ya Hati za ukaguzi	15
2.4 Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi katika Halmashauri	20

2.4.1 Mchanganuo wa ujumla wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa	20
2.4.2 Mchanganuo wa Hati za ukaguzi zilizotolewakwa Mamlaka za Serikali za Mitaa	22
2.5 Orodha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizopata Hati zenye shaka na sababu zilizopelekea kupata hati hizo	23
SURA YA TATU	26
3.0 UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKALIYOPITA	26
3.1 Ufutiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka iliyopita katika Ripoti ya jumla ya Ukaguzi	26
3.2 Ufutiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka iliyopita katika Ripoti ya kila Halmashauri	35
3.3 Ufutiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi katika Ripoti za Kagazi Maalum.....	38
SURA YA NNE	46
4.0 TATHMINI YA HALI YA FEDHA ZA HALMASHAURI	46
4.1 Ukaguzi wa Bajeti	46
4.1.1 Mwenendo wa Makusanyo katika Vyanzo vya Halmashauri ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa	46
4.2 Mwenendo wa Mapato kutoka Vyanzo vya Ndani vya Halmashauri ikilinganishwa na Ruzuku kutoka Serikali Kuu	48
4.3 Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida Isiyotumika	51
4.4 Matumizi ziada ya ruzuku ya matumizi ya kawaida iliyotolewa ...	53
4.5 Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo Isiyotumika	56
4.6 Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo Pungufu ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa	57

4.7	Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida Pungufu ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa	59
4.8	Makusanyo Pungufu katika Vyanzo Vikuu vya Mapato ya Ndani .	61
4.8.1	Makusanyo Pungufu ya kodi ya Majengo	61
4.8.2	Makusanyo Pungufu ya Ushuru wa Mazao	62
	SURA YA TANO	64
5.0	MASUALA MUHIMU YALIYOJIRI KATIKA UKAGUZI WA HESABU NA TATHMINI YA UDHIBITI WA NDANI	64
5.1	Tathmini ya Mfumo wa Udhiliti wa Ndani na Masuala ya Utawala Bora	64
5.1.1	Mapungufu katika Mifumo ya Kihasibu	64
5.1.2	Taarifa ya Uhasibu kuandaliwa nje ya Mfumo Funganifu	65
5.1.3	Mapungufu katika Utendaji wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa	67
5.1.4	Mapungufu katika Kamati za Ukaguzi	68
5.1.5	Tathmini ya Usimamizi wa Vihatarishi	69
5.1.6	Mazingira ya Udhiliti wa Teknolojia ya Habari	71
5.1.7	Kuzuia na Kudhibiti Udanganyifu	73
5.2	Usimamizi wa Maduhuli	75
5.2.1	Vitabu 2990 vya Makusanyo ya Mapato Kutowasilishwa	75
5.2.2	Maduhuli yasiyowasilishwa na Mawakala	78
5.2.3	Fedha zisizokusanya kutoka katika vyanzo vya ndani	79
5.2.4	Kukosekana kwa mikataba kati ya Halmashauri na wakala wa kukusanya mapato	82
5.2.5	Utafiti juu ya Mapato kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa.....	82
5.2.5.1	Mapungufu katika Mfumo wa Mapato ya Serikali za Mitaa	82
5.3	Usimamizi wa Fedha Taslimu	88
5.3.1	Masuala yaliyosalia katika usuluhishi wa benki	88

5.3.2 Ulaguzi wa kushtukiza katika Ofisi ya Fedha	91
5.3.3 Masurufu Yasiyorejeshwa	93
5.4 Usimamizi wa Rasilimali watu	95
5.4.1 Kutokuwepo na Kutoboresha Rejesta za Watumishi	96
5.4.2 Mishahara Isiyolipwa ambayo haikurejeshwa Hazina	98
5.4.3 Mishahara Iliyolipwa kwa Watumishi Waliostaafu, Walioachishwa Kazi,Waliofariki	98
5.4.4 Mikopo kwa Watumishi Isiyodhibitiwa	100
5.4.5 Utotauti kati ya fedha za mishahara zilizopokelewa na mishahara iliyolipwa	101
5.4.6 Kutokuwepo kwa usahihi wa tarehe ya Kuzaliwa kwa Watumishi katika Mfuko wa Malipo ya Mishahara.....	103
5.4.7 Watunishi Wasiochangia katika Mifuko ya Jamii na Bima ya Afya	104
5.4.8 Makato ya Kisheria ambayo hayakuwasilishwa katika Taasisi Husika	104
5.4.9 Kutowasilishwa kwa Stakabadhi za Kupokelea Mishahara Isiyolipwa na Makato ya Kisheria yaliyolipwa	105
5.4.10 Majina ya watumishi yanayotokea zaidi ya mara moja katika orodha ya malipo ya mshahara	106
5.4.11 Karadha za mishahara zisizorejeshwa	107
5.4.12 Wastaifu kuendelea kuonekana katika Orodha ya Mishahara ya Hazina	108
5.4.13 Uhaba wa Rasilimaliwatu	111
5.5 Usimamizi wa Mali katika Halmashauri	113
5.5.1 Mali za Kudumu zisizotumika na zisizo na matengenezo	112
5.5.1.2 Mali na vifaa vya kudumu ambavyo havikuthaminishwa	112
5.5.1.3 Kukosekana kwa nyaraka za umiliki wa mali za kudumu	113
5.5.2 Wadaiwa wasiolipa	115

5.5.3 Wadai wasiolipwa	117
5.6 Ukaguzi wa Miradi ya maendeleo	118
5.6.1 Mpango wa Taifa wa Ukimwi (NMSF)	119
5.6.1.1 Fedha za Mpango wa Taifa wa Ukimwi ambazo hazikutumika.....	119
5.6.1.2 Tofauti kati ya Fedha za mpango wa ukimwi zilizotumwa na zilizopokelewa	120
5.6.2 Ruzuku ya Maendeleo Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGDG) ...	121
5.6.2.1 Fedha za Mradi	121
5.6.2.2 Fedha za LGDG Zimetolewa Pungufu kwa	122
5.6.2.3 Fedha za LGDG ambazo hazikutumiwa na Halmashauri	123
5.6.2.4 Kutochangia asilimia 5% zinazotakiwa kuchangwa na Halmashauri kutokana na mapato ya ndani	123
5.6.3 Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo	124
5.6.4 Fedha za mpango maendeleo wa afya ya Msingi ambazo hazikutumika (MMAM)	130
5.6.5 Fedha ambazo hazikupelekwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Wanawake	130
5.6.6 Fedha za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ambazo hazikutumika	134
5.6.7 Fedha za mradi shirikishi wa usimamizi wa misitu (PFM) ambazo hazikutumika	135
5.6.8 Mfuko wa Afya ya Jamii	136
5.6.9 Fedha za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) ambazo hazikutumika	140
5.7 Mapitio ya usimamizi wa Matumizi	141
5.7.1 Malipo yenye Nyaraka Pungufu.....	141
5.7.2 Matumizi yasiyokuwa na hati za malipo.....	143

5.7.3 Kukosekana kwa stakabadhi za kukiri mapokezi kutoka kwa walipwaji.....	145
5.7.4 Matumizi yaliyofanywa kwa kutumia vifungu visivyohusika.....	147
5.7.5 Matumizi yaliyofanywa nje ya Bajeti iliyoidhinishwa.....	148
5.7.6 Uhamisho wa ndani wa fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ambayo haijarejeshwa.....	149
5.7.7 Madai ya miaka ya nyuma.....	152
5.8 Madeni na Miadi.....	153
5.9 Masuala Mengine.....	154
5.9.1 Ucheleweshaji wa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi kwa mwaka 2010/2011.....	154
5.9.2 Utekelezaji wa Kilimo Kwanza.....	157
SURA YA SITA.....	160
6.0 USIMAMIZI WA MIKATABA NA UZINGATIAJI WA TARATIBU ZA MANUNUZI.....	160
6.1 Usimamizi wa mikataba na uzingatiaji wa taratibu za manunuizi.....	160
6.2 Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za manunuizi.....	160
6.3 Ufanisi wa Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi (PMU).....	160
6.4 Tathmini ya usimamizi wa mikataba na ununuizi wa bidhaa, kazi za ujenzi, na huduma katika Serikali za Mitaa.....	162
6.5 Mapungufu katika Zoezi la kuhesabu mali/vifaa.....	174
SURA YA SABA.....	177
7.0 KAGUZI MAALUM.....	177
7.1 Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika kaguzi maalum ...	177
7.1.1 Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi.....	177
7.1.2 Halmashauri ya wilaya ya Kiteto.....	178
7.1.3 Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.....	179

7.1.4 Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa.....	180
7.1.5 Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.....	181
7.1.6 Halmashauri ya wilaya ya Kilwa.....	182
7.1.7 Halmashauri ya manispaa ya Temeke.....	183
7.1.8 Halmashauri ya Wilaya ya Songea.....	185
7.1.9 Halmashauri ya Manispaa ya Arusha.....	186
7.1.10 Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro.....	188
7.1.11 Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma.....	190
7.1.12 Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.....	192
7.1.13 Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.....	193
7.1.14 Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero.....	195
 7.2 Mambo ya kujifunza katika Kaguzi Maalumu zilizofanyika mwaka huu.....	195
7.2.1 Mfumo wa Udhibiti wa Ndani.....	195
7.2.2 Menejimenti kutokuwa na ufanisi katika usimamizi wa miradi ya maendeleo.....	197
7.2.3 Kuwepo kwa Maofisa wanaokaimu nafasi za juu muda mrefu ...	197
7.2.4 Kuwepo kwa watumishi katika kituo kimoja cha kazi kwa muda mrefu.....	198
 SURA YA NANE.....	199
 8.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	201
8.1 Udhaiifu katika mikataba ya ukusanyaji wa mapato.....	199
8.2 Uboreshaji wa makusanyo ya mapato ya Halmashauri kupitia vyanzo vya ndani.....	203
8.3 Uchelewaji katika kuwasilisha taarifa za Utekelezaji wa Miradi.	204
8.4 Usimamizi wa Makatibu Tawala wa Mikoa katika Miradi ya Maendeleo inayotekelzwa na Halmashauri.....	207

8.5 Kuendelea kula njama kati ya watumishi wa Halmashauri na wafanyakazi wa benki katika kufanya udanganyifu wa fedha za Halmashauri.....	207
8.6 Udfaifu katika mifumo ya Udhibiti wa ndani.....	209
8.7 Kuimarisha Usimamizi wa Rasilimali Watu.....	211
8.8 Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa kutumia Viwango vyakimataifa vyaa Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Sekta za Umma (IPSSAs).....	214
8.9 Udfaifu Uliobainika Katika Kaguzi Maalum.....	214
8.10 Udfaifu uliobainika katika Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.....	216
8.11 Udfaifu katika utekelezaji wa bajeti.....	217
8.12 Uboreshaji wa Usimamzi wa Miradi.....	219
8.13 Kuhamia Mfumo funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) kutoka picor.....	219
Viambatanisho.....	225

Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1 : Idadi ya Wakaguliwa	9
Jedwali Na. 2 : Upotoshwaji katika Uandaaji wa Taarifa za Hesabu za Mwaka	12
Jedwali Na. 3 : Halmashauri zilizorekebisha taarifa za fedha.....	13
Jedwali Na. 4 : Mchanganuo wa ujumla wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa	20
Jedwali Na. 5 : Mwenendo wa masuala yaliyosalia kwa miaka mitano mfululizo katika ripoti za kila Halmashauri.....	36
Jedwali Na. 6 : Masuala yaliyosalia katika kaguzi maalum	38
Jedwali Na. 7 : Mwelekeo unaoonesha bajeti iliyoidhinishwa dhidi ya makusanyo halisi	47
Jedwali Na. 8 : Mwelekeo wa mapato ya ndani dhidi ya matumizi ya kawaida.....	50
Jedwali Na. 9 : Mwenendo wa ruzuku ya kawaida ambayo haikutumika kwa miaka mitano mfululizo.....	51
Jedwali Na. 10 : Halmashauri zilizokuwa na matumizi ziada ya ruzuku ya matumizi ya kawaida iliyotolewa	53
Jedwali Na. 11 : Mwenendo wa matumizi zaidi kwa miaka mitano mfululizo.....	54
Jedwali Na. 12 : Mwenendo wa fedha ambazo hazikutumika za miradi ya maendeleo.....	56
Jedwali Na. 13 : Mwelekeo wa fedha za ruzuku ya maendeleo ambazo hazikutolewa kwa miaka mitano mfululizo	58
Jedwali Na. 14 : Mwelekeo wa fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida ambazo hazikutolewa kwa miaka mitano mfululizo	59
Jedwali Na. 15 : Orodha ya Halmashauri ikionesha makusanyo pungufu ya Kodi ya Majengo	62
Jedwali Na. 16 : Mwelekeo unaoonesha vitabu ambavyo havikuwasilishwa kwa ukaguzi.....	76
Jedwali Na. 17 : Muhtasari wa Maduhuli ambayo hayajawasilishwa na mawakala	78

Jedwali Na.18 : Mwelekeo wa fedha zisizo kusanywa kwa miaka miwili	80
Jedwali Na.19 : Halmashauri zilizokusanya mapato bila kuwa na mkataba	81
Jedwali Na. 20: Mwelekeo wa masuala yaliyosalia katika usuluuhishi wa taarifa za kibenki.....	89
Jedwali Na. 21: Mwenendo wa Halmashauri ambazo hazikufanya ukaguzi wa fedha wa kushtukiza na kutoweka kiwango cha juu cha fedha taslim kuwa katika ofisi ya fedha.....	92
Jedwali Na. 22: Mwelekeo wa masurufu ambayo hayakurejeshwa kwa miaka mitano	94
Jedwali Na. 23: Orodha ya Halmashauri ambazo hazitunzi na haziboreshi rejista za taarifa za watumishi.....	97
Jedwali Na. 24 : Mwenendo wa mishahara iliyolipwa kwa watumishi waliorokaa, waliostaafu na waliofariki.....	99
Jedwali Na. 25 : Halmashauri zilizolipa mishahara zaidi ya fedha za mishahara zilizopokelewa	101
Jedwali Na. 26 : Mwenendo unaoonesha utofauti kati ya fedha za mishahara zilizopokelewa na mishahara iliyolipwa	102
Jedwali Na. 27 : Orodha ya Halmashauri zinazoonesha Tarehe za Kuzaliwa za Watumishi zisizo sahihi katika Mfumo wa Malipo wa Mishahara	103
Jedwali Na. 28 : Watumishi wa Halmashauri ambao hawachangii mifuko ya jamii na bima ya afya.....	104
Jedwali Na. 29 : Makato ya Kisheria ambayo hayakuwasilishwa katika Taasisi husika	105
Jedwali Na. 30: Stakabadhi za Kupokelea Mishahara Isiyolipwa na Makato ya Kisheria yaliyolipwa ambazo hazikuwasilishwa kwa ukaguzi	106
Jedwali Na. 31 : Halmashauri zenye Karadha zisizorejeshwa ...	108
Jedwali Na. 32 : Halmashauri ambazo zina wastaafu ambao hawajafutwa kwenye orodha ya mishahara ya hazina	109

Jedwali Na. 33 : Orodha inayoonesha uhaba wa Rasilimaliwatu katika Halmashauri	110
Jedwali Na. 34 : Orodha ya halmashauri ambazo mali zake hazijathaminishwa.....	113
Jedwali Na. 35 : Orodha ya Halmashauri zenyne mali zisizokuwa na nyaraka za umiliki.....	114
Jedwali Na. 36: Mwelekeo wa wadaiwa ambao hawajalipa kwa miaka mitano mfululizo	115
Jedwali Na. 37 : Mwenendo wa madeni yasiyolipwa kwa miaka mitano mfululizo.....	117
Jedwali Na. 38 : Mwelekeo wa fedha za mpango wa Taifa wa Ukimwi ambazo hazikutumika	119
Jedwali Na. 39 : Orodha ya Wahisani wa Maendeleo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa	121
Jedwali Na. 40 : Kiasi cha Ruzuku kilichotolewa pungufu.....	122
Jedwali Na. 41 : Orodha ya Halmashauri ambazo hazikuchangia 5% ya fedha zinazotakiwa kuchangwa na Halmashauri kutokana na mapato ya ndani	124
Jedwali Na. 42 : Mwenendo wa fedha za CDCF ambazo hazikutumika	125
Jedwali Na. 43 : Orodha ya Halmashauri ambazo hazikuandaa taarifa na kuiziwasilisha OWM-TAMISEMI	126
Jedwali Na. 44 : Orodha ya Halmashauri ambazo hazikuibuwa Miradi ya CDCF	127
Jedwali Na. 45 : Orodha ya Halmashauri zilizofanya Malipo kutoka Mfuko wa Jimbo bila Kibali cha Kamati ya Mfuko.....	128
Jedwali Na. 46 : Orodha ya Halmashauri zilizohamisha Fedha toka Mradi mmoja kwenda mwingine kinyume na maagizo ya Mfuko	128
Jedwali Na. 47 : Mwenendo wa fedha ambazo hazikutumika katika mradi wa MMAM.....	130

Jedwali Na. 48: Orodha ya Halmashauri ambazo hazikupeleka fedha katika vikundi vya maendeleo vya wanawake na vijana.....	131
Jedwali Na. 49 : Mwenendo wa fedha ambazo hazikupelekwa kwenye mfuko wa wanawake na vijana kwa miaka miwili	132
Jedwali Na. 50 : Orodha ya Halmashauri ambazo zina mikopo kwa ajili ya akina mama na watoto ambayo hajarejeshwa.....	133
Jedwali Na. 51 : Orodha ya Halmashauri zenyenye fedha za MMEM ambazo hazikutumika	134
Jedwali Na. 52 : Mwenendo wa fedha za MMEM ambazo hazijatumika.....	135
Jedwali Na. 53 : Orodha ya Halmashauri ambazo hazikutumia fedha za PFM	135
Jedwali Na. 54 : Mwelekeo wa Halmashauri ambazo hazikutumia fedha za PFM.....	136
Jedwali Na. 55 : Fedha za mfuko wa Jamii ambazo hazikutumika	137
Jedwali Na. 56 : Orodha ya Halmashauri ambazo zina Madai yasiyolipwa na bima ya afya	139
Jedwali Na. 57 : Orodha ya Halmashauri ambazo zimesalia na fedha za MMES.....	140
Jedwali Na. 58 : Mwelekeo wa fedha za MMES zilizosalia	141
Jedwali Na. 59 : Mwenendo wa malipo yenye nyaraka pungufu	142
Jedwali Na. 60 : Mwenendo wa Matumizi yasiyokuwa na hati za malipo kwa miaka mitano mfululizo	144
Jedwali Na. 61 : Idadi ya Halmashauri ambazo stakabadhi za kukiri mapokezi kutoka kwa walipwaji zilikosekana.....	146
Jedwali Na. 62 : Idadi ya halmashauri yaliyofanya matumizi kwa kutumia vifungu visivyohusika	147
Jedwali Na. 63 : Idadi ya halmashauri yaliyofanya matumizi nje ya bajeti iliyoidhinishwa.....	148
Jedwali Na. 64 : Mlinganisho wa matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa.....	149

Jedwali Na. 65 : Idadi ya halmashauri zilizofanya uhamisho wa ndani wa fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ambazo hazijarejesha	150
Jedwali Na. 66 : Mlingano wa uhamisho wa ndani wa fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ambayo haijarejeshwa	151
Jedwali Na. 67 : Mwelekeo wa malipo ya madai ya miaka ya nyuma.....	152
Jedwali Na. 68 : Mlingano wa madeni ya kesi za sheria kwa miaka miwili	154
Jedwali Na. 69: idadi ya Halmashauri zilizochelewesha kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi	157
Jedwali Na. 70 : Orodha ya Halmashauri ambazo zilifanya manunuzi ya Bidhaa na Huduma bila kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.....	163
Jedwali Na. 71 : Mwenendo wa Ununuzi wa Bidhaa na Huduma uliofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni	164
Jedwali Na. 72 : Orodha ya Halmashauri ambazo zilifanya manunuzi kwa watoa huduma zaUgavi ambao hawakupitishwa .	165
Jedwali Na. 73 : Mwenendo kwa miaka miwili wa manunuzi kutoka kwa watoa huduma za ugavi ambao hawajathibitishwa	166
Jedwali Na. 74 : Orodha ya Halmashauri ambazo zilifanya Manunuzi bila ushindani wa wazabuni	168
Jedwali Na. 75 : Mwenendo wa Manunuzi yaliyofanywa bila kushindanisha wazabuni	169
Jedwali Na. 76 : Orodha ya Halmashauri ambazo vifaa vyake havikuingizwa katika leja	170
Jedwali Na. 77 : Mwenendo wa vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye leja la vifaa kwa miaka miwili	171
Jedwali Na. 78 : Orodha ya Halmashauri ambazo vifaa vililipiwa lakini havijapokelewa	172
Jedwali Na. 79 : Mwenendo wa Bidhaa zilizolipiwa lakini hazijapokelewa	172

Jedwali Na. 80 : Mapungufu katika utunzaji wa kumbukumbu za mikataba na miradi	174
Jedwali Na. 81 : Idadi ya Halmashauri ambazo zilikuwa na mapungufu katika zoezi la kuhesabu mali/vifaa	176

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wajibu na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimeainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) kama ilivyofafanuliwa zaidi na vifungu Na. 45 na 48 vya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) na kifungu Na.10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

Dira ya Ofisi

Kuwa kituo cha ubora katika ukaguzi wa hesabu katika sekta za umma

Lengo la Ofisi

Kutoa huduma bora za ukaguzi zenyenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

Katika kutoa huduma zenyenye ubora unaostahili, Ofisi inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:

Kutopendelea	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi isiyopendelea, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki.
Ubora	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni ya kitaalamu inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma.
Uadilifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha haki kwa kiwango cha juu na kuheshimu sheria.
Zingatio kwa Wadau	Tunalenga matakwa ya wadau wetu kwa kujenga utamanduni wa kutoa huduma bora kwa wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo na ari ya kazi.
Ubunifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya taasisi.

© Taarifa hii ni kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hata hivyo, baada ya taarifa hii kuwalishwa Bungeni, taarifa itakuwa ni kumbukumbu ya umma na usambazaji wake hautakuwa na kikomo.

TAFSIRI/VIFUPISHO

AFROSAI - E	Muungano wa Asasi Kuu za Ukaguzi katika nchi za Afrika zinazotumia lugha ya Kiingereza.
ASDP	Programu ya Maendeleo ya Kilimo na Mifugo.
BoQ	Mchanganuo wa Gharama za Kazi.
CAG	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
CDCF	Mfuko wa kuchochea Maendeleo ya Jimbo.
CDG	Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo.
CHF	Mfuko wa Afya ya Jamii.
CUIS	Mfumo wa Manunuzi wa Vifaa Vinavyotumika Mara kwa Mara.
DADPS	Mpango wa Maendeleo ya Kilimo Wilayani.
GPSA	Wakala wa Huduma ya Manunuzi Serikalini.
HBF	Mfuko wa Afya.
HSDP	Ruzuku ya Maendeleo ya Sekta ya Afya.
IFAC	Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu.
IFMS	Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha.
INTOSAI	Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi.
IPSAsS	Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma.
ISA	Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu.
ISSAIs	Viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi.
JRF	Mfuko wa Pamoja wa Ukarabati wa Vituo vya Afya.
Kif.	Kifungu.
LAAC	Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa.
LAAM	Kitabu cha Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009.
LAPF	Mfuko wa Pensheni ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.
LGAs	Mamlaka za Serikali za Mitaa.
LGCDG	Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa.

LGFA	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, 1982 (iliyorekebishwa 2000).
LGFM	Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009.
LGLB	Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa.
LGRP	Mpango wa Kuboresha Serikali za Mitaa.
LLG	Ngazi ya chini ya Serikali.
MMAM	Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi .
MMEM	Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi.
MMES	Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondar.
MTEF	Mpango wa kati ya Matumizi ya Fedha za Umma.
NAO	Ofisi ya Taifa ya Ugakuzi.
NHIF	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.
NMSF	Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI.
NRWSSP	Mpango wa Taifa wa Maji Safi na Maji Taka Vijijini.
NSSF	Mfuko wa Hifadhi ya Huduma ya Jamii.
OPRAS	Mfumo wa wazi Upimaji wa Utendaji Kazi kwa Watumishi.
OR-MUU	Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.
OWM -TAMISEMI	Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.
PEPFAR	Mpango wa dharura wa Rais wa Marekani Kupambana na UKIMWI.
PFM	Usimamizi Shirikishi wa Misitu.
PFMRP	Mradi wa Mpango wa Maboresho katika Usimamizi wa Fedha za Umma.
PMG	Mlipaji Mkuu wa Serikali.
PMU	Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi.
PPA	Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2004.
PPE	Mali, Mitambo na Vifaa.
PPF	Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Mashirika ya Umma.
PPR	Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2005.
PPRA	Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma.

PSPF	Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma.
RAS	Katibu Tawala Mkao.
SIDA	Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa ya Sweden.
SNAO	Ofisi ya Taifa ya Ugaguzi ya Sweden.
TACAIDS	Tume ya Kudhibiti UKIMWI.
TASAF	Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania.
TRA	Mamlaka ya Mapato Tanzania.
UDEM	Usimamizi wa Maendeleo ya Mazingira Mijini.
UNHCR	Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Wakimbizi.
URT	Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
VAT	Ongezeko la Thamani.
VEO	Afisa Mtendaji wa Kijiji.
VFM	Thamani ya Fedha.
WEO	Afisa Mtendaji wa Kata.
WSDP	Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji.
WYDF	Mfuko wa Maendeleo ya wanawake na Vijana.

Dibaji

Ninayo heshima kuwasilisha taarifa yangu ya mwaka ya ukaguzi wa hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012.

Ripoti hii ni majumuisho ya taarifa za ukaguzi katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa kwa muhtasari, ambapo maelezo ya kina ya taarifa hizo yanapatikana katika taarifa za Halmashauri zilizotumwa kwa waheshimiwa wenyeviti wa Halmashauri na Maafisa masuuli husika.

Ripoti hii inawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005), kifungu Na.48 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) pamoja na kifungu Na.34(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

Nia ya ripoti hii ni kuwajulisha wadau wetu ambao ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mahakama, wahisani, mashirika na jamii kwa ujumla, kwa muhtasari matokeo ya ukaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012.

Ripoti hii natoa matokeo ya ukaguzi wa jumla juu ya hali ya utendaji wa kifedha wa Serikali za Mitaa na kama zimefuata sheria, kanuni na viwango vya kimataifa vya uandaaji Hesabu katika Sekta ya Umma (IPSAS) kwa mwaka husika.

Mamlaka za Serikali za Mitaa, zilipewa nafasi ya kupitia na kujadiliana na wakaguzi kuhusu matokeo ya ukaguzi kwa kupitia Taarifa za ukaguzi zilizotolewa kwa Mamlaka zote za Serikali za Mitaa wakati wa ukaguzi na katika kikao cha mwisho baada ya ukaguzi. Ningependa kukiri kuwa, majadiliano na wakaguliwa

yalikuwa na umuhimu mkubwa. Ofisi yangu inatarajia kufuatilia katika muda muafaka juu ya maamuzi yatakayotolewa na Serikali kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Kifungu cha 40 cha Sheria ya Ukagazi Namba 11 ya mwaka 2008 kuhusiana na mapendekezo yaliyotolewa katika Ripoti hii.

Ukagazi wa mwaka huu wa fedha umegusa jumla ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 134 katika nchi.

Nina furaha kukuarifu kuwa Mamlaka zote za Serikali za Mitaa nchini zimekaguliwa na ofisi yangu.

Ni vema ikaelewaka kwamba, wakati Ofisi yangu inatoa taarifa juu ya utekelezaji wa sheria mbalimbali, kanuni na miongozo, na udhaifu katika mifumo ya taarifa za kifedha na udhibiti wa ndani katika taasisi za sekta ya umma na hasa Serikali za Mitaa, mwenye jukumu la msingi kabisa kwa ajili ya kutengeneza mfumo wenyewe ufanisi wa udhibiti wa ndani na mfumo wa ufuataji sheria ni jukumu la Menejimenti ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zina majukumu mbalimbali kwa ajili ya utoaji wa huduma muhimu na utawala bora kwa wananchi wa maeneo yao. Ili kutimiza majukumu haya, wanapaswa kukusanya mapato kwa njia ya kodi, vyanzo vya leseni, ada na mapato mengineyo. Katika suala hili, umadhubuti katika usimamizi wa fedha ni muhimu ili Serikali za Mitaa ziweze kuleta ushawishi kwa umma kuwa mapato hayo yamepokelewa kwa kufuata sheria na kutumika ipasavyo kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Ningependa kutambua mchango wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, hii ni moja ya kamati muhimu ya usimamizi ya Bunge kwa ajili ya kuchukua jukumu muhimu la kufuatilia taarifa za kagazi zilizopita pamoja na mapendekezo.

Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa watu wote waliotengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba na kukamilika kwa wakati

taarifa ya jumla ya Ukaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2012.

Natumaini kwamba, Bunge litaona taarifa zilizomo katika ripoti hii ni za muhimu katika kufanya Serikali kuwajibika kwa ajili ya usimamizi wake wa fedha za umma na utoaji wake wa huduma bora za umma kwa Watanzania ambao inawahudumia, katika suala hili, nami nitashukuru kama nitapokea maoni kutoka kwa watumiaji wa taarifa hii juu ya jinsi ya kuiboresha zaidi katika siku zijazo.



Ludovick S. L. Utouh

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Dar es Salaam,
28 Machi, 2013

Shukrani

Ripoti ya mwaka ya ukaguzi kwa hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni 2012 imekamilika kwa mafanikio. Mafanikio haya yamefikiwa kwa sababu ya msaada na ushirikiano nilioupata kutoka kwa wadau mbalimbali.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali yake yote, Bunge na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kusaidia ofisi yangu na kuchukua kwa umakini masuala yaliyojitekeza kwenye ripoti zangu za ukaguzi kwa lengo la kuboresha uwajibikaji katika ukusanyaji na utumiaji wa fedha nchini.

Pia, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu na ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) kwa juhudini kubwa katika kusisitiza uwajibikaji katika matumizi ya fedha za Umma kwa kutoa maelekezo kwa kila Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya, Meya, Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika kuhakikisha kuwa mapendekezo ya ukaguzi yanatekelezwa na kuhakikisha ukaguzi unahitimishwa kwa wakati, katika kuwasisitizia wakaguliwa kuwa wanatakiwa wafuate kalenda ya mwaka ya Ukaguzi.

Juhudi hizo zimeboresha ufanisi katika usimamizi wa fedha na uwajibikaji katika Serikali za Mitaa na utoaji wa huduma muhimu kama barabara, maji, elimu na afya kwa umma kwa ujumla.

Pia napenda kutoa shukrani zangu kwa wale ambao walinitengenezea mazingira mazuri ili kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba. Napenda kuwashukuru watumishi wote wa ofisi yangu kwa juhudini zao na kwa mara nyingine tena, kuwezesha ripoti kutoka ndani ya muda wa kisheria. Kwa moyo wa shukrani nyingi, nina wajibu wa kulipa fadhila kwa familia yangu na kwa familia za watumishi wa ofisi yangu kwa uvumilivu

waliokuwa nao kwa kipindi chote ambacho hatukuwa nao ili kutimiza majukumu haya ya Katiba.

Vilevile, shukrani zangu za dhati ziende kwa jumuiya ya Wafadhili hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden. Serikali ya Sweden kuitia mradi wa SIDA, Benki ya Dunia kuitia mradi wa PFMRP, Sekretarieti ya AFROSAI-E, Ofisi ya ushirikiano ya Ujerumani kuitia mradi wa GIZ unaofanya mafunzo kuhusu kuimarishe mifumo ya udhibiti wa ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa katika mikoa ya Tanga na Mtwara, na wote wenye mapenzi mema waliochangia katika kufanikisha mageuzi ndani ya Ofisi yangu.

Michango yao katika kuendeleza Watumishi, mifumo ya teknolojia ya mawasiliano na ununuzi wa vitendea kazi vingine kama magari imekuwa msaada mkubwa sana katika maendeleo ya Ofisi yetu.

Pia, ninawiwa kuwashukuru wadau wetu wengine wote ikiwa ni pamoja na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Hazina, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Maafisa Masuuli wote wa Serikali za Mitaa kwa ajili ya msaada uliohitajika na ushirikiano mkubwa waliotupatia. Hata hivyo, shukrani maalum ziwaendee Baraza la ujenzi la Taifa pamoja na Wakala wa barabara nchini kwa ushiriki wao katika kaguzi maalum zilizofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Nitakuwa mchache wa shukrani kama sitatambua jukumu la vyombo mbalimbali vyta habari katika kuujulisha umma wa Tanzania juu ya matokeo na mapendekezo yaliyopo katika Ripoti yangu.

Pia natoa shukrani kwa watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kutumia utaalamu wao katika ukaguzi na kujituma wakati wote wa ukaguzi na kuweza kufanikiwa kukamilisha kazi ambayo imebainishwa katika ripoti hii inayohusu Mamlaka za Serikali za Mitaa 134 katika nchi yetu. Juhudi kubwa katika kazi imewezesha Ripoti hii kukamilika na kuwasilishwa Bungeni kwa wakati.

Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru kwa namna ya kipekee watanzania wote tunaowatumikia kwa ujumla. Nawasisitizia kwamba waendelee kuhitaji na kuhimiza juu ya uwazi na uwajibikaji katika kusimamia ukusanyaji na matumizi mazuri ya fedha na rasilimali za Umma.

Wakati tunatambua michango ya wadau wetu wote, sisi pia tunaahidi kuendelea kuchangia katika kukuza uwajibikaji na uzingatiaji wa thamani ya fedha katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma.

Muhtasari wa Mambo Muhimu katika Taarifa ya Ukaguzi

Taarifa hii inatoa muhtasari na majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012. Sehemu hii ya ripoti inatoa maelezo ya jumla ya matokeo ya ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kufuatiwa na mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi pamoja na muhtasari wa mapendekezo.

1. Maelezo ya matokeo ya ukaguzi

Ukaguzi wa kisheria wa hesabu za Halmashauri 134 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2012 umekamilika. Muhtasari wa masuala muhimu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi upo katika ripoti hii na masuala haya kwa kirefu yamefanuliwa katika taarifa zilizopelekwa kwa Menejimenti na Wenyeviti wa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika.

Mwelekeo wa jumla wa hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Sehemu hii inaonesha tathmini ya mwelekeo wa hati za ukaguzi kwa miaka ya fedha ya 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010, 2010/2011 na 2010/2012. Madhumuni ya mwelekeo huu ni kuonesha kiwango cha utendaji na uwajibikaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha miaka mitano.

Mwelekeo wa Hati zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo

Miaka	Hati Zinazoridhisha		Hati zenye shaka		Hati Zisizoridhisha		Hati Mbaya		Idadi ya Halmashauri
	Jumla	%	Jumla	%	Jumla	%	Jumla	%	
2007/08	72	54	61	46	0	0	0	0	133
2008/09	77	58	55	41	1	1	0	0	133
2009/10	66	49	64	48	4	3	0	0	134
2010/11	72	54	56	42	5	4	0	0	133
2011/12	104	78	29	21	0	0	1	1	134

Ukaguzi wa marudio katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora uliofanyika baada ya kutoa ripoti yangu ya mwaka umepelekea Manispaa hiyo kupata hati isiyoridhisha. Kwa hiyo basi, idadi ya hati zisizoridhisha kwa mamlaka za serikali za mitaa kwa mwaka wa fedha 2010/2011 zilikuwa sita na si tano kama nilivyotolea taarifa katika ripoti ya mwaka 2010/2011.

Jedwali hapo juu linaonesha kuwa, hati zinazoridhisha zimeongezeka kwa 4% kutoka mwaka 2007/2008 hadi 2008/2009, zimepungua kwa 9% toka mwaka 2008/2009 hadi 2009/2010 na kuongezeka kwa 5% toka mwaka 2009/2010 hadi 2010/11 na 24% toka mwaka 2010/2011 hadi 2010/2012.

Hati zenyeshaka zimepungua kwa 5% toka mwaka 2007/2008 hadi 2008/2009 na kuongezeka kwa 7% toka mwaka 2008/2009 hadi mwaka 2009/2010 na kupungua kwa 6% toka 2009/2010 hadimwaka 2010/2011 halikadhalika kwa 21% toka 2010/2011 hadimwaka 2011/2012.

Hati zisizoridhisha zimeongezeka kwa 1% toka mwaka 2007/2008 hadi 2008/2009, zimeongezeka kwa 2% toka mwaka 2008/2009 hadi 2009/2010 na pia kuongezeka kwa 1% toka mwaka 2009/2010 hadi mwaka 2010/2011 na kupungua kwa 4% toka mwaka 2010/2011 hadi mwaka 2011/2012.

Hakukuwa na Hati Mbaya iliyotolewa katika Miaka ya 2007/08, 2008/09, 2009/10 na 2010/11. Hata hivyo katika mwaka wa fedha 2011/12, Hati Mbaya ilitolewa kwa Halmashauri moja (1) ambayo ni sawa na asilimia moja (1).

Kama jedwali la mwelekeo wa hati linavyoonekana hapo juu, kwa ujumla utendaji wa serikali za Mitaa umeboreka. Mafanikio haya yamechangiwa na sababu mbalimbali zikiwemo sababu zifuatazo:

- Mikakati iliyowekwa na Serikali kwa ajili kushughulikia mapendekezo ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

- Ufutiliaji wa Waheshimiwa Wabunge katika kuhakikisha Serikali inaimarisha Utawala bora.
 - Usimamizi imara wa Waheshimiwa Madiwani katika kuhakikisha kuwa mapendekezo ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yanatekelezwa na kufanya ufuutiliaji wa miradi ya maendeleo.
 - Wananchi wamekuwa wakihitaji uwazi na uwajibikaji zaidi katika utendaji wa Halmashauri.
 - Uguzi shirikishi kati ya Wakaguzi na Wakaguliwa umeimarika.
 - Hatua madhubuti zinazochukuliwa na Taasisi za uchunguzi kama vile Mkurugenzi wa Mashtaka, Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa katika kufuutilia ripoti za Uguzi ikiwa ni pamoja kaguzi maalum.
 - Kumekuwepo na uboreshaji wa taarifa za fedha zilizotolewa na Halmashauri kulingana na viwango vya Kimataifa vya utayarishaji wa Hesabu katika Sekta ya Umma.
2. **Muhtasari wa mambo muhimu yaliyojitekeza katika ukaguzi wa Hesabu za mwaka 2011/2012 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**
Mapungufu na madhaifu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi ni pamoja na yafuatayo:
- (a) **Mapendekezo ya Kaguzi zilizopita ambayo hayajatekelezwa**

(i) Ripoti Kuu

Majibu ya serikali pamoja na Mpango wa utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti ya mwaka uliopita ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2011 yamepokelewa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa Barua Na. EB/AG/AUDIT/12/VOL.I/53 ya 20 Juni, 2012. Ufutiliaji mpango kazi uliotayarishwa na Mlipaji Mkuu wa Fedha za Serikali utafuatiliwa.

(ii) Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LAAC)

Katika kukamilisha na kujibu Ripoti ya ukaguzi kwa Taarifa za Fedha zilizoishia tarehe 30 Juni 2011, Mlipaji Mkuu wa Serikali pia aliweza kujibu maagizo ya LAAC katika Ripoti yake iliwasilishwa Bungeni tarehe 4 April, 2011.

Katika kupitia majibu niliyoyapokea nimebaini kuwa, maagizo yote Saba yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (LAAC) yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Kwa maoni yangu, nasisitiza kuwa, hatua stahiki zichukuliwe na Serikali ili maoni yote ya Ukaguzi yashughulikiwe kwa ajili ya kuleta ufanisi na uwajibikaji katika Halmashauri za Serikali za Mitaa. Hata hivyo, ninasubiri majibu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kuhusiana na Ripoti ya LAAC iliyowasilishwa Bungeni tarehe 17.4.2012.

(iii) Ripoti za Halmashauri mbalimbali

Kati ya Halmashuri 134 zilizokaguliwa kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2012, Halmashuri 131 zilikuwa na masuala ambayo hayajatekelezwa ya miaka ya nyuma kiasi cha Sh. 78,489,936,013. Pia kuna masuala mbalimbali ambayo hayakuthamishwa kama vile mapungufu ya udhibiti wa mfumo wa ndani katika Halmashauri.

(iv) Kaguzi maalum

Katika Kaguzi zilizopita,jumla ya kaguzi maalum kumi na tisa (19) zilifanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kaguzi hizi maalum zilipelekea kuwepo kwa mapendekezo kadhaa ya ukaguzi ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi na Halmashauri husika. Pia masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika taarifa za kaguzi maalum yanaendelea kushughulikiwa na taasisi mbalimbali za kiuchunguzi kwa mujibu wa kifungu cha 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008.

(v) Hoja za Ukaguzi kwa mwaka husika

a) Utayarishaji ambao siyo sahihi wa Taarifa za Fedha

- Taarifa za Fedha za Halmashauri 67 zilizowasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi, zilikuwa na makosa mbali mbali kama vile kutooneshwa kwa baadhi ya taarifa, baadhi ya tarakimu kuoneshwa pungufu au zaidi, kutooneshwa kwa taarifa muhimu na vilevile taarifa za Fedha zilizoandaliwa kutokuwa sahihi.

Kwa ujumla, makosa yaliyobainishwa katika Taarifa za fedha zilioneshwa pungufu kwa Sh.126,432,283,544 ambayo ni 10% ya matumizi yote na kuoneshwa zaidi kwa Sh.84,862,411,758 ambayo ni 7% ya matumizi yote. Kutokana na wingi wa makosa haya, Halmashauri zilifanya marekebisho ya taarifa za fedha na kuzileta tena kwa ajili ya ukaguzi kitu ambacho kinakwaza katika kukamilika kwa ukaguzi kwa wakati. Idadi ya mabadiliko mengi yaliyofanywa yanaonesha kiwango cha chini cha uwezo wa Wahasibu wa Halmashauri katika uandaji ya taarifa za fedha kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya uandaaji wa Hesabu (IPSAS).

- Wakati wa ukaguzi wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa,imebainika kuwa,taratibu kwa ajili ya maandalizi ya taarifa za fedha zilileta usumbufu kwa kuwa ziliandaliwa bila kutumia mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS- Epicor). Zaidi ya hayo, taarifa za fedha hazikuandaliwa moja kwa moja kwa kutumia mfumo huo wa IFMS- Epicor.

b) Mapungufu katika Mfumo wa Udhhibit wa Ndani

Ukaguzi wangu wa taarifa za fedha katika Halmashauri mbalimbali ulijumuisha tathmini ya Mfumo wa Udhhibit wa Ndani ikitumia na Mfumo wa kihasibu, Mfumo wa udhibiti wa Mawasiliano, utendaji wa Ukaguzi wa ndani, uanzishwaji na utendaji wa Kamati za Ukaguzi wa Hesabu,

Udhibiti wa Vihatarishi na udanganyifu. Katika kupitia mfumo mzima wa udhibiti na Ndani kunaniwezesha kufanya tathmini na kuona kama mfumo ni imara ambao unaweza kutoa taarifa sahihi ambazo zinaweza kusaidia kuandaa taarifa za fedha.

Kama nilivyotoa taarifa katika miaka iliyopita kuwa Mfumo wa Udhibiti wa Ndani kwa baadhi ya Halmashauri siyo mzuri kwani hazitumii ipasavyo mfumo wa kihasibu uliopo, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani hakifanyi kazi ipasavyo, Kamati za Hesabu hazifanyi kazi kama inavyotakiwa na tathmini ya Vihatarishi pia haifanyiki.

Mapungufu katika Mfumo wa udhibiti wa Ndani yanaongeza hatari ya kuwa na makosa mengi, kutoingizwa kwa taarifa muhimu katika taarifa za fedha na udanganyifu, pia kunazifanya Menejimenti za Halmashauri na Wakaguzi kutokuwa na uhakika na taarifa za Fedha zinazoandaliliwa kwa kiwango kikubwa kuwa ni sahihi.

(c) Udhafu katika Usimamizi wa Mapato ya Ndani

Kama nilivyobainisha katika Ripoti za miaka ya nyuma, usimamizi wa Maduhuli kutoka katika vyanzo vya Ndani vya Mamlaka za Serikali za Mitaa bado ni changamoto. Muhtasari wa mapungufu mbali mbali yaliyobainika katika eneo hilo katika mwaka husika ni kama ifuatavyo:

- Jumla ya vitabu 2990 vya stakabadhi za mapato kutoka Halmashauri 36 vilikosekana na hivyo havikutolewa kwa ajili ya ukaguzi. Hivyo, wakaguzi hawakuweza kujua ukamilifu wa ukusanyaji wa mapato. Hii ilipelekea kudhibiti mawanda ya ukaguzi.
- Wakati wa ukaguzi wa mwaka wa fedha husika, kati ya Halmashauri zilizochaguliwa na kukaguliwa, Halmashauri 56 zilikuwa na jumla ya Sh.4,466,028,478

ikiwa ni mapato yaliyokusanya na mawakala ambayo yalikuwa bado hayajawasilishwa kwenye Halmashauri.

- Ulegevu katika udhibiti wa ndani na ufuatiliaji wa makusanyo ya mapato ulisababisha kutokusanya kwa mapato kutoka kwenye vyanzo vya ndani yenye jumla ya Sh. 8,008,669,844 kutoka kwa wadaiwa wa kodi mbalimbali katika Halmashauri 30 zilizojaribiwa.
- Halmashauri 17 hazikukusanya kodi ya majengo kiasi cha Sh.4,345,570,497 ikiwa ni sawa na 38% ya makisio ya Sh.11,405,440,517.
- Kutokuwa makini katika kubuni vyanzo vya Mapato kumepelekea Kodi ya mazao kiasi cha Sh.1,797,972,949 sawa 4% ya Makisio ya Sh.45,312,189,317 kutokusanya katika Halmashauri kumi na nne (14).

(d) Udhaifu katika usimamizi wa Fedha

Usimamizi na udhibiti wa fedha ni muhimu ili kuhakikisha fedha zote zinazotokana na mapato zinakusanya vizuri, kupelekwa benki na kuweka kumbukumbu zake. Mambo yafuatayo yalibainika katika mwaka 2011/2012:

- Suluhisho za benki ambazo ni msingi wa kiuhasibu wa kudhibiti hatari na udanganyifu au miamala isiyo sahihi kufanyika kupitia benki katika akaunti za Halmashauri. Udhaifu katika suluhisho za benki ulibainika katika Halmashauri 86. Hizi ni pamoja na Sh.3,872,146,712 ikiwa ni jumla ya mapato katika vitabu vya fedha za Halmashauri lakini hayapo katika taarifa za benki. Jumla ya Sh.18,368,780,081 kutoka katika Halmashauri mbalimbali ni hundi zilizolipwa na kuingizwa kwenye vitabu vya halmashauri lakini hazikuwasilishwa benki kwa ajili ya malipo hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012. Pia, j umlaya Sh.842,758,166 zilikuwa zimekipwa benki kutoka

katika akaunti za Halmashauri bila ya kuingizwa katika vitabu vya fedha vya Halmashauri.

Mwisho kabisa, jumla ya Sh.136,065,798 zililipwa benki kwa niaba ya Halmashauri, lakini Halmashauri hazikukiri mapokezi ya fedha hizo.

- Kaguzi za kushtukiza za fedha taslimu zilikuwa hazifanyiki katika Halmashauri 46.
- Halmashauri 24 zimeshindwa kuweka kiwango fedha taslimu anachotakiwa kuwa nacho Mtunza Fedha wa Halmashauri.
- Masurufu ya jumla ya Sh. 1,999,406,423 katika Halmashauri 70 bado hayajarejeshwa mpaka wakati wa Ukaguzi (Ni wastani wa miezi sita kuanzia 30 Juni, 2012).

e) Mapungufu katika usimamizi wa matumizi

Udhibiti wa mifumo ya matumizi ni muhimu ili kuhakikisha kwamba gharama zote zilizotumika zimelipwa kwa usahihi na kurekodiwa. Mambo muhimu yaliyoainishwa katika mwaka 2011/2012 ni pamoja na:

- Malipo yenyе hati pungufu yalibainika katika Halmashauri 74 yenyе jumla ya Sh.3,367,208,321.
- Halmashauri 22 kati ya 134 zilizokaguliwa zilifanya malipo yenyе jumla ya Sh.1,509,529,810 ambayo hayakuwa na hati za malipo zilizotolewa kwa ajili ya ukaguzi, na hivyo kudhibiti mawanda ya ukaguzi.
- Jumla ya Sh. 650,356,980 zilizokaguliwa kutoka katika Halmashauri 20 zimelipwa kwa Taasisi mbali mbali na nyingine zimepelekwa katika Ngazi ya Vijiji lakini fedha hizo hazikuthibitika kupokelewa kutokana na kukosekana kwa Risiti za kukiri mapokezi ya fedha hizo.
- Matumizi yenyе jumla ya Sh.1,577,463,978 yalifanyika katika vifungu ambavyo siyo sahihi katika Halmashauri 41 bila kuidhinishwa na Kamati ya Fedha ya Halmashauri husika.

(f) Mapungufu katika menejimenti ya rasilimaliwatu na udhibiti wa mishahara

Menejimenti ya Rasilimaliwatu na udhibiti wa mishahara bado ni changamoto zilizopo katika Halmashauri nyingi ambayo inahitaji usimamizi wa kina. Kama ilivyoripotiwa katika miaka ya nyuma, hata katika mwaka huu, madhaifu mbalimbali yilibainika ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

- Katika sampuli ya Halmashauri 25, ulibainika uhaba wa Watumishi 14,663 ikilinganishwa na idadi inayotakiwa ya watumishi 73,087. Upungufu wa idadi ya wafanyakazi unaathari ya moja kwa moja katika utendaji kazi wa siku hadi sikuna unaweza kukwamisha utekelezaji wa shughuli za Halmashauri. Na pia imeonekana kwamba, mabadiliko ya mara kwa mara ya watumishi viongozi yamepunguza uwajibikaji na hivyo kuathiri utendaji kazi wa Halmashauri.
- Ukaguzi uliofanyika katika sampuli ya Halmashauri sita(6) katika mwezi wa Juni 2012 umebaini kuwepo kwa watumishi 659 ambaao hawachangii Mifuko ya PensheninaMfuko wa Bima ya Afya kama ilivoonekana katika vifungu vya makato ya mishahara.
- Ukaguzi uliofanyika katika sampuli ya Halmashauri kumi na tano (15) kwa kuangalia taaarifa za mishahara kutoka Hazina za tarehe 30/6/2012 umebaini kuwa, tarehe ya kuzaliwa ya wafanyakazi 1531 zilikuwa si sahihi. Tarehe ya kuzaliwa kwa watumishi zilionekana kuwa 01/01/1700, 01/01/1900 na 01/01/2012.
- Suluhisho za mara kwa mara na kaguzi za mishahara zilikuwa hazifanywi na menejimenti ya Halmashauri ili kuthibitisha uhalali wa maingizo yote ya malipo ya mishahara na kupelekea malipo ya Sh. 693,132,772 kulipwa kwa wastaafu, watoro, walioacha kazi na walioachishwa kazi kuitia akaunti zao za benki bila kubainika. Malipo hayo yamehusisha jumla ya Halmashauri 43.

- Mishahara yenyeye jumla ya Sh.1,599,387,243 inayohusiana na watumishi waliofariki, wastaafu na watoro katika Halmashauri 43 haikuwasilishwa Hazina kinyume na maelekezo yaliyotolewa na wizara ya fedha kwa barua yenyeye kumbukumbu No.EB/AG/5/03/01/Vol .IV/136 ya tarehe 31, Agosti 2007. Kuna uwezekano kwamba kiasi hicho kimetumika vibaya kwa sababu Halmashauri bado hazijarejesha hata baada ya hoja za ukaguzi kutolewa.
- Katika mwaka huu wa ukaguzi, pia nimebaini matukio mbalimbali ambayo mishahara ya watumishi wa Halmashauri inakatwa hadi kufikia kiasi kinachozidi theluthi mbili (2/3) ya mishahara yao kwa sababu ya ukopaji unaozidi kiasi kutoka kwenye taasisi za fedha na nyinginezo. Na katika Halmashauri nyingine, kuna watumishi walikuwa hawalipwi chochote kabisa kutokana na makato hayo. Ukaguzi uliofanyika katika Halmashauri 87 umeonesha kuwa zaidi ya watumishi 17,710 walikuwa wakipokea pungufu ya 1/3 ya mishahara yao. Hii ni kinyume na matakwa ya Waraka No.CCE.45.271/01/87 wa tarehe 19, Machi, 2010 iliyotolewa na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya utumishi wa Umma ambao unakataza makato ya mshahara wa mtumishi wa serikali kuwa zaidi ya 2/3 ya mshahara wa kila mwezi.

g) Kuwepo kwa kiwango cha chini cha uzingatiaji wa taratibu na Sheria za Manunuzi

Katika kufanya tathmini juu ya uzingatiaji wa Sheria za Manunuzi ya umma, mapungufu mbalimbali yalibainika ikiwa ni pamoja na:

- Taarifa muhimu/nyaraka zilibainika kukosekana katika mafaili ya mikataba husika ikiwa ni pamoja na makubaliano ya mikataba, orodha ya manunuzi ya vifaa, makadirio ya Wahandisi, vyeti ya awali na manunuzi

yaliyofanywa nje ya mpango wa manunuzi. Kiasi kinachohusika na mapungufu haya kinafikia Sh.660,529,264 kikihusisha Halmashauri 16 zilizokaguliwa kwa sampuli. Mapungufu mengine ya kutofuata sheria za manunuzi ni kama ituatavyo:

- Manunuzi yenyе thamani ya Sh.443,107,149 katika Serikali za Mitaa 25 yalifanyika kutoka kwa wauzaji mbalimbali wa bidhaa na huduma bila ushindani wa bei kinyume na matakwa ya kifungu Na. 63 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005.
- Ununuzi wa Bidhaa na Huduma wa thamani ya Sh.541,013,405 ulifanyika bila kibali cha Bodi ya Zabuni katika Halmashauri 24.
- Ugazi wa usimamizi wa vifaa mbalimbali ulionesha kwamba, Halmashauri 17 hazikuingiza katika leja vifaa vilivyonunuliwa vyenye thamani ya Sh.271,711,263. Hii inapingana na Agizo Na. 54(3) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.
- Vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh.125,681,000 viliagizwa na kulipwa na Halmashauri 6 lakini havikupelekwa kwenye Halmashauri husika kinyume na kifungu Na.122(1) cha Kanuni za manunuzi (Vifaa, ujenzi, Huduma zisizo za ushauri na uuzaji wa mali za Umma kwa Zabuni) ya mwaka 2005.
- Aidha, udhaifu katika taratibu za kuhesabu mali na vifaa ulibainika katika sampuli ya Halmashauri 28. Kutofuata kwa taratibu za manunuzi zilizopendekezwa kunadhoofisha kanuni ya ushindani na thamani ya fedha katika manunuzi husika.

h) Ufanisi duni wa uendeshaji wa Mfuko ya maendeleo

- **Mfuko wa kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF)**
Jumla ya kiasi cha Sh. 2,561,882,820 zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za Mfuko wa kuchochea Maendeleo ya Jimbo hazikutumika katika sampuli ya Halmashauri 69, hivyo malengo ya kuanzisha Mfuko hayakutimia.

Kwa kuongezea, kama nilivyokwishatoa taarifa katika Ripoti yangu ya mwaka uliopita, Halmashauri nyingi hazikuandaa na kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa taarifa ya kiasi kilichopokelewa na kutumiwa kwa kila Kamati ya kuchochera Maendeleo ya jimbo kama ilivyoagizwa katika Kifungu 7 (3) cha Sheria ya Mfuko wa kuchochera Maendeleo ya Jimbo ya mwaka 2009.

- **Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)**
ukaguzi uliofanyika juu ya usimamizi wa Mfuko wa Afya ya Jamii katika Halmashauri 38 zilizochaguliwa ulibaini kuwa, Halmashauri hizi zilikuwa na bakaa ya Sh.1,710,747,467 ambayo hasa ilisababishwa na kutofungua na kuendesha akaunti tofauti kwa ajili ya Mfuko wa Afya ya Jamii na kuchelewesha kutolewa kwa ruzuku.
- **Mfuko wa Wanawake na Vijana**
Ukaguzi uliofanyika katika Halmashauri 31 umebaini kuwa Sh.511,761,787 zipo katika akaunti ya benki za Halmashauri bila kutolewa kama mikopo kwa vikundi vya Wanawake na Vijana.
- i) **Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo**
Sampuli ya miradi mitatu ya maendeleo ya wafadhili ambayo ni Mradi wa kudhibiti UKIMWI, Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi na Miradi ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa ilioneshwa kasi ndogo ya utekelezaji kwa kuwa na kiasi kikubwa kisichotumika cha Sh.1,545,629,527 kwa Mradi wa kudhibiti UKIMWI (Halmashauri 59), Sh.2,586,958,015 kwa Mradi wa Maendeleo ya afya ya Msingi (Halmashauri 32) na Sh. 14,295,289,503 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (Halmashauri 70).

Utekelezaji wa Miradi kwa kiwango cha chini ina maana kwamba, idadi kubwa ya shughuli zilizopangwa hazikutekelezwa kikamilifu au hazikutekelezwa kabisa. Kwa ajili hiyo basi, huduma/ malengo yaliyotarajiwa na Halmashauri kwa jamii husika yamecheleweshwa. Hii pia inaweza kupelekea marekebisho ya bajeti katika siku zijazo kwa sababu ya uwezekano wa kupanda kwa bei kutokana na athari za mfumuko wa bei.

j) Changamoto katika utekelezaji wa Bajeti

Katika kupitia na kujiridisha kama Halmashauri zimetumia fedha kulingana na Bajeti iliyoidhinishwa, nimebaini mapungufu yafuatayo:

- Bunge lilipitisha bajeti kwa baadhi ya vifungu vya fedha za maendeleo vyenye jumla ya Sh. 595,064,422,505 katika Halmashauri 113. Hata hivyo, ni Sh. 345,568,067,477 tu ndizo zilizopokelewa na Halmashauri husika, na kufanya kuwepo upungufu wa Sh. 249,496,355,027 sawa 42%.
- Hadi mwisho wa mwaka kulikuwa na bakaa ya fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha Sh. 188,405,740,589 ambayo ni sawa na 35% ya kiasi cha fedha zilizokuwepo katika mwaka husika. Kiasi hicho cha fedha kimehusisha Halmashauri zipatazo 132.
- Pia fedha kwa ajili ya Matumizi ya kawaida zilitolewa pungufu kwa Sh. 171,002,394,849 (sawa na 11%) katika Halmashauri 87. Bajeti iliyoidhinishwa ilikuwa Sh.1,618,877,128,175, wakati kiasi cha fedha kilichopokelewa na Halmashauri kilikuwa ni Sh.1,447,874,733,324 tu.
- Katika mwaka husika Sh.124,594,256,692 sawa na 5.4% ya fedha za matumizi ya kawaida zilizokuwepo hazikutumika.
- Jumla ya kiasi cha fedha Sh.1,688,848,579 katika Halmashauri 38 kimetumika nje ya Bajeti iliyoidhinishwa bila kupata kibali kutoka katika mamlaka husika

kinyume na Kifungu 10(3) cha Sheria ya Fedha Na.9 ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000).

- Fedha zilizohamishwa kutoka Akaunti moja kwenda Akaunti nyingine kiasi cha Sh. 2,673,964,170 hazikuweza kurejeshwa katika Akaunti husika katika Halmashauri 45.

k) Madeni Tarajiwa

Halmashauri 18 zilikuwa na kesi mbalimbali zilizokuwa zikisubiri uamuzi wa mahakama. Jumla ya Sh. 8,698,124,431 zikiwa ni madeni tarajiwa zilioneshwa katika taarifa za fedha kuhusiana na kesi hizo. Hata hivyo, ilibainika kwamba ikama ya watumishi wa idara ya sheria bado haitoshelezi ili kuziwezesha Serikali za Mitaa kumudu kushughulikia masuala yote ya kisheria. Hali hii mara nyingine ilisababisha Serikali za Mitaa kutokuwa na wawakilishi katika mahakama. Serikali za Mitaa zinakabiliwa na hatari ya kushindwa kesi mahakamani na hasara zisizo na lazima. Hali hii inahitaji kuimarisha idara ya kisheria katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

l) Matokeo ya kaguzi maalum

Masuala mbali mbali yalijitokeza katika Kaguzi Maalum 14 zilizofanyika katika mwaka husika. Matokeo ya Kaguzi hizo maalum ni kama yalivyoainishwa hapa chini:

- Hati za Malipo zenye thamani ya Sh.4,996,554,685 na viambatanisho vyenye jumla ya Sh.1,075,263,998 havikuwasilishwa wakati wa Ukaguzi.
- Malipo ya mishahara kwa Watumishi ambao hawako katika utumishi wa serikali na majina hayajafutwa katika Orodha ya mishahara kiasi cha Sh.82,372,936. Vilevile kuna mishahara kiasi cha Sh. 275,206,250.53 isiyolipwa kwa sababu mbali mbali haikurejeshwa Hazina, Halmashauri zilizohusika ni za Ruangwa, Songea, Kilwa, Morogoro, Manispaa za Dodoma na Arusha.

- Kumekuwa na matumizi katika Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ambayo hayaruhusiwa na Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya mwaka 2009.
- Mapungufu katika mikataba ya kukusanya Maduhuli katika vyanzo vikuu vya mapato, mapungufu hayo ni: kiasi cha fedha kinachotakiwa kuwasilishwa katika Halmashauri kutojulikana, tarehe ya kuwasilisha mapato haikuainishwa na kiasi cha dhamana ambacho kinatakiwa kutolewa kwa Mawakala hakikuainishwa katika Halmashauri za Kiteto, Manispaa za Arusha na Dodoma.
- Udhaifu katika usimamizi wa Manunuzi na mikataba ambayo imepelekea Halmashauri kuingia mikataba ambayo haikufuata sheria, kuwa na makadirio ya kazi ambayo siyo sahihi, ucheleweshaji wa kumaliza kazi ambao siyo wa lazima, kutokukata tozo ya ucheleweshaji wa kazi; na kuwa na malipo yanayosigana. Hayo yote yamebainika katika Halmashauri za Kilwa, Muheza, Ruangwa, Morogoro na Manispaa ya Temeke.
- Kutokuwa na uaminifu katika Sehemu za kazi kumepelekea baadhi ya Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kufanya ubadhirifu wa Sh.23,219,089 na Watumishi wengine kuwa na Kesi ya kugushi ya Sh.12,735,000.
- Hundu ambazo zilionekana kuwa zimefutwa katika Regista ya Hundu lakini hali halisi ni kwamba hundi hizo zililipwa katika Benki kiasi cha Sh.2,750,000. Pia malipo yalifanyika katika Akaunti za Benki tano(5) kwa kutumia hundi za kughushi za jumla ya Sh.55,825,000 kwa kushirikiana kati watumishi wa Halmashauri na Watumishi wa Benki. Wizi huo umebainika katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa.
- Ubadhirifu katika fedha za TASAF kiasi cha Sh.60,446,710 ambazo zilitumika katika matumizi mengine tofauti na yale yaliyoidhinishwa na TASAF (Halmashauri ya Wilaya za Kilindi na Ruangwa).

- Makusanyo ya kodi ya Ardhi ambayo hayajakusanya kiasi cha Sh. 123,081,730.24 katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.
- Fedha kiasi cha Sh.42,080,000 zilizopokelewa kwa ajili ya kusafirisha mahindi ya njaa ambazo mapokezi na matumizi ya fedha hizo hayakuthibitishwa (Halmashauri ya Kilwa na Ruangwa).
- Kuna masuala yaliyosalia katika usuluhishi wa kibenki ambayo yanajumuisha mapato katika daftari ya fedha lakini hayaonekani katika taarifa za benki Sh.74,398,220.64 na hundi zisizo wasilishwa benki za Sh.16,514,982 hii ilibainika kutoka katika orodha ya hundi ambazo hazijalipwa. Pia hundi Na.000116 yenyе thamani ya Sh.9,860,812 ilipokelewa tarehe 10/7/2008 lakini haikuoneshwa katika taarifa za benki hadi tarehe ya ukaguzi (Manispaa ya Temeke)
- Jumla ya Sh.109,874,000 zilitumika kutekeleza miradi mbalimbali ambayo haikuwa katika Mpango Kazi katika mwaka wa fedha 2010/2011. Jumla ya Sh.113,927,250 zilitumika zaidi ya bajeti kwa miradi iliyopangwa kutekelezwa (Halmashauri ya Songea)
- Lita 8,060 za diseli zenye thamani ya Sh.16,330,600 zilinunuliwa na kutumika katika magari ya Halmashauri ambayo hayatembe (yaliyoharibika) yaliyohifadhiwa katika gereji ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea.
- Matumizi ya vitabu vya mapato ambavyo si vya Halmashauri na wizi wa kughushi tarakimu kwenye stakabadhi za mapato(Manispaa za Arusha na Dodoma).
- Halmashauri ilitoza bei ya chini ambayo ilikuwa na tofauti kubwa ukilinganisha na bei ya soko, kutokusanya kodi za vyumba/vibanda walivyopangisha ambavyo vinamilikiwa na Halmashauri-mapato zaidi ya Sh.3,888,314,960 yamepotea (Manispaa ya Arusha).
- Upotevu wa Sh.817,263,062 kutokana na watumishi kutokuwa waaminifu katika mikataba ya mapato ya ada za kuegesha magari na upotevu wa Sh.307,000,000

kutokana na mikataba mibovu na uzembe wa watumishi(Manispaa ya Arusha).

- Ubadhilifu na kughushi malipo Sh.10,250,000 (Manispaa ya Arusha)
- Kutokuwa na udhibiti wa kutosha dhidi ya utoaji na urejeshaji wa masurufu Sh.201,145,280 (Manispaa ya Arusha).
- Nyaraka kadhaa hazikuletwa kwa ajili ya ukaguzi zikiwemo taarifa za benki kwa miezi ya Januari 2011-Novemba 2011, na hundi Na. 812792 yenye thamani ya Sh.19,800,000 iliyolipwa na benki ya NMB tawi la Wami (H/W Morogoro)
- Malipo yaliyofanyika benki bila kutumia hundi Sh.156,460,259 (H/W Morogoro)
- Mishahara iliyolipwa zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa cha watumishi husika Sh.25,146,020 (H/W Morogoro)
- Bakaa ya ruzuku ya mishahara iliyotumika katika matumizi mengine ya Halmashauri Sh.452,015,896.44 (H/W Morogoro)
- Kutokuwa na idhini ya kuhamisha fedha kutoka akaunti ya Miradi ya maji vijijini kwenda katika akaunti ya Maji ya malipo mengineyo (OC) Sh.24,915,460; Matumizi mabaya ya fedha za maendeleo yaliyotumika katika matumizi yasiyohusiana na kusudio Sh.50,791,000; na malipo katika Akaunti ya Amana yasiyozingatia sheria Sh.78,256,289.40 (H/W Morogoro)
- Ilibainika kwamba Halmashauri ilitoa vitabu vya mapato 1,254 (vya wazi) na 1,292 (vyenye kiwango maalum) kwa Mawakala wa kukusanya mapato. Hata hivyo, hadi kipindi cha ukaguzi Novemba, 2012 vitabu hivyo havikurejeshwa Halmashauri. (H/W Mbarali).
- Upembusi yakinifu haukufanyika na mshauri juu ya udhaifu wa aina ya udongo wakati wa maandalizi ya Mchanganuo wa Gherama za Kazi na michoro, hivyo kusababisha hasara ya Sh.122,780,704. (H/W Mvomero);
- Malipo ya ujenzi kwa mkandarasi aliyepatikana bila kuwepo ushindanishi Sh.91,724,822 na malipo mengine

- ya ujenzi ya Sh.443,941,442 yaliyofanyika bila kufuata taratibu za manunuizi; na hakuna uthibitisho wa majadiliano kabla ya kuingia mikataba (H/W Mvomero).
- Manunuizi yaliyofanyika bila kuwa na ushindani wa zabuni ambao umepelekea hasara ya Sh.17,339,000. (H/W Mvomero);

3. Mapendekezo ya jumla kwa ufupi

Pamoja na kuwa na mapendekezo ya kina yaliyotolewa kwa kila Menejimenti ya Halmashauri kwa kuititia ripoti za menejimenti kwa mwaka huu wa ukaguzi, nina mapendekezo yafuatayo:

(i) Ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita

Maafisa Masuuli wanaowajibika katika udhibiti na usimamizi wa fedha za Serikali za Mitaa wanapaswa kuweka juhud zaidi ili kuhakikisha kwamba mapendekezo ya ukaguzi yanayohusu miaka ya nyuma yanashughulikiwa ipasavyo ili kuondoa uwezekano kurudia makosa hayo hayo katika kaguzi zijazo.

(ii) Maandalizinauwasilishaji wataarifa za Hesabu kulingana na viwango vya kimataifa vya uandaaji wa Hesabu kwa Sekta ya Umma (IPSAS)

- Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali inapaswa kujenga uwezo wa Serikali za Mitaa katika maandalizi ya taarifa za fedha kulingana na IPSAS kuititia mafunzo mbalimbali. Mbali na hayo, OWM-TAMISEMI na Mhasibu Mkuu wa Serikali pia wanapaswa kuweka utaratibu wenye ufanisi wa kufuatilia uandaaji wa taarifa za fedha kama unakidhi matakwa ya IPSAS katika Halmashauri zote kabla ya kumaliza kipindi cha miaka mitano cha mpito tangu kuanza kutumika kwa IPSAs.

- Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinapaswa kuimarisha uwekaji wa taarifa katika uandaaji wa taarifa za fedha, na hasa kwa kuifanyia na kutoa mapendekezo ya maboresho ya mwongozo wa Kihasibu wa Serikali za Mitaa(LAAM), wa mwaka 2009.
- Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali ya Tanzania ilifanya mabadiliko kwenye Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha kwa kutoka Epicor 7.3.5 kwenda Epicor 9.05, lakini kunachangamoto kadhaa katika utekelezaji wa mabadiliko hayo. Katika suala hili, naweka tahadhari juu yachangamoto hizo ili kuimarisha na kuboresha mchakato wa uandaaji pia kuimarisha wa uwasilishaji wa taarifa kwa wakati katika matumizi ya fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI inapaswa kufanya mafunzo ya mara kwa mara ili kujenga uwezo wa watumishi wanaoshiriki katika maandalizi ya Taarifa za FedhakupitiaEpicor9.05kutokana na ukweli kwamba, toleo hili la Epicor ni jipya kwa watumishi wengi wa Serikali za Mitaa na ina maboresho mengi katika utendaji wake.

(iii) Mikataba ya ukusanyaji mapato

Kutokana na Matokeo ya ukaguzi ninapendekeza yafuatayo:

- Kuwepo mipango mizuri kabla ya uamuvi wa kutoa kazi ya ukusanyaji mapato kwa mawakala ikiwemo utafiti mzuri wa hali ya soko kwa shughuli zinazoainishwa, kabla ya kutoa uamuvi wa kubinafsisha vyanzo vya mapato kwa mawakala wa ukusanyaji mapato. Upembusi yakinifu lazima ufanyike kikamilifu ili kujuua kiasi ambacho kitakusanywa kutoka kila chanzo cha mapato kama msingi wa kubinafsisha.
- Mchakato sahihi wa manunuvi ufuatwe ili kupata ushindani mzuri wa kumpata mzabuni. Hii ni pamoja na kuandaa nyaraka nzuri za zabuni, kuwepo muda wa

kutosha kwa ajili ya wazabuni kuwasilisha zabuni zao, na mchakato sahihi wa tathmini na wafanyakazi wenye uujuzi wa kiufundi.

- Mikataba kati ya Halmashauri na mawakala wa ukusanyaji wa mapato iandaliwe vema ili iweze kulinda maslahi ya halmashauri. Utendaji wa mawakala wa ukusanyaji wa mapato ufuatiliwe kwa karibu ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa ya kila mwezi na robo mwaka.
- Tozo/adhabu zinazotokana na kukiukwa kwa vipengele vya mkataba zitekelezwe kama ilivyo katika mkataba husika.
- Kwa Serikali kuu na Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa (RAS), inashauriwa kwamba wao watoe msaada wa kiufundi, ushauri na uongozi kwa Serikali za Mitaa juu ya masuala yanayohusiana na ubinafsishaji wa vyanzo vya mapato.
- OWM-TAMISEMI inashauriwa kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa watumishi wa Halmashauri na madiwani ili kuwawezesha kusimamia vizuri mapato kutoka kwa mawakala. OWM-TAMISEMI pia imependekezwa kudai taarifa juu ya ukusanyaji wa mapato kutoka Serikali za Mitaa kwa ajili ya ufuatiliaji mzuri na tathmini ya utendaji Halmashauri.
- OWM-TAMISEMI kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhhibit wa Ununuvi wa Umma (PPRA) inashauriwa kuunda nyaraka za zabuni maalum kwa ajili ya mapato yanayokusanywa na mawakala katika Serikali za Mitaa. Hii italeta uthabiti katika shughuli za ukusanyaji wa mapato ya Serikali za Mitaa.

(iv) Uboreshaji wa makusanyo katika vyanzo vya Mapato ya Serikali za mitaa

Serikali Kuukupitia OWM-TAMISEMI inapaswa kufanya tathmini ya kina ya mfumo uliopo wa makusanyo ya mapato ili kuhakikisha kwamba inasaidia Halmashauri husika kuongeza mapato ya ndani ya kutosha. Halmashauri

inapaswa kupitisha sheria ndogo ndogo kwa ajili ya vyanzo vyote vya mapato; hii itahakikisha kwamba kuna sheria inayokubalika kwa ajili ya ukusanyaji kwa wanaofuata na wanaokiuka sheria hizo. Halmashauri inapaswa kufuatilia utekelezaji wa mikataba iliyoingia kati yake na mawakala wa ukusanyaji wa mapato. Viongozi wa kisiasa wanapaswa waelimishwe na mara kwa mara wakumbushwe juu ya jukumu lao la kutoa msaada katika ukusanyaji wa mapato ya ndani.

(v) Kuboresha Usimamizi wa Matumizi

Maafisa Masuuli wanatakiwa kuimarisha usimamizi wa matumizi ili kuhakikisha kwamba rasilimali zinatumika kwa tija, ufanisi, kwa gharama nafuu na kwa uwazi; na kwamba matumizi yote ni muhimu, sahihi, yanalipwa kwa wakati na kumbukumbu zinawekwa vema na taarifa zinatolewa. Uwepo mkachato sahihi wa kuzuia, kutambua na kukabiliana na matumizi yasiyoidhinishwa, matumizi yasiyo na hati za malipo, matumizi yenye mapungufu, matumizi yenye hati pungufu, na matumizi yasiyo na tija.

Tatizo la kukosekana kwa hati za malipo ni moja ya kiashiria cha kutokuwa na ufanisi wa mfumo wa udhibiti wa ndani. Hili tatizo limekuwa likiendelea kujirudia kwa muda mrefu katika Halmashauri, napenda kuwakumbusha uongozi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa juu ya wajibu wao wa msingi katika kuhakikisha kwamba, nyaraka muhimu za Halmashauri kama hati za malipo zinahifadhiwa na kulindwa kikamilifu.

(vi) Kuimarisha menejimenti ya rasilimali watu na udhibiti mishahara

- Rasilimaliwatu ni mali muhimu katika taasisi, kwa hiyo Maafisa Masuuli wa Serikali za Mitaa wanapaswa kuhakikisha kwamba, menejimenti ya rasilimaliwatu inapewa kipaumbele na umakini ili kusaidia kufikia Malengo ya Kimkakati ya Halmashauri. Tunasitisiza mapendekezo yetu ya awali kwamba, Serikali za Mitaa

kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI zinapaswa kuhakikisha mfumo endelevu wa kufuatilia idadi ya watumishi inayohitajika na kuchukua hatua sahihi kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika Halmashauri ili kuboresha utoaji wa huduma katika sekta ya umma.

- OWM-TAMISEMI inatakiwa kuhakikisha kwamba kuna usawa wa kugawa watumishi katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa badala ya kuwapanga watumishi wengi katika miji na Halmashauri ya Manispaa. Hii itapunguza utendaji duni wa shughuli katika baadhi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, hivyo kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii.
- Kuweka watu kukaimu katika nafasi za juu katika Serikali za Mitaa kwa muda mrefu bila kuthibitishwa si vema kwa ajili ya menejimenti na maafikiano ya kanuni ya utawala bora. Uongozi wa Halmashauri unapaswa kuangalia njia sahihi ili kupunguza tatizo la kukaimu na wale ambao wanakaimu ni vema wathibitishwe ikiwa wana sifa.
- Pamoja nakuanzishwa kwa Mfumo wa kushughulikia taarifa za rasilimaliwatu (HCMIS) Mwaka 2010 chini yamfumo wa LAWSON toleo la 9, baadhi Halmashauri bado zinakutana na matatizo katika usimamizi wa mishahara ikiwa ni pamoja na kumbukumbu batili katika orodha za mishahara. Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Fedha inapaswa kuhakikisha Mfumo wa kushughulikia taarifa za rasilimaliwatu (HCMIS) kwa kutumia LAWSON unatekelezwa kwa ufanisi na kwa tija katika utayarishaji na utoaji wa taarifa za watumishi ambazo ni kamili za kuaminika na sahihi.
- **Malipo ya mishahara kwa watumishi hewa**
Malipo ya mishahara kwa watumishi hewa ni tatizo kubwa katika Serikali za Mitaa. Napendekeza kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Serikali za

Mitaa itoze faini kwa maafisa ambao wanachangia malipo ya mishahara hewa.

- Mbali na uvunjaji wa sheria, pia kuna ukosefu wa motisha kwa watumishi katika kufanya kazi kwa ufanisi kwa sababu ya athari kubwa za kukopa kupindukia ambayo inapelekea utendaji duni wa kazi. Menejimenti ya Halmashauri inapaswa kuelimisha watumishi wake kuhusu madhara ya kukopa kutoka taasisi nyingi mbalimbali za fedha na kuhakikisha kuwa maombi yote ya mikopo yapitie kwa Maafisa Masuuli na Maafisa Rasilimaliwatu kwa madhumuni ya kudhibiti. Serikali inapaswa kuwa na mikakati ya kujenga motisha ili kuwahamasisha watumishi hasa wa kipato cha chini. Hii itaepusha tatizo la kukopa kupindukia kwa watumishi wa Halmashauri.

(vii) Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo (CDCF)

Uongozi wa Halmashauri pamoja na Kamati ya Mfuko wa jimbo wanapaswa kutumia mfuko kwa mujibu wa Sheria Namba¹⁶ ya Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo ya 2009 na sheria nyingine zilizopo kwa ajili ya kusimamia rasilimali za umma.

(viii) Mapungufu/changamoto katika utekelezaji wa bajeti

Uongozi wa Halmashauri unapaswa kuendelea kufuatilia Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa fedha imetolewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za bajeti na kama hilo halikuwezekana, kurekebisha bajeti zao kulingana na uhalisia. Aidha, Serikali za Mitaa zinashauriwa kuhakikisha taratibu kwa ajili ya matumizi ya ruzuku zinazingatiwa, kwa kuongeza kasi katika kutekeleza kazi zilizopangwa katika matumizi ya kawaida ambayo italeta matokeo mazuri katika kuongeza utoaji huduma zinazotarajiwा.

- (ix) Uimarishaji Usimamizi wa miradi**
- Uongozi wa Halmashauri unapaswa kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo ambayo itahakikisha kwamba changamoto zilizoonekana zinatatuliwa kwa ya utekelezaji mzuri wa miradi iliyopangwa.
 - Kiasi cha fedha kinachohamishiwa Halmashauri kizingatie bajeti iliyopitishwa na bunge ili kuharakisha maendeleo kwa jamii.
- (x) Makatibu Tawala wa Mikoa kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Halmashauri**
- Sekretarieti ya Mkoa inapaswa kuwa na orodha ya miradi yote inayotekelawa katika ngazi ya Halmashauri na kufanya usimamizi juu ya miradi yoyote itakayoiteua bila kuongozwa na viongozi wa Halmashauri au Wilaya.
 - Sekretarieti ya Mkoa inatakiwa kuhakikisha kwamba, nyaraka kuhusiana na miradi kama vile mchanganuo wa gharama za kazi (BOQ), makubaliano kati ya Halmashauri na Wafadhili (MoU), Mkataba, Muhtasari wa bodi ya Zabuni, ripoti ya tathmini na kama inawezekana kuhudhuria baadhi ya mikutano inayofanyika katika mradi.
 - Ufuatiliaji wa karibu unatakiwa ufanyike kwa mapendekezo yaliyotolewa kipindi cha usimamizi wa miradi husika.
 - Menejimenti ya Sekretarieti ya Mkoa inatakiwa kuhakikisha kwamba, usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hasa katika Halmashauri unafanyika angalau mara moja katika kila robo ya mwaka na Wahandisi wanapaswa kushiriki katika zoezi hilo.
- (xi) Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake**
Maafisa Masuuli wanapaswa kuimarisha mchakato wa manunuzi ikiwa ni pamoja na manunuzi ya ufanisi na

usimamizi wa mikataba kwa kuzingatia sheria za manunuzi ili kufikia thamani ya fedha.

(xii) **Kuchelewa kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa miradi**

Maafisa Masuuliwote wanapaswa kuzingatia maelekezo ya kuwawezesha wakaguzi kukagua utekelezaji wa miradi kwa kipindi husika pamoja na ripoti zingine za fedha, na kufanya ziara kuthibitisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa pia kutathmini mafanikio yaliyofikiwa. Hii itachangia juhud ya wakaguzi kupelekea uwepo wa thamani ya fedha katika miradi kama hiyo iliyofanywa na Halmashauri na kutoa taarifa juu ya matokeo ya tathmini.

(xiii) **Kaguzi maalum**

Kutokana na matokeo ya kaguzi maalum, ninapendekeza kuwa:

- Pamoja na kuimarisha udhibiti wa ndani kama kipimo cha kushughulikia udhaifu uliobainika katika kaguzi maalum, hatua za kinidhamu na kisheria zichukuliwe kwa maafisa wale amba wamekuwa wakihuishwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
- Wanasheria wa Halmashauri wana wajibu wa msingi wakuhakikisha mikataba inaandaliwa vizuri na kutekelezwa. Wajibu huu ni kuhakikisha kwamba kesi zote zinazotokana na uvunjaji wa mikataba zinafikishwa mahakamani na kusimamiwa.
- Maafisa Masuuli wanatakiwa kuteua wajumbe wa Bodi ya Zabuni amba ni mahiri katika sheria ya manunuzi. Pia wanatakiwa kuendelea kutoa mafunzo juu ya Sheria ya manunuzi ya umma na kanuni zake. Kitengo cha manunuzi (PMU), kama wataalamu katika ununuzi, wanatakiwa kuendelea kushauri wajumbe wa kamati masuala ya kiutaalam katika vikao vya Bodi ya Zabuni badala ya

kuwapotosha kama ilivyobainika katika kaguzi maalum mbalimbali.

- Ili kutekeleza nidhamu katika eneo la kazi, ninapendekeza kwamba wafanyakazi wote waliothibitika kuwa si waminifu na ambao wameonekana kuwa na makosa katika utendaji kazi wao katika ofisi za umma, hatua stahiki zichukuliwe mara moja dhidi yao badala ya kuwahamishia vituo vingine nya kazi.
- Wakuu wa idara katika Halmashauri nyingi wanafanya kazi kwa kukaimu. Hii huathiri utendaji wao wa kazi. OWM-TAMISEMI inatakiwa kuhakikisha kwamba wale maofisa ambao wamekuwa wanakaimu na ambao wana ujuzi na wazuri wanatakiwa wathibitishwe katika nafasi zao.
- Kitengo cha Fedha ni sehemu muhimu katika shughuli za Halmashauri hasa katika kuainisha vyanzo nya mapato na matumizi yake. Ili kuwa na uwezo wa kutambua na kukusanya mapato, Halmashauri inahitaji kuwa na wafanyakazi wenye sifa na kiwango cha juu cha uadilifu. Kwa hiyo, tunapendekeza kwamba wafanyakazi wa kitengo cha fedha ambao hawajafuzu wanatakiwa wajiendoeleze kupata sifa zinazostahili.
- Ili kupunguza wizi wa mapato ya ndani, tunapendekeza kwamba mapato yote kutoka vyanzo visivyo na mikataba na ambayo kiasi kinacholipwa kinajulikana, kinapaswa kulipwa kwa hundi iliyofungwa au zipelekwe moja kwa moja benki.
- Halmashauri zinapaswa kukuzingatia mahitaji ya masharti ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Na.21 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za msingi. Kitengo cha manunuza cha Halmashauri (PMU) wanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria zilizowekwa, sera na taratibu.
- Halmashauri zinapaswa kuanzisha utaratibu wa kutoa mafunzo kwa maafisa ambao ni watumishi

wanaoshiriki katika kutambua na kukusanya vyanzo vya mapato ya ndani kuimarisha uwezo wao. Hii itasababisha ukusanyaji na ufanisi wa mapato ya vyanzo vya ndani.

(xiv) **Kuendelea kula njama kati ya Watumishi wa Halmashauri na wafanyakazi wa benki na kuiba fedha za Halmashauri.**

- OWM-TAMISEMI na serikali kwa ujumla inatakiwa kuwa na mikakati mabsusi ya kukomesha tabia ya ubadhilifu wa fedha za umma ikihusisha taasisi za benki ambazo zimeaminiwa kama sehemu ya kudhibiti na kulinda fedha za umma.
Kwa kuongezea, OWM-TAMISEMI na Halmashauri zinatakiwa kuwa na mfumo wa imara wa kuwachunguza watumishi wao.
- Kuendelea kwa matumizi mabaya ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa kunaashiria udhaifu wa udhibiti wa mfumo wa ndani. Hivyo, inashauriwa kwamba Halmashauri kwa kushirikia na na OWM-TAMISEMI inatakiwa kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani katika usimamizi wa fedha za umma ikiwa ni pamoja na kuimarisha utendaji kazi wenye ufanisi katika vitengo vya ukaguzi wa ndani.
- Uongozi wa Serikali za Mitaa unatakiwa kuhakikisha kwamba bakaa la benki la kila siku kwenye akaunti za Halmashauri zinajulikana kwa ajili ya kubaini miamala isiyoidhinishwa katika akaunti za Halmashauri husika. Aidha, uhakiki na usuluhishi wa kibenki ufanyike kila mwezi na kutiwa saini na Afisa Masuuli.
- Hatua za kinidhamu na kisheria zichukuliwe dhidi ya watumishi wote ambao kwa njia moja au nyingine, walihusika katika utovu wa nidhamu kama vile matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

- Taasisi za benki zimeaminiwa hasa katika kulinda na kutunza fedha kwa niaba ya wadau wao ikiwa ni pamoja na Serikali za Mitaa. Hata hivyo, katika matukio hayo benki imechangia sana upotevu wa fedha za Umma. Kwa hiyo Serikali inapaswa kutoa maelekezo kwa Taasisi za kibenki ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi ambao wanaohusika katika udanganyifu wanapatikana na hatua sahihi za kisheria zinachukuliwa dhidi yao.

(xv) Utendaji wa Bohari Kuu ya Madawa kuhusiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa

- Wizara ya Ustawi wa Afya na Ustawi inatakiwa kuhakikisha kuwa kiasi cha fedha kinachopokelewa toka Hazina kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa vyta zinapelekwa Bohari Kuu ya Madawa, na Bohari Kuu ya Madawa inapaswa kuzijulisha Halmashauri kiasi kilichotengwa kwa ajili yao.
- Menejimenti ya Bohari Kuu ya Madawa inapaswa kuhakikisha kuwa kuna akiba ya kutosha ya madawa muhimu na vifaa vyta tiba. Aidha, vifaa na madawa zilizonunuliwa na Bohari Kuu ya Madawa vinapaswa kuwa na viwango vinavyohitajika ili kuepuka kupokea vifaa vyta tiba duni na madawa yasiyokuwa na ubora.

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI WA MAMBO YA JUMLA

1.1 Mamlaka na Madhumuni ya Ukaguzi

1.1.1 Mamlaka ya kufanya Ukaguzi

Ripoti hii imetolewa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu Na.45 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) pamoja na Kifungu Na.10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 ambavyo kisheria vinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa ndiye Mkaguzi wa mapato na matumizi yote ya Serikali ikiwa ni pamoja na Mapato na Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (2) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kukagua na kutoa taarifa, angalau mara moja kila mwaka, juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, taarifa za fedha zilizoandaliwa na maafisa wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; taarifa za fedha za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taarifa za fedha zinazotayarishwa na Katibu wa Bunge.

Kwa upande mwingine, kifungu 45 (1) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) kinabainisha kuwa Mkaguzi wa nje wa hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Pia Kifungu Na. 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Zaidi ya hayo, kifungu cha 45 (5) cha Sheria Na.9 ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kukagua fedha, uwekezaji au mali nyingine ambazo zinamilikiwa au zilizo chini ya uthibiti wa Halmashauri, kuwa na fursa kwa muda wowote ya kukagua hesabu, vitabu, hati za malipo na nyaraka zote zinazohusiana.

Aidha, kifungu cha 48 (1), (2) na (4) cha Sheria Namba 9 ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuandaa na kusaini ripoti ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo ni Mizania ya hesabu za mwaka na taarifa nyingine zinazohusiana nazo, ambapo nakala moja ya kila ripoti pamoja na mizania ya hesabu na taarifa nyingine zinazohusiana zitapelekwa kwa Waziri, Mkuu wa Mkoa na Mkurugenzi Mtendaji ambaye anatakiwa kuziwasilisha kwenye kikao cha Baraza la Madiwani.

Kifungu hicho pia kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kubainisha kila kifungu cha matumizi ambacho kimetumika bila kufuata Sheria kuidhinishwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu pia anapaswa kubainisha mapungufu au hasara ambayo imetokea aidha kwa uzembe au mtu yejete kushindwa kutoa taarifa ya matumizi ya fedha alizokabidhiwa. Pia suala lingine ni kuthibitisha kiasi cha matumizi yaliyofanyika kinyume na sheria, matumizi yenye upungufu au hasara ambayo haijaoneshwa vitabuni.

Taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizowasilishwa kwa ukaguzi zimetayarishwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta za Umma (IPSASs), pamoja na sehemu ya (iv) ya Sheria Na.9 ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000), na pia kulingana na Agizo

Na.31(4) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka, 2009 kama msingi wa utayarishaji wa taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Seti kamili ya taarifa za hesabu zilizotayarishwa kwa kutumia viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma ambayo inatakiwa kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi inajumuisha:

- (a) Taarifa ya Mizania ya hesabu;
- (b) Taarifa ya mapato na matumizi;
- (c) Taarifa kuhusu mabadiliko ya mtaji;
- (d) Taarifa ya mtiririko wa fedha;
- (e) Taarifa ya uwiano wa bajeti na kiasi halisi cha matumizi kama yalivyojitekeza;
- (f) Taarifa ya uwiano wa bajeti na kiasi halisi cha matumizi kwa kila idara;
- (g) Maelezo ya ziada yanayohusiana na taarifa za hesabu.

Kwa uwazi na uwajibikaji, Kifungu Na. 49 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) na kama iliyoyositisitwa kwenye Agizo Na. 31 (9) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009, inazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kutangaza katika Ofisi zake au kwa kadri itakavyoolekezwa na Mkuu wa Mkoa kutangaza taarifa zifuatazo katika eneo lake:

- (i) Muhtasari wa taarifa jumuifu ya Mizania ya hesabu na taarifa ya mapato na matumizi zilizokaguliwa.
- (ii) Ripoti yoyote inayohusu hesabu husika na kusainiwa na Mkaguzi katika kipindi cha miezi sita baada ya kufungwa kwa mahesabu ya mwaka au katika kipindi cha miezi sita baada ya kupata taarifa ya ukaguzi au kadri itakavyokuwa.

Nimeridhia kuwa, kufuatwa kwa msingi wa utaarishaji wa taarifa za Hesabu na kuchapishwa kwa hesabu na ripoti

za ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni fursa nyingine kwa Mamlaka hizo kuongeza mawasiliano kwa upana zaidi na kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Umma.

1.1.2 Madhumuni ya ukaguzi

Lengo kuu la kufanya ukaguzi ni kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa na uhuru wa kutoa maoni ya ukaguzi kuhusiana na hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012 na kubainisha endapo kama zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango vinavyotakiwa kulingana na misingi ya utayarishaji wa hesabu, ikiwa ni pamoja na:

- Kuhakikisha kuwa fedha zote zimepokelewa na kutumiwa kwa matumizi halali kama ilivyoidhinishwa na Bunge kwa kufuata Kanuni zinazosimamia matumizi ya fedha za Serikali kwa kuzingatia bajeti iliyopitishwa.
- Kuhakikisha iwapo mapato yote yaliyokusanya yameingizwa vema katika vitabu.
- Kuhakikisha kuwa nyaraka zote muhimu, vitabu, regista, taarifa za fedha na taarifa mbalimbali zimetayarishwa vizuri zikionesha miamala yote na bakaa husika.
- Kuhakikisha kwamba vitu vyote muhimu vilivyo kwenye taarifa za fedha vinawasilishwa na kutolewa taarifa vizuri.
- Kufanya tathmini na kupima mifumo mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kubaini uimara na ubora wa Uthibiti wa Mfumo wa ndani ikiwa ni pamoja na uthibiti wa teknologia ya mawasiliano.
- Kutathmini hatari inayoweza kutokea kutokana na makosa ya kiukaguzi.

- Kuhakikisha kuwa malengo yaliyo tegemewa au mafanikio yamepatikana na kwamba malengo yaliyowekwa na Bunge au chombo kingine kilichoidhinishwa yamefikiwa.
- Kufanya tathmini ili kuona kama Mamlaka za Serikali za Mitaa zinafuata taratibu za manunuza kama zilivyoelezwa katika Sheria ya manunuza ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004, pamoja na Kanuni zake za mwaka, 2005.
- Kuhakikisha kuwa utawala bora umejengeka katika kufanikisha shughuli za kila siku za Hal mashauri na katika kutekeleza malengo yote kwa ujumla na jinsi menejimenti inavyosimamia masuala ya kijamii na mazingira.

1.2 Viwango na taratibu zinazotumika kutoa taarifa

1.2.1 Viwango vinavyotumika wakati wa Ukaguzi

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Asasi za Ukaguzi (INTOSAI), Shirika la Afrika la Asasi Kuu za Ukaguzi (AFROSAI), na Shirika la Afrika la Asasi Kuu za Ukaguzi - kwa nchi zinazozungumza lugha ya Kiingereza (AFROSAI-E) ambazo zinasaidiana katika kubadilishana mawazo na uzoefu kati ya nchi wanachama duniani katika ukaguzi wa taasisi za Umma.

Ikiwa ni mwanachama wa Asasi hizo za kimataifa, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inawajibika kutumia viwango vya ukaguzi vilivyotolewa na INTOSAI ambavyo ni viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAI) na viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) vilivyotolewa na Shirikisho la Wahasibu la Kimataifa (IFAC) wakati wa ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

1.2.2 Taratibu zinazotumika kutoa taarifa

Hatua mbalimbali zimefanyika ikiwa ni pamoja na kufanya mawasiliano na uongozi wa Halmashauri inayokaguliwa kabla ya kutoa ripoti hii ya mwaka. Kwa hiyo basi, ni vyema kubainisha hatua zote za ukaguzi kwa watumiaji wa Ripoti hii ili waweze kufahamu juu ya ripoti hii ya mwaka na taratibu zinazotumika katika kukamilisha ripoti. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:

- (i) Kutoa barua ya kuanza ukaguzi kwa mkaguliwa inayoeleza madhumuni na mawanda ya ukaguzi, na maeneo yanayotarajiwa kufanyiwa ukaguzi na kuelezea kazi na majukumu ya mkaguzi na uongozi wa Halmashauri inayokaguliwa.
- (ii) Kuandaa mpango mkakati wa ukaguzi unaoonesha mwelekeo mzima wa ukaguzi, vigezo vitakavyotumika katika hatua za mwanzo za kutathmini Halmashauri inayokaguliwa.
- (iii) Kufanya kikao cha kwanza na uongozi wa Halmashauri inayokaguliwa kabla ya kuanza ukaguzi. Kikao hiki kinatoa nafasi ya kuueleza Uongozi madhumuni na malengo ya kufanya ukaguzi na kinampa nafasi mkaguliwa kuelezea maeneo ya ukaguzi.
- (iv) Kuanza ukaguzi wa awali kwa kutathmini udhibiti wa ndani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika na kujiridhisha kama unafanya kazi ipasavyo.
- (v) Kutoa ripoti kwa uongozi wa Halmashauri kwa kipindi cha kati inayoonesha matokeo ya ukaguzi ikiwa ni pamoja na hoja za ukaguzi na kutoa nafasi kwa uongozi wa mkaguliwa ili kuweza kujibu hoja hizo.

- (vi) Kufanya ukaguzi wa taarifa za fedha kwa kujiridhisha kwamba zimeandaliwa kwa kufuata misingi ya utayarishaji wa taarifa za Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- (vii) Kufanya kikao cha mwisho na Uongozi wa Halmashauri inayokaguliwa baada ya kumaliza ukaguzi kwa kuwajulisha matokeo ya ukaguzi na kuwapa nafasi ya kutoa maoni yao kabla ya taarifa ya mwisho ya ukaguzi hajatolewa.
- (viii) Kutoa taarifa ya mwisho ya ukaguzi kwa Uongozi wa Halmashauri inayokaguliwa kwa kuujulisha Uongozi wa Halmashauri iliyokaguliwa mambo yote yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi na kutoa nafasi zaidi ya kuyashughulikia. Hatua hii pia ni ya msingi katika kutayarisha ripoti ya mwaka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- (ix) Kuandaa ripoti kuu ya mwaka ya Mamlaka za Serikali za Mtaa na kuiwasilisha Bungeni kupitia kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- (x) Kufuutilia matokeo ya ukaguzi yaliyotolewa katika ripoti kama ilivyoainishwa katika Kifungu Na.40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 kwa kubainisha na kutoa taarifa kama kila Mkaguliwa ameandaa mkakati au ametekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti pamoja na kuonesha hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi katika Ripoti ijayo ya Ukaguzi kama inavyotakiwa na Kifungu Na.40 (4) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

Kwa kifupi mchoro ufuatao hapa chini unaonesha hatua zinazofuatwa wakati wa ukaguzi:



1.3 Idadi ya Halmashauri zinazokaguliwa na mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

1.3.1 Idadi ya Halmashauri zinazokaguliwa


Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2011/2012, kulikuwa na Mamlaka za Serikali za mitaa 134 katika Tanzania bara ambazo zilikaguliwa na kutolewa ripoti ya ukaguzi kwa kila Halmashauri husika. Mamlaka hizi za Serikali za Mitaa zina hadhi tofauti kuanzia Halmashauri za Wilaya hadi Halmashauri za jiji kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 1 : Idadi ya Wakaguliwa

Na.	Halmashauri	Jumla	Asilimia (%)
1.	Halmashauri za Jiji	4	3
2.	Halmashauri za Manispaa	17	13
3.	Halmashauri za Miji	7	5
4.	Halmashauri za Wilaya	106	79
	Jumla	134	100

1.3.2 Mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Kuna jumla ya Halmashauri 134 ambazo zinakaguliwa na Ofisi 24 za Ukaguzi zilizopo mikoani kote Tanzania Bara. Ofisi za Ukaguzi Mikoani zinaongozwa na Wakaguzi Wakazi ambao wanasmamiwa na Wakaguzi wasaidizi wa Mkaguzi mkuu wa kila Kanda. Kwa madhumuni ya Ukaguzi unaofanyika katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa nchini, Ofisi hizo zimegawanywa katika Kanda sita. Ofisi za Kanda zinaongozwa za Wasaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa kila Kanda ambao wanasmamiwa na Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Divisheni ya Serikali za Mitaa. Kwa mujibu wa Muundo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Divisheni ya Serikali za Mitaa anawajibika moja kwa moja kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyoonekana katika Sehemu ya Muundo wa Ofisi hapa chini:



1.4 Majukumu ya kisheria ya Mamlaka za Serikali za mitaa katika kuandaa Taarifa za Fedha

Uongozi wa kila Halmashauri una wajibu wa kuandaa na kuonesha kwa usahihi taarifa za fedha kwa kufuata udhibiti wa ndani ambao uongozi umejiwekea katika kuandaa taarifa za fedha ambazo hazina dosari kutokana na udanganyifu au makosa mengine.

Kifungu cha 40(1) cha Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (Iliyorekebishwa 2000) imeainisha kuwa, kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa ina wajibu wa kutunza vitabu vya hesabu na kumbukumbu zinazohusu:

- a. Mapato na matumizi ya fedha na miamala mingine katika mamlaka
- b. Mali na dhima; mapato na matumizi ya mamlaka

Kifungu kilichotajwa hapo juu kimehuishwa na Agizo Na.11 mpaka 14 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009 inayotaka Halmashauri kuanzisha na kusimamia udhibiti wa ndani wa shughuli za Halmashauri. Kwa nyongeza, Agizo Na.31 inazipa majukumu menejimenti za Halmashauri kuandaa taarifa za fedha kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, miongozo inayotolewa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa na kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSAWs).

Pamoja na majukumu ya uaandaaji wa taarifa za hesabu, Kifungu cha 49 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya 1982 (Iliyorekebishwa 2000) na Agizo Na.31 (9) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 2009 vinaitaka kila Mamlaka ya Serikali ya mtaa kuchapisha taarifa za fedha zilizokaguliwa ndani ya maeneo yao ya uwajibikaji.

1.5 Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha

Agizo Na. 31(1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2009 na Kifungu 45(4) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa, 2000) inamtaka kila Afisa Masuuli kuandaa taarifa za mwisho za Hesabu na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya ukaguzi tarehe 30 Septemba au kabla ya tarehe hiyo kila mwaka.

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2012, Halmashauri ziliwasilisha hesabu zao kulingana na tarehe iliyokubalika kisheria au kabla ya tarehe 30 Septemba 2012.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa taarifa hizo za fedha imebainika kwamba, kuna baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliwasilisha taarifa za fedha zikiwa na makosa makubwa na kutooneshwa kabisa kwa mambo mengine muhimu. Taarifa hizo za fedha ziliwasilishwa tu kwa lengo la kutimiza wajibu wa kisheria wa kuwasilisha taarifa za fedha kwa wakati kwa ajili ya ukaguzi.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zipatazo sitinina saba (67) ziliwasilisha taarifa za fedha zikiwa na makosa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuonesha tarakimu katika mahesabu ambazo ni zaidi au pungufu ikilinganishwa na tarakimu zilizotakiwa kuoneshwa katika taarifa hizo za fedha. Kwa ujumla taarifa hizo zilizowasilishwa awali zilionesha jumla ya kiasi cha Sh.126,432,283,544 pungufu ya kiasi ambacho kilitakiwa kuoneshwa sawa na 10% ya matumizi yote na kiasi cha Sh.84,862,411,758 kilioneshwa zaidi ambacho ni sawa na 7% ya matumizi yote ya fedha kama inavyooneshwa katika jedwali hapo chini. Orodha kamili ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo taarifa zake za fedha zilionesha tarakimu zaidi au pungufu imeoneshwa katika **Kiambatisho (i)**.

Jedwali Na.2 : Upotoshwaji katika Uandaaji wa Taarifa za Hesabu za Mwaka

Maelezo	Kiasi kilichooneshwa pungufu (Sh.)	Kiasi kilichooneshwa zaidi (Sh.)
Jumla ya matumizi	1,294,973,777,766	1,294,973,777,766
Jumla ya makosa	126,432,283,544	84,862,411,758
Asilimia (%)	10%	7%

Kutokana na makosa hayo yaliyopelekea kuoneshwa kwa kiasi pungufu au zaidi katika taarifa hizo za fedha, Mamlaka za Serikali za Mitaa husika zilirejeshewa taarifa za fedha zilizowasilishwa awali kwa minajili ya kuzifanyia marekebisho na baadaye ziliwasilishwa tena kwa ajili ya ukaguzi.

Mwelekeo wa taarifa za fedha zilizorekeblishwa kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo ni kama ufuatao:

Jedwali Na. 3 : Halmashauri zilizorekebisha taarifa za fedha

Mwaka wa fedha	Idadi ya Halmashauri zilizokaguliwa	Idadi ya Halmashauri zilizoleta taarifa za fedha zilizorekeblishwa	Asilimia
2007/08	133	15	11%
2008/09	133	24	18%
2009/10	134	44	33%
2010/11	133	60	45%
2011/12	134	67	50%

Mchanganuo huo hapo juu unaonekana pia katika chati iliooneshwa hapa chini:



Mwelekeo wa taarifa za fedha zilizorekebishwa kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo hapo juu unaonesha kuwa, kuna ongezeko kubwa la Halmashauri ambazo zilirejeshewa taarifa za hesabu zilizowasilishwa awali na kuzifanyia marekebisho na baadaye kuziwasilisha tena kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo imejitokeza kwa sababu ya kutokuwepo kwa mafunzo ya kutosha kwa watumishi ili waweze kuandaa hesabu kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSASs) na uhamisho wa watumishi ambao wamebobea kwenye kuandaa taarifa kwa kufuata IPSASs.

Idadi kubwa ya makosa na marekebisho yaliyofanywa kwenye taarifa za fedha zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na masuala ya uhasibu yanayohusiana nayo yanaashiria kutakiwa kuwepo kwa jitihada za dhati katika kuhakikisha taarifa zinazoletwa kwa ukaguzi zinakuwa sahihi na zinazoonesha mambo yote yanayotakiwa.

Ninapendekeza kuwa, katika miaka ijayo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa zianzishe mchakato wa uhakiki na udhibiti wa ubora kwa ajili ya maandalizi ya taarifa za fedha ili kuhakikisha usahihi wa taarifa hizo kabla hazijawasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Kwa kuongezea, OWM-TAMISEMI inatakiwa kuandaa mafunzo ya mara kwa mara katika kujenga uwezo wa watumishi wanaoanda taarifa za fedha.

SURA YA PILI

2.0 MAANA, AINA, VIGEZO NA MWELEKEO WA HATI ZA UKAGUZI

2.1 Hati za Ukaguzi

Katika kutekeleza matakwa ya Kisheria, ninawajibika kutoa uhakika kwa wadau wa Halmashauri kwamba, taarifa za fedha zilizotayarishwa na Halmashauri zinatoa picha halisi ya matokeo ya shughuli zilizofanyika, mtiririko wa fedha pia mali na madeni ya Halmashauri kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012. Maoni ya ukaguzi yanatolewa kwa wadau kama uhakikisho wa usahihi wa taarifa za fedha za Halmashauri pamoja na uzingatiaji wa taratibu zinazotakiwa.

2.2 Maana ya Hati za Ukaguzi

Hati ya ukaguzi ni maoni ya mkaguzi yanayoeleza kama taarifa za fedha zilizokaguliwa zimetayarishwa katika mambo yote muhimu, kwa mujibu wa misingi inayotumika katika uandaaji wa tarifa hizo. Hati ya ukaguzi pia inazungumzia kama taarifa za fedha zilizowasilishwa zina maelezo ya kutosha katika kuelezea vizuri na kwa upana zaidi taarifa hizo.

2.3 Aina ya Hati za ukaguzi

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) na Viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs), zifuatazo ni aina za Hati za Ukaguzi ambazo zimetolewa kama kipimo katika utayarishaji wa taarifa za fedha:

2.3.1 Hati inayoridhisha

Hati ya aina hii inatolewa wakati nimeridhika kuwa, taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetayarishwa kulingana misingi ya utaarishaji wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Hata hivyo, utoaji wa hati inayoridhisha haina maana kwamba Halmashauri ina mfumo safi kabisa wa udhibiti wa ndani. Hati hii ina maana kwamba hakuna jambo lolote nililoliona ambalo lingesababisha kutolewa kwa hati yenye shaka. Kila Halmashauri iliyopata aina hii ya hati imeandikiwa taarifa nyingine ya ukaguzi kwa ajili ya menejimenti inayoeleza masuala ambayo yasipoangaliwa, yanaweza kuisababishia Halmashauri kupata hati yenye shaka miaka ijayo.

2.3.2 Hati inayoridhisha na yenye masuala ya msisitizo

Masuala ya msisitizo na masuala mengine yanawekwa kama mawasiliano ya ziada kuitia katika ripoti ambayo Mkaguzi anaona inafaa:

- (a) Kuvuta dhamira ya watumiaji wa hesabu zilizoandalowi katika suala au masuala yaliyooneshwa ndani ya taarifa za fedha, kwamba ni muhimu na ya msingi kwa watumiaji katika kuelewa taarifa za fedha.
- (b) Kuvuta dhamira ya watumiaji wa hesabu katika suala au masuala yale yaliyo oneshwa kwenye taarifa za hesabu ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuuelewa vizuri ukaguzi, majukumu ya wakaguzi au ripoti ya ukaguzi.

2.3.2.1 Masuala ya msisitizo

Katika baadhi ya maeneo, nimejumuisha aya inayohusu masuala ya msisitizo ili kuweka bayana masuala ambayo hata kama yameoneshwa vema katika taarifa za fedha, kwa mtizamo wangu, yana umuhimu na ya msingi kwa watumiaji wa taarifa za fedha. Nyongeza ya aya ya masuala hayo yenye msisitizo haiathiri maoni ya ukaguzi. Aya ya masuala yenye msisitizo inajumuishwa pale panapokuwa na mazingira yafuatayo:

- Kuweka angalizo juu ya mambo yanayoweza kuwa na athari ambapo ufumbuzi wake unategemea mambo ya baadaye yasiyo moja kwa moja ndani ya uwezo wa taasisi yenewe na ambayo yanaweza kuleta athari katika taarifa za fedha, kwa mfano matokeo ya baadae yasiyo ya kawaida yanayohitaji kushughulikiwa mahakamani au kisheria.
- Kuweka angalizo juu ya mambo mengineyo yaliyooneshwa katika taarifa ya utekelezaji ya mkaguliwa ya mwaka ambayo kuyafanya marekebisho ni muhimu lakini Mkaguliwa amekataa kufanya marekebisho.
- Kuweka angalizo katika masuala yanayoathiri taarifa za fedha yaliyooneshwa katika taarifa za fedha ambayo ni muhimu kuleta karibu uelewa wa taarifa za hesabu kama vile janga kubwa lililotoka au linaloendelea kutokea na kuleta madhara makubwa ya hali ya kifedha katika taasisi.

2.3.2.2 Masuala mengine

Aya ya masuala mengine inahusu mambo ambayo hayakuoneshwa katika taarifa za fedha na kwamba kwa mtazamo wa mkaguzi ni muhimu mtumiaji wa taarifa za fedha kuelewa ukaguzi, majukumu ya mkaguzi na ripoti ya mkaguzi.

Endapo nitaona inafaa kuwasilisha masuala mengine kuliko yale yaliyooneshwa katika taarifa za hesabu, nitatumia aya ya masuala mengine kwa masuala hayo yenyе kichwa cha masuala mengine, ambayo itakuwa baada ya aya ya hati ya ukaguzi na masuala yenyе msisitizo kama yapo. Haya masuala mengine yapo katika sehemu tofauti ya ripoti ya mwaka ya ukaguzi ili kutenganisha wazi wazi kutoka katika majukumu ya mkaguzi, na hati ya ukaguzi juu ya taarifa za fedha na masuala mengine yaliyokuwa na angalizo katika aya zilizotangulia za msisitizo wa masuala. Mifano ya

masuala mengine ni pamoja na kutofuata sheria na udhaifu katika udhibiti wa ndani.

2.3.3 Hati yenyе shaka

Hati yenyе shaka inatolewa iwapo ninaridhika kuwa, taarifa za fedha hazikuonesha usahihi, kutokukubaliana na uongozi au kukwazwa kwa mawanda ambapo athari yake ni kubwa lakini si muhimu na kwamba ukiacha athari zilizopelekea kutoa hati yenyе shaka, taarifa za hesabu zimetengenezwa kulingana na misingi ya utayarishaji wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa hivyo hazihitaji kutolewa hati isiyoridhisha.

Kwa maana nyingine, Hati yenyе shaka inatolewa endapo kuna kutolewana na Uongozi katika sehemu moja au zaidi ya taarifa za fedha lakini makosa hayo hayaathiri eneo lililosalia la taarifa za fedha na halisababishi taarifa za fedha kwa ujumla kuonekana zina makosa.

2.3.4 Hati isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha inatolewa pale ninapothibitisha kwamba, taarifa za fedha hazikutengenezwa kwa kufuata misingi inayokubalika ya utayarishaji wa taarifa za fedha au viwango vya uhasibu ambapo, kunakuwa na kiasi kikubwa cha kutokukubaliana na menejimenti na kuna madhara makubwa kwenye taarifa za hesabu kwa aidha kutofuata taratibu za fedha zilizowekwa au taarifa za hesabu zilizowasilishwa hazina maelezo ya kutosha ambayo yanawezesha taarifa za fedha kueleze ka vizuri na kwa upana zaidi.

Kwa maana nyingine, aina hii ya Hati inatolewa kama nikiona kuwa taarifa za fedha zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi kama zimeonekana zimekosewa kwa kiwango kikubwa na zimetayarishwa bila kufuata misingi wa utayarishaji wa taarifa za Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa ujumla, aina hii ya hati inatolewa wakati

kumekuwa na mapungufu makubwa katika taarifa za fedha kiasi kwamba zinapotosha kabisa ukweli wa taarifa hizo.

2.3.5 Hati mbaya

Hati mbaya hutolewa wakati ninaposhindwa kupata uthibitisho wa ukaguzi wa kutosha na hivyo kushindwa kutoa maoni juu ya taarifa za fedha zilizowasilishwa. Hali hiyo inaathiri kwa kiasi kikubwa taarifa za hesabu kiasi ambacho ninashindwa kutoa maoni yangu juu ya hesabu husika. Endapo taarifa za fedha zitakuwa na mapungufu makubwa, sitaweza kutoa maoni yangu juu ya taarifa zilizowasilishwa.

Hati hii ya ukaguzi inatolewa endapo kumekuwa na mambo ambayo si rahisi kwangu kupata taarifa na nyaraka ambazo zimetumika kuandaa taarifa za fedha.

Kwa maana hiyo, hati mbaya inatolewa katika taarifa za fedha ambazo uwezekano wa kufanya ukaguzi umeshindikana ili kubaini kama kuna mapungufu yoyote au kubaini kwamba utayarishaji wa taarifa za fedha umefuata msingi wa utayarishaji wa taarifa za Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

2.3.6 Vigezo au mambo yanayopelekea kutoa hati yenye shaka

Vifuatavyo ni vigezo au mambo ambayo yanaweza kumuwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa hati yenye shaka:

(a) Kukwazwa kwa mawanda ya Ukaguzi kwa kushindwa kupata taarifa na nyaraka za kutosha wakati wa ukaguzi.

(b) Mambo ambayo yanaendana na kutokufuata sheria:

i) Utayarishaji wa taarifa za fedha ambao haukufuata misingi ya utayarishaji wa taarifa za Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

- ii) Uingizaji wa taarifa katika vitabu nya fedha ambao haujafuata taratibu zinazostahili.
- iii) Taarifa muhimu na za msingi zinazoathiri vitabu nya fedha na hivyo kusababisha kupata hati yenye shaka.

2.4 Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi katika Halmashauri

2.4.1 Mchanganuo wa ujumla wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Sehemu hii ya ripoti inaonesha mwelekeo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010, 2010/2011 na 2011/2012. Umuhimu wa taarifa hii ni kuonesha mwelekeo wa hali ya utendaji na uwajibikaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha miaka mitano. Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Hati za ukaguzi zilizopata kwa miaka mitano imeoneshwa katika **Kiambatisho (ii)**.


Mchanganuo wa ujumla wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka ya fedha 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010, 2010/2011 na 2011/2012 ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo.

Jedwali Na. 4 : Mchanganuo wa ujumla wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Miaka	Hati Zinazoridhisha		Hati zenye shaka		Hati Zisizoridhisha		Hati Mbaya		Idadi ya Halma-shauri
	Jumla	%	Jumla	%	Jumla	%	Jumla	%	
2007/08	72	54	61	46	0	0	0	0	133
2008/09	77	58	55	41	1	1	0	0	133
2009/10	66	49	64	48	4	3	0	0	134
2010/11	72	54	56	42	5	4	0	0	133
2011/12	104	78	29	21	0	0	1	1	134

Ukaguzi wa marudio katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora uliofanyika baada ya kutoa ripoti yangu ya mwaka umepelekea Manispaa hiyo kupata hati isiyoridhisha. Kwa hiyo basi, idadi ya hati zisizoridhisha kwa mamlaka za serikali za mitaa kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ziliikuwa sita na si tano kama nilivyotolea taarifa katika ripoti ya mwaka 2010/2011.

Mchanganuo wa Hati za ukaguzi uliooneshwa hapo juu umeoneshwa pia katika grafu zifuatazo:



Kielelezo hapo juu linaonesha kuwa, hati zinazoridhisha zimeongezeka kwa Halmashauri 5 (4%) kutoka mwaka 2007/2008 hadi 2008/2009, zimepungua kwa Halmashauri 11 (9%) toka mwaka 2008/2009 hadi 2009/2010 na

kuongezeka kwa Halmashauri 6(5%) toka mwaka 2009/2010 hadi 2010/11 na Halmashauri 32 (24%) toka mwaka 2010/11 hadi 2010/12.

Hati zenyeshaka zimepungua kwa Halmashauri 6 (5%) toka mwaka 2007/2008 hadi 2008/2009 na kuongezeka kwa Halmashauri 9 (7%) toka mwaka 2008/2009 hadi mwaka 2009/2010 na kupungua kwa Halmashauri 8 (6%) toka 2009/2010 hadi mwaka 2010/2011 halikadhalika kwa Halmashauri 27 (21%) toka 2010/2011 hadi mwaka 2011/2012.

Hati zisizoridhisha zimeongezeka kwa Halmashauri 1 (1%) toka mwaka 2007/2008 hadi 2008/2009, zimeongezeka kwa Halmashauri 3 (2%) toka mwaka 2008/2009 hadi 2009/2010 na pia kuongezeka kwa Halmashauri 1 (1%) toka mwaka 2009/2010 hadi mwaka 2010/2011 na kupungua kwa 4% toka mwaka 2010/2011 hadi mwaka 2011/2012.

Hakukuwa na Hati Mbaya iliyotolewa katika Miaka ya 2007/08, 2008/09, 2009/10 na 2010/11. Hata hivyo katika mwaka wa fedha 2011/12, Hati Mbaya ilitolewa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ambayo ni sawa na 1%.

2.4.2 Mchanganuo wa Hati za ukaguzi zilizotolewakwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kutokana na mchanganuo wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka mitano, yafuatayo yamebainika:

- i) Halmashauri tisa (9) zimeendelea kuwa na hadhi ya kupata Hati zinazoridhisha kwa miaka mitano. Halmashauri husika ni H/W Biharamulo, H/W Missenyi, H/W Serengeti, H/W Kisarawe, H/W Mufindi, H/W

Siha, H/W Nachingwea, H/W Maswa na Manispaa ya Shinyanga.

- ii) Halmashauri saba (7) zimefanya vizuri ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo zilipata Hati zenye mashaka na Hati isiyoridhisha na kwa mwaka huu wa fedha zimepata Hati zinazoridhisha ambazo ni H/W Longido, H/W Moshi, H/W Namtumbo, H/W Kilosa, H/W Ngorongoro, H/W Morogoro na H/J Mwanza.
- iii) Halmashauri tano (5) zimeendelea kupata Hati zenye shaka kwa miaka mitano mfululizo ambazo ni H/M Arusha, H/W Makete, H/W Mvomero, H/Mji Korogwe na H/W Monduli.
- iv) H/W Kyela ndiyo pekee iliyoshuka ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo ilipata Hati inayoridhisha lakini katika ukaguzi wa mwaka husika imeweza kupata Hati yenye shaka.
- v) H/W Mbarali ndiyo pekee iliyopata Hati Mbaya katika ukaguzi wa mwaka 2011/2012.

2.5 Orodha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizopata Hati Mbaya na zenye shakana sababu zilizopelekea kupata hati hizo

Katika mwaka husika wa ukaguzi, kulikuwa na Halmashauri moja iliyopata hati isiyoridhisha na Mamlaka za Serikali za Mitaa zipatazo ishirini na tisa (29) zilizopata Hati zenye Shaka. Mchanganuo wa mambo ambayo yalikuwa ni vigezo katika kutoa Hati yenye shaka kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (iii)**.

Kutokana na Kiambatisho hicho, sampuli ya mambo yaliyokuwa ni kigezo cha kutoa Hati zenye shaka ni kama yafuatayo:

- Pamoja na kutolea taarifa katika mwaka uliopita, bado kumekuwa na Mishahara iliyolipwa kwa watumishi ambao wamestaafu, kufariki, kuachishwa kazi, watoro na watumishi waliohamishiwa utumishi wao sehemu nyingine. Malipo haya yalifanyika kupitia kwenye akaunti zao binafsi za benki, Serikali haikunufaika kutokana na malipo ya jinsi hii.
- Kulikuwa kutotoa taarifa ya uwekezaji katika taarifa za fedha za baadhi ya Halmashauri ambayo imapelekea mali za Halmashauri kutolewa taarifa pungufu.
- Malipo hayakuthibitishwa kupokelewa na walipwaji. Hakuna ushahidi wa mapokezi ya fedha hizo hivyo kudhibiti mawanda ya ukaguzi.
- Mali za kudumu zilioneshwa katika taarifa za fedha bila kuwa na michanganuo.
- Hati za malipo pamoja na viambatanisho vyake havikupatikana kwenye makabrasha yake na hivyo kudhibiti mawanda ya ukaguzi.
- Baadhi ya hati za malipo hazikuwa na viambatanisho vya kutosha na hivyo kufanya ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.
- Kulikuwa na upotoshwaji na kutooneshwa kwa mali, madeni, mapato na matumizi ambayo hayaonyeshi ukweli na hali halisi ya taarifa za fedha zilizowasilishwa.
- Kutotayarishwa kwa majedwali ya viambatanisho na taarifa za ziada za taarifa za fedha kulikosababisha kutokamilika kwa kumbukumbu zinazohusiana na taarifa za fedha zilizowasilishwa.
- Hapakuwa na michanganuo ya wadai na wadaiwa, hivyo ukaguzi ulishindwa kuthibitisha uhalali na usahihi wa taarifa hizo.
- Idadi kubwa ya vitabu vya kukusanya mapato havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, hivyo kiasi cha mapato yaliyokusanya kwa kutumia vitabu hivyo hayakuweza kuthibitika.

- Vifungu vya matumizi vililipiwa kimakosa kwenye vifungu vingine na hivyo kupotosha taarifa za fedha zilizoletwa. Mapungufu yote yaliyoainishwa hapo juu yalisababishwa kwa kiasi kikubwa na sababu zifuatazo:
 - ❖ Mafunzo ya kutosha hayatolewi kwa ajili ya kuandaa taarifa za fedha kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma.
 - ❖ Usimamizi usioridhisha unaofanywa na menejimenti ya Halmashauri kuhusiana na menejimenti ya fedha za Umma
 - ❖ Kula njama baina ya watumishi wa Halmashauri na watumishi wa benki katika kufuja fedha za Halmashauri.
 - ❖ Kuna udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani kwa ujumla katika Halmashauri.

Menejimenti za Halmashauri zinashauriwa kuimarisha mifumo ya Udhibiti wa Ndani, kutokana na kuwa, udhaifu mwangi niliouonesha hapo juu umetokana na udhaifu wa mfumo wa udhibiti wa ndani. Maeneo muhimu ya kuzingatiwa ni kama ifuatavyo:

- Kuimarisha matumizi ya Mfumo wa kushughulikia taarifa za rasilimaliwatu (HCMIS) kwa kutumia LAWSON. Hii inaweza kuondoa na changamoto ya kuwa na watumishi hewa.
- Kuimarishana kuhakikisha kuwa Mfumo funganifu wa kihasibu kwa kutumia Epicor 9.05 unatumika ipasavyo kwa kila Halmashauri. Hii itaimarisha mchakato wa utayarishaji wa taarifa za fedha wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Mafunzo endelevu juu ya IPSAS ni suluhisho kwa baadhi ya mapungufu yaliyobainishwa hapo juu. Viwango vya Kimataifa vinabadilika kila mara, hivyo kuna haja ya mafunzo hayo kuwa endelevu kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi.

SURA YA TATU

3.0 UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA

Sehemu hii inajumuisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika ripoti za miaka ya nyuma na muhtasari wa masuala yasiyo na tarakimu (qualitative) na yale yenye tarakimu (quantitative) ambayo yalioneckana katika taarifa za ukaguzi za mwaka na taarifa za ukaguzi maalum ambayo ama hayakutekelezwa au yelitekelezwa kwa sehemu. Pia sehemu hii inajumuisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa Halmashauri husika. Sura hii inamalizia na ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyomo katika ripoti ya mwaka ya LAAC iliyopitishwa na Bunge.

3.1 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka iliyopita katika Ripoti ya jumla ya Ukaguzi

Kifungu 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 kinawataka Maafisa Masuuli kutoa majibu na/au mpango wa utekelezaji wa ripoti ya kila mwaka ya ukaguzi na kuyawasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Zaidi ya hayo, Kifungu 40 (4) kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kujumuisha hali halisi ya utekelezaji wa mpango kazi katika ripoti ya ukaguzi wa mwaka ujao. Aya hii inaonesha hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya taarifa za fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2010/11.

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 40(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008, Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) anapaswa kupokea majibu kutoka kwa Maafisa Masuuli na baada ya hapo kuwasilisha kwa Waziri ambaye atapeleka

mbele ya Bunge. Pia, Mlipaji Mkuu anawajibika kuwasilisha nakala jumuifu ya majibu na mpango wa utekelezaji kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Majibu juu ya masuala yaliyojitokeza katika ukaguzi wa mwaka wa fedha uliomalizika Juni 30, 2011 yalitolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) kwa barua yenye Kumb. Na. EB/AG/AUDIT/12/VOL.I/53 ya tarehe 20 Juni, 2012. Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa juhudini zinazofanywa na Serikali kuitia Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) na Maafisa Masuuli wote kwa ajili ya kujibu masuala yaliyotolewa juu ya taarifa za ukaguzi na hatua zilizochukuliwa juu ya mapendekezo yaliyomo katika taarifa hiyo.

Hata hivyo, baada ya kupokea majibu, ifuatayo ni hali halisi ya masuala ambayo yanahitaji ufuutiliaji kwa ajili ya utekelezaji wa mipango iliyoinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

(i) Ukosefu wa mwongozo kwa ajili ya Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Nilipendekeza kwamba OWM-TAMISEMI inapaswa kuja na muundo sahihi wa udhibiti wa ndani ili kusaidia Halmashauri katika kuweka kumbukumbu za udhibiti wa ndani katika Halmashauri kwa ajili ya mafanikio ya malengo yao.

Hii ni pamoja na mwongozo wa ujumla katika maandalizi ya teknolojia ya habari, mfumo wa usimamizi wa majanga, mkataba wa utendaji wa kamati ya Ukaguzi, mkataba wa utendaji wa ukaguzi wa ndani na miongozo mingine muhimu katika kujenga mfumo madhubuti wa udhibiti wa ndani katika Halmashauri.

Utekelezaji

Serikali imeanzisha ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani ambayo tayari imeanza kazi. Mkaguzi Mkuu wa Ndani kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI waliendesha mafunzo yaliyofanyika miezi ya Februari na Machi 2012 ambayo ilikuwa inalenga kutoa mafunzo kuhusu kitabu cha mwongozo wa kazi za Mkaguzi wa Ndani.

Serikali kupitia Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa ndani, wamechukua hatua za kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani kwa kufanya yafuatayo:

- Kuandaa mwongozo juu ya Mfumo wa usimamizi wa majanga ambayo itatoa ufahamu juu ya hatua za kufuatwa wakati wa kuandaa miongozo bora ya usimamizi wa majanga katika sekta ya Umma itakayofanya kazi kuanzia mwaka 2013.
- Kutengeneza mwongozo kwa ajili ya kuandaa mkatuba wa huduma ya Ukaguzi wa Ndani kwa ajili ya kazi za ukaguzi wa ndani katika Serikali za Mitaa.
- Kupitia Kanuni zinazohusiana na Kamati ya ukaguzi na kuandaa miongozo ya kutumika kama mwongozo kwa kamati zote za ukaguzi katika Halmashauri.

(ii) Utofauti wa ripoti za fedha na kuitwa na wakati kwa Sheria za Serikaliza Mitaa

Ilipendekezwa kwamba, miongozo iliyopo ambayo ni Mwongozo wa Uandaaji Hesabu za Serikali za Mitaa wa mwaka 1993 na Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997 inatakiwa kuboresha ili kuendana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma.

Pia Halmashauri ziandae taarifa za fedha za mwezi na robo mwaka ikiwa ni pamoja na leja kuu, Urari, taarifa za fedha, taarifa ya mapato na matumizi, taarifa ya mtiririko wa fedha, taarifa ya mlinganisho wa bajeti na

matumizi na taarifa ya matumizi ya miradi ya maendeleo na ugharimiaji. Vile vile Uongozi wa Halmashauri unapaswa kutambua na kufahamu wajibu wa pamoja katika kuandaa taarifa za fedha za Halmashauri na pia kuwapa mafunzo watumishi wanaohusika na uandaaji wa taarifa za fedha.

Utekelezaji

Serikali iliamua kupitia upya sheria za serikali za Mitaa ili kuboresha mfumo wa kuripoti baada kuridhia mfumo wa viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma, hivyo Mwongozo wa Uandaaji Hesabu za Serikali za Mitaa wa mwaka 1993 na Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997 umerekebishwa mwaka 2009 na kutiwa saini na Waziri Mkuu kwa ajili ya matumizi.

Aidha, Sheria ya Serikali za Mitaa itapitiwa upya katika mwaka wa fedha 2012/2013. Kulingana na Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997 iliyorekebishwa 2009, Halmashauri zinatakiwa kuandaa/kutoa taarifa ya fedha ya kila mwezi na robo mwaka, (ripoti ya fedha ya Halmashauri na ripoti ya maendeleo ya Halmashauri) na kuwasilishwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa kwa ajili ya mapitio na majumuisho kabla ya kuwasilisha kwa OWM-TAMISEMI na nakala kwenda Hazina. Aidha Msaidizi wa Mhasibu Mkuu wa Serikali anayesimamia Serikali za Mitaa atasimamia na kushauri juu ya mapungufu yoyote yanayohusu taarifa hizo.

(iii) Uandaaji wa Taarifa za Fedha na Ukaguzi wa Hesabu za Vijiji

Katika suala hili, ilipendekezwa kwamba Uongozi wa Halmashauri unapaswa kuchukua jukumu la kuongoza na kuhakikisha kuwa masharti ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) yanazingatiwa. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa

uongozi wa kijiji husika unandaa taarifa za fedha na Halmashauri iwatumie ipasavyo wakaguzi wa ndani kwa ajili ya kufuatilia maandalizi ya taarifa hizo. Utaratibu huu unatarajiwa kuimarisha usimamizi katika ngazi ya Vijiji na kuboresha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi ya chini ya Serikali (Vijiji na kata).

Utekelezaji

Mafunzo kwa ajili ya watendaji wa serikali za vijiji/mtaa na kata kuhusu manejimenti ya fedha chini ya Mpango wa Maboresho wa serikali za mitaa II yamepangwa kukamilika mwezi Juni, 2013. Muundo mpya wa ufuatiliaji utafanyika ili kutumia Sekretarieti ya Mkoa kusaidia serikali za mitaa na kufanya utaratibu muhimu kufufua ufanisi katika uwajibikaji katika ngazi ya vijiji/mtaa na kata.

Serikali imeanza hatua za makusudi kuhakikisha kazi za ukaguzi katika Halmashauri inaongezewa nguvu na kufikia katika ngazi ya kijiji. Magari 65 yamesambazwa katika Halmashauri mbalimbali ili kuwawezesha wakaguzi wa ndani kufikia katika ngazi ya kijiji ambapo wahasibu wa vijiji wanatarajiwa kukaguliwa.

(iv) Kujenga uwezo kwa uongozi wa ngazi za chini za Serikali

Ilipendekezwa kwamba, Uongozi wa Halmashauri unapaswa kuanzisha mpango wa mafunzo ambayo yatasaidia viongozi wa Vijiji na Kamati za usimamizi wa Miradi ya Maendeleo kusimamia vizuri utekelezaji wa miradi ya maendeleo na wakati huo huo kuhakikisha kwamba kuna udhibiti sahihi juu ya ukusanyaji na matumizi ya mali za umma. Mpango wa mafunzo haya unaweza pia kusaidia kujenga uwezo wa Madiwani katika kusimamia rasilimali za Halmashauri.

Utekelezaji

Katika kujenga uwezo wa uongozi wa ngazi za chini za serikali, mpango rahisi wa kuwanoa viongozi wa vijiji katika kusimamia fedha za umma na upangaji wa miradi pamoja na ufuatiliaji ulianzishwa na kusambazwa kwa vijiji vyote katika mpango wa maboresho I. Hata hivyo, OWM-TAMISEMI itapitia upya nyenzo hizo katika Mpango wa Maboresho II na bajeti kwa mwaka 2012/2013.

(v) Udhafu ulioonekana wakati wa kaguzi maalum

Ilipendekezwa kwamba, pamoja na uimarishaji wa mfumo wa udhibiti wa ndani kama kipimo cha kurekebisha mapungufu yaliyoonekana katika ukaguzi wa kawaida na kaguzi maalum, Halmashauri zinashauriwa kuimarisha mfumo wa manunuzi katika kila Halmashauri husika. Hii inajumuisha utayarishaji wa taarifa za manunuzi kwa mujibu wa sheria, Halmashauri kutumia huduma zinazotolewa na Wakala wa Manunuzi wa Serikali (GPSA) ambao wana jukumu la kupanga na kusimamia manunuzi ya bidhaa za kawaida na huduma za manunuzi kupitia mfumo wa makubaliano.

Utekelezaji

Ili kuboresha mfumo wa manunuzi na kufanya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ilikuwa inafuatilia mfululizo wa kutathmini utendaji wa manunuzi ya Serikali za Mitaa. Hivyo hati za manunuzi katika miaka ya hivi karibuni zinapatikana na rahisi zaidi kukagua kuliko ilivyokuwa kabla. Lengo la baadae ni kushirikisha wafanyakazi zaidi na wenye uwezo katika Vitengo vya Ununuzi.

(vi) Fedha za Mfuko wa kuchochera Maendeleo ya Jimbo (CDCF)

Ilipendekezwa kwamba Halmashauri zinashauriwa kuhakikisha kuwa mfumo wa uwajibikaji unatekelezwa kwa mujibu wa Sheria Na.16 ya Mfuko wa kuchochera

Maendeleo ya Jimbo ya mwaka 2009 na sheria zilizopo sasa kwa ajili ya kusimamia mali za umma.

Pia, kwakutokutayarisha na kuwasilisha taarifa za mapokezi na matumizi ya fedha hizo zilizotumiwa na kamati za CDCF, OWM-TAMISEMI inashauriwa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa sheria ya Mfuko wa Jimbo kwa kuhakikisha kwamba hakuna matumizi yatakayofanyika kwa mwaka unaofuata kabla ya kuandaa taarifa ya mwaka uliotangulia, kuwasilisha taarifa hiyo na kuhakikisha kwamba imekubaliwa.

Utekelezaji

Mikoa na mamlaka za Serikali za Mitaa zinakumbushwa kuwa na uwazi zaidi katika usimamizi na uwajibikaji wa Mfuko wa Jimbo na kuhakikisha kuwa fedha hazitumiki kwa nia ya kisiasa

(vii) Ucheleweshaji wa ukamilishaji wa miradi na miradi iliyokamilika ambayo haitumiki

Yalitolewa mapendekezo kuwa, Uongozi wa Halmashauri uimarische ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara ambayo itahakikisha kwamba ufuatiliaji unaimarishwa na changamoto zinatatuliwa haraka kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyopangwa.

Pia, Halmashauri zihakikishe kwamba mara tu baada ya miradi kukamilika itumike kutoa huduma zilizokusudiwa. Pia ilishauriwa kuwa, wanasiasa wote katika ngazi zote waongeze mchango wao wa uhamasishaji katika kuhakikisha jamii inashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao. Hii si tu kuhakikisha kukamilika kwa miradi lakini pia kuwezesha jamii kujenga utamaduni wa kujitegemea.

Utekelezaji

Ili kurekebisha mapungufu haya, Serikali ilipitia upya mipango ya kimkoa ili kuboresha ufuatiliaji na tathmini ya Serikali za Mitaa. Mpango huu umeundwa ili kuonesha

udhaifu katika mifumo ya uendeshaji wa Serikali za Mitaa na ubora wa matokeo.

Mkakati mpya wa kuhakikisha upatikanaji wa miradi iliyobora na kukamilika kwa wakati, itatumika kwa miradi michache iliyochaguliwa kwa wakati huo, katika kila Wilaya ili fedha kidogo iliyohamishiwa na kupokelewa na Halmashauri ioneshe thamani ya fedha iliyowekezwa. Huu mpango utasaidia kupunguza gharama za uendeshaji kwa wasimamizi wa miradi iliyotawanyika sehemu mbalimbali.

(viii) Uwajibikaji katika mfuko wa LGDG na NMSF

Ilipendekezwa kwamba, taarifa juu ya fedha zilizopelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa lazima itolewe kwa Halmashauri mara tu pesa hizo zinapopelekwa. Taarifa hii lazima iwe na ufanuzi wa kutosha juu ya lengo la fedha zilizotumwa. Utoaji wa fedha zilizoidhinishwa kwa wakati, ni muhimu ili kuhakikisha kwamba shughuli zilizopangwa zinatekelezwa kwa wakati muafaka.

Utekelezaji

Mipango imefanywa na kuhakikisha kuwa fedha zote zilizohamishiwa Halmashauri zinaambatana na taarifa za kutosha/maelekezo na nakala ya taarifa hizo zitapelekwa Halmashauri husika. Pia Halmashauri zinashauriwa kutembelea tovuti ya wizara ya fedha na mipango.

(ix) Kuimarisha uratibu na usimamizi wa majukumu ya Sekretarieti yaMikoa

Ilipendekezwa kwamba, ili kuwa na matokeo yanayotarajiwa katika Serikali za Mitaa, Serikali inatakiwa kuimarisha uratibu na majukumu ya usimamizi waMakatibu Tawala wa Mikoa. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba, Sekretarieti za mikoa zinakuwa na uwezo unaotakiwa katika suala la kuwezesha ukuaji,

kuinua maendeleo na kuzisimamia Serikali za Mitaa na utambuzi wa malengo na shabaha ya Serikali za Mitaa kwa kuhusisha malengo ya maendeleo ya kitaifa.

Utekelezaji

Katika kuimarisha majukumu ya uratibu na usimamizi wa Sekretarieti za Mkoa, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI ilifanya mikutano miwili iliyofanyika St. Gasper Dodoma Mei, 2012 ambayo ilikuwa na maana ya kuwa mafunzo kwa viongozi wa kila mkoa na wilaya kupata fursa ya kujifunza matukio mbalimbali ili kubadilisha hali ya sasa kuwa na uongozi wa vitendo zaidi kati ya Sekretarieti ya Mkoa na Serikali za Mitaa.

(x) Ukopaji uliokithiri kwa watumishi wa Halmashauri ambao haukudhibitiwa na uongozi.

Nilipendekeza kwamba, Uongozi wa Halmashauri upewe maelekezo kuwa kila maombi ya mkopo ni lazima yapitishwe na Afisa Masuuli kwa ajili ya kudhibiti mikopo hiyo na makato. Pia uongozi wa Halmashauri uwe na usimamizi na utaratibu wa kuhakikisha kwamba elimu inatolewa mionganoni mwa watumishi ili waelewe kwamba mikopo iliyozidi kiwango hairuhusiwi na hiyo ina madhara makubwa kwao.

Utekelezaji

Serikali inaguswa sana na watumishi wa Serikali kukopa kwa kupindukia. Wakati wa warsha iliyofanyika Dodoma suala hili lilikuwa mionganoni mwa yale masuala ambayo yalijadiliwa kwa kina na kila upande unaohusika na mikopo hii kuwa na wajibu wa kufuata kanuni za utumishi zilizopo ambazo zinazuia watumishi wa umma kukopa kiasi cha kubakiwa na mshahara wa mwisho wa mwezi chini ya moja ya tatu.

Kutokana na maelezo hayo hapo juu, inaonesha wazi kwamba, majibu yaliyotolewa yanaridhisha, kwa kuwa

juhudini zimeoneshwa katika kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa kwa lengo la kuboresha usimamizi wa fedha za umma kwenye Halmashauri. Majibu yaliyotolewa yameonesha jitihaja za dhati za Serikali katika kutekeleza kikamilifu na kutatua mapungufu yaliyojitokeza. Ofisi yangu itaendelea kufanya ufuatiliaji wa majibu/mikakati hii.

- 3.2 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi**
Kwa miaka iliyopita katika Ripoti ya kila Halmashauri
Madhumuni ya mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) yaliyotolewa kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kuziwezesha Serikali za Mitaa husika kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa taarifa za fedha na mara moja kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa ili kuboresha udhibiti wa ndani na usimamizi wa rasilimali za Halmashauri.

Wakati wa kaguzi zilizopita, mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa ambayo yalizitaka Menejimenti za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuchukua hatua stahiki za utekelezaji wa mapendekezo hayo. Baadhi ya Halmashauri zilifanya jitihada za kutekeleza mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu.

Kati ya Hamashauri 134, Halmashauri 131 hazikutekeleza mapendekezo ya ukaguzi ya miaka ya nyuma yenyе jumla ya Sh. 78,489,936,013 katika kiasi hicho, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ilikuwa na mapendekezo yasiyotekelawa yenyе kiasi kikubwa cha Sh. 7,410,552,143 ikifuatiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Arusha yenyе Sh. 6,465,702,779. Halmashauri ya Wilaya ya Siha ambayo ilikuwa na mapendekezo yasiyotekelawa yenyе kiasi kidogo kuliko Halmashauri zote yenyе kiasi cha fedha cha Sh.2,700,000.

Hulka au tabia ya kutotekeleza mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inapelekea kujirudia kwa hoja ambazo zimetolewa na wakaguzi kwa miaka ya nyuma. Hii inaashiria kuwepo kwa mapungufu katika uwajibikaji kwa maafisa masuuli na uongozi kwa ujumla wa Halmashauri husika.

Jedwali hapa chini linaonesha kwa muhtasari hoja za ukaguzi ambazo hazijajibiwa katika kaguzi za miaka iliyopita kuanzia mwaka 2006/2007, 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010 na 2010/2011 kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 5: Mwenendo wa masuala yaliyosalia kwa miaka mitano mfululizo katika ripoti za kila Halmashauri

Mwaka wa fedha	Hoja za ukaguzi ambazo hazijajibiwa (Sh.)	Idadi ya Halmashauri husika
2006/2007	32,903,395,306	112
2007/2008	53,463,558,647	126
2008/2009	122,128,377,615	129
2009/2010	105,263,165,967	130
2010/2011	78,489,936,013	131

Mwelekeo wa masuala yasiyotekelawa ni kama inavyooneshwa katika chati mstari ifuatayo:



Chati mstari hapo juu inaonesha kwamba, jumla ya mapendekezo ya miaka ya nyuma ambayo hayakutekelezwa kwa mwaka 2006/2007 yalikuwa Sh.32.9 bilioni yakihuisha Halmashauri 112. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 idadi ya Halmashauri ambazo hazikutekeleza mapendekezo ya ukaguzi ziliongezeka kutoka 112 hadi 126 zikiwa na jumla ya kiasi cha Sh.53.5 bilioni na kusababisha ongezeko la Sh.20.6 bilioni. Pia katika mwaka wa fedha 2008/2009 idadi ya Halmashauri ambazo hazikutekeleza mapendekezo ya ukaguzi ziliongezeka kutoka 126 hadi 129 zikiwa na jumla ya kiasi cha Sh.122.1 bilioni na kusababisha ongezeko la Sh.68.7 bilioni. Zaidi katika mwaka wa fedha 2009/2010 idadi ya Halmashauri zimeongezeka kutoka 129 hadi kufikia 130 zikiwa na jumla ya kiasi cha Sh.105.2 bilioni na kusababisha kupungua kwa mapendekezo ambayo hayajatekelezwa kwa Sh.16.8 bilioni na kwa kipindi cha mwaka 2010/11 idadi ya Halmashauri zilizo na mapendekezo yasiyotekeliza kutokana na ukaguzi wa nyuma imeongezeka kutoka 130 hadi 131 ikiwa na jumla ya Sh.78.7 bilioni na kupelekea punguzo la 26.8 bilioni.

Mwenendo hapo juu unaonesha kwamba, Uongozi wa Serikali za Mitaa umejitahidi kuchukua hatua madhubuti katika kushughulikia mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Muhtasari wa Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokuwa na hoja za ukaguzi ambazo hazijajibiwa ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (iv)**.

3.3 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi katika Ripoti za Kaguzi Maalum

Kifungu 36 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya kaguzi maalumu. Sheria hii inaeleza kuwa, iwapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataona kuwa kuna jambo lolote lihusulo fedha au mali ya umma ambalo inabidi Bunge lijulishwe pasipo kuchelewa, ataandaa taarifa maalumu kuhusiana na jambo hilo na kuwasilisha taarifa hiyo Bungeni kuitia kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika mwaka wa ukaguzi uliopita, mapendekezo mbalimbali yaliyotokana na hoja za kaguzi maalum yalitolewa, mapendekezo hayo yalihitaji uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuchukua hatua madhubuti za utekelezaji ili kuboresha utendaji na uwajibikaji wa Halmashauri.

Orodha ya Halmashauri zilizo na hoja za ukaguzi ambazo hazijajibiwa ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (v)**.

Jedwali hapa chini linaonesha mapendekezo ya kaguzi maalum ambayo hayajatekelezwa kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2008/2009, 2009/2010 na 2010/2011.

Jedwali Na. 6: Masuala yaliyosalia katika kaguzi maalum

Mwaka wa fedha	Hoja za ukaguzi ambazo hazikujibiwa (Sh.)	Hoja za ukaguzi zilizosalia ambazo hazikuthaminishwa (Idadi ya Halmashauri)	Idadi ya Halmashauri
2008/2009	2,532,943,672	8	8
2009/2010	43,012,029,632	40	7
2010/2011	31,408,213,793	69	13

3.4 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC)

Sehemu hii inajumuisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) yaliyotolewa katika ripoti ya Kamati ya Mwaka kama inavyohitajika katika Kifungu Na. 40(3) cha Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma ya mwaka 2008.

Kifungu hicho kinamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kuandaa majibu na mpango wa utekelezaji wa ripoti ya CAG yakizingatia udhaifu uliobainika na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge za Usimamizi.

Mwenyekiti wa LAAC aliwasilisha ripoti ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ikijumuisha mapendekezo juu ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2010.

Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) wakati wa kuwasilisha majibu ya hoja za ukaguzi kwa taarifa za fedha za kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni 2011, hakujumuisha mapendekezo ya LAAC kama yalivyowasilishwa Bungeni tarehe 17 Aprili 2012 kama inavyooneshwa hapa chini:

(a) Mishahara iliyolipwa kwa Watumishi hewa

LAAC ilipendekeza kwamba, Serikali inapaswa kuwasilisha ripoti kuonesha jinsi ya kushughulika na tatizo hili ili kulimaliza kabisa. Serikali pia inapaswa kuwasilisha ripoti maalum juu ya hatua za kisheria zilizochukuliwa dhidi ya maafisa wahusika. Hii ni kutokana na kwamba tatizo hili limeripotiwa na CAG na LAAC kwa muda mrefu sasa na linaathiri matumizi ya fedha za umma.

(b) Hatua mahsusizi zinazopaswa kuchukuliwa ilikuimarisha

Mfumo wa Udhibiti wa Ndani wa Serikali za Mitaa

LAAC imebaini kwamba, suala la mapungufu katika mfumo wa udhibiti wa ndani una uhusiano wa moja kwa

moja na ulipwaji wa mishahara kwa wafanyakazi hewa pamoja na manunuzi yenye bei zenyenye mashaka na malipo yasiyokuwa na viambatanisho.

Kamati ilipendekeza kwamba Serikali ichukue hatua madhubuti katika kuimarishe mifumo ya udhibiti wa ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hii pia ijumuushe uimarisaji wa kazi za mkaguzi wa ndani kwa kuongeza uhuru kutoka udhibiti wa Wakurugenzi wa Halmashauri.

(c) Kujenga uwezo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania inatakiwa kuimarishe kwa kuongeza idadi ya wakaguzi na kupanua mawanda ya ukaguzi wa thamani ya fedha ili kufikia idadi kubwa ya halmashauri.

(d) Utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti ya ukaguzi Maalum ya Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu

Serikali iliagizwa kutoa maelezo ya kina kuwa, kwa nini ubadhirifu na wizi mkubwa umetokea kwenye Halmashauri ya wilaya ya Kishapu umeachwa bila kushughulikiwa kwa miaka mitatu mfululizo (2007/8-2009/10) bila wahusika wa wizi huo kuchukuliwa hatua za kisheria.

(e) Kutowasilisha kwa wakati ruzuku toka serikalini katika serikali za mitaa

- Serikali imeshauriwa juu ya umuhimu wa kuwa na bajeti ya uhakika. Hii itasaidia kuwepo kwa uwiano kati ya kiasi cha fedha kwenye bajeti inayopitishwa na Bunge kwa ajili ya Serikali za Mitaa na kiasi halisi ya fedha iliyotolewa na Hazina.
- Serikali inashauriwa kutoa ruzuku kwa wakati na kwa kiwango kinachostahili katika halmashauri.
- Serikali imeagizwa kuwasilisha Bungeni kila mwaka ripoti ya fedha zinazohusiana na fedha zinazopitishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika

Serikali za Mitaa. Taarifa hizo zioneshe kiasi cha fedha kilichopelekwa kwenye Halmashauri mbalimbali kwa mwaka husika.

- Serikali (Hazina) imeshauriwa kuanzisha utaratibu wa kuwa na mwakilishi ambae ni Afisa Bajeti Serikali za Mitaa kwenye Vikao vya LAAC. Mwakilishi huyo atasaidia kutoa ufanuzi wa baadhi ya masuala yanayohusu upelekaji wa ruzuku kwenye Serikali za Mitaa.

(f) Uzembe katika kukusanya mapato ya ndani

Kamati ilipendekeza kwamba Bunge likubali kuitaka Serikali:

- Kuandaa na kusimamia Mpango Mkakati Maalum wa Miaka Mitano kwa ajili ya kuhimiza na kukuza jitihada za Halmashauri kuongeza juhudzi za kubuni na kusimamia ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali.
- Kutathmini kwa pamoja (kulingana na mazingira ya kila Halmashauri) vyanzo vipya vya mapato.
- Kutoa taarifa ya tathmini ya ufanisi uliotokana na kuitumia Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) kukusanya kodi ya majengo katika Halmashauri za manispaa mbalimbali nchini.
- Kuona uwezekanao wa kuziachia Halmashauri baadhi ya vyanzo vya mapato vilivyoko kwenye maeneo yao (mfano ushuru wa minara ya simu na usajili wa zahanati binafsi). Lakini pia kuongeza asilimia ya mgawo wa mapato kwa Halmashauri (kwa mapato ambayo yanakusanywa na Halmashauri na kupelekwa Serikali Kuu).
- Kutoa maelezo na kisha ufumbuzi wa suala la nyumba za Halmashauri ya mbalimbali ilizouza. Mfano ukiwa ni

nyumba tatu za Manispaa ya Temeke zilizokuwa katika maeneo ya Masaki.

(g) Mkanganyiko wa Maelekezo yanayohusiana na mapato kutokana na ushuru wa kusafirisha korosho nje ya nchi.

Kamati inapendekeza kwamba Bunge liitake Serikali kuwianisha miongozo na maelekezo hayo mara moja ili kuondoa utata wa kutokupeleka gawio la ushuru huo kwa Halmashauri husika.

(h) Kusaini Mkataba wa pamoja kati ya Halmashauri za Dar es Salaam (yaani Ilala, Kinondoni, Temeke na Jiji) na Kampuni ya R&M kutoka Malaysia kwa ajili ya Kiwanda cha nyama mradi ambao haukuwa unafanya kazi.

- Kutoa maelezo Bungeni juu ya uwepo wa Mkataba wa mradi huo na kiasi cha fedha/ mali ambayo kila Halmashauri ilichangia
- Kutoa maelezo kuhusu nani alikuwa mkusanyaji wa michango hiyo na alikuwa akiiweka wapi
- Maelezo haya yaweke bayana kampuni ya R & M kutoka Malaysia na EAMEATCO zilipatikanaje na zilikuwa na nafasi gani katika Mradi/ Mkataba huo.
- Kutoa maelezo kuhusu namna Halmashauri za Mkoa wa Dare s Salaam zilivyofaidika na mradi huo ikiwa ni pamoja na hatma ya fedha/ mali ambazo Halmashauri hizo zilichangia katika Mradi huo.

(i) Uhamisho wa wafanyakazi wanaohusishwa na kesi ya matumizi mabaya yamefanywa kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine kwa sababu ya kutoa nafasi kwa ajili ya uchunguzi.

Kamati ilipendekeza kwamba Bunge liitake Serikali;

- Kutoa maelezo ya kuridhisha ni kwa nini baadhi ya watuhumiwa wa ubadhirifu katika Halmashauri hawachukuliwi hatua za kisheria badala yake wanahamishwa vituo vya kazi.
- Kutoa ufanuzi ni kwa namna gani kumhamisha mtuhumiwa wa ubadhirifu kwenda kituo kingine cha kazi kunatumika kama mbinu ya kukomesha tabia za kibadhirifu kwa mhusika.

(j) Kuendelea kuwepo kwa hati za malipo bila viambatanisho ni kiashiria cha upotevu wa mapato na matumizi holela ya fedha za serikali ambapo Sh.2.4 bilioni kilitolewa taarifa katika Mwaka wa Fedha 2009/2010

Kamati ilipendekeza kwamba Bunge liitake Serikali kueleza sababu za kuwepo kwa tatizo hili na Mkakati wake katika kulidhibiti.

(k) Kuwepo kwa Wakuu wengi wa Idara wanaokaimu majukumu yao katika kusimamia ina athari hasa katika kupanga mikakati mikubwa ya Serikali na matumizi bora ya fedha za umma

Bunge liliombwa likubali kuishauri Serikali ione uwezekano wa kulegeza sharti la uzoefu wa miaka saba badala yake iwe miaka mitatu ili isaidie kupunguza tatizo la kukaimu na madhara ya kukaimu katika usimamizi na matumizi bora ya fedha za umma katika Halmashauri.

(l) Udhafu katika usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya halmashauri

Kamati ilipendekeza kwamba Bunge likubali kuishauri Serikali,

- Kuandaa na kutekeleza Mpango Maalumu wa kuwaelimisha Madiwani na wananchi kwa ujumla juu ya umuhimu wao katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

- Kuwaelimisha Madiwani kwamba wao siyo watendaji na hivyo siyo jukumu lao kusaini mikataba ya miradi ya maendeleo na wazabuni kwa niaba ya Halmashauri.
- Kuzisimamia Halmashauri kwa ukaribu zaidi kwa lengo la kuimarisha ufanisi.

(m) Fedha kwa ajili ya ruzuku ya maendeleo (LGCDG) kwa ajili ya shule za sekondari nchini zimetumwa katika halmashauri za kata badala ya Bodi za Shule.

Kamati ilipendekeza kwamba Bunge likubali kuishauri Serikali kuwa badala ya kupeleka fedha hizo kwenye Mabaraza tajwa zipelekwe kwenye Bodi za Shule ili kuimarisha Utawala Bora katika Mabaraza hayo. Na kama Bodi za shule hizo hazijaundwa basi iwe sehemu ya ushauri huu kwamba Shule zote ambazo tayari zimekwisha anza kudahiri wanafunzi ziunde Bodi kwa ajili ya usimamizi wa shughuli zao.

(n) Tofauti ya tarakimu zilizo katika vitabu vya LAAC na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali.

Serikali imetakiwa kutoa maeleo kwa nini Taarifa zinazowasilishwa kwenye Kamati zinatofautiana na Taarifa zinazowasilishwa kwa CAG hasa katika kipengele cha matumizi.

(o) Kuwasilisha Taarifa ya LAAC pamoja na Hesabu za mwisho wa Mwaka.

Kamati inapendekeza kwamba Bunge likubali kuitaka Serikali (Halmashauri) kuwasilisha kwa CAG Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka (final Accounts) na Taarifa kwa ajili ya vikao vya LAAC kwa wakati sawa (kuanzia Hesabu za 2010/2011). Lakini pia pawekwe Kanuni za adhabu kwa Halmashauri ambayo itashindwa kutimiza sharti hili.

Kutokana na maelezo hayo hapo inaonesha kuwa hakuna hatua zilizochukuliwa na serikali kutekeleza maelekezo yaliyotolewa 17th April 2012 kuhusiana na hesabu zilizoishia tarhe 30th June 2010.

Hivyo basi hatua stahiki ziendelee kuchukuliwa na serikali kuhakikisha kuwa maelekezo yote yanatekelezwa kikamilifu ili kuleta ufanisi na uwajibikaji katika Mamlaka ya Serikali za mitaa.

SURA YA NNE

4.0 TATHMINI YA HALI YA FEDHA ZA HALMASHAURI

4.1 Ukaguzi wa Bajeti

Uandaaji wa bajeti ni sehemu muhimu katika mchakato wa kuandaa mipango, kudhibiti na kutathmini hali ya fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kwa uhalisia wake, ni njia ya kugawa rasilimali ili kufikia malengo yaliyowekwa. Ni chombo kinachosaidia viongozi kupanga pamoja na kudhibiti fedha ili kuhakikisha kwamba, kwa kadri inavyowezekana malengo yaliyopangwa yanafikiwa.

Kif. 43(1) cha Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) imeainisha kwamba, kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa muda usiopungua miezi miwili kabla ya mwanzo wa kila mwaka wa fedha, katika mukutano maalum utakaoitishwa, ipitishe bajeti ya makadirio ya kiasi (a) inachotarajia kupokea na (b) inachotarajia kutolewa, na Mamlaka katika mwaka wa fedha husika, na wakati wowote itakapohitajika, Mamlaka inaweza kupitisha bajeti ya ziada katika mwaka wa fedha husika. Katika kipindi cha ukaguzi wa mwaka uliomalizika, mapungufu yafuatayo yalioneckana katika ukaguzi wa bajeti:

4.1.1 Mwenendo wa Makusanyo katika Vyanzo vya

Halmashauri ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa

Mapato ya ndani kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa nikiasi cha fedha ambacho kimekadiriwa na kukusanya na Halmashauri kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vilivyoainishwa ambavyo havikusanywi na Serikali kuu. Kiasi hiki kinabakia Halmashauri ili kuongezea ruzuku inayopatikana kutoka Serikali kuu na wafadhili katika shughuli za kila siku za Halmashauri. Kwa hali hiyo, Mapato kutoka vyanzo vya ndani ni fedha zinazokusanya katika vyanzo vya umma kama vile kodi, ada, leseni na


fidia ya makosa mbalimbali. Wakati wa ukaguzi katika mwaka husika, Mamlaka ya Serikali za Mitaa 134 zilipanga kukusanya mapato kuitia vyanzo vyao vya ndani kwa kiasi cha Sh.297,383,435,946. Hata hivyo Halmashauri ziliweza kukusanya kiasi cha Sh.236,716,345,736. Hii inamaanisha kwamba Halmashauri zilikusanya chini ya bajeti kwa Sh.60,667,090,210 sawa na 20% ya bajeti.

Mchanganuo ufuatao unaonesha mwelekeo wa bajeti iliyopitishwa kwa miaka mitano na makusanyo halisi kutoka kwenye vyanzo vya ndani vya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Maelezo ya makusanyo ya mapato kwa kila Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2011/2012 yameoneshwaa kwenye **Kiambatisho (vi)**

Jedwali Na. 7: Mwelekeo unaonesha bajeti iliyoidhinishwa dhidi ya makusanyo halisi

Mwaka wa Fedha	Bajeti ya Mapato Iliyoidhinishwa (Sh.)	Mapato yaliyokusanywa na Halmashauri (Sh.)	Mapato Zaidi/ (Pungufu) ya Bajeti(Sh.)	%
2007/08	90,477,657,278	93,545,987,812	3,068,330,534	3.4%
2008/09	111,327,810,815	110,852,341,512	(475,469,303)	(0.4%)
2009/10	136,673,109,767	137,416,106,722	742,996,955	0.5%
2010/11	183,470,314,765	184,344,284,252	873,969,486	0.5%
2011/12	297,383,435,946	236,716,345,736	(60,667,090,210)	(20.4%)

Mchanganuo uliooneshwaa hapo juu unaonekana pia katika chati mhimili kama inavyoonekana hapo chini:



Chati hapo juu, inaonesha kwamba, kumekuwa na ongezeko katika sehemu zote za bajeti na makusanyo halisi ya mapato kuanzia 2007/08 hadi 2010/11 kwa ongezeko la kuanzia asilimia 0.4% hadi 3.4%. Hata hivyo, kumekuwepo kupungua kwa kiasi kikubwa kwenye makusanyo ya mapato ukilinganisha na bajeti iliyopitishwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kwa 20% sawa na Sh.60.7 bil. Hata hivyo, kiasi halisi cha makusanyo kimeongezeka kwa Sh. 52,372,061,484 (28%) katika mwaka 2011/2012 ikilinganishwa na mwaka 2010/2011.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuandaa bajeti yenye uhalisia vilevile kuwa na mikakati imara katika ukusanyaji wa mapato kwa lengo la kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato na hatimaye kuwezesha Halmashauri kujiendesha zenyewe kwa ufanisi zaidi.Pia, kuna vyanzo zaidi vya mapato ambavyo havijatambuliwa hivyo kupelekea kutokusanywa; inapendekezwa kuwa Serikali za Mitaa zifanye upembuzi yakinifu ili kuweza kubaini na kuvitumia vyanzo vipyta ili kuongeza mapato ili kupunguza kiwango cha utegemezi wa ruzuku.

4.2 Mwenendo wa Mapato kutoka Vyanzo vya Ndani vya Halmashauri ikilinganishwa na Ruzuku kutoka Serikali Kuu

Ruzuku ya matumizi ya kawaida ni ruzuku toka Serikali Kuu kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika kuendesha

shughuli za kila siku za Halmashauri, mishahara, manunuzi ya vifaa na huduma ambazo zinapewa fedha kwa ruzuku ya matumizi ya kawaida na misaada.

Wakati wa ukaguzi katika mwaka husika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikusanya jumla ya Sh.236,716,345,736 kutoka vyanzo vyao vya ndani na kutumia jumla ya Sh.2,277,035,217,362 katika matumizi ya kawaida. Hata hivyo, ulinganisho kati ya mapato na matumizi ya fedha ya Serikali za Mitaa umebaini kuwa Serikali za Mitaa, kwa kutumia mapato yake ya ndani zinaweza kugharimia matumizi ya shughuli za kawaida kwa 10.4% bila kutegemea fedha kutoka serikali kuu na wafadhili. Mchanganuo kwa kila Halmashauri ni kama yanavyoonekana katika **Kiambatisho (vii)**.


Zaidi ya hayo, Halmashauri zenye asilimia kubwa ya makusanyo ya mapato dhidi ya matumizi ya kawaida bila kutegemea kwa kiasi kikubwa katika Serikali Kuu na Wafadhili ni Halmashauri ya Mji wa Masasi ambayo imekusanya mapato kutoka vyanzo vyake jumla ya Sh.276,414,826 ikilinganishwa na ruzuku halisi ya matumizi ya kawaida iliyotumia ya Sh. 240,410,227 ambayo ni sawa na 115%, ikifuatiwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam yenye 78.4% na ya tatu ni Halmashauri ya Manispaa ya Temeke yenye 57.8%. Hata hivyo, Halmashauri yenye kiwango kikubwa cha utegemezi wa ruzuku toka Serikali kuu na wafadhili ni H/W Mwanga ambayo uwezo wake wa kujitegemea ni 1.5%.

Mwelekeo wa vyanzo vya mapato ya ndani vilivyokusanywa dhidi ya matumizi ya kawaida kwa miaka mitano ni kama inavyoonekana katika Jedwali hapo chini:

Jedwali Na. 8: Mwelekeo wa mapato ya ndani dhidi ya matumizi ya kawaida

Mwaka Wa Fedha	Mapato toka vyanzo vya ndani (Sh.)	Matumizi ya Kawaida (Sh.)	%
2007/08	93,545,987,812	1,140,847,566,087	8.2
2008/09	110,852,341,512	1,437,216,933,939	7.7
2009/10	137,416,106,722	1,823,788,009,947	7.5
2010/11	184,344,284,252	2,153,971,770,095	8.6
2011/12	236,716,345,736	2,277,035,217,362	10.4

Mwenendo kati ya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani vya Halmashauri dhidi ya matumizi ya kawaida, yameoneshwa pia kwa kutumia grafu mstari ifuatayo:



Chati mstari hapo juu inaonesha kwamba, kiwango cha utegemezi cha Halmashauri juu ya Ruzuku ya Serikali kimekuwa kikiongezeka kila mwaka. Wakati matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka Sh.1,141bil. mwaka 2007/08 hadi Sh.2,276bil. katika 2011/12; wakati makusanyo ya mapato ya ndani yameongezeka kutoka Sh.94bil. hadi Sh.237bil. kwa mtiririko huo. Hii inaashiria

ongezeko dogo sana katika mapato ya ndani katika kufadhili ongezeko matumizi ya kawaida.

Inapendekezwa kwamba, Serikali za Mitaa lazima zijidhatiti kuongeza ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vyta ndani kwa kuhakikisha vyanzo zaidi vinatambuliwa, udhibiti katika ukusanyaji wa mapato unaongezeka kwa kuzuia mianya ya upotevu na kutathmini upya mikakati ya ukusanyaji ili kutambua sehemu dhaifu na baadaye kuandaa mikakati bora wa utatuzi.

4.3 Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida Isiyotumika Sh.124,594,256,692


Kwa mwaka wa fedha 2011/12, Jumla ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa 129 zilitumia kiasi cha Sh.2,186,486,605,144 katika shughuli za kila siku ukilinganisha na Ruzuku kutoka Serikali Kuu ya Sh.2,311,080,861,836 hivyo kupelekea bakaa ya Sh.124,594,256,692 sawa na 5.4% ya Ruzuku kutoka Serikali Kuu ambacho hakikutumika. Mchanganuo umeoneshwa katika **kiambatisho (viii)**

Jedwali hapo chini linaonesha mwenendo wa ruzuku ya kawaida ambayo haikutumika kwa miaka mitano.

Jedwali Na. 9: Mwenendo wa ruzuku ya kawaida ambayo haikutumika kwa miaka mitano mfululizo

Mwaka wa Fedha	Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida (Sh.)	Matumizi ya Kawaida (Sh.)	Ruzuku isiyotumika (Sh.)	% ya Ruzuku isiyotumika
2007/08	1,014,488,715,963	929,417,430,857	85,071,285,107	8.4%
2008/09	1,023,504,263,229	976,332,807,352	47,171,455,877	4.6%
2009/10	1,521,937,206,309	1,373,576,272,098	148,360,934,211	9.7%
2010/11	2,105,926,241,086	1,978,117,478,839	146,774,839,643	7.0%
2011/12	2,311,080,861,836	2,186,486,605,144	124,594,256,692	5.4%

Mwenendo wa Ruzuku isiyotumika kwa miaka mitano mfululizo unaweza kuoneshwa kwa kutumia chati mstari ifuatayo:



Chati hapo juu inaonesha kwamba, Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida ambayo haijatumika imepungua kutoka mwaka 2007/08 hadi 2008/09 kwa 8.4% hadi 4.6% ya jumla ya ruzuku ya matumizi ya kawaida iliyopokelewa. Hata hivyo, ikaongezeka kwa kiasi kikubwa katika mwaka 2009/10 hadi 9.7% na ikapungua hadi 5.4% katika mwaka 2011/12.

Kuwepo kwa kiasi kikubwa cha Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida ambacho hakijatumika inamaanisha, Serikali kuu haikuwa na ufanisi katika kupeleka ruzuku kwa wakati au kulikuwa na ukiritimba wa utumiaji fedha katika Halmashauri. Hivyo, ufanisi wa uendeshaji wa shughuli za kila siku katika Halmashauri unaathirika na hivyo huzuia utekelezaji wa huduma zilizoainishwa kwa umma. Hii pia inaweza kuleta marekebisho ya bajeti Kufidia athari zilizosababishwa na mfumuko wa bei.

Kwa hiyo inapendekezwa kuwa, ruzuku ya kawaida ni vema ikatolewa kwa wakati. Hii itapunguza mrundikano na msongamano wa shughuli kwa miaka ijayo.

Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuhakikisha kuwa, taratibu za ruzuku ya matumizi ya kawaida zinazingatiwa, kwa kuwezesha matumizi ya kawaida ambayo yanachochea kuongeza utoajiwa huduma bora.

4.4 Matumizi ziada ya ruzuku ya matumizi ya kawaida iliyotolewa Sh. Sh.1,996,930,176

Wakati wa ukaguzi katika mwaka husika, Halmashauri nne (4) zilitumia kiasi cha Sh.89,763,386,494 zidi ya Ruzuku ya kawaida iliyopokelewa ya Sh.87,766,456,318 hivyo kufanya matumizi ya ziada kwa Sh.1,996,930,176 kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini:

Jedwali Na. 10 : Halmashauri zilizokuwa namatumizi ziada ya ruzuku ya matumizi ya kawaida iliyotolewa


Na.	Halmashauri Husika	Ruzuku ya matumizi ya kawaida (Sh.)	Matumizi ya kawaida (Sh.)	Matumizi ya ziada (Sh.)	% ya Matumizi ya ziada
1	H/W Sikonge	6,951,984,924	7,213,491,678	261,506,754	-3.8%
2	H/M Iringa	12,989,819,587	13,385,296,623	395,477,036	-3.0%
3	H/W Ludewa	13,251,180,213	13,683,027,774	431,847,561	-3.3%
4	H/M Ilala	54,573,471,594	55,481,570,419	908,098,825	-1.7%
jumla		87,766,456,318	89,763,386,494	1,996,930,176	

Mchanganuo wa matumizi yaliyozidi kwa miaka mitano mfululizo ni kama ifuatavyo hapa chini:

Jedwali Na. 11: mwenendo wa matumizi zaidi kwa miaka mitano mfululizo

Mwaka wa Fedha	Ruzuku ya matumizi ya kawaida (Sh.)	Matumizi ya kawaida (Sh.)	Matumizi ya ziada (Sh.)	Idadi ya H/w
2007/08	232,989,909,648	260,559,263,689	27,569,354,041	28
2008/09	463,622,503,151	489,438,406,774	25,815,903,623	46
2009/10	426,419,510,511	451,774,320,398	25,354,809,887	31
2010/11	88,436,141,286	92,477,645,440	4,041,504,154	6
2011/12	87,766,456,318	89,763,386,494	1,996,930,176	4

Mwenendo katika Jedwali hapo juu umeoneshwa kwa kutumia pia chati ifuatayo:



Jedwali na chati hapo juu vinaonesha kwamba, idadi ya Halmashauri zilizotumia zaidi katika matumizi ya kawaida zimeongezeka kutoka Halmashauri 28 hadi 46 mwaka 2007/08 kwenda mwaka 2008/09. Tangia hapo, idadi imekuwa ikipungua kutoka Halmashauri 46, hadi 4 katika mwaka wa ukaguzi (2011/12). Ikilinganishwa na kiasi cha fedha kilichotumika zaidi cha Sh.25,815,903,623 kwa mwaka 2008/09 hadi Sh.1,996,930,176 mwaka 2011/12.

Hivyo ninapendekeza, Mamlaka za Serikali za Mitaa ziimarishe udhibiti katika matumizi ya ruzuku kwa

kuhakikisha mamlaka zinazoidhinisha zinafahamu kiasi cha fedha kilichopo kabla ya kuidhinisha malipo husika. Hii itapunguza ongezeko la madeni makubwa yatokanayo na matumizi ya ziada ambayo yanaweza kuathiri shughuli katika miaka ya fedha ijao.

4.5 Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo Isiyotumika Sh.188,405,740,589

Ruzuku ya miradi ya maendeleo hutolewa kwa Halmashauri kwa ajili ya kujenga miundombinu au kufanya ukarabati wa miundo mbinu iliyopo kulingana na maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa lengo la kujenga uwezo katika jamii, kuboresha huduma na kupunguza umaskini. Ruzuku ya miradi ya maendeleo hutumika katika maeneo yanayohusu kupunguza umaskini kama vile Afya, Elimu, Maji, Barabara na Kilimo.

Katika mwaka wa fedha 2011/12, kiasi cha Sh.535,017,077,030 kilitolewa katika Halmashauri 132 ikiwa ni ruzuku ya fedha za maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.


Hata hivyo hadi kufikia Juni 30, 2012 kiasi cha Sh.346,716,653,619 kilitumika, na kubakia kiasi cha Sh.188,405,740,589 sawa na 35% ya fedha zote zilizotolewa. Mchanganuo wa Halmashauri zilizokuwa na fedha za maendeleo ambazo zimebaki bila kutumika ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (ix)**

Mwenendo wa fedha za ruzuku za miradi ya maendeleo za Serikali zisizotumika kwa miaka mitano mfululizo 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010, 2010/2011 na 2011/2012 ni kama ilivyooneshwa hapa chini:

Jedwali Na. 12: mwenendo wa fedha ambazo hazikutumika za miradi ya maendeleo

Mwaka wa Fedha	Ruzuku iliyotolewa (Sh.)	Kiasi kilichotumika (Sh.)	Kiasi kilichosalia (Sh.)	%	Idadi ya Halma-shauri
2007/08	270,547,629,434	171,791,488,611	99,114,082,540	37	111
2008/09	328,203,178,845	239,482,549,650	88,720,629,195	27	118
2009/10	507,866,599,666	332,092,443,562	175,774,156,104	35	133
2010/11	542,339,143,645	367,778,247,642	174,560,896,003	32	130
2011/12	535,017,077,030	346,716,653,619	188,405,740,589	35	132

Mwenendo wa maelezo katika jedwali hapo juu ni kama inavyooneshwa kwa kutumia Chati mstari ifuatayo:



Jedwali na Chati mstari hapo juu inaonesha kwamba, kutoka mwaka wa fedha 2007/08 hadi 2008/09 ruzuku ya miradi ya maendeleo isiyotumika ilipungua kwa 10% (37-27%), wakati kwa mwaka wa fedha 2008/09 hadi 2009/10 ruzuku ya miradi ya maendeleo isiyotumika iliongezeka kwa 8% (35-27%). Hata hivyo kwa mwaka wa fedha 2009/10 hadi 2010/11 kiasi cha fedha ambacho hakikutumika kilipungua kwa 3% (35-32%). Wakati huo huo idadi ya Halmashauri ambazo zilionekana kubaki na fedha zisizotumika ziliongezeka kutoka 111 hadi 132 ikilinganisha kama ilivyo elezewa kwenye taarifa za fedha katika mwaka 2007/08 hadi 2011/12.

H/W Kondoa inaongoza kwa kuwa na kiasi kikubwa cha fedha za maendeleo ambazo hazijatumika ambacho ni 79% ya fedha iliyokuwepo katika mwaka ikifuatiwa na H/W Misungwi (77%). Hata hivyo, Manispaa ya Dodoma na H/W Mbarali zilitumia fedha yote iliyokuwepo kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Kuwepo kwa fedha za ruzuku za miradi ya maendeleo zisizotumika ni uthibitisho kwamba, miradi ya maendeleo ambayo ilitengewa ruzuku hizi haikutekelezwa kikamilifu kama ilivyopangwa na hivyo huduma au faida zinazotokana na miradi hiyo kwa jamii husika hazijafikiwa. Hii pia inaweza ikasababisha mabadiliko ya bajeti ili kufidia athari/mapungufu yaliyojitokeza kutokana na mfumuko wa bei.

4.6 Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo Pungufu ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa Sh.249,496,355,027

Katika mwaka wa fedha 2011/12, ukaguzi wa bajeti ya miradi ya maendeleo katika Halmashauri 113 ulibaini kuwa, kiasi cha Sh.595,064,422,505 kiliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hata hivyo kiasi cha Sh.345,568,067,477 ndicho kilichopokelewa Halmashauri na kubakiza kiasi kisichopokelewa cha Sh.249,496,355,027. Hii inamaanisha kuwa, baadhi ya miradi ya maendeleo haikutekelezwa kabisa na mingine imeteklezwa kwa sehemu. Angalia **Kiambatisho (x)**

Kupitia michanganuo kwa miaka ya fedha mitano ya 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010, 2010/2011 na 2011/2012, mwenendo wa fedha za miradi ya maendeleo ambazo hazikutolewa ni kama ilivyooneshwa katika Jedwali hapa chini:

Jedwali Na.13: Mwelekeo wa fedha za ruzuku ya maendeleo ambazo hazikutolewa kwa miaka mitano mfululizo

Mwaka wa Fedha	Ruzuku iliyoidhinishwa (Sh.)	Ruzuku iliyopokelewa (Sh.)	Ruzuku isiyopokelewa (Sh.)	% Ruzuku isiyopok elewa	idadi ya Halma-shauri
2007/ 08	315,433,507,115	208,242,130,208	107,191,356,911	34%	95
2008/ 09	386,165,146,158	245,623,406,798	140,541,739,360	36%	105
2009/ 10	395,038,612,520	246,475,254,935	151,115,612,816	38%	86
2010/ 11	529,494,590,274	308,572,669,609	220,921,920,666	42%	105
2011/ 12	595,064,422,505	345,568,067,477	249,496,355,027	42%	113

Jedwali hapo juu linaweza pia kuonekana katika chati mstari kama ifuatavyo:



Chati hapo juu inaonesha kwamba, ingawa kwa miaka mitano mfululizo bajeti ya ruzuku ya miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa imeongezeka kutoka Sh.315bil. mwaka 2007/08 hadi Sh.595bil. mwaka 2011/12, Ruzuku Iliyopokelewa na Halmashauri iliongezeka kutoka Sh.208bil. mwaka 2007/08 hadi Sh.346bil. mwaka 2011/12. Katika mwaka husika, kulikuwa na wastani wa 42% ya fedha za ruzuku zilizoidhinishwa lakini hazikutolewa. Hii ina maana kwamba, kuna shughuli za maendeleo zilizoidhinishwa lakini hazikutekelezwa kabisa kutokana na kutolewa kwa fedha pungufu.

Hivyo, Halmashauri zinapaswa kuendelea kufuatilia ruzuku zao wizara ya fedha kwa ajili ya kuhakikisha fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo zinatolewa. pia kwa kuendelea kuzijumuisha shughuli hizo katika bajeti ya mwaka ujao.

4.7 Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida Pungufu ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa Sh.171,394,985,514


Katika mwaka wa fedha 2011/12, ukagazi wa bajeti ya matumizi ya kawaida katika Halmashauri 87 ulibaini kuwa, kiasi cha Sh.1,618,877,128,175 kiliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa matumizi ya kawaida. Hata hivyo kiasi cha Sh.1,447,482,142,661 ndicho kilichopokelewa Halmashauri na kubakiza kiasi kisichopokelewa cha Sh. 171,394,985,514. Hii inamaanisha kuwa, kuna shughuli za kawaida ambazo hazikutekelezwa au zilitekelezwa kwa kiasi zikiwa zinasubiria kupatiwa fedha zilizosalia kama ilivyopangwa. Angalia **Kiambatisho (xi)**

Kupitia michanganuo kwa miaka ya fedha mitano ya 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010, 2010/2011 na 2011/2012, mwenendo wa fedha za matumizi ya kawaida ambazo hazikutolewa ni kama ilivyooneshwa katika Jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 14: Mwelekeo wa fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida ambazo hazikutolewa kwa miaka mitano mfululizo

Mwaka wa Fedha	Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.)	Ruzuku iliyopokelewa (Sh.)	Ruzuku isiyopokelewa (Sh.)	% Ruzuku Isiyopokelewa	Idadi ya Halma-shauri
2007/08	573,056,547,037	490,828,169,222	82,232,377,904	14%	67
2008/09	848,2744,823,445	757,195,467,343	91,162,719,876	11%	73
2009/10	1,248,60,338,699	1,104,588,746,584	144,171,592,119	12%	87
2010/11	1,242,318,963,483	1,111,762,925,260	130,556,038,222	11%	78
2011/12	1,618,877,128,175	1,447,482,142,661	171,394,985,514	11%	87

Jedwali hapo juu ni kama inavyooneshwa kwa kutumia Chati mstari ifuatayo:



Chati hapo juu, inaonesha kwamba, Kwa miaka mitano mfululizo ruzuku ya matumizi ya kawaida iliyopitishwa iliongezeka kutoka Sh.573bil. mwaka 2007/08 hadi Sh.1,619bil. mwaka 2011/12, wakati ruzuku iliyopokelewa kwa matumizi ya kawaida iliongezeka kutoka Sh.491bil. mwaka 2007/08 hadi Sh.1,448bil. mwaka 2011/12. hivyo kupelekea ongezeko la Sh.88bil sawa na 8.5% ya ruzuku iliyopitishwa.

Hii ina maana kwamba, kuna shughuli hazikutekelezwa kutokana kutopata ruzuku hivyo kusababisha matumizi mabaya ya ruzuku ya maendeleo kwa kufadhili shughuli za kawaida.

Hivyo, Halmashauri zinapaswa kuendelea kufuatilia Wizara ya Fedha ili kufanikisha upatikanaji wa ruzuku kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kila siku, na kama sivyo pafanyike marekebisho ya bajeti ili kuonesha hali

halisi. Kwa shughuli ambazo hazikupokea fedha waweze kuzijumuisha shughuli hizo katika bajeti ya mwaka ujao

4.8 Makusanyo Pungufu katika Vyanzo Vikuu vya Mapato ya Ndani

Wakati wa ukaguzi katika mwaka husika, vyanzo vikuu viwili yaani kodi ya Majengo kwa Halmashauri za Manispaa na Majiji, na kwa upande mwingine ushuru wa mazao katika Halmashauri za Wilaya viliaangaliwa na kuchanganuliwa. Yafuatayo ni maelezo ya kina.

4.8.1 Makusanyo Pungufu ya kodi ya Majengo

Sh.4,345,570,497

Mamlaka ya Mapato Tanzania imekuwa ikikusanya kodi ya majengo kwa niaba ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Mkoa wa Dar es salaam tokea mwaka 2008 wakati kwa mikoa mingine halmashauri husika hujikusanya yenye. Kwa mwaka wa fedha 2011/12, jumla ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa 17 zilipanga kukusanya mapato ya kiasi cha Sh.11,405,440,517 kutokana na kodi ya majengo. Hata hivyo Halmashauri ziliweza kukusanya mapato ya Sh.7,059,870,020. Hii inamaanisha kwamba Halmashauri zilikusanya pungufu ya bajeti kwa Sh.7,059,870,020 sawa na 38% ya bajeti.

Orodha ya Halmashauri na mapato husika yaliyokusanya kutoka kodi ya majengo ni kama inavyoonekana hapa chini:

Jedwali Na. 15: Orodha ya Halmashauri ikionesha makusanyo pungufu ya Kodi ya Majengo

Na.	Halmashauri	Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.)	Mapato Halisi (Sh.)	Mapato Pungufu (Sh.)	% ya Mapato Pungufu
1	H/W Kibaha	11,436,000	595,000	(10,841,000)	95%
2	H/M Ilala	4,000,000,000	2,991,316,985	(1,008,683,015)	25%
3	H/M Kinondoni	2,200,000,000	2,177,820,324	(22,179,676)	1%
4	H/M Temeke	2,567,218,000	703,149,798	(1,864,068,202)	73%
5	H/W Kilolo	11,287,440	9,486,681	(1,800,759)	16%
6	H/W Kasulu	29,700,000	12,120,000	(17,580,000)	59%
7	H/M Morogoro	460,000,000	235,277,192	(224,722,808)	49%
8	H/M Mtwara	110,000,000	41,726,000	(68,274,000)	62%
9	H/W Geita	8,000,000	3,132,150	(4,867,850)	61%
10	H/W Magu	2,340,980	0	(2,340,980)	100%
11	H/J Mwanza	1,423,368,300	709,168,748	(714,199,552)	50%
12	H/W Mbanga	4,000,000	2,596,970	(1,403,030)	35%
13	H/W Bariadi	7,164,797	6,833,700	(331,097)	5%
14	H/M Shinyanga	51,885,000	39,636,007	(12,248,993)	24%
15	H/W Iramba	3,000,000	1,343,777	(1,656,223)	55%
16	H/Jiji Tanga	517,480,000	165,417,962	(352,062,038)	68%
17	H/W Nzega	108,450,000	1,933,000	(106,517,000)	98%
Jumla		11,405,440,517	7,059,870,020	(4,345,570,497)	38%

Jedwali hapo juu linadhihirisha kwamba, Halmashauri tajwa hazikukusanya kodi ya majengo kama zilivyo bajetiwa kwa wastani wa 38%. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuandaa bajeti yenye uhalisia na ukweli na vile vile kuwa na mikakati imara katika ukusanyaji wa kodi za majengo kwa lengo la kuongeza wigo la mapato na hatimaye kuwezesha Halmashauri husika kujiendesha zenyewe kwa ufanisi zaidi.

4.8.2 Makusanyo Pungufu ya Ushuru wa Mazao Sh.1,797,972,949

Ushuru wa Mazao ni moja ya chanzo kikuu cha mapato ya ndani kwa halmashauri za wilaya na hutozwa kwa mazao mbalimbali yanayo patikana ndani ya halmashauri husika. Hii inahusisha mazao yote ya biashara na chakula. Hii inajumuisha mazao kama mahindi, pamba, nazi, na mawese.

Wakati wa ukaguzi katika mwaka husika, Halmashauri za wilaya 77 zilibajeti kiasi cha Sh.45,312,189,317 kama ushuru kutoka kwenye mazao mbalimbali. Hata hivyo hadi kufikia mwisho wa mwaka, Halmashauri hizo zilikusanya kiasi cha Sh.43,222,428,289 na kupelekea upungufu wa Sh.1,797,972,949 sawa na 4% ya kiasi kilicho bajetiwa.

Orodha za Halmashauri na mapato yao husika yaliyokusanywa kutoka ushuru wa mazao ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xii)**.

SURA YA TANO

5.0 MASUALA MUHIMU YALIYOJIRI KATIKA UKAGUZI WA HESABU NA TATHMINI YA UDHIBITI WA NDANI

5.1 Tathmini ya Mfumo wa Udhibiti wa Ndani na Masuala ya Utawala Bora

Udhibiti wa ndani ni mfumo ulioundwa katika kuhakikisha kuwa malengo yanafikiwa kwa ufanisi na ustadi katika utendaji, taarifa za fedha ni za kuaminika, sheria na kanuni husika zinafuatwa. Kwa madhumuni ya ripoti hii, Udhibiti wa ndani ni jinsi Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinavyojihakikishia zenyewe kwamba taarifa zao za fedha ni za kuaminika, ufanisi na ustadi katika utendaji vinazingatiwa na pia wanafuata sheria na kanuni husika.

Sehemu hii ya ripoti inaonesha matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na baadhi ya vipengele vya udhibiti wa ndani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na; mifumo ya kihasibu, udhibiti wa mazingira ya utendaji kazi, tathmini za vihatarishi, udhibiti wa utendaji, teknolojia ya habari na mawasiliano, ufuatiliaji wa udhibiti, na kuzuia na kudhibiti udanganyifu.

5.1.1 Mapungufu katika Mifumo ya Kihasibu

Shughuli zote za kihasibu za Serikali zinapaswa kufanyika katika Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS). Mfumo huu una baadhi ya vipengele vinavyoshughulika na; maandalizi ya bajeti, fedha kutoka Serikali Kuu na hati za kuidhinisha uhamisho wa fedha, usimamizi wa mali, kudhibiti manunuvi, miadi na matumizi, malipo ya wadai/usuluhihiwa wa taarifa za kibenki, usimamizi wa fedha za maendeleo, vitabu vya majumuisho na taarifa za fedha.

Katika mwaka wa ukaguzi ilibainika kwamba, Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) hautumiki

ipasavyo kwenye utengenezaji wa taarifa katika Halmashauri zote 134 ingawa udhaifu ulibainika katika Halmashauri 38 kama zilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho (xiii)**. Mapungufu hayo ni kama yafuatavyo:

- Vipengele vitatu ambavyo ni usimamizi wa mali, manunuzi na mishahara havikuwekwa kwa matakwa ya watumiaji wa mifumo ili viweze kutumika ipasavyo.
- Taarifa za mizania ya hesabu, taarifa za mapato na matumizi, urari na taarifa ya mtiririko wa fedha hazizalishwi kupitia mfumo.
- Mfumo hautumiki katika kuchapisha hundi.

Mapungufu yalioainishwa hapojuu yanaashiria kwamba, watumiaji wa Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS/Epicor) katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa hawana uwezo mkubwa kuhusu matumizi sahihi ya Mfumo katika kuandaa baadhi ya taarifa za fedha.

Inapendekezwa kwamba, OWM - TAMISEMI inapaswa kuhakikisha kuwa vipengele vyote vya Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha vinaboreshw na mfumo unatumika kikamilifu.

Aidha, uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na OWM -TAMISEMI wanatakiwa kuhakikisha kuwa, watumiaji wanapata mafunzo sahihi ya mfumo wa IFMS/Epicor ili kuongeza ufanisi katika matumizi ya mfumo.

5.1.2 Taarifa ya Uhasibu kuandaliwa nje ya Mfumo Funganifu

Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa, jumla ya Halmashauri 24 zilizooneshwa kwenye **Kiambatisho (xiii)** hazitumii Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha katika kuandaa taarifa za fedha

Vihatarishi vinavyohusishwa na kutotumia Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha ni pamoja na kuwa na

taarifa za fedha zilizokabiliwa na makosa na zinaweza kufanyiwa mabadiliko na mtu yeote hivyo kupunguza uaminifu wa taarifa za fedha zinazoandaliwa nje ya mfumo. Kutotumia mfumo pia kunaathiri umakini, upatikanaji wa taarifa kwa wakati na inasababisha utata wa utoaji taarifa za fedha katika ngazi zote.

Kutokana masuala yaliyojitekeza hapo juu, ninashauri kwamba kuna haja kwa Halmashauri zote kuhakikisha kuwa watumishi walioko katika idara ya fedha wanapatiwa mafunzo ya kutosha ili kuwawezesha kutumia kikamilifu mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha kwa kutumia Epicor toleo jipya la 9.05.

Kwa kuongezea OWM-TAMISEMI na Wizara ya Fedha zinatakiwa kuhakikisha kuwa utumiaji wa mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha kwa kutumia Epicor toleo jipya la 9.05 unapewa kipaumbele katika Halmashauri zote ili kuandaa na kutoa taarifa za fedha na taarifa nyingine zinazohusiana na hizo kwa wakati. Utumiaji wa mfumo huu unatakiwa uwe ni wa lazima kwa kila Halmashauri, vilevile OWM-TAMISEMI na Wizara ya Fedha zinatakiwa zisimamie utekelezaji wa matumizi ya mfumo huo. Pale inapohitajika, Katibu Mkuu Kiongozi aingilie kati katika kuhakikisha kwamba, mfumo huo unatumika kwa Halmashauri zote za Tanzania bara.

5.1.3 Mapungufu katika Utendaji wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ni kitengo kinachojitegemea katika kutoa ushauri ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa Taasisi. Kinawezesha Taasisi kufikia malengo kwa kuleta utaratibu uliopangwa katika kutathmini na kuongeza ufanisi wa usimamizi na udhibiti wa viharishi na katika masuala ya utawala bora.

Kif. 45 (1) cha Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1982 (iliyorekebishwa 2000) na Agizo Na. 13 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2009 inamtaka Afisa Masuuli katika kila Halmashauri kuanzisha na kuendeleza kitengo imara cha ukaguzi wa ndani kama sehemu ya mfumo wa udhibiti wa ndani. Kitengo imara cha ukaguzi wa ndani kinatakiwa kutoa tathmini juu ya usalama na matumizi ya kihasibu, fedha na udhibiti wa utendaji ndani ya Halmashauri kwa kufanya mapitio kwa utaratibu, kutoa taarifa katika ufanisi wa kiutendaji, fedha, mifumo ya uendeshaji na udhibiti wa bajeti.

Kinyume na mahitaji ya kisheria hapo juu, kutokana na tathmini za utendaji wa kitengo cha ukaguzi wa ndani, mapungufu yafuatayo yamebainika katika Halmashauri 106 kama inavyooneshwa katika **kiambatisho (xiii)**.

- Vitengo bado vina upungufu wa watumishi, baadhi wana mtumishi mmoja au wawili na baadhi hawajawezeshwa kifedha. Kwa kuzingatia shughuli mbalimbali za Halmashauri, mkaguzi mmoja au wawili hawatoshi katika mawanda ya ukaguzi yaliyojitosheleza.
- Wakati wa ukaguzi, mawanda na ukaguzi uliojitosheleza katika kitengo cha ukaguzi wa ndani yalizuiwa kwasababu ya upungufu wa rasilimaliwatu na fedha. Hivyo udhibiti wa fedha na utendaji haukuweza kufanyiwa tathmini kama ilivyotakiwa, hivyo sikuweza kutegemea kazi za kitengo cha ukaguzi wa ndani ili kupunguza kiwango cha vipimo vyta ukaguzi.
- Nafasi ya ukaguzi wa ndani katika mfumo wa utawala bora pamoja na majukumu na wajibu wake hayakubainishwa wazi katika mkataba kwa wateja wa ukaguzi wa ndani.

- Kuna ukosefu wa nyaraka zinazoonesa taarifa ya maeneo yaliyokaguliwa ambayo yangewezesha mchakato wa mapitio na kutengeneza msingi wa matokeo ya ukaguzi na mapendekezo yaliyomo katika taarifa ya ukaguzi wa ndani.

Naendelea kusisitiza kwamba, Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI na Kitengo cha Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali chini ya Wizara ya Fedha zinashauriwa kuwa, kuna umuhimu wa kuimarisha kazi za ukaguzi wa ndani kwa kuongeza rasilimali fedha na rasilimali watu. Aidha wakaguzi wa ndani wanapaswa kupatiwa elimu na ujuzi ili waweze kuongeza wigo wa ukaguzi na kuboresha utendaji wao.

5.1.4 Mapungufu katika Kamati za Ukaguzi

Kamati za Ukaguzi ni sehemu muhimu katika mfumo wa utawala iliyoundwa kuimarisha mfumo wa udhibiti wa Halmashauri. Kamati imara ya ukaguzi ina uwezo wa kuimarisha udhibiti wa mazingira ya utendaji na hivyo kusaidia Maafisa Masuuli kutimiza wajibu wao katika uongozi na majukumu ya udhibiti na pia kuwezesha ufanisi wa kazi za ukaguzi wa ndani na kuimarisha utoaji taarifa za fedha.

Kwa kuongezea, kamati ya ukaguzi wa hesabu inapaswa kutoa usimamizi unaojitegemea wa kazi na matokeo ya ukaguzi wa ndani na wa nje, kutathmini juu ya rasilimali zinazohitajika katika ukaguzi na kusuluhisha mahusiano kati ya wakaguzi na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Kamati za ukaguzi zinatakiwa zihakikishe kuwa, matokeo ya ukaguzi yanawekwa wazi, na ushauri wa maboresho yoyote au hatua za marekebisho zinatekelezwa.

Kwa mujibu wa Agizo Na. 12 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009, kila

Mamlaka ya Serikali za Mitaa inatakiwa iunde Kamati imara ya Ukaguzi.

Wakati wa kupitia mchakato wa utendaji wa Kamati za Ukaguzi ilibainika kuwa, jumla ya Halmashauri 106 kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xiii)** hazikuwa wa ufanisi kutokana na mapungufu yafuatayo:

- Udmaifu wa kiutendaji katika Kamati za Ukaguzi umepelekea kushindwa kusimamia majukumu ya wakaguzi wa ndani.
- Kamati za Ukaguzi hazikuweza kupitia taarifa za fedha na ripoti za Halmashauri.
- Katika baadhi ya matukio hakukuwa na ushahidi kuwa, ripoti za kamati za kila mwaka zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa Maafisa Masuuli kwa ajili ya kuchukua hatua sahihi juu ya mapendekezo ya Kamati.
- Kamati za Ukaguzi zilizo nyingi hazikutani wala haziwaaliki wakaguzi wa nje katika vikao vyake ili kujadili kwa pamoja mambo yaliyokosa ufumbuzi kama ilivyoelekezwa na Agizo Na. 12(7) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009.

Utendaji usio wa ufanisi wa Kamati ya Ukaguzi unaweza kusababisha udhaifu katika udhibiti wa mazingira ya utendaji kazi na utawala bora katika Halmashauri kwa ujumla. Ni muhimu kwa OWM-TAMISEMI kuongeza majukumu zaidi katika hadidu za rejea za Kamati za Ukaguzi kama vile mapitio ya taarifa za fedha na ripoti, usimamizi na udhibiti wa vihatarishi na udanganyifu ili kuifanya Kamati kuwa ni chombo imara katika ufuatiliaji wa udhibiti wa ndani.

5.1.5 Tathmini ya Usimamizi wa Vihatarishi

Usimamizi wa vihatarishi ni sehemu ya mfumo wa udhibiti katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kusimamia

vihatarishi kwa kuwa vinahusiana na ufahamu wa malengo ya Halmashauri, kutambua, kuchambua na kutathmini vihatarishi vinavyohusiana na kufikia malengo na mara kwa mara kuendeleza na kutekeleza mipango/taratibu za kuwasilisha vihatarishi vilivyotambuliwa.

Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinahitajika mara kwa mara kufuutilia na kuboresha mifumo ya usimamizi wa vihatarishi ili kujihakikishia kuwa, ni chombo imara kwa Halmashauri katika mchakato na utaratibu wa kutoa huduma kwa jamii.

Ukaguzi uliofanyika katika sampuli ya jumla ya Halmashauri 93 kama zinavyoonekana katika **kiambatisho (xiii)** unadhihirisha kuwa, Halmashauri husika hazina mfumo wa usimamizi wa vihatarishi na hawajafanya tathmini ya hivi karibuni ya vihatarishi hivyo ili kutambua vihatarishi vilivyomo na vile vilivyoibuka baada ya mabadiliko ya mazingira na jinsi ya kutoa huduma. Pia, ilibainika kuwa sera na taratibu za usimamizi wa vihatarishi havikuanzishwa.

Kukosekana kwa sera na mipango imara ya usimamizi wa vihatarishi, Halmashauri husika hazitakuwa katika nafasi ya kukabiliana kwa wakati na vihatarishi ambavyo vinaweza kuleta madhara makubwa katika utendaji wa sasa na wa baadae wa Halmashauri.

Uongozi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa unatakiwa kuanzisha utaratibu unaojitosheleza kutambua, kuchambua, na kutathmini madhara ya vihatarishi, pamoja na udhibiti wa utendaji katika ufuatiliaji na kukabiliana na vihatarishi husika kwa sababu ni chombo imara kwa halmashauri katika mchakato na taratibu za utoaji huduma kwa jamii.

5.1.6 Mazingira ya Udhibiti wa Teknolojia ya Habari

Wakati wa kufanya tathmini katika mazingira ya udhibiti wa teknolojia ya habari, mapungufu yafuatayo yilibainika katika jumla ya Halmashauri 95 kama zinavyooneshwa katika **kiambatisho (xiii)**:

- Mamlaka za Serikali za Mitaa hazina sera ya teknolojia ya habari, kitu ambacho kinaweza kuashiria udhaifu katika usimamizi na utumiaji wa vifaa vya teknolojia ya habari ikiwa ni pamoja na vifaa na programu za kompyuta.
- Haikuwezekana kutathmini na kuthaminisha mpango wa teknolojia ya habari ambao Halmashauri husika inao na mpango wa utekelezaji, na pia mpango mkakati wa teknolojia ya habari haukuweza kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.
- Kutokuwepo kwa vizuizi vya ruhusa katika seva ya hifadhidata. Seva za hifadhidata iko katika vyumba ambavyo shughuli zingine za kawaida zinafanyika kinyume na taratibu zinazohitaji seva za hifadhidata iwekwe katika chumba kilichotengwa, chenye ulinzi safi na kisichokuwa na vumbi.
- Kutokuwepo kwa sera na taratibu za teknolojia ya habari katika kuhakikisha usalama wa kumbukumbu ikiwa ni pamoja na taarifa inayosambazwa kwa kutumia mawasiliano ya simu, taarifa zilizopo katika mfumo na usafirishaji wa taarifa zilizohifadhiwa kwenda katika maeneo ya mbali
- Kuhifadhi taarifa katika vyombo kama kanda sio salama kwa sababu kanda hizo zinawekwa katika makabati yenye vumbi. Baadhi ya taarifa zilizohifadhiwa katika kanda zilionekana kuharibika

baada ya siku chache. Hii inaweza kusababisha upotevu wa taarifa husika.

- Kwa baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, taarifa hazihifadhiwi katika Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS/Epicor), hivyo inaweza kusababisha kutowezekana kurejesha mfumo katika hali ya kawaida wakati wa majanga. Pia, kutokuwepo kwa vifaa vyta kuhifadhi taarifa maeneo ya mbali na Halmashauri hali ambayo inaweza kusababisha upotevu wa taarifa wakati wa kuharibika kwa mfumo, kuharibika kwa hifadhidata au majanga mengine kama moto katika chumba kilichowekwa hifadhidata au majengo ya Halmashauri husika. Kutokana na hali hii, upotevu au kuharibika kwa taarifa kunaweza kupelekea kutopatikana kwa taarifa hizo pindi zinapohitajika.
- Kutokuwepo kwa mpango wa kujikinga na majanga na vipimo vyta kujikinga na majanga havijawahi kufanyika. Kukosekana kwa mpango wa kujikinga na majanga kunasababisha ugumu katika kurejesha mfumo kwa wakati na kukosekana kwa vyanzo vyta vipimo vyta taarifa kwa ajili ya kurejesha taarifa husika na hakuna atakayehusika na urejeshwaji wa taarifa. Hii inasababisha hatari katika mpango endelevu wa Halmashauri husika.

Kutokana na haya ninashauri yafutayo yafanyike;

- OWM-TAMISEMI inatakiwa izisaidie Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuanzisha sera na taratibu za teknolojia ya habari ili kila mtumiaji aweze kuelewa majukumu na wajibu wake katika kutunza vifaa na programu za teknolojia ya habari.
- Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa zihakikishe kuwa, kumbukumbu za akiba zinachukuliwa mara kwa mara na kuhifadhiwa katika jengo lililo mbali na

hifadhidata. Sehemu ya kuhifadhia ni lazima iwe na usalama na ya kufikika kwa urahisi. Vilevile kuwe na majaribio ya kuangalia kumbukumbu za akiba kwa kutumia hifadhidata na mabadiliko mapya katika Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS).

- Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa ziwe na mpango wa kujikinga na majanga, hii ina maana ya kuandaa, kuandika, kujaribu na kutekeleza mpango wa kujikinga na majanga ambao unalenga mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) pamoja na mifumo mingine muhimu katika kila Halmashauri.

5.1.7 Kuzuia na Kudhibiti Udanganyifu

Viwango vya Kimataifa vya Ulaguzi (ISA) 240 vinafafanua udanganyifu kama "kitendo cha makusudi kinachofanywa na mtu mmoja au zaidi ndani ya menejimenti, wale wanaohusika na utawala bora, wafanyakazi, au watu wa nje, wakishiriki kwa njia ya udanganyifu ili kupata faida kwa njia isiyo ya haki au haramu." Jukumu la msingi la kuzuia na kutambua udanganyifu ni la wale wanaohusika na utawala bora, watumishi wa Halmashauri na uongozi.

Ni muhimu kuzuia na kudhibiti Udanganyifu katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ni moja kati ya masuala mengi ambayo yanahitaji kusimamiwa kwa ufanisi na kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinafuata kanuni za utawala bora.

Lengo la kutathmini udanganyifu ni kulihakikishia Bunge kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zina mfumo sahihi katika kusaidia, kuzuia na kupambana na udanganyifu na kutambua maeneo ya kufanyia maboresho.

Tathmini zilizofanyika katika jumla ya Halmashauri 71 zinaonesha kuwa, uongozi wa Halmashauri husika haukuwa na kumbukumbu za kimaandishi zilizoidhinishwa za mipango ya kuzuia udanganyifu. Hakukuwa na mchakato uliowekwa na menejimenti za Halmashauri

katika kubaini na kushughulikia vihatarishi vya ubadhirifu ndani ya Halmashauri kama inavyooneshwa katika **kiambatisho (xiii)**

Pia, hapakuwa na mchakato uliowekwa bayana kutoka katika uongozi wa Halmashauri husika wa kutambua na kukabiliana na vihatarishi vinavyohusiana na udanganyifu katika Halmashauri husika. Aidha, viashiria hatari ambavyo ni dalili za udanganyifu ni kama vifuatavyo:

- Mapungufu katika vitengo vya ukaguzi wa ndani,
- Hati za malipo kuwa na nyaraka pungufu,
- Kukosekana kwa hati za malipo,
- Kukosekana kwa stakabadhi za kukusanya mapato.
- Kuwepo kwa matukio ambayo mapato hayakuwasilisha benki kwenye akaunti za Halmashauri.
- Taarifa za hesabu kuwa na makosa.
- Kutokuwepo kwa kamati ya ukaguzi na mapokezi wa mali zilizonunuliwa.
- Mapungufu katika usimamizi wa mali, utunzaji wa kumbukumbu na kufanya tathmini ya mali za kudumu.
- Mishahara ambayo haikulipwa kwa watumishi kutopelekwa Hazina.
- Ukosefu wa udhibiti ili kuhakikisha kuwa mapato yote ambayo hayajakusanywa yanakusanywa na yanaingizwa kwa usahihi katika mfumo wa fedha unaotumika.
- Malipo ya mishahara kwa watumishi hewa
- Mapungufu katika kamati ya ukaguzi

Asili ya viashiria vya udanganyifu vilivyoainishwa hapo juu, vinaathiri udhibiti wa ndani na hivyo kuna hatari kubwa ya kuficha udanganyifu unaofanywa na menejimenti au watumishi katika ngazi tofauti. Udhhibiti wa udanganyifu usio na ufanisi unaweza kupelekea menejimenti za Halmashauri kushindwa kugundua na kuzuia udanganyifu.

Kwa kuwa wajibu wa kugundua na kuzuia udanganyifu ni wa menejimenti za Halmashauri husika, mianya iliyoinishwa inaweza kuwa ni chanzo cha udanganyifu na ni lazima izuiwe pamoja na kuandaa sera za kuzuia udanganyifu. Aidha, uongozi unatakiwa kuweka kumbukumbu na kuidhinisha mipango ya kuzuia udanganyifu na kufanya tathimini za mara kwa mara za vihatarishi.

Udhibiti wa udanganyifu ni lazima uunganishwe na majukumu na mipango ya Halmashauri na ionekane kwamba ni jukumu la kila mtu katika Halmashauri. Mpango wa kudhibiti udanganyifu unapaswa kubainisha jukumu la pamoja la kubaini vihatarishi na kufanya kila liwezekanalo kuzuia na kugundua, kuepuka makosa yasitendeke na mafunzo ya ufahamu yatolewe kwa watumishi.

5.2 Usimamizi wa Maduhuli

Usimamizi wa maduhuli ni mchakato ambao Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapanga, kuandaa bajeti, kutabiri, kutekeleza, kusimamia na kudhibiti makusanyo ya maduhuli na kutoa taarifa, pia kuhakikisha upatikanaji wa huduma za jamii na kuinua kiwango cha mapato. Lengo kuu la usimamizi wa maduhuli ni kutoa huduma inayotakiwa katika jamii sahihi kwa muda unaotakiwa na kwa kiasi kinachotakiwa.

Wakati wa ukaguzi, baadhi ya mapungufu yalibainika katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa yanayohusiana na usimamizi wa maduhuli kama ifuatavyo:

5.2.1 Vitabu 2990 vya Makusanyo ya Mapato Kutowasilishwa

Agizo 34(6) na 34(7) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009 imebainishwa kuwa, maafisa wote waliopewa vitabu vya makusanyo lazima wawasilishe taarifa ya vitabu vilivytumika na vile ambavyo havijatumika kila mwisho wa mwezi na endapo kuna upotevu wowote wa vitabu, utolewe taarifa kwa

Afisa Masuuli anayehusika mapema iwezekanavyo ambaye atotoa taarifa polisi. Kama upotevu umetokea nje ya makao makuu, afisa mhusika atoe taarifa polisi mapema iwezekanavyo na baadae Afisa Masuuli ajulishwe. Kwa nyongeza Agizo 34 (9) linabainisha kuwa, Afisa Masuuli anatakiwa kutoa taarifa kwenye Kamati ya Fedha kuhusu upotevu wa nyaraka na nakala ya taarifa hiyo iwasilishwe kwa Mkuu wa Mkoa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.


Kinyume na maagizo haya, vitabu 2990 vya makusanyo kutoka katika jumla ya Halmashauri 36 havikuwasilishwa kwa ukaguzi kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xiv)**

Mwelekeo wa vitabu vya makusanyo visivyowasilishwa kwa miaka ya fedhaya 2007/08, 2008/09 2009/10, 2010/11 na 2011/12 unaweza kuainishwa kama ifuatavyo;

Jedwali Na. 16: Mwelekeo unaoonesha vitabu ambavyo havikuwasilishwa kwa ukaguzi

Mwaka	Idadi ya vitabu vilivyo kosekana	Idadi ya Halmashauri
2007/08	860	43
2008/09	1341	50
2009/10	948	48
2010/11	682	36
2011/12	2990	36

Taarifa zilizoainishwa hapo juu zinaweza kuoneshwa kwenye chati mstari ifuatayo:



Tafsiri ya chati mstari hapo juu ni kwamba, hakuna mahusiano kati ya idadi ya vitabu vya mapato vilivyokosekana na idadi ya Halmashauri zilizohusika. Kwa wastani wa Halmashauri 43 katika miaka mitano (5) mfululizo, idadi ya vitabu vilivyokosekana iliongezeka kwa vitabu 481 kutoka mwaka 2007/08 hadi 2008/09. Kutoka mwaka 2008/09 hadi 2009/10 hadi 2010/11 idadi ya vitabu visivyowasilishwa imepungua kwa vitabu 393 na 266 katika mfululizo huohuo na kwa mwaka 2010/11 hadi 2011/12 viliongezeka kwa 2308.

Kwa kuwa vitabu hivi vilikusudiwa kukusanya mapato ya Halmashauri, kiasi kilichokusanywa kwa kutumia vitabu hivyo hakikiweza kujulikana. Hali hii inadhihirisha kuwa, kuna uwezekano mkubwa wa wizi wa mapato ya Halmashauri na kupotosha makisio ya mapato ya Halmashauri.

Hivyo inashauriwa kuwa, menejimenti za Halmashauri zinatakiwa kuweka mifumo imara ya udhibiti katika usimamizi wa vitabu vya makusanyo ili kuondoa uwezekano wa upotevu wa fedha za Halmashauri. Vilevile Halmashauri husika zinatakiwa kuwasilisha vitabu vilivyokosekana kwa ajili ya ukaguzi.

Hatua za haraka zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote walioshindwa kuwasilisha makusanyo ya Halmashauri.

5.2.2 Maduhuli yasiyowasilishwa na

Mawakala Sh.4,466,028,478

Agizo 37(2) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009 limeainisha kuwa, makusanyo yote ya Halmashauri yawasilishwe kwa watanza fedha wa Halmashauri husika kwa usalama.


Kinyume na Agizo hilo, ukaguzi uliofanywa katika jumla ya Halmashauri 56 kama zinavyooneshwa katika **kiambatisho (xv)** ulibaini kuwa, kiasi cha Sh.4,466,028,478 kilichokusanywa na Mawakala mbalimbali hakikuwasilishwa kwa watanza fedha wa Halmashauri husika.

Mchanganuo wa maduhuli yasiyowasilishwa kwenye Halmashauri husika kwa miaka mitano ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 17: Muhtasari wa Maduhuli ambayo hayajawasilishwa na mawakala

Mwaka	Maduhuli yasiyowasilishwa (Sh.)	Idadi ya Halmashauri Husika
2007/08	421,213,641	22
2008/09	1,095,113,399	43
2009/10	2,756,763,702	43
2010/11	4,360,299,618	48
2011/12	4,466,028,478	56

Mchanganuo kwenye jedwali hapo juu unaweza kuwasilishwa katika chati mstari kama ifuatavyo:



Kutokana na jedwali pamoja chati hapo juu imedhihirika kuwa, kiasi cha makusanyo yasiyowasilishwa kimeongezeka kwa miaka mitano mfululizo kwa kiasi cha Sh.4,044,814,837 kutoka Sh.421,213,641 mwaka 2007/08 hadi Sh.4,466,028,478 katika mwaka 2011/12 ambayo pia inaendana na ongezeko la halmashauri kutoka 22 hadi 56. Hii inaonesha udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani na mapungufu katika usimamizi wa mikataba ya makusanyo.

Inashauriwa kuwa, Menejimenti za Halmashauri zinatakiwa kuimarisha udhibiti wa ndani katika makusanyo ya maduhuli yatokanayo na vyanzo vya ndani. Hii inajumuisha kuboresha taratibu za kuingia mikataba na kufuatilia marejesho kutoka kwa mawakala wa makusanyo.

5.2.3 Fedha zisizokusanywa kutoka katika vyanzo vya ndani Sh.8,008,669,844

Agizo 38(1) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009 linaleleza kuwa, itakuwa jukumu la Mweka Hazina wa Halmashauri kuweka mipango thabiti ya kifedha na kihasibu ili kuhakikisha usahihi katika utunzaji


kumbukumbu za maduhuli yote yatokanayo na makusanyo sahihi, utunzaji na upelekaji fedha benki unaofanyika. Kinyume na agizo hili, ukaguzi umebaini kuwa, kiasi cha fedha cha Sh.8,008,669,844 kutoka vyanzo nya ndani nya Halmashauri hakikukusanya kutoka kwa walipa kodi husika kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho (xvi)**

Jedwali Na.18: Mwelekeo wa fedha zisizo kusanywa kwa miaka miwili

Mwaka	Fedha zisizokusanywa na Halmashauri	Idadi ya Halmashauri
2010/11	8,332,986,175	22
2011/12	8,008,669,844	30

Jedwali hapo juu linaonesha mwenendo wa mapato yasiyokusanywa na Halmashauri kwa kipindi cha miaka miwili. Kiasi cha maduhuli yasiyokusanywa kilipungua kwa Sh.272,866,780 sawa na 3.3% kutoka mwaka wa fedha 2010/11 hadi 2011/12.

Mchanganuo huu unaweza kuwasilishwa pia na chati ifuatayo hapa chini



Kutoka na jedwali pamoja na chati hapo juu, inaashiria kwamba, kuna udhaifu wa usimamizi wa Halmashauri katika kukusanya mapato katika vyanzo vingine na inaonesha jinsi Halmashauri zilivyoshindwa kuboresha vyanzo vya mapato vilivyopo.

Kwa hiyo ni wajibu na jukumu la menejimenti za Halmashauri kuweka mipango thabiti ya kiuhasibu ili kuhakikisha kumbukumbu za mapato zinawekwa vema, ukusanyaji sahihi, utunzaji na upelekaji fedha benki wa maduhuli.

5.2.4 Kukosekana kwa mikataba kati ya Halmashauri na wakala wa kukusanya mapato

Katika mwaka wa ukaguzi, Halmashauri mbili (2) ziliwaruhusu mawakala kukusanya mapato bila ya kuwa na mikataba au makubaliano yalifanyika kwa mazungumzo ya mdomo (orally). Orodha ya wakusanyaji mapato na vyanzo husika vimeoneshwa katika jedwali hapo chini:

Jedwali Na.19: Halmashauri zilizokusanya mapato bila kuwa na mkataba

Jina la Halmashauri	Chanzo cha Mapato	Jina la Wakala	Kiasi (Sh.)
H/Jiji Mbeya	Ada ya usajili wa taxi, magari binafsi na magari ya biashara	Mbuza Auction Mart and Court Brokers	3,796,700
H/Jiji Mbeya	Ada ya vyoo vya kulipia katika soko la Matola.	Daudi Shonga	150,000
H/W Urambo	Ushuru wa Mazao	M/S Zaya General Supply, M/S Laurent Makundi and M/S Joseph Chayo (Kwa Mwaka)	61,750,000

Hii ina maana kwamba mawakala wanaweza kuwasilisha ushuru kidogo au kutowasilisha kabisa kutohana na ukosefu wa mikataba ya kisheria.

Hivyo nashauri kuwa, Halmashauri ziingie mikataba ya kisheria na mawakala wa kukusanya mapato ili kuepuka kupoteza mapato ya Halmashauri.

5.2.5 Utafiti juu ya Mapato kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa

Kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya 2008, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anaweza kupendekeza kwa Serikali juu ya namna ya kuboresha na kuongeza makusanyo ya mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ni katika hali hii, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu aliikasimisha ‘Ernst and Young’ kufanya utafiti wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kubaini mapungufu katika mfumo wa mapato ya Serikali za Mitaa na kutoa mapendeleko juu ya njia bora ya kuimarisha ukusanyaji mapato katika Serikali za Mitaa.

5.2.5.1 Mapungufu katika Mfumo wa Mapato ya Serikali za Mitaa

(a) Upungufu wa vyanzo vya ndani vya mapato

Mapato ya ndani yameathirika kwa kiasi kikubwa tangu kukomeshwa kwa kodi zinazojulikana kama zenye kero. Matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa, kodi inaweza kuwa kero katika Halmashauri moja, na wakati huohuo ikawa chanzo muhimu cha mapato katika Halmashauri nyingine. Mfano kutoza ada ya umiliki wa baiskeli inaweza kuwakero katika Halmashauri za mijini lakini kikawa chanzo kizuri cha mapato kwa Halmashauri katika maeneo ya vijijini.

Ilipendekezwa kwamba, Serikali Kuu kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI ifanye tathmini ya kina ya mfumo wa mapato uliopo sasa, ili kuhakikisha kwamba inasaidia Halmashauri husika kuongeza mapato ya ndani. Katika kufanya mapitio, wawakilishi kutoka kila halmashauri lazima washiriki. Lengo kubwa ni kuamua aina ya vyanzo vya mapato vinavyotakiwa kuwepo kwa kila Halmashauri. Hii inaweza kufanyika kwa kutofautisha vyanzo vya mapato kwa Halmashauri za mijini na halmashauri za Vijijini.

Hivi karibuni, Serikali imerejesha ukusanyaji wa ada ya leseni za biashara kwenye Serikali za Mitaa ambao ulikuwa umefutwa mwaka 2004.

- (b) **Kukosekana kwa sheria ndogo ndogo kwa baadhi ya vyanzo vya mapato**
Baadhi ya halmashauri hazina seti kamili za sheria ndogondogo kwa ajili ya vyanzo vyote vya mapato.

Ilipendekezwa kuwa, Halmashauri zinapaswa kupitisha sheria ndogo ndogo kwa ajili ya vyanzo vyote vya mapato ya ndani. Hii itahakikisha kwamba kuna nguvu ya kisheria kwa ajili ya ukusanyaji na kufuutilia juu ya wanaotii na wanaokiuka sheria.

- (c) **Sheria ndogo ndogo za ukusanyaji wa mapato zilizopitwa na wakati**
Kukosekana kwa ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kiasi kikubwa kumechangiwa na kuendelea kutumika kwa sheria ndogo ndogo zilizopitwa na wakati. Matokeo ya utafiti katika ukusanyaji wa mapato katika Serikali za Mitaa yalionesha kuwa baadhi ya sheria ndogo ndogo zinazotumika ziliundwa mwaka 1988. Viwango vyama pato vinavyokusanywa ni vya chini sana na havijafanyiwa marekebisho ili kuendana na mabadiliko ya mazingira. Mfano kodi ya majengo inayokusanywa katika

halmashauri za Manispaa ni Sh.10,000 tu kwa mwaka kwa ajili ya nyumba za kuishi bila kujali thamani ya nyumba kwa sasa. Vile vile viwango vyatua na faini kwa kutofuata sheria kwenye kulipa kodi, vimekuwa chini kutokana na ukosefu wa marekebisho ya mara kwa mara ya sheria hizo.

Ilipendekezwa kwamba, kuna haja ya kurekebisha kwa sheria ndogo ndogo zilizopitwa na wakati ili kuhakikisha kwamba viwango vinyavotozwa vinaendana na hali ya sasa ya kijamii na kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuzingatia mfumuko wa bei. Marekebisho ya sheria ndogo ndogo yanapaswa kufanyika mara kwa mara kwa mfano kila baada ya miaka 5.

- (d) **Usimamizi wa vyanzo vyatua na mapato vilivyokasimiwa**
Maboresho ya makusanyo katika Serikali za Mitaa yamepelekea halmashauri kukasimu sehemu kubwa ya makusanyo ya mapato ya vyanzo vyatua na. Hata hivyo Halmashauri zinapitia matatizo mbalimbali katika usimamizi wa baadhi ya makusanyo yaliyokasimiwa. Matatizo hayo ni pamoja na;
- Uandaaji mbovu wa mikataba
 - Udhafu waushindani wakati wa mchakato wa zabuni
 - Mawakala kutowasilisha maduhuli kwa mujibu wa makubaliano

Ilipendekezwa kwamba maboresho haya yatumike kwa vyanzo vyote vyatua na mapato, yaani mapato yanayokusanya na halmashauri husika na yanayokusanya na mawakala. Halmashauri zinapaswa kusimamia mikataba iliyoingiwa na mawakala. Aidha uwezekano wa Halmashauri kujenga uwezo wao wenyewe uangaliwe pamoja na motisha sahihi pale zinapochukuwa jukumu la kukusanya mapato yao.

(e) Mwingiliano wa kisiasa na ule unaofanywa na Serikali kuu

Kuingiliwa na wanasiasa katika ukusanyaji wa mapato imekuwa ni mfano mojawapo kati ya kero kubwa za ukusanyaji wa mapato katika ngazi ya Serikali za Mitaa. Kero hizi ni pamoja na kupotoshwa kwa wananchi kunakofanywa na viongozi wa kisiasa juu ya malipo ya kodi. Mfano baadhi ya madiwani kuwakataza wananchi kulipa kodi na malipo mengine ili kupata umaarufu wa kisiasa. Pia, serikali kuu kuitia Wizara huwa inaingilia ukusanyaji wa mapato ya ndani. Mfano ni ukusanyaji wa kodi ya mabango ambapo katika mwaka 2011, Wizara ya miundo mbinu ilielekeza kwamba Halmashauri hazipaswi kukusanya kodi ya mabango yaliyopo kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara chini ya wakala wa barabara (TANROADS).

Ilipendekezwa kwamba, Halmashauri mara kwa mara zijenge uwezo wa watumishi katika usimamizi wa mapato ya Serikali za Mitaa. Watumishi wanaohusika na ukusanyaji wa mapato kama vile maafisa waandamizi wanaowajibika kwa mapatoya ndani wanapaswa kuelimishwa katika utekelezaji na ufanisi wa mapato yatokanayo na kodi na yasiyo ya kodi ikiwa ni pamoja na kusimamia sheria husika na sheria ndogo ndogo.

Aidha, Viongozi wa kisiasa wanapaswa kuelimishwa mara kwa mara kwa kuwakumbusha umuhimu wa jukumu lao la kutoa msaada katika ukusanyajiwa mapato ya ndani.

(f) Kukosekana kwa Ufanisi wa Mikakati ya kukusanya Mapato

Kukosekana kwa ufanisi wa mikakati ya kukusanya mapato kumepelekea uwezo mdogo wa mapato kutoka Halmashauri. Halmashauri chache zimeweza kufanya utafiti kuhusu mapato na mikakati thabitii katika mamlaka

zao husika. Yafuatayo ni mapendekezo ya namna ya kuongeza mapato:

- **Kuanzishwa kwa Mali za Halmashauri kwa ajili ya Kukodi**
Ili kuhakikisha kuwa kuna mapato ya kuaminika kwa mamlaka za mitaa, kuna haja ya Halmashauri kujenga na kukodisha mali zake kama vile majengo ya Ofisi, nafasi ya maegesho, masoko ya kisasa na machinjio ya kisasa.
- **Kodi katika Minara ya Mawasiliano**
Serikali za Mitaa zinapaswa kuruhusiwa kutoza kodi za minara ya mawasiliano ya simu katika maeneo yao ya mamlaka.
- **Vyanzo vingine vya mapato mahsusini kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa**
Ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani, Halmashauri inapaswa kuchunguza vyanzo vingine maalum vya mapato katika maeneo yao na kutunga sheria ndogo ndogo kwa ajili yamakusanyo hayo. Mfano ada katika maeneo yenye vivutio vya utalii, uwindaji na uchimbaji mdogomdogo wa madini.

(g) Usimamizi dhaifu wa Kodi ya Majengo inayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Ukusanyaji wa kodi ya Majengo unafanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa niaba ya Serikali za Mitaa kwa Dar es Salaam kama majoribio. Taratibu ngumu za malipo ya kodi ya majengo kwa walipa kodi zimetajwa kuwa moja ya sababu ya makusanyo hafifu ya mapato. Taratibu za kukusanya kodi ya majengo za Mamlaka ya Mapato Tanzania zinamtaka mmiliki kulipa kodi ya majengo kupitia benki. Utaratibu huu umebainika kuwa mgumu kwa wamiliki wa majengo yenye thamani ndogo.

Ilipendekezwa kwamba, ili kuwezesha walipa kodi kufuata taratibu, baadhi ya kodi zinazokusanywa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zikusanywe kupitia watendaji wa kata.

Aidha, usajili wa walipa kodi ya majengo unaweza kuboreshwa kwa kusajili wamiliki wa majengo wakati wa kutoa hati ya kumiliki.

(h) Ufinyu wa uelewa wa walipakodi

Ufinyu wa uelewa kwa walipakodi umetajwa kama sababu mojawapo inayopelekea makusanyo hafifu ya mapato kwa ngazi ya mamlaka za Serikali za mitaa. Si wananchi wote wenye uelewa wa mapato wanayopaswa kulipa wala hawaoni umuhimu wa matumizi ya mapato yanayokusanywa katika kugharimia huduma za Umma.

Ilipendekezwa kwamba, Mamlaka za Serikali za Mitaa zipange kampeni za kuelimisha wananchi kuhusu makusanyo ya mapato na kampeni zifanywe na wanasiwa katika ngazi ya serikali za mitaa, wafanyakazi wa Halmashauri na Uongozi wa Halmashauri. Wananchi wanapaswa kuelimishwa kuhusu kodi husika na sheria ndogo ndogo zinazohusika, viwango vya kodi, tarehe za malipo, namna ya kulipa, na faida ya kulipa kodi na madhara ya kutolipa kodi.

Elimu kwa walipa kodi inaweza kufanyika kwa njia mbalimbali ikiwemo mikutano ya kawaida, vipeperushi, mafunzo kwa kundi maalum la walipa kodi.

(i) Kukosekana kwa kumbukumbu sahihi za Walipa Kodi

Halmashauri nyingi hazina mfumo wa kumbukumbu za walipa kodi. Halmashauri chache zimeweza kuanzisha mfumo wa kumbukumbu za walipa kodi japo hazijawa na ufanisi.

Ilipendekezwa kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuanzisha mfumo wa kumbukumbu za walipa

kodi wenye ufanisi kwa vyanzo vyote vya mapato na iwe katika mfumo wa kompyuta, Mfumo rahisi kama vile Mfumo wa kompyuta wa usimamizi wa mapato uanzishwe na kutumika. Mfumo utasaidia kutekeleza usajili wa walipa kodi, upembuzi, ukusanyaji, na uaandaaji na utoaji wa taarifa za kihasibu.

5.3 Usimamizi wa Fedha Taslimu

Usimamizi wa fedha taslim inahusisha makusanyo na mapokezi ya fedha za umma pamoja na usimamizi wa akaunti za benki lengo likiwa ni kuwa na fedha zinazojitosheleza kukidhi matakwa mbalimbali ya uendeshaji wa Halmashauri na pia kuwa na fedha kwa ajili ya kuwekeza; kwa kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani wa makusanyo ya fedha taslim na matumizi, na kuweka utaratibu mzuri wa kufikia malengo ya makusanyo na pia kukusanya mapato ya miaka ya nyuma ambayo yalikuwa bado hayajakusanya, kuweka mifumo imara ya masawiliano kati ya ofisi ya fedha na idara mbalimbali za Halmashauri na kuanzisha mawasiliano ya kitaalam na mabenki pamoja na wawekezaji.

Ukaguzi wa usimamizi wa fedha taslim ulibaini mapungufu mbalimbali kama inavyooneshwa hapa chini:

5.3.1 Masuala yaliyosalia katika usuluhishi wa benki

Agizo la 29 (2) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linamtaka mweka Hazina wa Halmashauri kuhakikisha kuwa suluhishi zote muhimu zinafanya ikiwa ni pamoja na udhibiti wa akaunti mbalimbali na daftari la fedha na kati ya daftari la fedha na akaunti za benki kila mwezi na kufanya marekebisho katika maeneo yaliyosuluhishwa. Kinyume na agizo hilo, Halmashauri 86 zimekutwa na masuala yaliyoonekana kwenye usuluhishi wa benki lakini bado kukamilishwa.

Pia, hakuna uthhibitisho uliowasilishwa ukaguzi kuwa suluhisho za benki zinapitiwa na afisa mwandamizi wa

Halmashauri. Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika suluhishi za taarifa za kibenki kwa hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni 2012 ni kama ifuatavyo:


- Kiasi cha Sh. 3,872,146,712 kutoka Halmashauri mbalimbali kimeingizwa kwenye daftari za fedha lakini hazionekani kwenye taarifa za benki.
- Jumla ya Sh.18,368,780,081 ikiwa ni hundi zilizolipwa lakini bado kuwasilishwa benki na walipwaji hadi tarehe 30 Juni 2012.
- Jumla ya Sh.842,758,166 zinaonekana kulipwa kwenye akaunti za benki za Halmashuri lakini hazijaingizwa katika daftari za fedha.
- Kiasi cha Sh.136,065,798 kimekusanywa na benki kwa niaba ya Halmashauri lakini hakionekani katika daftari za fedha za Halmashauri.

Jedwali hapa chini linaonesha ulinganisho wa masuala ambayo yalijitokeza katika suluhishi za benki lakini hayakuweza kukamilishwa kwa kipindi cha miaka mitano ambayo ni 2007/08, 2008/09, 2009/10, 2010/11 na 2011/2012.

Jedwali Na. 20: Mwelekeo wa masuala yaliyosalia katika usuluhishi wa taarifa za kibenki

Mwaka wa fedha	Mapato kwenye daftari la fedha lakini hayako benki (Sh.)	Hundi bado kuwasilishwa benki (Sh.)	Malipo yaliyo benki lakini hayaonekani kwenye daftari la fedha. (Sh.)	Mapokezi benki lakini hayako kwenye daftari la fedha. (Sh.)
2007/08	474,402,925	2,969,830,892	535,856,223	319,550,613
2008/09	3,511,801,077	10,895,917,505	838,210,104	1,634,905,409
2009/10	10,418,079,556	28,792,732,991	2,586,187,823	1,257,775,757
2010/11	5,088,963,792	10,897,078,986	1,002,195,882	401,528,675
2011/12	3,872,146,712	18,368,780,081	842,758,166	136,065,798

Mchanganuo huo unaweza kuoneshwa kwenye chati msitari kama ifuatavyo:



Mchoro huo hapo juu unaonesha kwamba:

- Mapato ambayo yapo kwenye daftari la fedha lakini hayaonekani benki yaliongezeka kwa kiasi cha Sh. 10,421,514,580 kutoka mwaka wa fedha 2007/08 kwenda mwaka wa fedha 2009/10, pia yalipungua kwa Sh.6,545,932,844 ambayo ni sawa na 63% hadi kufikia Sh.3,872,146,712 katika mwaka wa fedha 2011/12.
- Hundu ambazo hazijawasilishwa benki na walipwaji ziliongezeka kwa kiasi kikubwa kwa Sh.25,822,902,099 kutoka mwaka wa fedha 2007/08 kwenda mwaka 2009/10, halafu ilipungua kwa Sh.10,423,952,910 ambayo ni sawa na 36% hadi Sh.18,368,780,081 kwa mwaka wa fedha 2011/2012.
- Malipo yaliyo benki lakini hayapo kwenye daftari la fedha yaliongezeka kwa Sh.2,050,331,600 kutoka mwaka wa fedha 2007/08 kwenda mwaka wa fedha 2009/10 halafu yalipungua kwa Sh. 1,743,429,657 sawa na 67% hadi Sh.842,758,166 katika mwaka wa fedha 2011/2012.
- Mapato yaliyo benki lakini hayamo kwenye daftari ya fedha yaliongezeka kwa Sh. 1,315,354,796 kutoka mwaka wa fedha 2007/2008 kwenda mwaka wa fedha 2008/2009, na ikapungua tena katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Makosa na matumizi mabaya ya fedha za umma kutokana na masuala ambayo hayajakamilika katika usuluhishi wa benki yanaweza kutokea bila uongozi wa Halmashauri husika kufahamu, na hii inaweza kupelekea kupotea kwa rasilimali za Halmashauri na/au wizi. Kwa hali hiyo, uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuhakikisha usuluhishi wa benki unafanyika kila mwezi na lazima uhakikiwe na afisa mwandamizi wa Halmashuri. Pia marekebisho yote muhimu yanatakiwa kufanyika katika vitabu vya fedha.

Mchanganuo wa Halmashauri ambazo zina masuala ambayo hayajakamilishwa katika usuluhishi wa benki ni kama ulivyo katika **Kiambatisho**(xvii).

5.3.2 Ukaguzi wa kushtukiza katika Ofisi ya Fedha

(i) Ukaguzi wa kushtukiza wa Fedha Taslimu

Agizo la 46 (1) la Memoranda ya Fedha kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linamtaka afisa masuuli au mwakilishi wake kufanya ukaguzi wa kushtukiza wa mara kwa mara katika ofisi ya fedha. Hata hivyo imeonekana katika Halmashauri ambazo zimeangaliwa, Wakurungenzi au maafisa waliowaidhinisha katika Halmashauri 46 imeonekana hazikupanga kufanya na wala hazikufanya ukaguzi wa kushtukiza. Mapungufu yaliyojitokeza katika Halmashauri ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho** (xviii).

(ii) Kiwango cha juu cha Fedha Taslimu kuwa katika ofisi ya Fedha

Agizo la 99 (1) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linaeleza kwamba “kiasi cha juu cha fedha taslimu kinachotakiwa kuwa na mtunza fedha lazima kipitishwe na Halmashauri husika, na baada ya kipitishwa hakipaswi kuzidi bila kibali cha maandishi”. Ukaguzi wa ofisi za fedha umegundua kwamba, katika Halmashauri za wilaya 24


hakuna kiwango cha juu cha fedha kilichowekwa kwa ajili ya kukaa katika ofisi ya Fedha kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xviii)**.

Jedwali hapa chini linaonesha Halmashauri ambazo hazikufuata matakwa ya Agizo hilo kwa miaka mitano yaani 2007/08, 2008/09, 2009/10, 2010/11 na 2011/2012.

Jedwali Na. 21: Mwenendo wa Halmashauri ambazo hazikufanya ukaguzi wa fedha wa kushtukiza na kutoweka kiwango cha juu cha fedha taslim kuwa katika ofisi ya fedha

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Halmashauri ambazo hazikufanya ukaguzi wa kushtukiza	Idadi ya Halmashauri ambazo hazina kiwango cha juu cha Fedha Taslim
2007/08	23	3
2008/09	14	3
2009/10	34	6
2010/11	39	16
2011/12	46	24

Mtiririko katika jedwali hilo hapo juu unaweza kuoneshwa katika chati mstari kama ifuatavyo:



Chati mstari hapo juu inaonesha kuwa Halmashauri hazifuati agizo la kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika ofisi ya fedha na kuwa na kiwango cha juu cha fedha katika ofisi ya fedha, kwani kuna ongezeko la Halmashauri kutoka 23 hadi 46 na kutoka 3 hadi 24 kwa mtiririko huo. Hii inaonesha kuwa Halmashauri haziko makini kuhakikisha zinaimarisha mifumo ya ndani ya udhibiti wa fedha ili kupunguza uwezekano wa kuibwa na fedha taslim kutumika bila mpangilio.

Kwa hiyo, Halmashauri zinatakiwa kuanzisha mifumo imara ya usimamizi wa fedha taslim kama ilivyoainishwa katika memoranda ya fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

5.3.3. Masurufu Yasiyorejeshwa Sh. 1,999,406,423

Agizo la 40 (2) na 40(3) la Memoranda ya Fedha kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linaeleza kwamba “masurufu maalumu yanatakiwa kurejeshwa ndani ya wiki mbili baada ya kukamilika kwa shughuli husika, na kushindwa kufanya hivyo kutapelekea fedha hizo kukatwa kwenye mshahara wa Afisa Mhusika na/au kupewa tozo kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (tozo na fidia)

Vivyo hivyo, Agizo la 40 (4) na 40(5) linaeleza kuwa, masurufu mengine hayatakiwi kutolewa kwa afisa mhusika kama masurufu ya awali hayajarejeshwa. Pia

masurufu yaliyokaa mwezi mzima bila kurejeshwa yataambatana na tozo kama ilivyoelekezwa kwenye Kanuni za tozo za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kinyume na Agizo hilo, masurufu yenye thamani ya Sh.1,999,406,423 yanayohusu Halmashauri 70 yalikuwa bado kurejeshwa mpaka wakati wa kufanya ukaguzi kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho** (xix).

Kwa kuongezea, hakuna ushahidi kuwa maafisa masuuli wa Halmashauri za wilaya husika wamechukua hatua mahsusini kuhusiana na agizo hilo hapo juu kuhusiana na kuchelewesha kurejesha masurufu kwa baadhi ya watumishi wa Halmashauri.

Jedwali hapa chini linaonesha mtiririko wa masurufu ambayo hayajarejeshwa ya miaka ya fedha mitano (5) ambayo ni 2007/08, 2008/09, 2009/10, 2010/11 na 2011/2012.

Jedwali Na. 22: Mwelekeo wa masurufu ambayo hayakurejeshwa kwa miaka mitano

Mwaka	Kiasi (Sh.)	Idadi ya halmashauri husika
2007/08	214,489,665	18
2008/09	14,983,300	4
2009/10	1,574,632,616	72
2010/11	984,955,534	34
2011/12	1,999,406,423	70

Mchanganuo huo unaonekana kwenye chati mstari kama ifuatavyo:



Kutokana na jedwali na chati msitari hapo juu, inaonesha kuwa masurufu yasiyorejeshwa yameongezeka sana kwa Sh.1.6bil na Sh.1bil katika mwaka wa fedha 2009/10 na 2011/12 ambayo imesababishwa na kuongezeka kwa idadi ya Halmashauri husika kwa Halmashauri 68 na 36 kwa mtiririko huo.

Udhibiti zaidi unatakiwa katika kutoa, kuingiza, kurejesha na kufuatilia masurufu yanayotolewa ili kupunguza idadi ya masurufu yasiyorejeshwa kwa muda mrefu.

5.4 Usimamizi wa Rasilimali watu

Usimamizi wa Rasilimali watu katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni moja ya shughuli inayolenga uboreshaji wa Rejista ya taarifa zote zinazohusu watumishi ikiwemo mishahara, kupandishwa vyeo, uhamisho, vifo, kufukuzwa kazi, na watoro. Menejimenti ya rasilimali watu pia inaelekeza mifumo inayohakikisha kwamba, taarifa kuhusu mishahara na mabadiliko ya taarifa za malipo zinapatikana kwa wakati. Vilevile, Usimamizi wa rasilimali watu unahusiana na usimamizi wa upimaji wa utendajikazi wa wazi wa watumishi (OPRAS), mfumo ambao kila mtumishi anatakiwa kutimiza wajibu wake, na unaweka bayana misingi ya tathmini za kila mwaka.

Pia ni shughuli yaUsimamizi wa Rasilimaliwatu kuhakikisha kuwa idadi ya watumishi katika rejista ya mishahara inarandana na idadi iliyopitishwa.

Wakati wa Ukaguzi uliofanyika, tathmini zilifanyika katika ufanisi wa usimamizi wa rasilimaliwatu na mishahara kwa mwaka ilioisha 30 Juni, 2012 katika serikali za mitaa. Baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni kama yafuatayo:

5.4.1Kutokuwepo na Kutoboresha Rejesta za Watumishi

Agizo Na. 79(1) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009 linamtaka mkuu wa Idara ya Rasilimaliwatu kutunza na kuboresha rejesta yenyе orodha na kumbukumbu za watumishi wote. Pia Agizo Na. 79(5) la Memoranda hiyohiyo, linaagiza kuwa kumbukumbu za mishahara isiyolipwa zitunzwe na kuingizwa kwenye rejesta ya mishahara isiyolipwa. Kinyume na maagizo hayo, ukaguzi ulibaini mapungufu katika jumla ya Halmashauri 17 kama ifuatavyo:

- Rejesta za mishahara isiyolipwa hazitunzwi na mara nyingi taarifa za namba za wafanyakazi na sababu za kutokulipwa mishahara havionyeshwi katika rejesta hizo.
- Hakuna mfumo maalum ya kuhakikisha kuwa, taarifa zote za muhimu zinapokelewa katika kitengo cha mishahara.
- Vitengo vya mishahara havitunzi taarifa kudhibiti mishahara isiyolipwa.
Mapungufu haya yalipatikana katika Halmashauri zifuatazo;

**Jedwali Na. 23: Orodha ya Halmashauri ambazo
hazitunzi na haziboreshi rejista za taarifa za watumishi**

Na.	Jina la Halmashauri
1	H/M Arusha
2	H/W Monduli
3	H/W Arusha
4	H/W Bahi
5	H/W Mpwapwa
6	H/W Ludewa
7	H/W Makete
8	H/W Ngara
9	H/W Same
10	H/W Chunya
11	H/W Illeje
12	H/W Mbarali
13	H/W Mbeya
14	H/W Rungwe
15	H/W Kahama
16	H/M Singida
17	H/Jiji Tanga

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa zihakikishe kwamba zinatunza kumbukumbu sahihi za watumishi wake ili kuepuka uwezekano wa kulipa watumishi hewa.

Vile vile Idara za Rasilimaliwatu zinatakiwa kuanzisha na kuboresha rejesta za watumishi ili kuweza kusimamia masuala yote yanayohusu watumishi ikiwemo mishahara na stahili zao zingine.

Vile vile kunatakiwa kuwepo na uboreshwaji wa Rejesta za mishahara isiyolipwa.

5.4.2 Mishahara Isiyolipwa ambayo haikurejeshwa Hazina

Sh.1,599,387,243

Agizo Na.79(5) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009 linaagiza kwamba, mishahara isiyolipwa inatakiwa ipelekwe benki ndani ya siku kumi (10) za kazi. Pia maelekezo kutoka Wizara ya Fedha ambayo yalitolewa kwa barua yenyeye Kumb. Na.EB/AG/5/03/01/Vol.VI/136 ya Agosti 31, 2007 ambayo inaelekeza kwamba mishahara yote isiyolipwa inatakiwa kurejeshwa Hazina kupitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa. Kinyume na maagizo hayo, ukaguzi wa mishahara umberaini kwamba, kuna mishahara isiyolipwa ya kiasi cha Sh.1,599,387,243 katika Halmashauri 43 ambazo hazikurejeshwa Hazina kwa mujibu wa maelekezo. Hali hii inaweza kusababishwa na ukosefu wa uwajibikaji katika mishahara isiyolipwa ambayo inaweza kusababisha hasara katika Halmashauri husika. Orodha ya Halmashauri hizo 43 inaoneshwa katika **Kiambatisho (xx)**.

Inashauriwa kuwa, Halmashauri husika zihakikishe kuwa mishahara isiyolipwa inarejeshwa Hazina haraka kupitia Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa na Hazina ihakikishe kuwa kiasi husika kimepokelewa na kukatiwa stakabadhi kama inavyotakiwa.

5.4.3 Mishahara Iliyolipwa kwa Watumishi Waliostaifu, Walioachishwa Kazi,Waliofariki Sh.693,132,772

Wakati wa ukaguzi wa mfumo wa malipo ya mishahara na rejesta za mishahara isiyolipwa kwa mwaka wa fedha ulioishia 30Juni 2012 ilibainika kwamba, kiasi cha Sh.693,132,772 kililipwa na Halmashauri 43 ikiwa ni mishahara kwa watumishi ambao aidha wamestaifu,wamejiuzuru, wameachishwa kazi au

wametoroka na majina yao yameendelea kuonekana katika mfumo wa malipo ya mishahara ya Halmashauri husika. Rejea **Kiambatisho (xxi)**

Hii inaashiria udhaifu katika udhibiti wa ndani kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa jambo ambalo linaweza kuisababishia hasara serikali kwa kulipa watumishi hewa. Pia, hii inaweza kusababisha ongezeko la ziada la kiasi cha mishahara inayopaswa kulipwa.

Menejimenti za Halmashauri husika zinatakiwa ziimarishe udhibiti na kuhakikisha kuwa mishahara iliyolipwa kwa wasiokuwa watumishi inarejeshwa na kupelekwa Hazina kupitia ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa kama ilivyoelekezwa kwenye barua yenyε Kumb. Na.CA:307/334/01 iliyotolewa tarehe 15/01/2010. Ninasitiza kuwa, OWM-TAMISEMI, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Hazina wanatakiwa waanzishe uhusiano wa karibu wa kikazi na kuchukua takwimu za watumishi waliopo katika utumishi wa umma na baada ya hapo, waandae mfumo imara wa udhibiti wa ndani ili uweze kutumiwa na Mamlaka zaSerikali za Mitaa.

Ufuatao ni muainisho wa mfululizo wa mishahara wa miaka mitatu iliyolipwa kwa Watumishi Waliostaafu, Walioachishwa Kazi, na Waliofariki

Jedwali Na. 24: Mwenendo wa mishahara iliyolipwa kwa watumishi walitoroka, waliostaafu na waliofariki

Mwaka	Mishahara iliyolipwa(Sh.)	Idadi ya Halmashauri zilizohusika
2009/10	583,221,297	38
2010/11	961,394,959	36
2011/12	693,132,772	43

Mfululizo wa miaka mitatu unaonesha kuwa, mishahara iliyolipwa kwa watumishi waliokufa, waliostafu, na walioachishwa kazi imeongezeka kwa Sh.378,173,662 sawa na 65% toka mwaka 2009/10 hadi 2010/11 halafu imepungua kwa Sh.268,262,187 sawa na 28% toka mwaka 2010/11 hadi 2011/12.

5.4.4 Mikopo kwa Watumishi Isiyodhibitiwa

Waraka wa utumishi Na. CCE.45/271/01/87 wa tarehe 19/03/2010 unaelekeza kwamba, makato katika mishahara ya watumishi yanatakiwa yasizidi 2/3 ya mishahara yao.

Kama ilivyobainika katika taarifa za nyuma za ukaguzi, bado kuna idadi ya matukio ambapo kuna wafanyakazi wengi wa Halmashauri ambao bado wanakatwa zaidi ya 2/3 ya mishahara yao. Pia kuna baadhi ya watumishi wamekuwa wakikatwa mshahara wote. Katika jumla ya Halmashauri 87 zilizokaguliwa, imebainika kuwepo kwa jumla ya watumishi 17,710 ambao wanapokea chini ya 1/3 ya mishahara yao kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xxii)**.

Mikopo isiyodhibitiwa inaweza kuleta madhara makubwa kwa watumishi husika katika ufanisi wa kazi na katika Halmashauri husika. Matatizo hayo ya mishahara yanachangiwa na uongozi wa Halmashauri husika kutokuwa makini katika kuhakikisha maslahi ya wafanyakazi yanalindwa.

Inashauriwa kuwa, udhibiti wa malipo ya mishahara unapaswa, zaidi ya kuhakikisha kuwa watumishi husika wanalipwa mshahara unaotakiwa, pia usawa katika malipo lazima uangaliwe. Kwa kufanya hivyo kutazuia uwezekano wa kuwa na madhara katika ufanisi wa watumishi.

5.4.5 Utofauti kati ya fedha za mishahara zilizopokelewa na mishahara iliyolipwa Sh.783,575,845

Ukaguzi ulibaini kuletwa kwa fedha za mishahara pungufu kutoka hazina kwenda katika Halmashauri. Mapitio ya mishahara iliyopokelewa kutoka hazina kuitia taarifa ya kutolea fedha kutoka Hazina kwenda kwa Maafisa Masuuli, pamoja na kiasi halisi cha mishahara iliyolipwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ulibaini kuwa, halmashauri kumi na saba (17) zilipokea mishahara pungufu kwa kiasi cha Sh.783,575,845. Halmashauri zilizolipa mishahara zaidi ya kiasi cha mishahara kilichopokelewa ni kama inavyoonekana hapa chini;

Jedwali Na. 25: Halmashauri zilizolipa mishahara zaidi ya fedha za mishahara zilizopokelewa

Na.	Halmashauri	Kiasi kilichopokelewa (Sh.)	Kiasi kilicholipwa (Sh.)	Tofauti (Sh.)
1.	H/W Bariadi	13,826,389,127	13,880,776,382	(54,387,256)
2.	H/W Chunya	6,587,081,681	6,719,604,244	(132,522,563)
3.	H/W Ileje	5,411,105,043	5,431,204,691	(20,099,648)
4.	H/W Kilwa	5,804,036,212	5,849,982,604	(45,946,391)
5.	H/M Kinondoni	32,097,230,670	32,170,977,790	(73,747,120)
6.	H/W Kishapu	5,885,686,507	5,908,805,214	(23,118,707)
7.	H/W Maswa	8,938,015,766	8,939,442,893	(1,427,126)
8.	H/W Mbozi	5,830,969,083	5,913,312,489	(82,343,406)
9.	H/W Muleba	2,481,733,553	2,521,047,343	(39,313,790)
10.	H/W Musoma	10,714,400,496	10,728,581,581	(14,181,085)
11.	H/W Shinyanga	6,397,749,922	6,433,772,434	(36,022,513)
12.	H/W Tarime	11,588,647,209	11,595,263,855	(6,616,646)
12.	H/M Musoma	6,043,850,273	6,086,196,871	(42,346,598)
14.	H/M Iringa	7,747,209,863	7,792,642,896	(45,433,033)
15.	H/W Mbeya	11,984,397,415	12,137,572,243	(153,174,829)
16.	H/W Utanga	444,574,177	455,213,350	(10,639,173)
17.	H/W Mvomero	10,155,949,399	10,158,205,360	(2,255,961)
Jumla		151,939,026,396	152,722,602,240	(783,575,845)

Kwa kuwa halmashauri hazikupokea kiasi cha mishahara kinachotosheleza, ni dhahiri kwamba, halmashauri husika zilitumia fedha nyingine ambazo kazikubajetiwa kulipa mishahara.

Jedwali lifuatalo linaonesha mwenendo wa tofauti kati ya fedha za mishahara zilizopokelewa na halmashauri na mishahara iliyolipwakwa miaka mitatu.

Jedwali Na. 26: Mwenendo unaonesha utofauti kati ya fedha za mishahara zilizopokelewa na mishahara iliyolipwa

Mwaka	Kiasi (Sh)	Idadi ya Halmashauri
2009/10	(790,203,584)	6
2010/11	(267,544,718)	6
2011/12	(783,575,845)	17

Kutokana na jedwali hapo juu inaonesha kuwa, halmashauri sita (6) kwa mwaka 2009/10 na 2010/11 zilipokea kiasi pungufu cha kulipa mishahara, wakati kwa mwaka wa fedha 2011/12 halmashauri zilizopokea kiasi pungufu cha mishahara ziliongezeka na kufikia kumi na saba (17).

Inapendekezwa kuwa menejimenti za halmashauri zisuluhihe kumbukumbu za fedha za mishahara zinazopokelewa kwa taarifa ya kutolea fedha kutoka Hazina kwenda kwa Maafisa Masuuli na kuwasiliana na hazina ili kurejesha mishahara pungufu pale inapotokea.

5.4.6 Kutokuwepo kwa Usahihi wa Tarehe ya Kuzaliwa kwa Watumishi Katika Mfumo wa Malipo ya Mishahara
Mfumo wa malipo ya mishahara hauko imara. Ukaguzi uliofanyika katika taarifa kutoka katika mfumo wa malipo ya mishahara ya watumishi 1,531 wa Halmashauri 15

ulibaini kuwa, tarehe za kuzaliwa za kwa watumishi 1,531 hazikuwa sahihi. Imeonekana kuwa tarehe za kuzaliwa ziliingizwa kama 1/1/1700, 1/1/1900 na 1/1/2012 katika rejista kuu ya malipo ya Hazina kama ifuatavyo;

Jedwali Na. 27 : Orodha ya Halmashauri zinazoonesha Tarehe za Kuzaliwa za Watumishi zisizo sahihi katika Mfumo wa Malipo wa Mishahara

Na.	Jina la halmashauri	Idadi ya watumishi
1.	H/W Musoma	634
2.	H/W Serengeti	363
3.	H/W Illeje	197
4.	H/Jiji Mbeya	70
5.	H/W Rungwe	59
6.	H/W Moshi	50
7.	H/W Arusha	40
8.	H/W Mbarali	20
9.	H/W Nzega	20
10.	H/M Tabora	20
11.	H/W Tarime	16
12.	H/W Rarya	14
13.	H/M Temeke	10
14.	H/M Musoma	10
15.	H/W Longido	8
Jumla		1,531

Hii inamaanisha kuwa tarehe za kustaafu za watumishi husika hazijulikani na inaonekana kutosimamiwa na Hazina.

Uongozi wa Halmashauri husika unashauriwa kuwa, taarifa za watumishi nataarifa katika mfumo wa kulipia mishahara kutoka Hazina zinasuluhishwa na kwamba terehe za kuzaliwa zinasahihishwa ipasavyo. Kinyume na hapo, matatizo makubwa ya kifedha yanaweza kutokea wakati wa ulipwaji wamafao yao ya kustaafu.

5.4.7 Watumishi Wasiochangia katika Mifuko ya Jamii na Bima ya Afya

Ukaguzi katika sampuli ya Halmashauri 6 kwa mwezi wa Juni 2012 imebaini kuwepo kwa watumishi wasiochangia katika Mifuko ya Jamii na Bima ya Afya kwa kuwa vifungu vya makato hayo havikuonekana kwenye taarifa za mishahara ya watumishi kama ilivyo kwenye mfumo nakama inavyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 28: Watumishi wa Halmashauri ambao hawachangii mifuko ya jamii na bima ya afya

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Watumishi waliohusika
1	H/W Ukerewe	385
2	H/W Mvomero	109
3	H/W Kigoma	78
4	H/M Tabora	50
5	H/Mji Lindi	27
6	H/W Kilwa	10
Jumla		659

Madhara ya kutokuchangia makato haya ya kisheria ni kwamba, watumishi husika watakosa mafao yao wakati wa kustaaifu, na pia hawatapata huduma za afya.

Inashauriwa kwamba, wakaguzi wa ndani wa Halmashauri husika wafanye ukaguzi wa mishahara na pia kuitia mara kwa mara taarifa za watumishi ili kama kuna mapungufu yaweze kufanyiwa kazi mapema kwa mujibu wa sheria.

5.4.8 Makato ya Kisheria ambayo hayakuwasilishwa katika Taasisi husika Sh.1,067,659,142

Wakati wa kuitia nyaraka mbalimbali za mishahara ikiwa ni pamoja na nyaraka za benki na orodha Na.11 kutoka Hazina ilibainika kuwa, kiasi cha makato ya kisheria cha

Sh.1,067,659,142 katika jumla ya Halmashauri saba (7) hakikuwasilishwa katika taasisi husika kama vile LAPF, PSPF, NSSF, PPF na TRA kama ifuatavyo;

**Jedwali Na. 29 : Makato ya Kisheria ambayo
hayakuwasilishwa katika Taasisi husika**

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Makete	649,118,793
2	H/W Mbarali	162,549,337
3	H/W Kilosa	146,107,972
4	H/W Chamwino	44,571,144
5	H/M Morogoro	35,333,182
6	H/W Kibondo	15,246,040
7	H/Jiji Mwanza	14,732,674
Jumla		1,067,659,142

Kutokana na jedwali hapo juu, imedhihirika kuwa, kuna uwezekano wa Halmashauri husika kushtakiwa na taasisi husika kamavile Mifuko ya pensheni na Mamlaka ya mapato (TRA) kwa kutowasilisha makato ya kisheria. Pia, kiasi cha wadai kimetolewa taarifa pungufu katika taarifa za fedha za mwaka husika.

Inashauriwa kuwa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zihakikishe kuwa makato yote ya kisheria yanalipwa katika Taasisi husika na kuwasilisha uthibitisho wa nyaraka kwa ajili ya ukaguzi. Vile vile, kiasi cha madeni ambacho hakijawasilishwa katika Taasisi husika kioneshwe katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka.

**5.4.9 Kutowasilishwa kwa Stakabadhi za Kupokelea Mishahara
Isiyolipwa na Makato ya Kisheria yaliyolipwa
Sh.426,996,480**

Kiasi cha Sh.426,996,480 ikiwa ni mishahara iliyorudishwa Hazina kuitia Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa na makato ya kisheria yaliyolipwa katika taasisi mbalimbali

kutoka Halmashauri kumi (10) hakikuweza kuthibitika kama kimepokelewa na taasisi husika kwa vile stakabadhi za kukiri mapokezi hazikuwasilishwa kuthibitisha kupokelewa kwa kiasi cha fedha kilicholipwa kinyume na Agizo Na. 8 (2) (c) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009. Halmashauri husika ni kama zinavyooneshwa katika jedwali lifuatato:

**Jedwali Na. 30: Stakabadhi za Kupokelea Mishahara
Isiyolipwa naMakato ya Kisheria yaliyolipwa ambazo
hazikuwasilishwa kwa ukaguzi**

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi(Sh.)
1	H/M Dodoma	173,029,081
2	H/W Magu	67,784,630
3	H/W Misungwi	48,408,947
4	H/M Ilala	48,325,645
5	H/W Iringa	25,600,589
6	H/W Korogwe	21,474,797
7	H/W Sengerema	20,971,711
8	H/W Urambo	15,449,967
9	H/W Mpwapwa	3,777,236
10	H/W Kilindi	2,173,877
Jumla		426,996,480

Kukosekana kwa stakabadhi za kupokea malipo hayo kutoka kwa walipwaji kunadhihirisha kuwa, kuna uwezekano wa malipo hayo kufanyika kimakosa kwa walipwaji wengine.

Uongozi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa unatakiwa kuimariswa mfumo waudhibiti wa ndani katika kufuatilia wahusika mara moja ili kuhakikishakuwa malipo yote yamefanyika kwa walipwaji sahihi.

**5.4.10 Majina ya watumishi yanayotokea zaidi ya mara moja
katika orodha ya malipo ya mshahara**

Mapitio ya orodha ya malipo ya mishahara katika halmashauri mbili (2) kwa mwaka wa fedha 2011/2012 yalionesha kuwa, watumishi sita (6) wa halmashauri ya wilaya Rungwe na wanne (4) wa halmashauri ya wilaya

Namtumbo walikuwa na namba za watumishi zaidi ya moja na hivyo kufanya jumla yao kuwa kumi (10).

Kukosekana kwa usuluhisho wa mara kwa mara kati ya idadi ya watumishi halisi waliopo na kiwango kilichotengwa katika orodha ya malipo ya mishahara kunaweza kupelekea kuwa na kiasi zaidi cha fedha kwa ajili ya malipo ya mishahara iliyopokelewa.

Mtumishi mmoja kulipwa mshahara mara mbili inaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha za umma na hivyo kuathiri kazi nyingine ambazo zingeweza kutumia fedha hiyo.

Menejimenti za halmashauri zichunguze suala hili na kuhakikisha kuwa mapungufu yaliyotajwa yameshughulikiwa na taarifa zipelekwe katika mamlaka husika na kiasi kilicholipwa kinyume na taratibu kirejeshwe hazina kupitia Makatibu Tawala wa mikoa.

5.4.11 Karadha za mishahara zisizorejeshwa Sh.312,089,918

Agizo la 41(1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa (LGFM), 2009 inaeleza kuwa Mkurugezi anaweza kupitisha karadha kwa mtu kwa kiwango cha juu cha mshahara wa miezi mitatu na kurejeshwa katika kipindi kisichozidi miezi kumi na miwili katika mafungu yanayofanana kwa mwezi. Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika kupitia hati za malipo na viambatisho vingine katika halmashauri kumi (10) ilidhihirika kuwa, kiasi cha Sh.312,089,918 kilicholipwa kama karadha hakikurejeshwa kinyume na agizo lililotajwa hapo juu. Orodha ya halmashauri na kiasi kilicholipwa zimeoneshwa hapo chini:

Jedwali Na. 31 : Halmashauri zenye Karadha zisizorejeshwa

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Chunya	100,171,778
2	H/M Kinondoni	75,392,900
3	H/W Ileje	69,775,869
4	H/W Mwanga	20,585,543
5	H/W Morogoro	19,614,407
6	H/W Chamwino	10,246,313
7	H/Mji Mpanda	5,436,027
8	H/Jiji Dar es Salaam	4,608,684
9	H/W Meru	3,192,910
10	H/M Arusha	3,065,487
Jumla		312,089,918

Kutokurejeshwa kwa karadha za mishahara kwa muda, kunaathiri utekelezaji wa shughuli nyingine zilizopangwa na inaweza kuwa chanzo cha madeni yasiyolipika kwa watumishi.

Menejimenti ya halmashauri inatakiwa kuzingatia agizo la 41 (1) kwa kuhakikisha karadha za mishahara kwa watumishi zimerejeshwa na vielelezo viletwe kwa uhakiki.

5.4.12 Wastaafu kuendelea kuonekana katika Orodha ya Mishahara ya Hazina

Agizo 79 (1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka, 2009 inaelekeza kuwa wakuu wa idara wanatakiwa kutunza rejista hai ya watumishi wote ikiwa na maelezo yao ambayo itampa mweka hazina taarifa juu ya mambo yote yanayohusu ajira, kuacha kazi, kuachishwa kazi, kusimamishwa kazi, uhamisho na taarifa yoyote muhimu kwa utunzaji wa kumbukumbu za watumishi kwa ajili ya kodi ya mapato, mifuko ya hifadhi ya jamii n.k. Wakati huo huo kifungu cha 57(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 inataka kwamba “pale ambapo mtumishi wa umma hayupo kazini

kwa siku tano (5) bila sababu na wala si likizo mtumishi huyo atachukuliwa hatua za kinidhamu kwa kuwa nje ya kituo cha kazi na ataachishwa kazi”.

Kinyume na agizo hili, katika kuitia orodha ya mishahara ya watumishi na taarifa zao pamoja na rejista ya mishahara isiyolipwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012 watumishi 198 toka katika halmashauri kumi na tatu (13) ambao ni waliostaafu, kufariki, kuacha na kuachishwa kazi waliendelea kuonekana kwenye orodha ya mishahara ya Hazina,kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 32: Halmashauri ambazo zina wastaaafu ambao hawajafutwa kwenye orodha ya mishahara ya hazina

Na.	Jina la halmashauri	Idadi ya waliokuwa watumishi
1	H/W Newala	60
2	H/W Manyoni	26
3	H/M Singida	21
4	H/W Morogoro	19
5	H/W Mbeya	15
6	H/W Kilombero	13
7	H/W Mamtumbo	10
8	H/W Kondoa	9
9	H/W Kishapu	8
10	H/W Makete	5
11	H/W Songea	5
12	H/M Morogoro	4
13	H/W Ngara	3
Jumla		198

Kuchelewa kufuta majina ya watumishi wastaaafu, waliokufa, waliofukuzwa au kuacha kazi inaweza kupelekea kuongezeka kwa gharama ya mishahara na

upotevu wa fedha za umma zinazolipwa kwa watumishi hewa.

Menejimenti za halmashauri zihakikishe taarifa za watumishi waliostaafu, waliokufa, walioacha au kuachishwa kazi zinatunzwa vizuri na kuhakikisha majina ya watu hawa yanafutwa mara moja katika orodha ya mishahara ya hazina. Pamoja na hayo Halmashauri zikate mishahara iliyolipwa kutoka kwenye mafao ya wastaafu hao.

5.4.13 Uhaba wa Rasilimaliwatu

Utendaji na ufanisi wa taasisi yoyote unategemea upatikanaji wa rasilimali, rasilimaliwatu ikiwa ni moja ya rasilimali muhimu. Katika mwaka wa ukaguzi, Halmashauri 25 zilichaguliwa kama sampuli wakilishi ambapo ilionekana kwamba ikama zilionesha mahitaji ya watumishi 73,087 lakini idadi halisi iliyopo ilikuwani 58,424 tu na kusababisha kuwepo kwa upungufu wa watumishi 14,663 sawana 20% ya idadi inayotakiwa. Upungufu huo una madhara katika utendaji wa jumla wa Halmashauri ikiwa ni pamoja na utoaji duni wa huduma, kuzidiwa kwa kazi na kupungua kwa ari ya kazi kwa watumishi wa umma waliopo katika sekta mbalimbali kama Afya na Elimu.

Jedwali Na. 33 : Orodha inayoonesha uhaba wa Rasilimaliwatu katika Halmashauri

Na.	Halmashauri	Ikama	Watumishi waliopo	Tofauti
1	H/W Bahi	1,363	1,107	256
2	H/W Chamwino	2,192	1,894	298
3	H/W Kondoa	4,520	3,488	1,032
4	H/W Mpwapwa	3,473	2,883	590
5	H/W Mufindi	3,203	3,003	200
6	H/W Njombe	1,316	1,008	308

7	H/W Kasulu	8,360	4,220	4,140
8	H/W Kibondo	3,035	2,426	609
9	H/W Kigoma	4,384	3,666	718
10	H/W Moshi	5,506	5,382	124
11	H/W Siha	1,291	1,011	280
12	H/W Liwale	660	566	94
13	H/W Hanang	2,763	2,064	699
14	H/W Simanjiro	1,488	1,226	262
15	H/W Bunda	3,055	2,722	333
16	H/W Kyela	2,590	1,992	598
17	H/Jiji Mbeya	3,035	2,580	455
18	H/W Kilombero	3,850	3,792	58
19	H/W Songea	1,932	1,674	258
20	H/W Namtumbo	2,676	1,731	945
21	H/W Bariadi	3,930	3,739	191
22	H/W Iramba	785	436	349
23	H/W Igunga	2,843	2,265	578
24	H/W Sikonge	1,713	1,003	710
25	H/W Urambo	3,182	2,488	694
Total		73,087	58,424	14,663

Inapendekezwa kwamba:

- Serikali inapaswa kuimarisha uwezo wake wa kifedha kwa lengo la kuongeza fedha za kutosha kwa ajili ya kuajiri rasilimaliwatu zaidi kulingana na mahitaji kwa ajili ya utoaji wa huduma kwa ufanisi
- Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI iweke mkakati utakao punguza wimbi la wafanyakazi kuacha kazi
- Kurekebisha taratibu za ajira ambapo zinaweza kuhusisha ukiritimba, na hivyo kusababisha ugumu katika upatikanaji wa watumishi ambao wanaweza kukaa katika utumishi wa umma.
- Kuwe na utoaji wa motisha maalum kwa madhumuni ya kuwahamasisha wafanyakazi kufanya kazi katika

Halmashauri za pembezoni. Mapengo mengi ya ajira yaliyothibitishwa katika Halmashauri yapo katika maeneo ya pembezoni ikilinganishwa na maeneo ya mijini.

5.5 Usimamizi wa Mali katika Halmashauri

5.5.1 Mali za Kudumu zisizotumika na zisizo na matengenezo

Agizo 45(1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa la 2009 linataka mali zote ambazo hazitumiki kwa sababu ya thamani yake kwisha au kuharibika zitambuliwe na taratibu za kuziwa zifanyike baada ya kupata kibali cha Kamati ya fedha na uchumi; na baraza la Madiwani. Vilevile aya ya 26 ya IPSAS 21 inaeleza kuwa, mmiliki wa mali, kila anapoandaa hesabu zake, ni vizuri akaangalia kama kuna mali zozote ambazo hazina thamani ili aweze kukadiria gharama ya urejeshwaji wa mali hizo.

Mapitio ya michanganuo ya hesabu za Halmashauri 20 imegundua kuwa, michanganuo hiyo haioneshi thamani halisi ya mali hizo kwa sasa, hivyo kasoro hiyo imesababisha mali hizo kutolewa taarifa zikionesha kiasi kidogo kwenye hesabu hizo. Pamoja na hayo ukagazi uligundua magari mabovu yaliyoegeshwa kwa muda mrefu kwenye baadhi ya Halmashauri bila hatua madhubuti kuchukuliwa na Halmashauri hizo. Maelezo zaidi yanapatikana kwenye **Kiambatisho (xxiii)**.

Ukagazi unashauri kuwa, mali hizo ziangaliwe kwa kutumia vigezo vya aya ya 26 ya IPSAS 21 na kwa kufuata Agizo 45(1) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa la 2009 ili kubaini kama bado zina thamani na zinakidhi katika viwango vya matumizi au la; ili zifanyiwe matengenezo au kama hazifai ziuzwe.

5.5.1.2 Mali na vifaa vya kudumu ambavyohavikuthaminishwa

IPSAS 17 inataka, “mali zinazooneshwa kwenye taarifa ya hesabu zinazotolewa zithaminiwe na kutambuliwa na kwamba zitaendelea kutambuliwa katika hesabu kwa

kiasi ambacho kimethaminishwa. Thamani inayotambuliwa itazingatia kutolewa kwa thamani ya uchakavu na hasara inayotokana na ujumla wa kuharibika kwa mali". Kinyume na mwongozo huu, Uongozi wa Halmashauri 13 kama inavyoonekana katikajedwali hapa chini, haukuthaminisha mali zake ingawa baadhi ya mali hizo zilioneshwa katika hesabu kama ni mali ambazo hazina thamani kabisa wakati katika hali halisi mali hizi ziliendelea kutumiwa na Halmashauri. Kutokana na hali hii, thamani ya mali za kudumu zilizooneshwa katika taarifa za fedha za Halmashauri husika hazitoi taswira halisi ya Halmashauri.

Jedwali Na. 34: Orodha ya halmashauri ambazo mali zake hazijathaminishwa

Na.	Halmashauri	Idadi ya Mali
1	H/M Dodoma	44
2	H/W Bukoba	12
3	H/W Rungwe	1
4	H/W Morogoro	1
5	H/Jiji Mwanza	37
6	H/W Songea	1
7	H/W Tunduru	10
8	H/W Bariadi	4
9	H/W Kahama	25
10	H/M Shinyanga	1
11	H/W Maswa	20
12	H/W Nzega	1
13	H/Jiji Mbeya	43

Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuweka għarama za kuthaminisha mali katika makisio ya mwaka iliku hakikisha kuwa mali zinazoripotiwa zinaonesha hali halisi na sahihi.

5.5.1.3 Kukosekana kwa nyaraka za umiliki wa mali za kudumu Sh.73,880,624,609

Agizo Na.52 (4) na (5) la memoranda ya fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linaagiza kwamba, "Uwekezaji wa zaidi ya fedha taslimu utafanyika baada ya maazimio ya uongozi wa Halmashauri na utajumuishwa katika bajeti ya Maendeleo au bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Uwekezaji kama huo utathibitishwa kwa kuwa na hati ya dhamana au mkataba ambao utaingizwa katika rejista na kutunzwa katika sehemu ya usalama".

Kinyume na maagizo hayo hapo juu, wakati wa ukaguzi mali zenyе thamani ya Sh.73,880,624,609 katika Halmashauri kumi na nne (14) hazikuwa na ushahidi wa maandishi ya umiliki, kutokana na mazingira hayo ukaguzi ulizuiliwa kupata uhakika wa kuwepo, usahihi, umiliki, na uhalali wa mali hizo.

Inashauriwa kuwa, Mamlaka za Serikali za mitaa zitafute hati miliki na udhibiti wa mali zao kama vile kadi za usajili za magari na hati za viwanja kwa ajili ya majengo wanayoyamiliki.

Mali hizo ambazo hazina nyaraka za umiliki ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 35: Orodha ya Halmashauri zenyе mali zisizokuwa na nyaraka za umiliki

Na.	Jina la Halmashauri	Hati miliki inayokosekana	Kiasi (Sh.)
1	H/W Bagamoyo	Taarifa ya LGLB (Mali za kifedha zilizowekezwa)	86,691,100
2	H/W Rufiji/Utete	hati miliki	17,423,229,437
3	H/W Kiteto	Kadi za Usajili (stakabadhi)	0
4	H/W Rungwe	hati miliki na cheti cha uwekezaji	42,291,042,112
5	H/M Morogoro	Cheti cha umilikaji	8,658,060

6	H/W Newala	Kadi za Usajili	0
7	H/W Mpanda	Ushiriki/vyeti vya umiliki, mikataba ya mauziano	67,961,000
8	H/W Bariadi	hati miliki	450,860,432
9	H/W Kahama	Kadi za Usajili	230,412,314
10	H/W Shinyanga	Kadi za Usajili	0
11	H/M Shinyanga	hati miliki	330,750,845
12	H/W Kishapu	Kadi za Usajili	202,943,796
13	H/W Handeni	hati miliki	7,264,000,033
14	H/W Korogwe	hati miliki	5,524,075,478
Total			73,880,624,609

5.5.2 Wadaiwa wasiolipa Sh. 48,443,176,126


Sehemu kubwa ya wadaiwa wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanatokana na malipo ya kabla ya huduma, maduhuli yasiyowasilishwa na mawakala wa kukusanya mapato, karadha, masurufu na mikopo ya wanawake na vijana. Ukaguzi wa taarifa za fedha za Halmashauri mia moja na kumi na nane (118) umeonesha jumla ya Sh. 48,443,176,126 ikiwa ni madai mbalimbali ambayo hayajarejeshwa kama ilivyoainishwa kwenye **Kiambatisho (xxiv)**.

Mwelekeo wa wadaiwa ambao hawajalipa kwa miaka ya 2007/2008, 2008/09, 2009/10, 2010/11 na 2011/12 imeainishwa katika jedwali hapo chini:

Jedwali Na. 36: Mwelekeo wa wadaiwa ambao hawajalipa kwa miaka mitano mfululizo

Mwaka	Kiasi (Sh.)	Idadi ya Halmashauri zilizohusika
2007/2008	8,675,739,790	115
2008/2009	35,644,785,554	113
2009/2010	44,059,104,038	109
2010/2011	37,795,747,360	106
2011/2012	48,443,176,126	118

Mchanganuo hapo juu unaweza kuelezwa kwa kutumia chati mstari kama ifuatavyo:



Mwelekeo hapo juu unaonesha kupungua kwa wadaiwa kutoka mwaka 2009/10 kwenda mwaka 2010/11 kwa kiasi cha Sh.6,263,356,678. Lakini mwaka 2011/12 wadaiwa waliongezeka kwa Sh.10,647,428,766.

Kuwa na rasilimali ambazo zimeshikiliwa kwa njia ya wadaiwa kunaathiri mtaji wa kuendesha shughuli za Halmashauri na hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

5.5.3 Wadai wasiolipwa Sh. 62,192,971,408

Ulipaji wa madeni kwa wakati ni jambo muhimu na linaleta imani kati ya Halmashauri na wasambazaji wa vifaa na huduma na kuongeza hali ya kuaminiwa na jamii inayohudumiwa na Halmashauri.

Hata hivyo, ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2012 ulibaini kuwa Halmashauri 118 zilikuwa na wadai wasiolipwa wenye jumla ya Sh.62,192,971,408 ikiwa ni ongezeko la Sh.10,060,159,480 ikilinganishwa na Sh.52,132,811,928 kwa mwaka uliopita.


Halmashauri zilizoonekana kuongoza kuwa na madeni makubwa ni Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ambayo ilikuwa inadaiwa Sh.7,649,250,988, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Sh.2,142,814,890, na Halmashauri ya Jiji la Mwanza Sh.1,928,840,796.

Jedwali lifuatato linaloonesha mlinganisho wa madeni kwa miaka ya 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010, 2010/11 na 2011/12.

Jedwali Na. 37: Mwenendo wa madeni yasiyolipwa kwa miaka mitano mfululizo

Mwaka wa fedha	Kiasi (Sh.)	Idadi ya Halmashauri zinazohusika
2007/2008	15,610,406,163	101
2008/2009	51,311,586,762	113
2009/2010	52,041,114,397	113
2010/2011	52,132,811,928	111
2011/2012	62,192,971,408	118

Maelezo hapo juu yanaoneshwa zaidi kwenye chati hapa chini:



Chati hapo juu inaonesha kwamba, kiasi cha madeni kimeongezeka toka mwaka 2010/2011 hadi 2011/12 hadi Sh.9,683,016,148 au 5%.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kulipa madeni yake haraka yanapofikia wakati wa kulipa na zianzishe udhibiti thabiti, kanuni na taratibu katika kuhakikisha kuwa uongozi wa Halmashauri unawajibika kwa madeni ambayo hayana faida kwa halmashauri. Orodha ya Halmashauri zinazodaiwa imeoneshwa kwenye **kiambatisho (xxiv)**.

5.6 Ukaguzi wa Miradi ya maendeleo

Pamoja na mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani, Mamlaka za serikali za mitaa hupata ruzuku toka serikali kuu na wafadhili mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nilitathmini utekelezaji na kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo inayogharimiwa na ruzuku ya miradi ya maendeleo ya serikali za mitaa, ikiwa ni pamoja na mpango wa kupambana na ukimwi na mpango wa maendeleo wa afya ya msingi (MMAM). Pia, Mamlaka ya serikali za Mitaa zimepata ruzuku kwa ajili ya kuboresha huduma za jamii kuitia TASAF, Mfuko wa pamoja wa Afya, Mradi wa maendeleo ya kilimo (ASDP) na Mradi wa Maendeleo wa

Sekta ya maji (WSDP). Matokeo ya ukaguzi wa miradi iliyofadhiliwa kwa fedha hizo yameainishwa kwenye barua za ukaguzi zilizotolewa kwa Menijimenti za Halmashauri kwa kila mradi, na kwenye taarifa ya jumla ya miradi iliyopelekwa Bungeni.

5.6.1 Mpango wa Taifa wa Ukimwi (NMSF)

5.6.1.1 Fedha za Mpango wa Taifa wa Ukimwi ambazo hazikutumika Sh.1,545,629,527


Katika mwaka huu wa ukaguzi, Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) kuitia Wizara ya Fedha ilituma fedha kwenye Halmashauri chini ya Mpango wa kudhibiti Ukimwi (NMSF) 2008-2012 ambao wafadhili wakubwa ni pamoja na serikali ya Marekani kuitia USAID, PEPFAR, wafadhili mbalimbali pamoja na serikali ya Tanzania kuitia mpango wa kati wa matumizi. Hata hivyo, Ukaguzi wa sampuli kwenye Halmashauri 59 umeonesha fedha ambazo hazikutumika ni kiasi cha Sh.1,545,629,527mpaka tarehe 30 Juni, 2012 kama inavyoonyeshwa kwenye **kiambatisho (xxv)**.

Jedwali hapa chini linaonesha mlinganisho wa fedha ambazo hazikutumika kwa miaka miwili kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 38: Mwelekeo wa fedha za mpango wa Taifa wa Ukimwi ambazo hazikutumika

Mwaka	Fedha ambayo haikutumika	Idadi ya Halmashauri
2010/11	1,104,364,692	41
2011/12	1,545,629,527	59

Pia taarifa hizo zimeonyeshwa kwenye chati kama ifuatavyo:



Kutokana na chati hiyo hapo juu, inaonekana kuwa fedha ambazo hazikutumika ziliongezeka kwa Sh.441,264,835 ambayo ni sawa na 40%.

Hali hii inaonesha kuwa kazi nyingi zilizotakiwa kufanyika, hazijafanyika hivyo malengo kutofikiwa.

5.6.1.2 Tofauti kati ya Fedha za mpango wa ukimwi zilizotumwa na zilizopokelewa Sh.77,842,728

Ulingenisho wa fedha zilizopokelewa na Halmashauri na taarifa zilizopatikana kutoka kitengo cha kuratibu programu ya kitaifa ya kuzuia maambukizi ya UKIMWI cha TACAIDS kwa sampuli ya Halmashauri 56 imeonesha kuwa kiasi kilichotumwa katika halmshauri kwa ajili ya kupambana na UKIMWI kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2012 kilikuwa ni Sh.4,754,901,000. Lakini Halmashauri hizo zinaonesha kukiri mapokezi ya Sh.4,677,058,271.52 hivyo kupelekea tofauti ya Sh.77,842,728 iliyohusisha Halmashauri 19 kati ya 56. Hii inaonesha kuwa fedha hizo hazikutolewa kwa mujibu wa mchanganuo uliotolewa na TACAIDS au zilirekodiwa vibaya. Hata hivyo, Halmashauri 37 zilirekodi kiwango sahihi kilichotolewa.

Hali hii inaashiria kuwa, hakuna mawasiliano ya karibu kati ya Mamlaka ya Serikali za mitaa na ofisi ya Mratibu wa kupambana na UKIMWI. Ninapendekeza kwamba, Menejimenti za Halmshauri zifanye usuluuhishi wa tofauti zilizojitokeza na ofisi ya mratibu wa Mpango wa kupambana na UKIMWI. Tazama **kiambatisho (xxvi)**.

5.6.2 Ruzuku ya Maendeleo Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGDG)

5.6.2.1 Fedha za Mradi

Ruzuku ya maendeleo kwa mamlaka ya Serikali za mitaa inachangiwa na wahisani wa maendeleo ikiwa ni pamoja na KFW, Irish, Uhlanzi, Benki ya Tokyo-Japan na Cooperation Tech Belgium kuititia akaunti namba 9931206651 iliyoko benki kuu ya Tanzania.

Katika mwaka huu wa fedha, Mpango ulikuwa na jumla ya dola za kimarekani (USD) 35,817,420 ambazo ni sawa na Sh.55,988,000,526 ambazo zilichangwa na wahisani wa maendeleo. Pia kulikuwa na mchango toka serikali ya Tanzania unaofikia Sh.18,440,000,000 hivyo kufanya mpango uwe na jumla ya Sh.74,428,000,526 kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyoidhinishwa.

Michango ya USD 35,817,420.29 sawa na Sh.55,988,000,526 uliotolewa na Wahisani kama ilivoonyeshwa hapa chini:

Jedwali Na. 39: Orodha ya Wahisani wa Maendeleo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

Na.	Mfadhili	Kiasi kwa USD	Kiasi (Sh.)
1	KFW	8,048,619	12,581,198,790
2	Irish	2,651,600	4,144,848,540
3	Netherlands	14,796,122	23,128,558,151
4	Benki ya Tokyo - Japan	1,201,126	1,877,539,560
5	Cooperation Tech. Belgium	9,119,954	14,255,855,485
Jumla		35,817,420	55,988,000,526

Hata hivyo, akaunti kuu namba 9931206651 kwa ajili ya fedha za ruzuku ya maendeleao ilikuwa na bakaa anzia la USD 20,583,777tarehe 1 Julai 2011 sawa na Sh.32,175,531,721.

Kwa kuongezea, Mpango wa Maendeleo wa sekta ya Afya ikiwa kama sehemu ya LGDG ilipokea jumla ya Sh.3,575,935,400 kutoka serikali ya Tanzania na hapakuwa na michango toka kwa Wahisani.

Katika mwaka huu wa fedha ambao unakaguliwa, kiasi cha USD 56,401,197.74 sawa na Sh. 88,163,532,247 zilipelekwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

5.6.2.2 Fedha za LGDG Zimetolewa Pungufu kwa Sh.

159,079,906,189

Ukaguzi wa fedha za LGDG unaonesha kuwa fedha zilizotolewa ni pungufu ikilinganishwa na kiasi kilichopangwa kama inavyoonyeshwa hapa chini:

Jedwali Na. 40 : Kiasi cha Ruzuku kilichotolewa pungufu

Na.	Mradi	Fedha iliyotengwa	Kiasi Kilichohamishwa (Sh)	Kiasi ambacho hakikutolewa (Sh)
1	LGDG CORE	198,094,400,000	106,603,480,500	91,490,919,500
2	HSDG	30,752,132,800	3,575,935,400	27,176,197,400
3	RWSSP	84,828,165,539	44,415,376,250	40,412,789,289
Jumla		313,674,698,339	154,594,792,150	159,079,906,189

Hali hii inaonesha kwamba kazi zilizotakiwa kufanyika hazikutekelezwa kikamilifu, hivyo malengo husika hayakufikiwa

5.6.2.3 Fedha za LGCDG ambazo haizikutumiwa na Halmashauri Sh.14,295,289,503

Katika mwaka huu wa ukaguzi, OWM-TAMISEMI kupitia Wizara ya Fedha ilipeleka juma ya Sh.106,603,480,500 katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ili kuwezesha shughuli za maendeleo. Ukaguzi wa matumizi ya fedha katika sampuli ya Halmashauri 74 umeonesha kuwa, kiasi cha Sh.14,295,289,503 kutoka akaunti za LGCDG ziliwuwa hazijatumika hadi tarehe 30 Juni, 2012 kama ilivyoonesha katika **Kiambatisho (xxvii)**.

Hali hii inaonesha kuwa, mipango mingi haikuweza kutekelezwa, kwa hiyo malengo husika hayakuweza kufikiwa. Tunashauri uongozi wa Halmashauri uchukue hatua za makusudi kutekeleza kazi zilizopangwa ili kufikia malengo yaliyowekwa.

5.6.2.4 Kutochangia asilimia 5% zinazotakiwa kuchangwa na Halmashauri kutokana na mapato ya ndani Sh.197,234,003

Sura ya 3.3 (ukurasa wa 17) ya Mwongozo wa matumizi na uendeshaji wa Fedha za Ruzuku kwa Mamlaka ya serikali za Mitaa, Toleo la 1 la Julai 2005 unazitaka Halmashauri kuchangia si chini ya asilimia tano ya fedha za ruzuku zilizopokelewa. Utaratibu huu ulianzishwa kwa sababu zifuatazo:

- Kuwezesha Halmashauri kuwa na umiliki wa miradi hiyo.
- Kuwa na uhusiano kati ya matumizi na faida inayotokana na matumizi hayo kwa huduma zitolewazo na Halmashauri.
- Kuhakikisha kuwa miradi inayotekelawa inakuwa endelevu.
- Kuweka mikakati ya kuongeza makusanyo ya maduhuli kutoka vyanzo vya ndani.
- Kuwezesha Halmashauri kuwa makini katika uwekezaji na utekelezaji wa miradi.

Hata hivyo, Halmashauri zifuatazo hazikuweza kukidhi matakwa ya kuchangia fedha kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 41: Orodha ya Halmashauri ambazo hazikuchangia 5% ya fedha zinazotakiwa kuchangwa na Halmashauri kutokana na mapato ya ndani

Na.	Halmashauri	Fedha ambazo hazikulipwa (Sh)
1	H/W Kibondo	71,303,226
2	H/W Singida	35,073,688
3	H/W Manyoni	19,320,074
4	H/W Iramba	71,537,015
Jumla		197,234,003

Hali hii ya kutochangia asilima tano inakwamisha utekelezaji wa miradi katika ngazi ya chini za serikali.

Tunashauri kwa uongozi wa Halmashauri husika kuhakikisha zinachangia asilimia tano ili kuweza kufanikisha utekelezaji wa miradi.

5.6.3 Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo.

Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo umeanzishwa kwa Sheria ya Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo Namba 16 ya mwaka 2009 kwa ajili ya miradi ya mandeleo katika majimbo. Mapato yote, matumizi na bakaa ya mwisho wa mwaka zinabaki katika Halmashauri husika kwa ajili ya shughuli zilizokusudiwa.

Katika mwaka huu wa Ukaguzi, Halmashauri 69 zilikuwa na masuala kuhusu matumizi na uwajibikaji ambayo yanahitaji ufuatiliaji kama ifuatavyo:

(a) Fedha za CDCF ambazo hazikutumika Sh.2,561,822,820

Katika baadhi ya Halmashauri, ilionekana kuwa, fedha za CDCF hazikutumika kabisa na zilibaki katika akaunti za Halmashauri. Kwa mfano katika sampuli ya Halmashauri 69 zaidi ya Sh.2,561,822,820 zilikuwa hazijatumika. Hii

imesababishwa na usimamizi hafifu wa menejimenti unaofanywa na Kamati ya mfuko wa Jimbo; kushindwa kutumia fedha hizo kumechelewesha jamii kunufaika na mfuko na hivyo malengo yaliyokusudiwa hayakutimia. Angalia **Kiambatisho (xxviii).**

Hii imesababishwa na kamati zilizoteuliwa kuendesha Mfuko kutokuwa na usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wa uendeshaji wa Mfuko. Na hii inapelekea malengo ya uanzishwaji wa Mfuko huo kutofikiwa.

Ulingenishi wa fedha zisizotumika kwa miaka miwili ni kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 42: Mwenendo wa fedha za CDCF ambazo hazikutumika

Mwaka	Fedha ambayo haikutumika (Sh.)	Idadi ya Halmashauri
2010/11	2,683,368,422	51
2011/12	2,561,822,820	69

Mipangilio mahsus inapaswa kufanywa kati ya Menejimenti za Halmashauri na kamati za uendeshaji za Mfuko ili kuangalia uwezekano wa kutumia fedha hizo katika miradi ya maendeleo ili kutimiza malengo ya uanzishaji wa mfuko huo.

(b) Kutoandaliwa kwa Taarifa za CDCF na kuziwasilisha OWM-TAMISEMI

Baadhi ya Halmashauri haziandai taarifa na kuziwasilisha kwa waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ikioneshwa fedha zilizopokelewa na zilizotumika. Hii ni kinyume na matakwa ya kifungu 7(3) ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo ya mwaka 2009.

Inashauriwa kwamba, OWM-TAMISEMI inapaswa kuhakikisha kuwa fedha kwa ajili ya mwaka unaofuata hazitolewi kama Halmsahauri husika haijawasilisha

taarifa ya mapato na matumizi. Katika mwaka huu wa fedha inaonekana kuwa Halmashauri 15 hazikuandaa taarifa na kuziwasilisha OWM-TAMISEMI kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 43: Orodha ya Halmashauri ambazo hazikuandaa taarifa na kuziwasilisha OWM-TAMISEMI

Na.	Jina la Halmashauri
1	H/W Masasi
2	H/W Hanang
3	H/W Mkinga
4	H/W Mtwara
5	H/M Mtwara
6	H/W Newala
7	H/W Nkasi
8	H/M Tabora
9	H/W Tandahimba
10	H/W Bariadi
11	H/W Bunda
12	H/W Maswa
13	H/W Urambo
14	H/M Musoma
15	H/W Mbarali

(b) Miradi ya CDCF ambayo haikuibuliwa na Wananchi Sh.71,687,000

Kifungu cha 12 cha 126 sheria ya Mfuko wa Jimbo ya mwaka 2009 kinaeleza kuwa, “orodha ya miradi inayoweza kutekelezwa na Mfuko inatakiwa kuibuliwa na wananchi ambao wanaishi katika jimbo husika”. Pia kifungu cha 10(4) kinaitaka kila kata kuja na miradi inayopewa kipaumbele na kuiwasilisha kwenye kamati ya Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya kuidhinisha au kutoidhinisha miradi hiyo:

Tofauti na matakwa ya vifungu hivyo, miradi yenye thamani ya Sh.71,687,000 iliyotekelizwa katika

Halmashauri zilizoorodheshwa hapa chini hazina ushahidi kwamba wananchi walihusika katika kuchagua miradi hiyo kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 44 : Orodha ya Halmashauri ambazo hazikuibuwa Miradi ya CDCF

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/Mji Korogwe	22,000,000
2	H/W Muheza	44,046,000
3	H/W Ukerewe	5,641,000
Jumla		71,687,000

Kamati ya Mfuko wa Jimbo inatakiwa kuidhinisha na kupeleka fedha kwenye miradi iliyoibuliwa na wananchi wenyewe.

Pia, kifungu cha 8 cha sheria ya mfuko wa Jimbo ya mwaka 2009 kinaneleza kuwa, mradi au sehemu yoyote ya mradi ambayo inatoa zawadi kwa mtu aidha kwa pesa taslimu au vifaa haitakiwi kuoneshwa kama sehemu ya fedha zilizotolewa kwenye Mfuko wa Jimbo.

Kinyume na matwaka ya sheria hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni imetoa jumla ya Sh.3,000,000 kusaidia klabu ya michezo ya Sumaria.

Tunashauri kamati za Mfuko wa Jimbo kuzigatia matakwa ya sheria ya Mfuko wa Jimbo.

- (d) **Malipo yaliyofanywa kutoka Mfuko wa Jimbo bila Kibali cha Kamati ya Mfuko Sh.34,341,000**

Kifungu 7 (1) cha Sheria ya Mfuko wa Jimbo ya mwaka 2009 kinaneleza kuwa, “kila mgawanyo na upelekaji wa fedha kutoka kwenye Mfuko wa Jimbo lazima upate idhini ya kamati ya Mfuko wa Jimbo”

Katika mwaka huu wa fedha, Halmashauri zifuatazo zilifanya malipo ya Sh.34,341,000, kwa ajili ya matumizi mbalimbali bila ya kuidhinishwa na kamati ya mfuko wa

Jimbo ikiwa ni kwenda kinyume na kifungu 7(1) cha Sheria ya Mfuko wa Jimbo ya mwaka 2009 kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 45 : Orodha ya Halmashauri zilizofanya
Malipo kutoka Mfuko wa Jimbo bila Kibali cha Kamati
ya Mfuko**

S/N	Jina la Halmashauri	Fedha ambayo haikutumika (Sh)
1	H/W Kilolo	1,924,000
2	H/M Mtwara	14,117,000
3	H/W Nzega	5,000,000
4	H/W Ruangwa	2,000,000
5	H/W Pangani	6,700,000
6	H/W Mbeya	4,600,000
Jumla		34,341,000

Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuhakikisha kuwa, malipo yote yanaidhinishwa na kamati ya mfuko wa Jimbo.

- (e) **Kuhamisha Fedha toka Mradi mmoja kwenda mwingine kinyume na maagizo ya Mfuko Sh. 65,627,714**
 Kifungu 5(6) cha Sheria ya Mfuko wa jimbo kinaeleza kuwa “mara fedha zinapotengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi kwenye jimbo, fedha hizo zitatakiwa kutumika katika kutekeleza mradi huo na hazitakiwi kuhamishwa au kutumika kwa madhumuni mengine katika jimbo”.
 Katika mwaka huu wa fedha, kamati za Mfuko wa Jimbo zilihamisha kiasi cha Sh.65,627,714 kwenda katika miradi mingine kama ilivyooneshwaha hapa chini:

**Jedwali Na. 46 : Orodha ya Halmashauri zilizohamisha
Fedha toka Mradi mmoja kwenda mwingine kinyume na
maagizo ya Mfuko**

Na.	Jina la Halmashauri	Miradi iliyoindhinishwa	Mradi uliotekelawa	Fedha zilizotengwa (Sh)

1	H/W Muheza	Ukarabati wa Barabara ya Kicheba-Jambe iliyopo kata ya Kicheba na Magila.	Ukarabati wa barabara ya Makole-Pangamilima katika kata ya Kwafungo	8,000,000
2	H/W Nkasi	Ujenzi wa Daraja la kuunganisha kijiji cha Mlambo na shule ya msingi Mlambo	Ujenzi wa Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji kata Sh.2,500,000 na ukarabati wa nyumba ya mwalimu na Sh.2,500,000	5,000,000
3	H/W Kasulu	Kwa ajili ya vijiji vya jimbo la Kasulu Sh.25,442,761 na Jimbo la Manyovu Sh.20,184,953	Miradi ya Jimbo la Kasulu Mjini	45,627,714
4	H/W Manyoni	Mradi wa Nyuki kijiji cha Damwelu	Kutengeneza madawati 40 ya shule ya msingi Damwelu (40)	2,000,000
5	H/W Manyoni	Ujenzi wa bweni shule ya sekondari Makuru	Umaliziaji wa madarasa shule ya msingi Mkuyuu.	5,000,000
Total				65,627,714

Ninashauri kamati za Mfuko wa jimbo ziisome na kuilewa Sheria inayoanzisha Mfuko wa jimbo ya mwaka 2009 na kanuni zake za mwaka 2010. Miradi iliyoidhinishwa inatakiwa kutengewa fedha na kutekelezwa kama ilivyopangwa.

5.6.4 Fedha za mpango maendeleo wa afya ya Msingi ambazo hazikutumika(MMAM) Sh.2,586,057,984

Ukaguzi wa fedha zilizopokelewa na kutumika kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa huduma ya afya ulionesha kiasi cha Sh. 2,586,057,984 kinachohusiana na Halmashauri 32 kilikuwa bado hakijatumika hadi tarehe 30 Juni, 2012 kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho (xxix)**.

Jedwali hapa chini linaonesha ulinganisho wa fedha ambazo hazikutumika kwa miaka miwili:

Jedwali Na. 47: Mwenendo wa fedha ambazo hazikutumika katika mradi wa MMAM

Mwaka	Fedha amabyo Haikutumika (Sh)	Idadi ya Halmashauri husika
2010/11	5,848,929,864	48
2011/12	2,586,057,984	32

Fedha ambazo hazikutumika zimeshuka kwa kiasi cha Sh.3,262,871,880 ambayo ni sawa na asilimia 55.8%. Lakini kiwango cha fedha ambacho hakijatumika bado ni kikubwa, kuwa na Sh.2.6 bilioni ina maana kazi zilizopangwa kutekelezwa hazikufanyika na kwa hiyo wananchi waliokusudiwa hawakuweza kunufaika na miradi hiyo.

5.6.5 (a) Fedha ambazo hazikupelekwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Wanawake Sh.511,761,787

Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Serikali Kuu zilianzisha Mfuko kwa ajili ya kuwezesha vikundi vya vijana na wakina mama kwa kuwapatia mikopo katika maeneo yao.

Wakati wa kuangalia uendeshaji wa Mfuko huo katika Halmashauri mbalimbali, ilibainika kuwa kiasi cha

Sh.511,761,787 zilikuwa hazijatolewa kama mkopo na Halmashauri 31. Hii ina maana kwamba Halmashauri husika haziko makini kuhakikisha kuwa mikopo inatolewa kwa vikundi husika.

Jedwali Na. 48: Orodha ya Halmashauri ambazo hazikupeleka fedha katika vikundi vyta maendeleo vya wanawake na vijana

Na.	Jina la Halmashauri	Fedha zisizotumika (Sh)
1	H/W Makete	11,922,700
2	H/W Handeni	11,067,742
3	H/W Ileje	11,039,345
4	H/W Mufindi	42,075,054
5	H/Jiji Mbeya	6,650,290
6	H/W Mkinga	2,741,953
7	H/W Mpwapwa	4,457,988
8	H/W Nachingwea	10,052,150
9	H/W Kyela	13,763,265
10	H/W Tabora	14,088,151
11	H/W Bukombe	1,326,150
12	H/M Shinyanga	8,056,667
13	H/W Lushoto	37,019,088
14	H/W Tunduru	14,307,988
15	H/W Karagwe	17,944,000
16	H/W Ngorongoro	59,655,689
17	H/W Kigoma	21,457,821
18	H/W Mbinga	9,048,338
19	H/W Meru	5,017,466
20	H/M Morogoro	6,502,929
21	H/W Namtumbo	404,400
22	H/W Pangani	1,387,756
23	H/W Rungwe	32,933,121
24	H/W Chato	20,032,500
25	H/W Misungwi	2,460,759
26	H/W Morogoro	2,592,000
27	H/W Mvomero	11,561,800
28	H/W Songea	29,754,932
29	H/W Sikonge	11,625,850
30	H/M Arusha	89,887,499
31	H/W Korogwe	2,656,946
Jumla		511,761,787

Jedwali hapa chini inaonesha mikopo ambayo haikutolewa kwa miaka 2

Jedwali Na. 49: Mwenendo wa fedha ambazo hazikupelekwa kwenye mfuko wa wanawake na vijana kwa miaka miwili

Mwaka	Fedha ambayo Haikutumika (Sh)	Halmashauri zilizohusika
2010/11	1,587,780,350	23
2011/12	511,761,787	31

Fedha ambazo hazikupelekwa kama mkopo katika mwaka wa fedha 2011/12 zilipungua kwa kiasi cha Sh.1,076,018,563 ambayo ni sawa 68%. Hii, inaonesha maendeleo katika usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo wa Vijana na Wanawake.

Taarifa hii inaweza kuonyeshwa kwenye chati mstatili kama ifuatavyo:



Pamoja na kwamba kuna maendeleo katika utoaji wa mikopo, lakini hali ya kuwa na kiasi kikubwa ambacho

hakijapelekwa kwenye vikundi vya Maendeleo wa Vijana na Wanawake inavinyima vikundi vya vijana na wanawake kupata manufaa yatokanayo na Mikopo hiyo.

Tunashauri kuwa Mamlaka ya serikali za mitaa zinatakiwa kuanzisha mikakati ya kutumia kiasi kilichopo kutoa mikopo kwa vikundi vikubwa ili kuviwezesha kujiendesha na kumudu maisha badala ya kubaki na kiasi kikubwa cha fedha kwenye akaunti za benki.

(b) Mikopo liyotolewa kwa vikundi vya kinamama na vijana bado kurejeshwa Sh.675,621,329

Ukaguzi katika Halmashauri 33 umeonesha kuwa na kiasi kikubwa cha mkopo ambacho hakijarudishwa kwa zaidi ya mwaka mmoja kinachofikia jumla ya Sh.675,621,329 kama inavyooneshwa hapa chini:

Jedwali Na. 50 : Orodha ya Halmashauri ambazo zina mikopo kwa ajili ya akina mama na watoto ambayo haijarejeshwa

Na	Jina la Hamashauri	Mkopo bado kurejeshwa (Sh.)	Na	Jina la Halmashauri	Mkopo bado kurejeshwa (Sh.)
1	H/W Makete	2,736,880	17	H/W Kahama	40,318,540
2	H/W Arusha	4,138,500	18	H/W Musoma	175,300
3	H/W Handeni	3,250,000	19	H/Mji Shinyanga	23,231,233
4	H/W Igunga	79,610,850	20	H/W Bukoba	9,850,000
5	H/W Ileje	5,592,000	21	H/W Maswa	37,051,273
6	H/W Karatu	14,036,817	22	H/W Rungwe	13,400,000
7	H/W Kilosa	25,285,000	23	H/W Biharamulo	1,930,000
8	H/W Mtwara	23,535,000	24	Mpanda H/W	24,400,000
9	H/Mji Mtwara	17,980,400	25	H/Mji Sumbawanga	15,017,600
10	H/W Muheza	5,762,350	26	H/Mji Bukoba	3,593,000
11	H/W Nachingwea	2,120,000	27	H/Mji Kigoma	29,364,511
12	H/W Nkasi	23,078,750	28	H/W Misenyi	25,548,875

13	H/W Mbozi	93,925,490	29	H/W Morogoro	3,000,000
14	H/W Kyela	35,267,000	30	H/W Mbalali	3,700,000
15	H/W Tabora	22,276,050	31	H/Mji Arusha	7,506,000
16	H/W Tandahimba	33,128,950	32	H/W Korogwe	20,305,160
			33	H/W Mwanga	25,505,800
				Total	675,621,329

Hii ina maana kuwa, juhudini zinazochukuliwa na uongozi wa Halmashauri katika kukusanya madeni hayo si za kuridhisha.

Menejimenti za Halmashauri zinatakiwa kuchukua hatua za makusudui katika kuelimisha na kukusanya madeni hayo kutoka kwa vikundi vya akina mama na vijana ili fedha za Mfuko huo ziweze kunufaisha makundi mengine.

5.6.6 Fedha za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ambazo hazikutumika Sh.305,361,658

Ukaguzi wa mapato na matumizi ya Fedha za MMEM ambazo zinatolewa kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa elimu na kuhakikisha wanafunzi hawaachi shule, inaonesha kuwa, kuna fedha ambazo hazikutumika kwenye Halmashauri tano zinazofikia jumla ya Sh.305,361,658 katika mwaka wa fedha 2011/2012 kama inavyoonekana hapa chini:

Jedwali Na. 51: Orodha ya Halmashauri zenyehi fedha za MMEM ambazo hazikutumika

Na.	Halmashauri	Fedha iliyopo (Sh)	Fedha iliyotumika (Sh)	Fedha ambayo haikutumika (Sh.)	% ya fedha isiyotumika
1	H/W Karatu	191,591,755	114,765,337	76,826,418	40.1%
2	H/Mji Iringa	41,630,267	8,512,000	33,118,267	79.6%
3	H/W Bariadi	209,070,777	110,867,008	98,203,769	47.0%
4	H/W Bukombe	129,734,088	39,461,883	90,272,205	69.6%
5	H/W Urambo	171,660,500	164,719,500	6,941,000	4.0%

Jumla	305,361,658	48%
-------	-------------	-----

Ulinganishi wa fedha ambazo hazikutumika kwa miaka miwili yaani 2010/11 na 2011/12 inaonesha kuwa kuna maendeleo kama inavyoonekana hapa chini:

Jedwali Na. 52: Mwenendo wa fedha za MMEM ambazo hazijatumika

Mwaka	Fedha isiyotumika	Idadi ya Halmashauri
2010/11	997,528,258	12
2011/12	305,361,658	5

Ingawa kuna maendeleo katika matumizi ya fedha, uongozi wa Halmashauri unashauriwa kuongeza juhudini katika kutumia fedha iliyotengwa katika kipindi husika ili kunufaisha wanafunzi.

5.6.7 Fedha za mradi shirikishi wa usimamizi wa misitu (PFM) ambazo hazikutumika Sh.32,366,811

Ukaguzi wa mapato na matumizi wa mradi shirikishi wa usimamizi wa misitu kwa mwaka wa fedha 2011/12 umeonesha kuwa na kiasi kisichotumika kinachofikia Sh.32,366,811 kwa halmashauri 9 kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini :

Jedwali Na. 53: Orodha ya Halmashauri ambazo hazikutumia fedha za PFM

Na.	Halmashauri	Fedha iliyopo	Fedha iliyotumika	Fedha ambayo haikutumika	% fedha isiyotumika
		(Sh)	(Sh)	(Sh)	
1	H/W Handeni	54,019,010	51,974,524	2,044,486	3
2	H/W Kilosa	95,905,011	94,042,870	1,862,141	2
3	H/W Liwale	11,820,000	7,049,000	4,771,000	40
4	H/Jiji Mbeya	35,115,395	27,589,240	7,526,155	21
5	H/W Lushoto	45,007,574	42,412,500	2,595,074	5
6	H/W Kilindi	50,039,165	48,824,780	1,214,385	2
7	H/W	23,881,273	16,379,450	7,501,823	31

	Morogoro				
8	H/W Songea	39,935,435	38,804,915	1,130,520	3
9	H/W Ulanga	50,553,897	46,832,670	3,721,227	7
	Jumla	406,276,760	373,909,949	32,366,811	13%

Jedwali hapa chini linaonesha ulinganisho wa fedha ambazo hazikutumika kwa miaka miwili ikiwa ni 2010/11 na 2011/12 kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 54 : Mwelekeo wa Halmashauri ambazo hazikutumia fedha za PFM

Mwaka	Fedha isiyotumika	Idadi ya Halmashauri
2010/11	178,826,876	11
2011/12	32,366,811	9

Fedha ambazo hazikutumika zimepungua kwa kiasi cha Sh.146,460,065 sawa na asilimia 82%. Katika mwaka wa fedha 2011/12 kulikuwa na maendeleo katika matumizi ya fedha za PFM. Uongozi wa Halmashauri uongeze juhudii za kutumia fedha a PFM katika muda uliopangwa.

5.6.8 Mfuko wa Afya ya Jamii

Mfuko wa Afya ya Jamii ulianzishwa mwaka 1997 ikiwa ni sehemu ya fedha zilizoainishwa na serikali kushawishi wananchi kuchangia katika sekta ya afya.

Makusanyo na matumizi kwa ajili ya mfuko huo yameainishwa bayana katika waraka namba 2 ya mwaka 1997 uliotolewa na Wizara ya afya ambao umeeleza kuwa fedha hizo zitatumika kununua dawa, vifaa vyta hospitali, matengenezo madogo, mafuta na posho ya safari. Waraka huo pia unaeleza kuwa madawa na vifaa vyta hospitali lazima vinunuliwe kwa wazabuni waliodhinishwa. Katika mwaka huu wa fedha, masuala yafuatayo yalioneekana katika usimamizi wa Mfuko:

(a) Fedha za mfuko wa Jamii ambazo hazikutumika Sh.1,709,747,559


Katika mwaka wa fedha uliokaguliwa tulifanya uhakiki katika usimamizi wa mfuko kwa sampuli ya Halmashauri 38, na tulibaini kuwa halmashauri hizi zina fedha ambazo hazikutumika zinazofikia Sh.1,709,747,559 iliyosababishwa na kutokufungua akaunti tofauti ya Mfuko na kuchelewa kutolewa kwa fedha hizo. Hii ina maana kuwa wananchi hawakuweza kupata huduma ya afya ambayo ingetolewa kuititia fedha hizo. Halmashauri zenyenye bakaa ni kama zinavyoonekana kwenye **Kiambatisho (xxx)**.

Jedwali hapa chini linaonesha fedha ambazo hazikutumika kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 55: Fedha za mfuko wa Jamii ambazo hazikutumika

Mwaka	Fedha isiyotumika (Sh)	Idadi ya halmashauri
2009/10	383,337,857	10
2010/11	2,963,900,725	33
2011/12	1,709,747,559	38

Maelezo hayo hapo juu yanaweza kuonekana kwenye chati mstari kama ifuatavyo:



Kutokana na jedwali na chati mstari hapo juu, fedha ambazo hazikutumika ziliongezeka kwa Sh.2,580,562,868 katika mwaka wa fedha 2009/10 hadi 2010/11 . Pia kutoka mwaka wa fedha 2010/11 kwenda 2011/12 zilipungua kwa Sh.1,254,153,166 ambayo ni sawa na asilima 42%.

Inashauriwa kuwa, Halmashauri zitekeleze kazi zilizopangwa zinazohusiana na sekta ya afya kwa mwaka husika ili kuongeza uwajibikaji kwa manufaa ya jamii husika.

(b) Malipo yaliyofanyika kinyume na waraka wa uendeshaji wa mfuko Manispaa ya Dodoma Sh.30,011,290

Mwongozo wa Mfuko wa afya ya Jamii wa Juni, 1999 unaeleza kwamba “fedha za Mfuko zitatumika kwa matumizi yanayohusiana na afya”. Matumizi yanayoruhusiwa ni pamoja na manunuzi ya dawa, vifaa vya hospitali, ukarabati wa miundombinu ya afya, sare za wauguzi, kulipa posho ya wataalam wanapo kuwa zamu, posho ya safari, na posho ya wauguzi kama zipo kwenye mpango wa afya wa kata.

Wakati wa ukaguzi, ilionekana kuwa kiasi cha Sh. 30,011,290 katika H/Mji Dodoma kilitumika kinyume na mwongozo wa Mfuko. Matumizi hayo yalikuwa kama ifuatavyo; Kiasi cha Sh.13,654,678 kililipa karadha ya mshahara kwa watumishi wapya na Sh.16,356,612 zilihamishiwa kwenye mfuko wa afya na akaunti ya amana kwa ajili ya matumizi mengine. Mpaka wakati wa Ukaguzi fedha hizi zilikuwa bado hazijarejeshwa katika Mfuko wa afya wa jamii.

Inashauriwa kuwa Halmashuri zitumie michango ya Mfuko wa Afya ya jamii kwa Madhumuni yaliyokusudiwa kama ilivyoelekezwa katika Waraka Na.2 wa mwaka 1997 uliotolewa na Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii.

(c) Madai ambayo hayajalipwa na bima ya afya Sh.321,247,691

Ukaguzi wa uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii, umeonesha kuwa katika Halmashuri kumi kuna madai yenye thamani ya Sh.321,247,691 ambayo hayajalipwa na Bima ya Afya kama marejesho kwa ajili ya huduma za afya zilizotolewa kwa wanachama wa Mfuko ambao pia ni wanachama wa Bima ya Afya kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 56 : Orodha ya Halmashauri ambazo zina Madai yasiyolipwa na bima ya afya

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi bado kulipwa(Sh)
1	H/W Kibondo	36,756,500
2	H/W Kilombero	1,507,443
3	H/W Kilosa	14,272,611
4	H/W Kyela	43,089,605
5	H/W Chunya	26,347,900
6	H/W Singida	1,945,398
7	H/W Kahama	24,170,998
8	H/W Maswa	16,482,864

9	H/W Iramba	148,266,000
10	H/W Meatu	8,408,372
	Jumla	321,247,691

Inashauriwa kuwa, uongozi wa Halmashauri ufanye ufuatiliaji wa karibu ili deni hilo liweze kulipwa na Mfuko wa Bima ya Afya.

5.6.9 Fedha za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) ambazo hazikutumika Sh.1,075,614,880

Wizara ya fedha ilipeleka fedha katika Mamlaka za Serikali za mitaa kwa ajili ya shughuli za MMES lengo ikiwa ni kuboresha elimu ya sekondari na kuongeza idadi ya wanafunzi.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa mapato na matumizi ya Halmashauri imebainika kuwa Halmashauri 12 zilipokea jumla ya Sh.3,348,375,155 na kati ya hizo, kiasi cha Sh.2,272,760,275 zilitumika na kuacha bakaa ya Sh.1,075,614,880ambayo ni sawa na asilimia 32% ya fedha iliyokuwepo kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 57 : Orodha ya Halmashauri ambazo zimesalia na fedha za MMES

Na.	Halma-shauri	Fedha iliyopo (Sh)	Fedha iliyotumika (Sh)	Fedha ambayo haikutumika (Sh)	% ya fedha ambayo haikutumika
1	H/W Karatu	425,886,289	197,945,818	227,940,471	53.5%
2	H/W Kilombero	388,864,000	234,683,484	154,180,516	39.6%
3	H/M Lindi	368,054,466	366,326,136	1,728,330	0.5%
4	H/W Liwale	687,351,169	628,628,012	58,723,157	8.5%
5	H/W Nachingwea	145,576,680	121,576,539	24,000,141	16.5%
6	H/W Bariadi	182,558,720	84,512,000	98,046,720	53.7%
7	H/W Bukombe	143,284,760	104,136,800	39,147,960	27.3%
8	H/W Musoma	155,600,000	105,600,000	50,000,000	32.1%

9	H/W Shinyanga	158,726,800	140,283,100	18,443,700	11.6%
10	H/W Serengeti	222,111,400	198,111,400	24,000,000	10.8%
11	H/M Moshi	270,878,283	0	270,878,283	100.0%
12	H/W Misungwi	199,482,588	90,956,985	108,525,603	54.4%
Jumla		3,348,375,155	2,272,760,275	1,075,614,880	31.4%

Jedwali lililopo hapa chini linaonesha mtiririko wa fedha ambazo hazikutumika kwa miaka 2 kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 58 : Mwelekeo wa fedha za MMES zilizosalia

Mwaka	Fedha ambayo haikutumika	Idadi ya Halmashauri
2010/11	724,673,833	11
2011/12	1,075,614,880	12

Jedwali hapo linaonesha kuwa, fedha ambayo haikutumika imeongezeka kwa kiasi cha Sh.350,941,047 katika mwaka 2011/12 sawa na asilimia 48.4%. Fedha nyingi iliyobaki inaonesha kuwa, baadhi ya kazi zilizotakiwa kufanyika aidha zimefanyika kidogo au hazikufanyika kabisa. Hii ina maana kuwa malengo hayakutimizwa na Halmashauri husika.

Menejimenti za Halmashauri husika ziongeze juhudi katika kutekeleza na kukamilisha miradi yote iliyopangwa.

5.7 Mapitio ya usimamizi wa Matumizi

5.7.1 Malipo yenge Nyaraka Pungufu Sh.3,367,208,321

Wakati wa ukaguzi wa kumbukumbu za matumizi katika sampuli iliyochaguliwa, matumizi yenge jumla ya Sh.3,367,208,321 yaliyohusiana na Halmashauri 74 yalikuwa na nyaraka pungufu kinyume na Agizo. 8(2)(c) na 104 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 ambayo inaagiza malipo yote yanayofanywa na Halmashauri yaambatanishwe na nyaraka sahihi. Halmashauri husika zimeorodheshwa katika **Kiambatisho (xxxii)**.


Malipo yaliyofanyika bila viambatisho yanakwaza mawanda ya ukaguzi katika kuhakiki uhalali wa malipo husika.

Malipo yenyne nyaraka pungufu kwa miaka mitano mfululizo 2007/08, 2008/09, 2009/10, 2010/11 na 2011/12 ni kama inavyoainishwa hapa chini:-

Jedwali Na. 59:Mwenendo wa malipo yenyne nyaraka pungufu

Mwaka wa Fedha	Kiasi (Sh.)	Idadi ya Halmashauri
2007/08	3,590,228,595	69
2008/09	2,526,117,587	33
2009/10	2,830,338,208	34
2010/11	5,692,624,802	63
2011/12	3,367,208,321	74

Taarifa hiyo inawezakuonyeshwa pia katika Chati Mistari zifuatayo:



Jedwali na chati mistari zilizotangulia inaonesha kwamba,

Kutoka mwaka 2007/08 hadi mwaka 2008/09 kiasi cha matumizi yasiyo na hati za malipo kilipungua kwa 29.6% pamoa na kupungua kwa idadi ya halmashauri husika kutoka 69 hadi 33.

Kutoka mwaka 2008/09 hadi mwaka 2009/10 kiasi cha matumizi yasiyo na hati za malipo kimeongezeka kwa 12% pamoja na ongezeko dogo la idadi ya halimashauri husika kutoka 33 hadi 34.

Kutoka mwaka 2009/10 hadi mwaka 2010/11 kiasi cha matumizi yasiyo na hati za malipo kiliongezeka kwa 101% pamoja na kuongezeka kwa idadi ya halmashauri husika kutoka 34 hadi 63.

Kutoka mwaka 2010/11 hadi mwaka 2011/12 kiasi cha matumizi yasiyo na hati za malipo kilipungua kwa 40.8% pamoja na kuongezeka kwa idadi ya halimashauri husika kutoka 63 hadi 74.

Halmashauri zinatakiwa kuimarisha mfumo wa udhibiti katika kuifadhi nyaraka zote zikiwemo zinazothibitisha malipo yaliyotolewa na uhalali wake ili kupunguza malipo yenye nyaraka pungufu na idadi ya Halmashauri zenyne matatizo ya kuwepo na Malipo yenye Nyaraka Pungufu.

5.7.2 Matumizi yasiyokuwa na hati za malipo

Sh.1,509,529,810

Jumla ya Sh.1,509,529,810 zilizotumika katika halmashauri 22 Kwa mwaka wa fedha 2011/12, hati za malipo pamoja na viambatanisho vya matumizi hayo havikupatikana kwa ajili ya ukaguzi, hivyo uhalali wa matumizi haya pamoja na uhalisia wa taarifa haukuweza kuthibitishwa kutoptana na kukwazwa kwa mawanda ya ukaguzi. Halmashauri husika ni kama zinavyoonyeshwa katika **Kiambatisho (xxxii)**.

Kutokuwepo kwa hati za malipo ni kinyume na Agizo Na.104 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009, ambayo kwa pamoja yanaelekeza kuwa hati za malipo pamoja na viambatisho vyake


vinatakiwa kuweka vizuri na kutunzwa kwa muda usiopungua miaka mitano (5).

Kwa muhtasari idadi ya Halmashauri zilizokuwa na matumizi yasiyokuwa na hati za malipo kwa miaka mitano mfululizo; 2007/08, 2008/09, 2009/10, 2010/11 na 2011/12 imeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 60: Mwenendo wa Matumizi yasiyokuwa na hati za malipo kwa miaka mitano mfululizo

Mwaka wa Fedha	Kiasi (Sh.)	Idadi ya Halmashauri
2007/08	1,370,245,729	45
2008/09	2,526,117,587	33
2009/10	2,830,338,208	34
2010/11	1,080,519,637	32
2011/12	1,509,529,810	22

Mwenendo wa Matumizi yasiyokuwa na hati za malipo kwa miaka mitano kama inavyoonekana hapo juu unaweza kuoneshwa katika chati mistari kama ifuatayo:



Kutokana na chati mistari iliyotangulia inaonekana kuwa:-
Kutoka mwaka 2007/8 hadi mwaka 2008/09 kiasi cha matumizi yasiyo na hati za malipo kimeongezeka kwa 84.4% pamoja na kupungua kwa idadi ya halmashauri husika kutoka 45 hadi 33

Kutoka mwaka 2008/09 hadi mwaka 2009/10 kiasi cha matumizi yasiyo na hati za malipo kimeongezeka kwa 12% pamoja na ongezeko dogo la idadi ya halimashauri husika kutoka 33 hadi 34

Kutoka mwaka 2009/10 hadi mwaka 2010/11 kiasi cha matumizi yasiyo na hati za malipo kimebungua kwa 61.8% pamoja na kupungua kwa idadi ya halmashauri husika kutoka 34 hadi 32

Kutoka mwaka 2010/11 hadi mwaka 2011/12 kiasi cha matumizi yasiyo na hati za malipo kimeongezeka kwa 39.7% pamoja na kupungua kwa idadi ya halimashauri husika kutoka 32 hadi 22

Kwa kuwa tatizo hili limekuwa likiendelea kujirudia katika Halmashauri nyingi kwa muda mrefu, napenda kuwakumbusha viongozi wa halmashauri juu ya wajibu wao wa msingi katika kuhakikisha kwamba, nyaraka zote muhimu za halmashauri zikiwemo hati za malipo ni vizuri kutunzwa, kulindwa na lazima zitolewe kwa ajili ya ukaguzi pindi zinapohitajika.

5.7.3 Kukosekana kwa stakabadhi za kukiri mapokezi kutoka kwa walipwaji Sh.650,356,980

Jumla ya Sh.650,356,980 kutoka Halmashauri 20 ambayo aidha yalilipwa moja kwa moja na Hazina ikiwa ni makato ya kisheria, au yalilipwa na Halmashauri hizo kwenda kwenye Taasisi mbalimbali kwa ajili ya huduma mbalimbali zilizotolewa na taasisi hizo, lakini malipo hayo hayakuweza kuthibitika kama yamepokelewa na Taasisi husika kwa kuwa stakabadhi/risiti ya kukiri kupokea kiasi hicho cha

fedha hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hii inapingana na Agizo Na. 8(2)(c) la Memoranda ya fedha za Serikali za Mitaa la mwaka 2009.

Jedwali Na. 61: Idadi ya Halmashauri ambazo stakabadhi za kukiri mapokezi kutoka kwa walipwaji zilikosekana

Na.	Jina la Halmashauri husika	Kiasi (Sh.)
1	H/M Kinondoni	191,051,000
2	H/M Dodoma	173,029,081
3	H/W Songea	77,561,638
4	H/W Ilala	48,325,645
5	H/W Korogwe	32,905,750
6	H/W Rungwe	23,232,489
7	H/W Karagwe	17,196,071
8	H/W Urambo	16,815,967
9	H/W Handeni	16,025,177
10	H/W Sumbawanga	15,704,189
11	H/W Meru	6,099,397
12	H/W Kibondo	5,615,325
13	H/W Karatu	5,474,706
14	H/M Musoma	5,150,000
15	H/W Kiteto	4,500,000
16	H/W Mpwapwa	3,777,236
17	H/W Pangani	3,403,121
18	H/W Kilindi	2,173,877
19	H/W Nkasi	1,580,843
20	H/M Songea	735,467
Total		650,356,980

Kukosekana kwa nyaraka za kukiri mapokezi kunakwaza mawanda ya ukaguzi katika kuthibitisha matumizi katika vifungu husika na uhalisia wa malipo.

Tatizo hili limekuwa likijirudia mara kwa mara katika halmashauri nyingi licha ya kupendekeza mara nyingi juu ya suala hilo, Hivyo napenda kuwakumbusha viongozi wa

Serikali za Mitaa juu ya wajibu wao katika kuhakikisha kwamba, kila Halmashauri inatunza, inalinda nyaraka vizuri na lazima zitolewe kwa ajili ya ukaguzi pindi zinapohitajika.

5.7.4 Matumizi yaliyofanywa kwa kutumia vifungu visivyohusika Sh.1,577,463,978

Kinyume na Kifungu 43(5) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, 1982 (Iliyorekebishwa 2000), matumizi ya jumla ya Sh.1,577,463,978 kutoka Halmashauri (41) kama zilivyoainishwa katika jedwali lifuatalo yalilipwa kwa kutumia vifungu visivyohusika bila kibali cha kamati ya fedha kuidhinisha ili fedha zihamishwe kwenda vifungu vingine.

Jedwali Na. 62: Idadi ya halmashauri yaliyofanya matumizi kwa kutumia vifungu visivyohusika

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/M Dodoma	694,718,508	21	H/W Sumbawanga	13,503,500
2	H/M Morogoro	116,316,508	22	H/W Babati	12,260,000
3	H/Jiji Mbeya	98,877,546	23	H/W Meru	10,490,000
4	H/M Arusha	87,636,749	24	H/W Mbinga	10,459,000
5	H/W Muheza	66,352,537	25	H/W Kyela	9,987,700
6	H/W Handeni	57,811,233	26	H/W Mbeya	8,770,360
7	H/W Magu	51,941,300	27	H/W Urambo	7,225,000
8	H/M Temeke	41,144,717	28	H/W Rungwe	7,065,689
9	H/Mji Korogwe	30,956,984	29	H/W Simanjiro	6,422,600
10	H/W Sengerema	24,182,470	30	H/W Mufindi	5,712,479
11	H/Jiji Mwanza	22,459,297	31	H/W Nzega	5,277,000
12	H/W Kiteto	22,450,500	32	H/W Shinyanga	4,782,000
13	H/W Bukoba	21,637,432	33	H/W Mvomero	4,770,000
14	H/W Songea	21,632,734	34	H/W Biharamulo	3,540,000
15	H/W Korogwe	17,602,026	35	H/Mji Njombe	3,538,898
16	H/W Chamwino	16,652,312	36	H/W Morogoro	2,430,000

17	H/W Mbulu	16,318,525	37	H/W Monduli	1,642,373
18	H/W Makete	16,310,000	38	H/W Namtumbo	1,624,500
19	H/W Misungwi	15,831,500	39	H/M Songea	1,130,000
20	H/W Kilwa	14,440,000	40	H/W Ukerewe	960,000
			41	H/W Mkinga	600,000
	Total				1,577,463,978

Hii ina maana kwamba, kuna miradi na kazi zilizopangwa na kupitishwa zenyet thamani ya Sh.1,577,463,978 ambazo hazijatekelezwa.

Jambo hili bado linaendelea kuonekana katika halmashauri mbalimbali na kusababisha makosa ya taarifa ya hesabu za halmashauri, napenda kushauri Serikali za Mitaa juu ya wajibu wao katika kuhakikisha halmashauri inaimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani ilikuwawezesha kuandaa taarifa za hesabu ambazo hazina makosa na pia kufuata mwongozo wa bajeti.

5.7.5 Matumizi yaliyofanywa nje ya Bajeti iliyoidhinishwa

Sh.1,688,848,579

Katika Ukaguzi wa mwaka wa fedha 2011/12, matumizi ya kiasi cha Shs.1,688,848,579 yalifanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa kinyume na kifungu Na. 10 (3) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Namba 9 ya mwaka 1982 (Iliyorekebishwa 2000).

Matumizi hayo yalifanywa na Halmashauri (38) kama zilivyoorodheshwa hapa chini:-

Jedwali Na. 63: Idadi ya halmashauri yaliyofanya matumizi nje ya bajeti iliyoidhinishwa

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Mbarali	482,830,864	20	H/W Kongwa	13,471,700
2	H/W Singida	427,692,000	21	H/M Sumbawanga	10,975,000
3	H/W Kyela	133,373,820	22	H/W Karatu	10,428,800
4	H/W Kahama	101,022,311	23	H/W Illeje	8,330,000
5	H/W Kishapu	85,154,180	24	H/M Lindi	7,985,500

6	H/W Meatu	46,352,000	25	H/W Kwiimba	7,373,700
7	H/W Kilwa	34,819,896	26	H/W Misungwi	7,250,000
8	H/M Singida	34,011,368	27	H/Jiji Mbeya	6,578,800
9	H/W Kasulu	31,596,989	28	H/W Mbulu	6,418,000
10	H/Mji Njombe	23,250,000	29	H/M Kigoma	5,915,000
11	H/W Manyoni	23,189,400	30	H/M Bukoba	5,567,000
12	H/W Mbeya	23,163,051	31	H/W Mvomero	4,660,000
13	H/W Bukombe	21,491,800	32	H/W Mpanda	3,888,000
14	H/W Rufiji	21,367,750	33	H/W Namtumbo	3,459,100
15	H/W Mbinga	20,000,000	34	H/W Same	2,940,000
16	H/W Makete	19,300,000	35	H/W Nkasi	2,340,000
17	H/M Morogoro	18,365,000	36	H/W Ludewa	1,800,000
18	H/W Hanang	15,626,550	37	H/W Ruangwa	1,624,000
19	H/W Kilosa	13,767,000	38	H/W Shinyanga	1,470,000
Total					1,688,848,579

Mlinganisho wa Matumizi yaliyofanywa nje ya Bajeti iliyoidhinishwa kwa miaka miwili ni kama ilivyoainishwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 64: Mlinganisho wa matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa

Mwaka wa Fedha	Kiasi (Sh.)	Idadi ya Halmashauri
2010/2011	549,421,946.00	9
2011/2012	1,688,848,579.17	38

Jedwali hapo juu linaonyesha kwamba, tatizo la matumizi kufanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa limeongezeka kwa kiasi cha Sh.1.1bil kutoka Halmashauri 38. Hivyo, menejimenti ya halmashauri husika zinashauriwa kufuata sheria na muswada wa fedha kama zinavyopitishwa na bunge

5.7.6 Uhamisho wa ndani wa fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njiaya mikopo ambayo haijarejeshwa Sh.2,673,964,170

Ukaguzi wa malipo na kumbukumbu za nyaraka za malipo katika sampuli ya Halmashauri (45) ulifanyika na kubaini kwamba kulifanyika uhamisho wa ndani wa fedha kiasi

cha Sh.2,673,964,170 kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ndani ya halmashauri hizo ambazo hazikurejeshwa hadi mwisho wa mwaka wa fedha wa 2011/2012 kinyume na Agizo Na. 23 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

Halmashauri zilizohusika ni kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 65: Idadi ya halmashauri zilizofanya uhamisho wa ndani wa fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ambazo hazijarejesha

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Mbarali	465,532,500	24	H/W Nkasi	16,779,500
2	H/W Mbozi	421,069,560	25	H/M Dodoma	16,356,612
3	H/W Kasulu	326,048,600	26	H/Mj wa Babati	15,000,000
4	H/M Kigoma	182,620,000	27	H/W Meatu	14,967,232
5	H/W Bariadi	137,104,348	28	H/W Kondoa	14,537,000
6	H/W Masasi	135,000,709	29	H/Mj wa Njombe	11,000,000
7	H/W Morogoro	120,038,000	30	H/W Illeje	10,900,000
8	H/W Mbulu	119,783,000	31	H/W Mwanga	10,599,000
9	H/W Manyoni	78,355,049	32	H/W Mpanda	10,212,000
10	H/W Maswa	67,600,000	33	H/W Ludewa	10,000,000
11	H/Mji Mpanda	62,500,000	34	H/W Kiteto	10,000,000
12	H/W Kishapu	52,663,800	35	H/W Tunduru	10,000,000
13	H/W Misungwi	51,818,000	36	H/W Mvomero	9,867,710
14	H/W Kilosa	44,090,000	37	H/W Kwigoma	8,070,000
15	H/W Iramba	31,000,000	38	H/W Karagwe	7,921,300
16	H/W Sumbawanga	26,774,700	39	H/W Tandahimba	7,600,000
17	H/Jiji Mbeya	25,000,000	40	H/M Bukoba	5,243,000
18	H/W Bukoba	24,125,000	41	H/W Kilolo	5,226,360

19	H/W Kibondo	23,098,990	42	H/W Bahi	4,500,000
20	H/W Biharamulo	22,659,900	43	H/W Bukombe	1,990,000
21	H/W Sengerema	18,500,000	44	H/W Karatu	1,397,300
22	H/W Mufindi	18,415,000	45	H/W Ngara	500,000
23	H/W Handeni	17,500,000			
Total					2,673,964,170

Mlingano kati ya Uhamisho wa ndani kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo kwa miaka miwili mfululizo ni kama inavyo ainishwa katika jedwali lifuatalo;

Jedwali Na. 66: Mlingano wa uhamisho wa ndani wa fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ambayo hajarejeshwa

Mwaka wa Fedha	Kiasi (Sh.)	Idadi ya Halmashauri
2010/11	750,621,650	20
2011/12	2,673,964,170	45

Jedwali hapo juu linaweza kuoneshwa katika chati mstari kama ifuatavyo;



Jedwali na chati hapo juu inaonesha kwamba, uhamisho wa ndani wa fedha kutoka akaunti moja kwenda akaunti nyingine umeongezeka kwa Sh.1.9bil kutokana na ongezeko la halmashauri 25 zenyenye matatizo na uhamishaji usiofuata sheria.

5.7.7 Madai ya miaka ya nyuma Sh.348,701,810


Katika mwaka husika wa ukaguzi, ilibainika kwamba kiasi cha Sh.348,701,810 katika Halmashauri 32 kilitakiwa kilipwe katika mwaka wa fedha 2010/11, lakini malipo hayo yamefanyika katika mwaka wa fedha 2011/12 kinyume na Agizo Na. 22(1) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2009. Pia hakuna uthibitisho kuwa malipo hayoyalioneshwa katika orodha ya wadai wa Halmashauri katika mwaka wa fedha 2010/11. Mchanganuo ni kama ulivyooneshwa katika **Kiambatisho (xxxiii)**.

Mwelekeo wa malipo ya Madai ya miaka ya nyuma bila kufuata sheria kwa miaka mitano mfululizo; 2007/08, 2008/09, 2009/10, 2010/11 na 2011/12 ni kama inavyoidhinishwa katika jedwali lifuatalo;

Jedwali Na. 67: mwelekeo wa malipo ya madai ya miaka ya nyuma

Mwaka wa Fedha	Kiasi (Sh.)	Idadi ya Halmashauri
2007/08	754,886,927	23
2008/09	725,288,165	36
2009/10	620,278,565	24
2010/11	412,414,001	24
2011/12	348,701,810	32

Jedwali lililotangulia linaweza kuoneshwa katika chati mistari zifuatazo;



Kama ilivyoainishwa katika chati mistari iliyotangulia, kutoka mwaka 2007/08 hadi 2011/12 kiasi cha malipo ya madai ya miaka ya nyuma yamekua yakipungua kwa uwiano wa asilimia 16.8% huku idadi ya halmashauri ikiongezeka kwa 13 kutoka mwaka 2007/08 hadi 2008/09, kupungua kwa idadi ya halmashauri kwa 12 kutoka mwaka 2008/09 hadi 2009/10 na kuongezeka kwa uwiano kwa idadi ya halmashauri kwa 8 kutoka mwaka 2009/10 hadi 2011/12

Hivyo Uongozi wa Halmashauri husika unashauriwa kuonesha madeni yote ya miaka iliyopita katika rejestra ya madai na taarifa za fedha

5.8 Madeni na Miadi Sh.8,698,124,431

Halmashauri kwa Uwezo wake wa kisheria zinaweza kushitaki au kushtakiwa. Katika mwaka wa fedha 2011/12 imebainika kuwa halmashauri 18 zimekuwa na kesi mbalimbali za kisheria zenye jumla ya Sh.8,698,124,431 ambazo karibu zote ni kesi za madai ambapo matokeo yake hayawezi kutabirika na vile vile kukadirika. Halmashauri husika zimeorodheshwa katika **Kiambatisho** (xxxiv).

Mlingano wa madeni ya kesi mbalimbali za kisheria kwa miaka miwili mfululizo 2010/11 and 2011/12 ni kama inavyoainishwa katika jedwali lifuatalo;

Jedwali Na. 68: Mlingano wa madeni ya kesi za sheria kwa miaka miwili

Na.	Mwaka	Madeni ya kesi za kisheria (Sh.)
1.	2010/2011	5,852,750,556
2.	2011/2012	8,698,124,431

Jedwali lililotangulia linaweza kuoneshwa kwa kutumia milinganyo duara ifuatayo;



Milinganyo duara iliyotangulia inaashiria kuwa Kumekua na ongezeko la kesi za kisheria zenyet thamani ya Sh.2.8bil kutoka mwaka 2010/11 hadi 2011/12

Kesi zingine hazisimamiwi vizuri na uongozi wa halmashauri husika na kusababishia halmashauri hasara.

Pia halmashauri inakuwa katika hatari ya kuingia gharama batili kutohana na faini ambazo zinaweza kuepukika.

5.9 Masuala Mengine

5.9.1 Ucheleweshaji wa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi kwa mwaka 2010/2011

Kufuatia makubaliano kati ya TAMISEMI, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Bunge katika ukaguzi wa miradi iliyotekelizwa na Halmashauri, Katibu Mkuu wa OWM - TAMISEMI aliamua kutoa maelekezo kwa

barua yenye Kumb. Na.2/CA.26/215/01/1 ya tarehe 10 Novemba, 2010 ambayo inawataka Maafisa Masuuli wote kuandaa taarifa za utekelezaji wa mradi kwa kufuata mwongozo wa taarifa zinazopelekwa mbele ya Kamati ya Bunge ya hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na kuziwasilisha pamoja na hesabu zamwisho kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa ajili ya ukaguzi kabla au tarehe 30 Septemba ya kila mwaka wa fedha.

Katika sampuli iliyochaguliwa, Halmashauri tano (5), ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Halmashauri ya Wilaya ya Tabora, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Halmashauri ya Wilaya ya Songea na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa hazikuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi ya maendeleo kinyume na maelekezo yaliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI.

Kati ya halmashauri zilizopitiwa; Halmashauri Kumi (10) ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo, Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Halmashauri ya Wilaya Lindi na Halmashauri ya Wilaya ya Meatu hazijawasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi kinyume na maelekezo yaliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI.

Halmashauri Kumi na moja (11) hazikuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mradi yao ndani ya tarehe ya kisheria (kabla au 30 Septemba, 2012) na kuchelewa kwa kipindi kati ya siku 11-110; Halmashauri ya wilaya ya Kasulu, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ziliwasilisha taarifa za utekelezaji wa miadi yao chini ya kiwango ukilinganisha mpango unaohitajika na kupitishwa na

Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Orodha ya Halmashauri ambazo hazijawasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi yao katika muda uliopangwa ni kama ifuatayo;

**Jedwali Na. 69: idadi ya Halmashauri zilizochewesha
kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi**

Na.	Jina la Halmashauri	Tarehe ya Kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji	Siku za ziada
1.	H/W Mpwapwa	11-10-12	11
2.	H/M Morogoro	03-11-12	33
3.	H/W Ulanga	25-11-12	55
4.	H/W Morogoro	25-11-12	55
5.	H/W Mvomero	26-11-12	56
6.	H/W Kahama	29-11-12	59
7.	H/W Tabora	21-12-12	81
8.	H/W Chamwino	27-12-12	87
9.	H/W Bariadi	31-12-12	91
10.	H/W Kondoa	02-01-13	93
11.	H/W Kishapu	19-01-13	110

Kwa Halmashauri ambazo hazikuwasilisha ripoti husika, ukaguzi hakuweza kuthibitisha uhalali wa taarifa zao kama inaonesha uhalisia. Hii inamaanisha kuwa Halmashauri husika hazikufuata maelekezo yaliyotolewa na serikali kuititia Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI.

5.9.2 Utekelezaji wa Kilimo Kwanza

Kilimo Kwanza ni kauli mbiu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inalenga kufufua na kuendeleza sekta ya kilimo kwa mfumo wa utekelezaji nguzo za Kilimo Kwanza ambazo hutekelezwa na wadau mbalimbali muhimu ambao ni pamoja na Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji ambazo zipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Ukaguzi na tathmini ya utekelezaji wa "Kilimo Kwanza" katika ulibaini madhaifu mbalimbali ambayo yanakwamisha utekelezaji wa Kilimo Kwanza:

- Kuchelewa kutolewa kwa vocha za pembejeo kutoka Wizara ya Kilimo,
- Uchaguzi wa Mawakala wa Pembejeo za Kilimo wasiofaa katika ngazi ya Halmashauri,
- Matumizi ya vocha za ruzuku ya pembejeo za kilimo chini ya kiwango kilichokuwa kinatakiwa,
- Kuchelewa kwa Wakala kusambaza Vocha za pembejeo za Kilimo kwa wakulima,
- Wizi na uharibifu wa Vocha za pembejeo kilimo,
- Ukosefu wa semina kwa Halmashauri za vijiji na Kamati za vijiji za vocha za pembejeo,
- Ukosefu bajeti zilizo tengwa kwa ajili ya usimamizi katika idara ya Kilimo.

Maelezo zaidi yameoneshwa katika **Kiambatisho (xxxv)**.

Ili kufikia malengo ya Kilimo Kwanza ninapendekezayafuatayo:

- Menejimenti za Halmashauri lazima zihakikishe kuwa mawakala wanawajibika kusambaza pembejeo za kilimo kulingana na mikataba yao,
- Uongozi wa Halmashauri kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo zinapaswa kuhakikisha kuwa pembejeo za kilimo zinatolewa kwa wakati na kulingana na mahitaji ili kuchochaea kilimo ndani ya Halmashauri,
- Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inapaswa kutenga bajeti ya kutosha ili kuwezesha usimamizi na kuhakikisha kuwa utekelezaji unafanyika kwa wakati na kwa ufanisi,
- Kamati husika inatakiwa kuanzisha mikakati ya kudhibiti na kufuatilia kwa karibu vocha za kilimo na kuhakikisha kuwa, hatua za kisheria zinachukuliwa

dhidi ya wale wote ambao watasababisha hasara na uharibifu.

- Menejimenti za Halmashauri lazima zihakikishe kwamba, Serikali za vijiji na wakulima wanapata mafunzojuu ya jinsi ya kutumia mfumo wa vocha za pembejeo za kilimo kabla ya utekelezaji wake

SURA YA SITA

6.0 USIMAMIZI WA MIKATABA NA UZINGATIAJI WA TARATIBU ZA MANUNUZI

6.1 Usimamizi wa mikataba na uzingatiaji wa taratibu za manunuizi

Sheria ya Manunuizi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 kifungu cha 3(1) kimefafanua manunuizi kama mchakato wa kununua, kukodisha, au vinginevyo kupata bidhaa na huduma yoyote au kazi za ujenzi unaofanywa na taasisi inayonunua kwa kutumia fedha za umma na mchakato huo unahusisha kazi zote za kutoa maelezo ya mahitaji, maandalizi ya zabuni, kufanya uteuzi wa mzabuni au mkandarasi na hatimaye kuandaa na kutoa mkataba. Kutokana na ukweli kwamba kiasi kikubwa cha rasilimali za Serikali huelekezwa katika ununuizi wa bidhaa na huduma, kuna haja ya kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha na uwazi katika ngazi zote za mchakato wa ununuizi kwa ajili ya kupata thamani ya matumizi ya fedha za umma.

6.2 Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za manunuizi

Kifungu cha 44(2) cha Sheria ya Manunuizi ya Umma ya mwaka, 2004 na kanuni ya 31 ya Kanuni za Manunuizi ya Umma (Vifaa, ujenzi na huduma zisizo za ushauri, kuuza mali za umma kwa Zabuni) za mwaka 2005 zinanitaka kueleza katika ripoti yangu ya mwaka kama taasisi niliyoikagua imezingatia sheria na kanuni za manunuizi. Kwa kuzingatia jukumu hili katika taasisi za manunuizi ikiwa ni pamoja na Halmashauri, ninaweza kusema kwa ujumla kuwa hali ya uzingatiaji wa sheria ya manunuizi na kanuni zake bado si ya kuridhisha.

6.3 Ufanisi wa Kitengo cha Usimamizi wa Manunuizi (PMU)

Kifungu cha 34 cha Sheria ya Manunuizi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 na kanuni ya 22 ya Kanuni za Bodi ya Zabunikwa Serikali za Mitaa ya 2007, inazitaka taasisi

zinazofanya manunuzi zianzishe kitengo cha usimamizi wa manunuzi kilicho na wajumbe wa kutosha. Kitengo hiki kinatakiwa kuwa na wataalamu wa manunuzi na wataalamu wenye fani mbalimbali wakisaidiwa na watumishi wa utawala.

Mapitio ya ufanisi wa utendaji kazi wa vitengo nya manunuzi kwa mwaka huu katika Halmashauri mbalimbali vimeonesha kuzorota ikilinganishwa na miaka iliyotangulia. Katika ukaguzi wa mwaka huu, Halmashauri 63 zilibainika kuwa na vitengo nya manunuzi visivyo na ufanisi wa kuridhisha ukilinganisha na Halmashauri 35 zilizoripotiwa katika mwaka wa fedha uliopita. Udhafu uliobainika ni pamoja na manunuzi ya bidhaa kupitia masurufu kinyume na agizo la 69(1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009; manunuzi ambayo hayakuwa kwenye mpango wa manunuzi kinyume na kifungu 45(b) cha sheria za manunuzi (2004) na kifungu 46(9) cha kanuni za manunuzi ya umma ya mwaka 2005. Mapungufu mengine yalikuwa kwenye manunuzi ya huduma na bidhaa ambayo yamefanyika kabla ya kuidhinishwa hati ya manunuzi/mikataba midogo (LPO) kinyume na Agizo 69 (1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009, vilevile Halmashauri hizi zilionekana kuwa na mapungufu ya kutokuanzishwa kwa bodi za zabuni na vitengo nya usimamizi wa manunuzi kinyume cha vifungu 33 na 34 nya sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2004; kutawanya manunuzi kwa lengo la kukwepa manunuzi kwa njia ya kushindanisha zabuni ambapo ni kinyume na kifungu 45(b) cha sheria za manunuzi, 2004 na Kanuni ya 49(1) ya kanuni za manunuzi ya 2005; kuongeza kazi katika mikataba kusikoidhinishwa na bodi ya zabuni kinyume na sheria 117(2) ya kanuni za manunuzi ya 2005.

Kiambatisho(xxxvi).

Sababu kubwa yakutozingatiwa kwa kanuni ya manunuvi ya umma ya mwaka 2005 na sheria ya manunuvi ya (2004) pamoja na Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 ni kutokuanzishwa kwa bodi za zabuni na vitengo vya usimamizi wa manunuvi na hata vile vilivyopo kutokuwa na idadi ya kutosha ya watumishi na baadhi ya wajumbe wa bodi za zabuni na vitengo vya usimamizi wa manunuvi hawana sifa stahiki zinazohusiana na manunuvi.

6.4 Tathmini ya usimamizi wa mikataba na ununuvi wa bidhaa, kazi za ujenzi, na huduma katika Serikali za Mitaa

Aya hii inafafanua kwa ujumla masuala ya uzingatiaji wa Sheria ya Manunuvi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2005, pia Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Aya hii inahusika pia na usimamizi wa mikataba na masuala ya uzingatiwaji wa sheria ya manunuvi ya umma ambayo yalionekana kuwa ya msingi na muhimu kuripotiva katika taarifa hii na taarifa za ukaguzi zilizotolewa kwa kila Halmashauri husika katika mwaka wa fedha 2011/2012. Tathmini yangu kwa ujumla juu ya uzingatiaji sheria tajwa hapo juu ilibainisha mapungufu yafuatayo:

a) Ununuvi wa bidhaa na huduma bila kuidhinishwa na Bodi ya ZabuniSh.541,013,405

Kifungu cha 7 cha sheria za Bodi za Zabuni ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, kanuni GN Na. 177 iliyochapishwa tarehe 03/08/2007 na kifungu cha 34 cha sheria za Manunuvi ya Umma ya mwaka 2004 inazitaka Halmashuri kuwa na Bodi za Zabuni. Kanuni za Bodi za Zabuni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliundwa ili kuhakikisha kuwa thamani ya fedha na ubora wa bidhaa na huduma zinazonunuliwa na Halmashauri vinapatikana. Ukiachilia mbali uzingatiaji wa sheria na kanuni za manunuvi thamani ya fedha pia haikupatikana kama ilivotorajiwa.

Hata hivyo, kinyume na sheria zilizotajwa hapo juu katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2011/12 ilibainika kuwa Halmashauri ishirini na nne (24) zilifanya manunuvi ya jumla ya Sh.541,013,405 bila kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni. Orodha ya Halmashauri hizo zimeoneshwa hapo chini:

Jedwali Na. 70: Orodha ya Halmashauri ambazo zilifanya manunuvi ya Bidhaa na Huduma bila kuithinishwa na Bodi ya Zabuni

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Mafia	9,320,000
2	H/W Makete	44,450,000
3	H/Wa Mufindi	192,969,715
4	H/Mji Njombe	10,000,000
5	H/W Biharamulo	13,675,000
6	H/M Bukoba	10,000,000
7	H/W Missenyi	20,812,965
8	H/W Chato	3,090,000
9	H/W Kibondo	23,800,000
10	H/W Nachingwea	15,824,532
11	H/W Ruangwa	15,410,890
12	H/W Hanang'	7,078,600
13	H/W Kyela	30,840,800
14	H/W Rungwe	16,731,000
15	H/W Kilombero	3,200,000
16	H/W Ulanga	29,519,000
17	H/W Mvomero	3,120,000
18	H/M Mtwara	16,843,600
19	H/W Kwimba	9,413,875
20	H/M Songea	5,311,200


21	H/W Songea	21,468,000
22	H/W Namtumbo	3,200,000
23	H/W Manyoni	27,475,100
24	H/Jiji la Tanga	7,459,128
	Jumla	541,013,405

Mchanganuo wa manunuzi ambayo hayakuidhinishwa na Bodi ya Zabuni kwa miaka miwili ni kama ufuatavyo:

Jedwali Na. 71: Mwenendo wa Ununuzi wa Bidhaa na Huduma uliofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni

Mwaka	Kiasi ambacho hakikuidhinishwa na Bodi ya Zabuni	Idadi ya Halmashauri
2010/11	239,984,297	7
2011/12	541,013,405	24

Uchambuzi huo hapo juu unaweza kuonyeshwa katika chati ya mstari kama ifuatavyo:-



Kutokana na jedwali na grafu hapo juu, inaonesha kuwa kiasi kisicho idhinishwa na Bodi ya Zabuni kiliongezeka kwa Sh.301,029,108 kutoka mwaka 2010/2011 hadi

mwaka 2011/2012 sawa na 125%. Hivyo kiasi kikubwa kinaonesha kuna ongezeko kubwa la idadi ya Halmashauri ambazo zilifanya manunuzi bila kupata kibali cha Bodi ya Zabuni.

Mbali na Halmashauri hizo kutozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma, vilevile hapakuwa na thamani ya fedha iliyopatikana kwenye manunuzi haya.

- b) **Manunuzi ya bidhaa na huduma yaliyofanywa kutoka kwa watoa huduma za ugavi wasiothibitishwa Sh.375,057,680**

Kifungu cha 67(3) cha kanuni za manunuzi ya Umma, 2005 kinataja kuwa isipokuwa pale ambapo wazabuni, makandarasi au watoa huduma tayari wameainishwa (pre-qualified), taasisi inazofanya manunuzi ya bidhaa zilizodhibitiwa (restricted) itahitajika kutafuta mzabuni kutoka katika orodha ya watoa huduma za ugavi ambao walipitishwa ili kuleta ushindani zaidi wa bei.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa malipo ya jumla ya Sh. 375,057,680 yahusuyo manunuzi ya bidhaa na huduma katika Halmashauri 18, zililipwa kwa wazabuni mbalimbali ambao hawakuwa katika orodha ya watoa huduma za ugavi waliopitishwa katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Jedwali Na. 72: Orodha ya Halmashauri ambazo zilifanya manunuzi kwa watoa huduma za Ugavi ambao hawakupitishwa

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/M Ilala	70,143,708
2	H/M Iringa	17,204,260
3	H/M Bukoba	18,560,010
4	H/W Bunda	8,641,360
5	H/W Rarya	70,336,752
6	H/W Kyela	29,818,500
7	H/W Mbarali	2,801,050

8	H/W Mbeya	24,615,000
9	H/Jiji Mbeya	53,816,700
10	H/W Mbozi	19,997,000
11	H/W Rungwe	18,890,000
12	H/M Morogoro	10,988,500
13	H/W Mvomero	4,316,500
14	H/M Songea	3,853,100
15	H/W Tunduru	7, 505,920
16	H/W Namtumbo	3,800,900
17	H/W Shinyanga	9,942,500
18	H/W Kishapu	15,973,200
Jumla		375,057,680

Mwenendo kwa miaka miwili wa manunuzi kwa watoa huduma za ugavi ambao hawajathibitishwa.

Jedwali Na. 73: Mwenendo kwa miaka miwili wa manunuzi kutoka kwa watoa huduma za ugavi ambao hawajathibitishwa

Mwaka	Manunuzi yaliyofanywa kwa watoa huduma za ugavi ambao hawajathibitishwa. (Sh)	Idadi ya Halmashauri husika
2010/11	272,623,633	19
2011/12	375,057,680	18

Jedwali hilo hapo juu linaonesha mwenendo wa manunuzi kutoka kwa watoa huduma za ugavi ambao hawajathibitishwa kwa muda wa miaka miwili mfululizo. Kiasi kiliongezeka kutoka mwaka mwaka wa fedha 2010/11-2011/12 ni Sh.102,434,047 ambayo ni sawa na 37%.

Uchambuzi huupia anaweza kuoneshwa kwenye milinganyo duara ifuatayo:



Kutokana na chati hapo juu inaonesha kwamba mwenendo wa Halmashauri wa kutozingatia sheria ya Manunuzi ya Umma, 2004 na Kanuni zake, 2005 umeongezeka. Pamoja na hilo, ubora wa bidhaa zilizonunuliwa kutoka kwa watoa huduma za ugavi wasiopitishwa kisheria hakuweza kuthibitika.

c) **Manunuzi yaliyofanywa bila kushindanisha zabuni Sh.443,107,149**

Mapitio ya kumbukumbu za manunuzi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 uligundua kiasi cha Sh. 443,107,149 zikiwa zimetumiwa na Halmashauri kwa ajili ya manunuzi ya kazi za ujenzi, bidhaa na huduma za ushauri bila kufuata mchakato wa kushindanisha zabuni kinyume na kanuni ya 63 ya manunuzi ya umma ya 2005. Ukiukwaji wa taratibu za manunuzi kwa kiwango hicho unaweza kuleta shaka hasa upande wa thamani ya fedha na ubora wa bidhaa/huduma zilizonunuliwa na Halmashauri hizo.

Jedwali hapa chini linaonesha kiasi kilicholipwa na kila Halmashauri bila ushindani.

**Jedwali Na. 74: Orodha ya Halmashauri ambazo
zilifanya Manunuzibila ushindani wa wazabuni**

Na.	Jina la halmashauri	Kiwango (Sh.)
1	H/ M Arusha	9,980,000
2	H/W Mafia	5,902,000
3	H/ M Kinondoni	41,702,641
4	H/ M Temeke	66,629,510
5	H/ W Ludewa	38,977,650
6	H/ Mji Njombe	2,000,000
7	H M Bukoba	109,309,774
8	H/M Kigoma/Ujiji	1,036,500
9	H/ W Mwanga	28,478,600
10	H/W Liwale	2,975,018
11	H/W Nachingwea	4,292,990
12	H/W Babati	20,201,645
13	H/W Hanang'	19,638,871
14	H/W Simanjiro	9, 204,023
15	H/W Tarime	1, 498,000
16	H/W Ilaje	2,400,000
17	H/W Mbeya	17,621,318
18	H/ Jiji Mbeya	6,111,480
19	H/W Kilombero	4,596,250
20	H/W Ulanga	4,160,500
21	H/W Mtwara	2,700,000
22	H/W Sengerema	2,250,000
23	H/W Korogwe	29,999,928
24	H/W Nzega	5,571,600
25	H/W Urambo	18,570,874
Jumla		443,107,149

Jedwali hapo chini linaonesha ulinganifu wa Manunuzi yaliyofanyika bila zabuni za ushindani kwa miaka miwili.

Jedwali Na. 75: Mwenendo wa Manunuzi yaliyofanywa bila kushindanisha wazabuni

Mwaka	Zabuni ambazo hazikushindanishwa (Sh.)	Idadi ya Halmashauri husika
2010/11	397,571,968	20
2011/12	443,107,149	25

Jedwali hapo juu linaonesha kwamba manunuzi yaliyofanywa bila kufuata mchakato wa ushindani wa zabuni yameongezeka kwa Sh. 45,535,181 sawa na 11%. Kutoka mwaka 2010/11 hadi 2011/12.

Menejimenti ya Halmashauri inapaswa kuhakikisha kwamba angalau Nukuu tatu zinashindanishwa kutoka kwa wauzaji wa bidhaa na huduma kabla ya manunuzi kufanyika ili kuzingatia taratibu za manunuzi ya kiwango. Kwa upande wa manunuzi yanayofanywa kwa chanzo kimoja cha mtoa huduma, inapaswa kuonesha uhalali na uidhinishwaji wa manununzi hayo.

d) Manunuzi ya bidhaa na vifaa ambavyo havikuingizwa katika leja ya vifaa Sh.271,711,263

Agizo 54(3) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 inataka kumbukumbu za mapokezi, vifaa vilivyotoka stoo na kiasi halisi kilichobaki kwa kila bidhaa zilizopokelewa ziandikwe katika kurasa tofauti za leja ya stoo ikionesa taarifa zote za bidhaa zilizonunuliwa kama vile tarehe ya manunuzi, stakabadhi ya kutolea bidhaa, idadi na kiasi kwa kila aina ya bidhaa. Lakini pia, agizo hili linataka kuwe na kumbukumbu juu ya tarehe bidhaa hizo zilipotolewa stoo, idadi iliyotolewa, namba ya hati ya kutolea bidhaa hizo na kiasi kilichobaki stoo. Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika kuangalia udhibiti na usimamizi wa bidhaa katika stoo ulibaini kuwa Halmashauri 17 hazikuweza kukidhi matakwa ya agizo lililotajwa hapo juu. Orodha ya Halmashauri hizo ni:-

Jedwali Na. 76: Orodha ya Halmashauri ambazo vifaa vyake havikuingizwa katika leja

Na.	Jina la halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/M Dodoma	4,363,080
2	H/W Kongwa	727,000
3	H/W Missenyi	6,377,108
4	H/W Kibondo	45,424,460
5	H/M Kigoma/Ujiji	44,409,210
6	H/W Liwale	14,492,500
7	H/W Babati	6,744,500
8	H/W Hanang'	7,310,265
9	H/W Kyela	22,083,500
10	H/Jiji Mbeya	19,605,840
11	H/W Rungwe	11,936,400
12	H/W Newala	21,959,300
13	H/W Geita	16,279,500
14	H/M Songea	1,335,000
15	H/W Handeni	171,300
16	H/W Sikonge	37,352,300
17	H/W Tabora	11,140,000
Jumla		271,711,263

Jedwali lifuatalo linaoneshamwenendo wa vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye leja ya kurekodi vifaa kwa miaka miwili.

**Jedwali Na. 77: Mwenendo wa vifaa ambavyo
havikuingizwa kwenye leja la vifaa kwa miaka miwili**

Mwaka	Vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye leja ya vifaa (Sh.)	Idadi ya Halmashauri zinazohusika
2010/11	594,164,665	22
2011/12	271,711,263	17

Kiasi chama nunuzi kilichobainika kutokurekodiwa katika leja ya vifaa kwa mwaka wa fedha 2011/12 zimeonekana kupungua kwa kiasi cha Sh.322,453,402 ambacho ni sawa na 54%. Hii inaonyesha kuboreka katika kusimamia mapokezi na kurekodi vifaa kwenye leja.

Kwa vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye leja ya vifaa, inapunguza mawanda ya ukaguzi, hasa kutambua kama vifaa vilivyonunuliwa, na vimepokelewa vyote na kutumika kama inavyopaswa.

- e) Bidhaa zilizolipiwa lakini hazikupokelewa Sh.125,681,000

Kifungu cha 122(1) cha kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005 kinazitaka taasisi zinazofanya manunuzi kupata taarifa juu ya mapokezi ya bidhaa ambazo zimenunuliwa kulingana na mikataba ili kuidhinisha malipo mara moja kwa mzabuni. Kinyume na kanuni hii, bidhaa zenye thamani ya Sh.125,681,000 ziliagizwa na kulipiwa katika Halmashauri 6 lakini zilikuwa bado hazijapokelewa kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 78: Orodha ya Halmashauri ambazo vifaa vililipiwa lakini havijapokelewa


Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Monduli	2,100,000
2	H/W Kigoma	3,815,000
3	H/W Moshi	1,022,000
4	H/W Mbeya	3,589,000
5	H/W Nkasi	114,000,000
6	H/W Igunga	1,155,000
Jumla		125,681,000

Jedwali hapo chini linaonesha mlinganisho wamiakamiwiliwa bidhaa zilizolipiwa lakini hazijapokelewa

Jedwali Na. 79: Mwenendo wa Bidhaa zilizolipiwa lakini hazijapokelewa

Mwaka	Bidhaa ambazo zimelipiwa lakini hazijapokelewa (Sh.)	Idadi ya Halmashauri
2010/11	833,707,405	13
2011/12	125,681,000	6

Jedwali hapo juu pia linaweza kuoneshwa kwenye chati mihimili hapo chini:



Kutokana na jedwali hapo juu pamoja na chati mihimili inaonesha bidhaa zilizolipiwa lakini hazikupokelewa kupungua kwa Sh.708,026,405 ambayo ni sawa na 85%. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 kulikuwa na kuboreka kwa ufuatiliaji wa bidhaa ambazo zilikuwa hazikupokelewa.

f) Mapungufu katika utunzaji wa kumbukumbu za mikataba na miradi Sh.660,529,264

Upitiaji wa usimamizi wa mikataba ulibaini upungufu mkubwa wa utunzaji wa kumbukumbu muhimu za mikataba na miradi kama taarifa/nyaraka muhimu hazikuwa katika mafaili ya mkataba husika ikiwa ni pamoja na mikataba yenye, Mchanganuo wa gharama za kazi (BOQ), makadirio ya Wahandisi, hati za madai za kazi iliyofanyika, mihutasari ya vikao vilivyofanyika eneo la kazi, nakala za hati za malipo, ongezeko la kazi (ikiwa lilikuwepo) na manunuvi yaliyofanywa nje ya mpango wa mwaka wa manunuvi, vilevile kumekuwa na utunzaji wa rejestra ya mikataba usioridhisha.

Kiwango cha kufuata sheria ya manunuvi kinaendelea kuboreka. Hivyo mapungufu hayo kuendelea kupungua. Katika mwaka wa ukaguzi, jumla ya Shs.660, 529,264

ndizo zilibainika kuwa zimetumika kinyume na kanuni za manunuzi katika mwaka huu wa ukuguzi **kiambatisho (xxxvii)** hivyo zimeonekana kupungua ukilinganisha na Sh. 4,452,071,069 zilizotumika katika matumizi ya aina hii katika ripoti ya mwaka uliopita. Mlinganisho ni kama unavyoonekana katika jedwali hapo chini

Jedwali Na. 80: Mapungufu katika utunzaji wa kumbukumbu za mikataba na miradi

Mwaka	Idadi ya halmashauri	Kiasi (Sh.)
2009/10	10	1,755,429,901
2010/11	24	4,452,071,069
2011/12	16	660,529,264

Menejimenti za Halmashauri kwa mara nyingine tena zinasisitizwa kuimarisha vitengo vyta Usimamizi wa manunuzi na taratibu za manunuzi ili kupata thamani ya fedha katika matumizi ya fedha za Umma zinazotumika katika eneo hili.

6.5 Mapungufu katika Zoezi la kuhesabu mali/vifaa

Agizo la 64 (1) - (2) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2009 linaitaka halmashauri kuhesabu mali na vifaa kila mwisho wa mwaka wa fedha ikihusisha mali zilizopo stoo na mali nyingine zinazomilikiwa na Halmashauri. Hata hivyo kulikuwa na udhaifu uliobainika katika zoezi zima la kuhesabu mali kwa Halmashauri 23 kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xxxviii)**. Aidha, kulikuwa na Halmashauri nyingine zilizotajwa kufanya zoezi hili lakini uhakika wa kiasi kilichoripotiwa hakikuweza kuthibitishwa kwa kuwa hakukuwepo karatasi zilizotumika kuhesabu mali na vifaa zilizoshuhudiwa na Wakaguzi.

Aidha, wakati wa zoezi la kuhesabu mali ilibainika kuwa vitu mbalimbali katika stoo havikuwa vimepangwa kwa

namna nzuri. Kulikuwa na uhaba wa rafu (shelves) katika vyumba vya stoo na matokeo yake baadhi ya bidhaa na vifaa vilikuwa vimezagaa sakafuni. Lakini pia hakukuwa na kadi za kutambua bidhaa katika baadhi ya stoo, wakati katika hospitali za Halmashauri kulikuwa na madawa yaliyoisha muda wake wa matumizi na hakukuwa na hatua zilizochukuliwa kuhakikisha madawa hayo yameondolewa. Kutokana na mapungufu hayo ilikuwa vigumu kuhakiki usahihi wa kiasi kilichoripotiwa kama mali zilizopo stoo katika Halmashauri 23 zenye thamani ya Sh.130,152,017 katika taarifa za fedha.

Halmashauri lazima zipange vizuri utaratibu wa kuhesabu mali kwa kuzingatia matakwa ya agizo la 64(1)-(2) ya Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009, ili kuondoa mapungufu hayo tajwa hapo juu.

Aidha, Halmashauri zinashauriwa kuhakikisha kwamba stoo zimepangwa vizuri kabla ya kufanya zoezi la kuhesabu mali zake ili kuwezesha urahisi wa kuhesabu na kupunguza uwezekano wa mali nyingine kutoonekana au kusababisha hasara ya mali kuharibika. Katika siku zijazo, Halmashauri inapaswa kuzingatia agizo la 64 (1) - (2) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa na kukaribisha wakaguzi wakati wa zoezi hilo.

wakati wa zoezi la kuhesabu mali kwenye Halmashauri 27; kuna mapungufu yaliyobainika kwenye Halmashauri kumi na mbili (12) kati ya hizo, na mapungufu hayo ni kama zilivyooneshwa katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 81 : Idadi ya Halmashauri ambazo zilikuwa na mapungufu katika zoezi la kuhesabu mali/vifaa

Na.	Jina la halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/ W Bukombe	5,687,232
2	H/W Hanang	10,206,638
3	H/ W Ileje	32,992,320
4	H/ jiji Mbeya	21,683,240
5	H/ W Kyela	9,867,005
6	H/W Maswa	21,735,105
7	H/W Rombo	2,843,800
8	H/ W Kilindi	380,750
9	H/ W Kongwa	16,854,585
10	H/ W Mkuranga	6,892,192
11	H/ W Chato	339,200
12	H/W Iramba	1,389,900
Jumla		130,152,017

SURA YA SABA

7.0 KAGUZI MAALUM

7.1 Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika kaguzi maalum

Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya 2008 na Kanuni Na.79(1) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009 inampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum kutokana na maombi kutoka kwa Afisa masuuli au mtu yejote, Taasisi, Mamlaka ya Umma, Wizara, Idara, Wakala, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na vyombo vingine. Kanuni pia inampa CAG mamlaka ya kufanya ukaguzi maalum pale anapoona inafaa.

Katika mwaka husika, kaguzi maalum kumi na nne (14) zilifanyika. Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika kaguzi maalum ni kama ifuatavyo:

7.1.1 Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi

Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika ukaguzi maalum wa mfuko wa maendeleo ya jimbo (CDCF) katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2008/09 hadi 2011/12 ni kama ifuatavyo;

- Manunuzi ya kompyuta na vifaa vya stoo yenye thamani ya Sh.9,585,000 yamefanyika kwa kutumia masurufu na bila kuidhinishwa na kamati ya mfuko wa maendeleo ya jimbo kinyume Kanuni Na. 68(4) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005
- Ununuzi wa vifaa vya ujenzi yenye thamani ya Sh. 17,120,000 kwa ajili ya kukamilisha shule na vituo vya afya yamefanyika bila kufuata taratibu za manunuzi pia bila idhini ya kamati ya mfuko wa maendeleo
- Manunuzi ya madawati mia nne (400) yenye thamani ya Sh.37,550,000 yamefanyika bila kufuata taratibu za manunuzi na maelekezo ya mfuko.

- Malipo ya Sh.5,000,000 yasiyoidhinishwa na kamati ya mfuko wa jimbo yametumika katika ujenzi wa shimo la kukagulia magari
- Hati za malipo ya Sh.9,446,500 zimekosekana katika faili husika na viambatanishi vya ununuzi wa mafuta yenyе thamani ya Sh.5,520,100 havikuweza kuonekana
- Mafuta ya halmashauri yenyе thamani ya Shs.1,955,000 yametumika kwenye magari ya watu binafsi bila kibali cha Afisa masuuli.
- Malipo ya posho ya Sh.6,502,000 yamefanyika bila kuidhinishwa na kuthibitishwa na kamati ya mfuko wa jimbo
- Matumizi ya fedha ya Sh.11,800,000 za mfuko wa maendeleo ya jimbo yamefanyika katika shughuli zisizohusika na mfuko kinyume na sheria na kanuni za mfuko huo

7.1.2 Halmashauri ya wilaya ya Kiteto

Katika mwaka 2011/12, ukaguzi maalum ulifanyika katika ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto. Muhtasari wa masuala yaliyojiteze ni kama ifuatavyo;

- Makusanyo ya Mapato ya Sh.513,613,560 kutoka kwa wakala (AMCOS) hayakupelekwa benki
- Makusanyo ya Mapato ya Sh.99,516,950 yasiyopelekwa benki na mhasibu wa mapato
- Vitabu arobaini na nne (44) vya mapato ya ushuru wa mazao na stakabadhi kumi (10) za kukiri mapokezi ya fedha havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi
- Kuondolewa kwa nakala ya stakabadhi kutoka kwenye kitabu cha kukusanya mapato
- Udhifu wa mikataba ya makusanyo ya mapato ya ushuru wa mazao kama vile kutoonesha kiasi kinachotakiwa kurejeshwa halmashauri, tarehe ya kurejesha makusanyo, na kutowekwa wazi kwa

dhamana inayopaswa kulipwa na wakala husika wa makusanyo.

7.1.3 Halmashauri ya Wilaya ya Muheza

Ufuatayo ni muhtasari wa madhaifu yaliyobainika wakati wa kaguzi maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kwa kipindi cha Julai, 2006 hadi Juni, 2009;

- Kinyume na mwongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ‘TASAF’ kiasi cha fedha cha Sh.28,645,160 hakikutolewa na TASAF Makao Makuu kwa ajili ya vikundi sita vya MJADU, hata hivyo kulibainika hasara ya Sh.4,715,600 katika TASAF ngazi ya mkoa kitu ambacho ni kinyume na taratibu za manunuizi.
- Kulibainika manunuizi ya vifaa vyenye thamani ya Sh.75,520,250 yamefanyika bila kutumia zabuni au kushindanishwa katika mpango wa maji safi na maji taka vijijini.
- Manunuizi yenye thamani ya Sh.6,922,840 yanayo husiana na RWSSP yalijumuisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT) chini ya mpango wa maji safi na maji taka vijijini kinyume na Memoranda ya makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na washirika wa maendeleo.
- Malipo yenye thamani ya Sh.11,590,000 kama madeni ya muda mrefu katika mpango wa maendeleo ya kilimo ya wilaya hayakuoneshwa katika taarifa ya fedha za mwaka uliyopita na bajeti iliyoidhinishwa.
- Malipo ya posho yenye thamani ya Sh.124,445,500 hayakuuhakikiwa kutokana na ukosefu wa daftari la mahudhurio.
- Ujenzi wa machinjio na soko la mnada Sega na Mkanyageni/Muungano wenye thamani ya Sh.121,727,890 yamekamilika lakini hayatumiki.
- Mikataba yenye thamani ya Sh.144,188,600 haikuzingatia taratibu za manunuizi.
- gharama za kuchelewesha kazi kiasi cha Sh.2,343,600 hazikutozwa kwa Mkandarasi kwa kuchelewesha kazi.

- Malipo yenyе thamani ya Sh.10,644,400 hayakuthibitishwa kupokelewa na Bohari ya madawa Tanga
- Malipo yenyе thamani ya Sh.123,280,181 kwaajili ya ukarabati wa kituo cha afya Mkuzi, zahanati ya Misalai na ujenzi wa zahanati ya Ubwari yamefanyika kuitia akaunti ya JRF bila kukamilika kwa mradi
- Mapato ya ndani kiasi cha Sh.48,273,700 hayakuweza kuthibitishwa kupelekwa benki
- Kukosekana kwa hati za malipo zenye thamani ya Sh.81,430,530
- Udanganyifu katika eneo la kazi uliofanyika na baadhi ya watumishi ambao umepelekeea ubadhirifu wa fedha kiasi cha Sh.23,219,089 na wafanyakazi wenyе kesi za kughushi kiasi cha Sh.12,735,000

7.1.4 Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa

Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika ukaguzi wa halmashauri ya wilaya ya Ruangwa kwa kipindi cha mwaka 2010/11 ni kama ifuatavyo;

- Gharama za ucheleweshaji wa kazi kwa siku mia moja (100) kiasi cha Sh.6,778,720 hazikutozwa kwa Mkandarasi katika ujenzi wa nyumba mbili za watumishi -Nanjaru na Chunyu, kwenye mkataba wa kiasi cha Sh.67,787,200
- Malipo ya Sh.55,123,000 yalilipwa kutoka akaunti ya afya, kwa kazi ya ujenzi wa zahanati -Nanjaru na Ng'au bila ujenzi huo kufanyika.
- Mtendaji wa kata na afisa manunuzi kutorejesha mapato ya mauzo ya mahindi ya njaa yenyе thamani ya Sh.11,780,000 katika halmashauri
- Hundu yenyе malipo ya Sh.2,750,000 ililipwa benki ilhali inaonekana kufutwa kwenye rejestaa
- Malipo ya Sh.55,825,000 yaliyofanyika kutoka akaunti tano (5) za halmashauri kwa kutumia hundi bandia kutokana na njama kati ya watumishi wa halmashauri na watumishi wa benki.

- Malipo ya mishahara kiasi cha Sh.21,042,530 yamefanyika kwa watumishi waliostaafu/kufukuzwa kazi. Hata hivyo mishahara isiyolipwa yenyе thamani ya Sh. 34,354,759 yalibainika kutorejeshwa hazina.
- Kukosekana kwa hati za malipo yenyе thamani ya Sh.251,324,564 na viambatanisho katika hati za malipo zenyе thamani ya Sh.305,154,078 havikuambatanishwa
- Njama kati ya wafanyakazi wa benki na watumishi wa halmashauri iliyopelekea wizi wa fedha za halmashauri zenyе thamani ya Sh.160,421,335
- Kukosekana kwa vitabu nane (8) vya kukusanya mapato na kutokukusanya kwa mapato ya ushuru wa mazao ya Sh.150,619,711
- Malipo ya posho ya kukaimu kwa watumishi wawili (2) ya Sh.39,869,430 yamefanyika bila kukatwa kodi.
- Mfuko wa Ustawi wa Jamii - Makao makuu kuondoa fedha kiasi cha Sh.27,049,950 kwa halmashauri, kutokana na kushindwa kuzingatia vigezo na masharti.

7.1.5 Halmashauri ya Manispaa ya Musoma

Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza kwenye ukaguzi wa mfuko wa maendeleo ya jimbo (CDCF) kuhusiana na utengenezaji wa madawati kwa kipindi cha mwaka 2009/10 hadi 2010/11. Mambo yaliyobainika ni kama yafuatavyo:

- Katika mwaka wa fedha wa 2009/10 na 2010/11 halmashauri ilipokea fedha za mfuko wa maendeleo ya jimbo kiasi cha Sh.34,296,000 na Sh.34,615,478 kwa kufuatana, na kufanya jumla ya fedha zilizopokelewa kuwa Sh.68,911,478. Hata hivyo hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2010/11 halmashauri ilikuwa imetumia jumla ya Sh.34,740,000 na kubakiza kiasi cha Sh.34,171,478 bila kutumika.
- Kifungu Na.19(1) cha sheria ya mfuko wa maendeleo ya jimbo kinaitaka miradi yote kuwa na malengo ya kijamii ili kuhakikisha kwamba faida inayotegemewa

inaleta manufaa kwa wakazi wa eneo husika, kinyume na sheria hiyo fedha za mfuko wa jimbo zilitumika kutekeleza miradi ambayo haikuibuliwa na jamii husika.

- Halmashauri ilifanya manunuzi ya madawati mia tisa (900) kwa kutumia mzabuni Barnaba W. Mathayo ambaye hakuwa kwenye orodha ya wazabuni iliyoidhinishwa na bodi ya wazabuni ya halmashauri kwa mwaka husika. Pia hakukuwa na vielelezo kuthibitisha kama nukuu za bei zilikubaliwa na kamati ya mfuko wa jimbo kama inavyoolekezwa katika kifungu na.15(2) cha sheria na. 16 ya mwaka 2009 ya mfuko huo.
- Kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha kufanyika kwa ukaguzi wa manunuzi ya madawati kabla ya kusambazwa kwa ajili ya matumizi katika shule ya msingi, kama inavyo takiwa na Kanuni ya 27 ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya 2005.
- Kiasi cha sh. 9,000,000 kilichangwa na wananchi kama nyongeza kwa ajili ya kutengeneza madawati, kiasi hicho kiliwekwa benki akaunti nambari 01J1062049700-CRDB ambayo haimilikiwi na halmashauri. Ukaguzi haukuweza kubaini matumizi ya fedha hizo.
- Ilionekana kuwa madawati yaliyosambazwa kwenye shule hayakuingizwa kwenye vitabuni vya stoo vya shule zilizofaidika kama inavyotakiwa na Agizo nambari 54(3) la LGFM, 2009.

7.1.6 Halmashauri ya wilaya ya Kilwa

Ukaguzi maalumu ulihuisha masuala ya mwaka wa fedha 2008/09 na 2009/10. Muhtasari wa masuala muhimu yaliyojitokeza ni kama ifuatavyo;

- Malipo kiasi cha Sh.1,994,080 yalifanyika kwa mkandarasi zaidi ya kiwango cha mkataba wa ujenzi wa jengo la utawala uliofanyika mwaka wa fedha 2007/08 na 2008/09.

- Mkopo wa fedha kiasi cha Sh.48,000,000 kutoka akaunti ya amana zilizotumika katika ukarabati wa jengo la utawala, ambalo lilikuwa bado lipo mikononi mwa mkandarasi.
- Mapato yaliyokusanywa na Halmashauri ambayo hayakupelekwa benki, pia mapato yaliyopokelewa kwenye kitabu cha mapato kutofautiana na kiasi kilichopokelewa na kupelekwa benki kwa Sh.922,550.
- Jumla ya Sh.31,541,550 zilikusanywa na halmashauri lakini hazikuonyeshwa kwenye vitabu vyatya hesabu vyatya Halmashauri.
- Makusanyo ya mapato kiasi cha Sh.53,489,655 yaliyokusanywa na wakusanyaji mbalimbali hayakurejeshwa katika halmashauri.
- Kukosekana kwa vielelezo kuhusu matumizi ya fedha kiasi cha Sh.8,551,033 zilizobaki baada ya kusafirisha mahindi ya njaa katika maeneo yaliyoathirika kwa njaa.
- Kukosekana kwa vielelezo (fomu za kutuma pesa kwa njia ya benki, stakabadhi za kuwekea fedha benki, taarifa ya kukiri kutoka ofisi ya waziri mkuu) ili kuthibitisha kama halmashauri ya kilwa ilirejesha kiasi cha Sh.43,040,000 za mauzo ya mahindi ya njaa katika ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2008/09 na 2009/10.
- Hakuna ushahidi uliotolewa kama vile stakabadhi ya mapokezi ya fedha, taarifa za benki, kuthibitisha kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ilitumia fedha kiasi cha Sh.27,065,260 kutoka akaunti ya kilimo (NAEP-II) kwa ajili ya kulipia gharama za kusafirisha/kusambaza mahindi ya njaa

7.1.7 Halmashauri ya manispaa ya Temeke

Ukaguzi Maalum ulifanyika katika Manispaa ya Temeke ambaao ulihusisha mwaka wa fedha 2008/09 na 2009/10. Muhtasari wa masuala yaliyotokana na ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:

- Kukosekana kwa vitabu 88 vya kukusanya mapato na hati za malipo (Mfuko wa Afya) zenyе thamani ya Sh.302,528,633.
- Hundi mbili, Na.202185 na 006360 zenyе malipo ya jumla ya Sh.37,362,628 ziliendelea kuoneka kwenye usuluhishi wa kibenki mpaka Machi, 2011. Lakini hadi ukaguzi unakamilika Septemba, 2011 hundi hiso hazikuoneka kwenye taarifa ya benki kwa kipindi chote hicho wala kuonekana kwenye orodha ya hundi zilizochacha.
- Hundi yenye thamani ya Sh.79,598,494 ya makusanyo ya mapato kwa mwezi Septemba, 2011 haikuonekana kwenye taarifa ya benki.
- Makusanyo ya mapato ya Sh.74,398,221 hayakuonekana kwenye taarifa ya benki wala kwenye taarifa ya usuluhishi wa kibenki.
- Katika miaka ya fedha 2008/09 na 2009/10, mapato yaliyopotiwa kwenye kitabu cha mkusanyaji mapato yalikuwa Sh.522,372,243 ukilinganisha na kiasi kilichokuwa kinaonekana kwenye nyaraka za kuwekea fedha benki cha Sh.460,568,795 hivyo kupelekea upungufu wa kiasi kilichopelekwa benki kwa Sh.61,803,449.
- Marejesho ya bima yenye thamani ya Sh.13,214,451 hayakuthibitika kama yalikuwa kwenye kumbukumbu za vitabu vya halmashauri.
- Uwepo wa malipo ya Sh.42,621,500 yaliyofanyika kwa hundi iliyochacha na malipo batili ya Sh.8,715,000 yaliyofanywa kwa maafisa wa ardhi kama posho kwa kazi ambazo hazikufanyika.
- Ukaguzi maalum ulibaini kuwa waratibu wa miradi/wakuu wa idara walikuwa wakifanya semina na kulipwa bila kuonesha idadi ya siku na tarehe za kufanyika kwa semina hiso. Malipo ya shughuli hiso ya Sh.122,894,000 yanaashiria wizi wa fedha za umma kwa kukosa taarifa za kuthibitisha uhalali wake.

- Marejesho ya masurufu maalum yenyе thamani ya Sh.1,680,00 kwa kutumia hati za kugushi
- Halmashauri ilifanya malipo ya Sh.14,440,000 kwa maafisa wake kwa kutumia akaunti ya ‘CSDP’ na ‘Multi-sectoral’, hata hivyo hakukuwa na vithibitisho kama fedha zilipokelewa na wahusika.
- Kuingiliana kwa malipo ya Sh.29,085,000 yaliyolipwa kwa meneja wa mradi.
- Ununuzi wa madawa na vifaa vya hospitali vya thamani ya Sh.12,686,600 ambavyo havikuwasilishwa.

7.1.8 Halmashauri ya Wilaya ya Songea

Ukaguzi maalum ulifanyika kufuatia kuwepo kwa udhaifu mkubwa katika mfumo wa udhibiti wa ndani, na kutokamilika kwa taarifa za fedha. Muhtasari wa masuala muhimu yaliyojitekeza ni kama ifuatavyo;

- Wakati wa maandalizi ya taarifa za fedha kwa mwaka wa fedha 2010/11, hakukuwa na mhasibu mwingine mwenye ufahamu wa kuandaa taarifa hizo kwa kutumia viwango vya kimataifa vya utayarishaji wa hesabu za Umma (IPSAs), Mweka Hazina ambaye alikuwa akikaimu kama Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya kwa kipindi cha Julai 2011 hadi Oktoba 2011.
- Udhaifu katika mfumo wa utawala uliosababishwa na baadhi ya wakuu wa idara na vitengo ambao wamekaimu kwa muda mrefu bila kuthibitishwa, akiwemo mkuu wa idara ya maji na umwagiliaji, mifugo na maendeleo ya uvuvi, kitengo cha manunuzi, mahakama na kitengo cha uchaguzi.
- Makusanyo ya mapato jumla ya Sh.11,805,300 hayakuthibitika kupelekwa benki.
- Vitabu vitatu (3) vya kukusanya mapato havikurejeshwa halmashauri.
- Halmashauri ilifanya manunuzi ya huduma na bidhaa mbalimbali yenyе thamani ya Sh.279,700,481, ambayo ni zaidi ya kiwango kinachoruhusiwa kuidhinishwa na afisa masuuli kabla ya idhini ya bodi ya zabuni,

kitendo hicho ni kinyume na taratibu za Kanuni ya Uanzishwaji wa Bodi ya Zabuni ya Serikali za Mitaa 2007.

- Halmashauri ilitumia Sh.109,874,000 kutekeleza miradi mbalimbali ambayo haikuwa kwenye mpango kazi katika mwaka wa fedha 2010/11. Pia kiasi cha Sh.113,927,250 kilitumika, ikiwa ni zaidi ya bajeti iliokuwa imepangwa kutekelezwa.
- Lita 8,060 za dizeli zenye thamani ya Sh.16,330,600 zilinunuliwa na kutumika kwenye magari yaliyokuwa yameegeshwa kwenye karakana ya halmashauri.
- Kiasi cha Sh.34,192,723 kilitumika kulipa mishahara kwa watumishi ambao hawakuwa kwenye utumishi kwa sababu walikuwa hawajafutwa kwenye orodha ya mishahara.
- Kiasi cha Sh.135,000,000 kilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza miradi sita (6) ya kilimo (DADPS) kwa mwaka wa fedha 2010/11, hata hivyo kiasi hicho hakikuthibitika kuwepo kwenye akaunti japokuwa miradi husika haikutekelezwa.
- Kiasi cha Sh.13,475,500 kilitumika kufadhili michezo na shughuli za kidini kinyume na Kifungu Na.19(2) na 19(3) cha Kanuni ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya 2009.

7.1.9 Halmashauri ya Manispaa ya Arusha

Ukaguzi maalumu ulifanyika kufuatia udhaifu mkubwa katika mfumo wa udhibiti wa ndani wa halmashauri, uhifadhi mbovu wa nyaraka, kutowiana na kutoamilika kwa taarifa za fedha. Muhtasari wa masuala yaliyojiteze ni kama ifuatavyo;

- Fedha zilizokusanya kiasi cha Sh.33,097,138 hazikupelekwa benki.
- Mapato yanayokusanya na mawakala yenyе thamani ya Sh.1,496,466,886 hayakuwasilishwa halmashauri.
- Kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita tangu 2009/10 mpaka 2011/12, Halmashauri ya Manispaa ya Arusha

haikuweza kuthibitisha ukusanyaji wa mapato ya Sh.1,235,782,939 ya kodi ya huduma na Sh.1,105,011,423 ya kodi ya majengo.

- Halmashauri kutoza bei ya chini, ambayo ni tofauti sana nabei ya soko na kusababisha hasara ya mapato ya zaidi ya Sh.2,137,745,383
- Jumla ya Sh.148,500,000 zimekusanywa kupitia ada ya vyoo vyta umma kwenye kituo cha mabasi kwa kipindi cha miaka 11 (tangu 2011 hadi 2012). Hata hivyo mapato hayo hayakuwasilishwa halmashauri na wakala muhusika.
- Wapangaji kwenye soko la Kilombero na Soko kuu waliiingia mkataba na halmashauri ya manispaa, hata hivyo wapangaji hao hawajalipa kodi ya Sh.15,420,000.
- Jumla ya kiasi cha Sh.52,881,800 kutoka katika mikataba ya ukusanyaji wa mapato ilioongezwa mwezi mmoja kutoka tarehe 30/6/2010 mpaka 31/7/2010 hayakuthibitishwa kupokelewa na Halmashauri
- Halmashauri ilifanya manunuzi yenyе jumla ya Sh.204,621,407 yaliyohusisha gari aina ya TIPPER yenyе namba za usajili SM 8850 na pikipiki mbili. Hata hivyo manunuzi hayo hayakupitishwa na bodi ya zabuni ya Halmashauri.
- Katika mwaka wa fedha 2009/10 na 2010/11, halmashauri ilifanya manunuzi ya madawa na vifaa kwa thamani ya Sh.93,322,680 kutoka kwa wazabuni mbalimbali bila kupita bohari ya madawa (MSD) wala kuidhinishwa na bodi ya zabuni, kinyume na Kanuni Na.54 (1) ya Manunuzi ya Bodi ya Zabuni (Uanzishwaji na taratibu) ya Serikali za Mitaa ya 2007.
- Kiasi kikubwa cha mafuta yaliyonunuliwa kwa ajili ya idara ya afya yalitumika kibadhilifu kwa kuwekwa kwenye magari mengine kama magari yaliyoegeshwa. Hata hivyo utumiaji wa mafuta yenyе thamani ya

Sh.34,183,050 haukuoneshwa kwenye vitabu vyatubu za magari.

- Halmashauri ilitumia masurufu yenyeye thamani ya Sh.25,486,000 kwa ajili ya mafunzo ya UKIMWI na mpango wa bajeti wa mda mrefu, hata hivyo matumizi hayo hayakuthibitishwa kwani halmashauri ilishindwa kuwasilisha vielelezo vyatubu ya orodha ya washiriki na mahali mafunzo yalipofanyikia.
- Kutokana na nukuu za bei zilizofanyika, bei iliyonuna vifaa vyatubu ofisi ilikuwa kubwa na kupelekea halmashauri kupoteza kiasi cha Sh.25,554,620.
- Kwa kipindi cha miaka miwili na miezi tisa mfululizo, kiwanda cha nyama-Arusha kilikusanya fedha zitokanazo na ukaguzi wa awali wa nyama na mifugo ya jumla ya Sh.248,521,000. Hata hivyo kiasi cha Sh.52,063,300 kilirejeshwa halmashauri na Kiasi cha Sh.196,457,700 sawa na asilimia 79 ya jumla ya mapato ambayo haikurejeshwa halmashauri.
- Halmashauri ililipa fedha kiasi cha Sh.19,255,000 zaidi ya kiwango kilichotajwa kwenye mkataba wa manunuzi ya magari chakavu ya kuokoa na kuzima na moto. Hata hivyo hadi wakati wa ukaguzi, halmashauri ilikuwa haijapokea magari hayo kwa kutotimiza vigezo vilivyoko kwenye mkataba.
- Halmashauri inamiliki hisa zisizopungua asilimia 29 katika kampuni ya “Happy Sausage”, lakini imekuwa haihusishwi kabisa katika uongozi au katika maamuzi ya kampuni hiyo kwa muda wote usiopungua miaka 19. Pia Halmashauri yenye we inaonekana kutojua stahili yake wala kufuatilia haki zake katika kampuni hiyo.

7.1.10 Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro

Muhutasari wa udhaifu uliobainika kwenye ukaguzi maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kwa kipindi cha mwaka 2009/10 na 2010/11 ni kama ifuatavyo;

- Baadhi ya nyaraka hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, ikiwemo taarifa za benki za kipindi cha Januari, 2011 hadi Novemba, 2011, na hundi Na. 812792 yenyе thamani ya Sh.19,800,000 iliyotolewa katika tawi la benki ya NMB Wami.
- Ukusanyaji ya mapato ya jumla ya Sh.21,547,700 hayakupelekwa benki.
- Vitabu arobaini (40) vya kukusanya mapato havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.
- Kukosekana kwa hati za malipo zenyе jumla ya Sh.1,178,916,658
- Malipo yaliyofanywa na benki bila hundi Sh.156,460,259
- Malipo kwa ajili ya Ukarabati wa ofisi ya Sh.11,267,900 yamefanyika kwa kutumia masurufu badala ya nukuu za bei kinyume na Kanuni Na.68(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2005.
- Mishahara kulipwa zaidi ya stahili ya watumishi husika Sh.25,146,020
- Ruzuku ya ya posho ya kujikimu iliyobaki, kutumika kulipia shughuli nyingine za halmashauri Sh.452,015,896
- Mishahara isiyolipwa kutorejeshwa hazina Sh.112,437,637
- Kuhamisha fedha bila kudhinishwa kutoka akaunti ya mpango wa maji safi na maji takatifu vijijini (RWSSP) kwenda akaunti ya maji ya matumizi mengineyo.
- Ubadhilifu wa fedha za maendeleo kwa kutekeleza malipo yasiyokusudiwa yenyе thamani ya Sh.50,791,000
- Jumla ya Sh.53,333,400 zilihamishwa kutoka akaunti ya maendeleo kwenda kwenye akaunti ya mfuko mkuu kama mkopo wa kulipa posho za madiwani na matumizi mengine kwa kutegemea kurejesha mkopo huo pale halmashauri itakapofanikiwa kushinda kesi Na.10/2011 dhidi ya Alliance One (T), kesi ya madai

ya kulipwa kodi ya huduma ya thamani ya Sh.328,500,000.

- Malipo yasiyofuata utaratibu yenyе thamani ya Sh.78,256,289 yamefanyika kwenye akaunti ya amana
- Kiasi cha Sh.100,000,000 kilihamishwa toka akaunti ya maendeleo kwenda akaunti ya afya kwa ajili ya ujenzi wa hospitali kwa barua yenyе kum. Na. MDC/D/30/39 ya tarehe 16/11/2011, hadi ukaguzi huu unafanyika ujenzi ulikuwa haujaanza.

7.1.11 Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma

Ukaguzi maalum ulifanyika katika Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ikihusisha miaka ya fedha 2008/09 na 2009/10. Muhtasari wa yaliyojitekeza ni kama ifuatavyo;

- Kukosekana kwa hati za malipo zenyе jumla ya Sh.1,154,006,989
- Mtumishi asiyе na uzoefu (Mhasibu msaidizi) alikuwa akipokea vitabu vya kukusanya mapato na kuviorodhesha kwenye rejista ya vitabu, sambamba na hilo vitabu vingi vilitolewa kwa mkusanyaji mmoja kwa wakati mmoja.
- Wizi wa makusanyo ya halmashauri yenyе thamani ya Sh.1,312,000 uliofanywa na mmoja wa wakusanya mapato kwa kutumia ‘Carbon slipping’
- Halmashauri kushindwa kukusanya mapato ya ndani kutoka kwenye vibao vya matangazo yenyе thamani ya Sh.412,866,000 na kodi ya majengo ya Sh.148,899,787
- Mapato ya jumla ya Sh.16,928,100 yaliyokusanywa na mtunza fedha kwa kipindi cha septemba, 2010 mpaka septemba, 2011 hazikupelekwa benki kinyume na Agizo 37(3) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 2009.
- Usuluhishi wa kibenki kutofanyika kwa wakati (kila mwezi) kinyume na Agizo 29 (2) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 2009.

- Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ilifanya manunuzi na matumizi ya mafuta yenyé mashaka yenyé thamani ya shs.19,005,950 kama ifuatavyo; lita 4,099 za mafuta yenyé thamani ya Sh.7,645,350 yameoneshwa kuwekwa katika magari mabovu ambayo yalikuwa hayatumiki, pia Halmashauri ilitoa lita 3,482 za mafuta zenye thamani ya Sh.6,375,000 kwa cheo cha mtumishi badala ya namba za gari kwenye leja ya mafuta, na mafuta ya Sh.4,985,600 yalitumika bila ya kurekodiwa katika daftari la safari za magari.
- kwa kipindi cha mwaka 2010/11, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ilifanya ujenzi mbalimbali kwa kutumia masurufu kinyume na Kanuni Na.18 ya Kanuni za Bodi ya Zabuni (Uanzishwaji na Taratibu) ya Serikali za Mitaa, 2007
- Mishahara isiyolipwa yenyé thamani ya Sh.128,413,854 kutorejeshwa hazina kinyume na Agizo 79(6) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009
- Watumishi wengi hasa wa Idara za Kilimo, Afya, Ujenzi na Fedha wamekaa kwa muda mrefu katika sehemu zao za kazi wengine wamekaa zaidi ya miaka ishirini (20) bila kuhamishwa hivyo kuishia kufanya kazi kwa mazoea.
- Kesi zinazohusisha Sh.1,277,340,248 ambazo hazikuisha za mwaka 2009/10 hazikuoneshwa kwenye taarifaa ya fedha
- Kukosekana kwa idadi halisi ya nyumba ambazo zinamilikiwa na halmashauri, kwa sababu ya kutoorodheshwa kwenye rejista ya mali za kudumu.
- Kutofuatwa kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma kulikopelekea ukarabati wa nyumba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Dodoma uliogharimu kiasi cha Sh.87,767,950 kutofanyika kwa kiwango kilichotakiwa.

7.1.12 Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali

Ukaguzi maalumu uliofanyika katika halmashauri ya wilaya ya Mbarali ulihusisha miaka ya fedha ya 2010/11 na 2011/12. Muhtasari wa masuala yaliyojiteza ni kama ifuatavyo:

- Kutokuwepo na kumbukumbu za msingi kama vile mihutasari ya vikao, majina ya wajumbe wa kamati ya ujenzi, stakabadhi na vitabu vya malipo, hati za malipo, taarifa za benki n.k, kwa ajili ya fedha zinazokusanya katika ngazi ya serikali za vijiji.
- Zabuni kwa ajili ya makusanyo ya mapato ya ndani hazikutangazwa nje ya eneo la halmashauri kinyume na Kanuni 80(5) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005.
- Mawakala wa kukusanya mapato kutorejesha mapato ya jumla ya thamani ya Sh.150,900,133 katika halmashauri kinyume na Agizo 38(1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.
- Katika mwaka wa fedha 2011/12, mawakala wa kukusanya mapato hawakurejesha halmashauri jumla ya Sh.150,900,133 na katika kiasi hicho jumla ya Sh.75,410,000 zilizochukuliwa na watumishi wa halmashauri hazikurejeshwa halmashauri.
- Halmashauri ilitoa vitabu 1,254 (visivyo na viwango) na vitabu 1,292 (vyenye viwango) ya kukusanya mapato kwa mawakala hadi kipindi cha ukaguzi Novemba, 2012 vitabu hivyo vilikuwa havijarejeshwa.
- Rejista ya mapato ya mwaka 2012/13, ilionesa kuwa halmashauri iliwapa zabuni baadhi ya mawakala wa kukusanya mapato licha ya kushindwa kurejesha mapato kwa mwaka 2011/12. Hali hii inaonesha uwezekano wa njama ya udanganyifu wakati wa kutoa zabuni.
- Jumla ya Sh.16,475,000 zilikusanya kutoka vyanzo mbalimbali, hata hivyo hakukuwa na ushahidi wa mapato hayo kupelekwa benki au kuwepo katika ofisi ya fedha ya halmashauri.

- Halmashauri ililipa kiasi cha Sh.146,928,050 kutekeleza kazi zisizo za mradi wa afya.
- Halmashauri ilishindwa kupeleka kiasi cha Sh.370,000,000 kwenye ujenzi wa bwawa la umwagiliaji Mashalla na Uturo, na kutumia fedha hizo kutekeleza kazi nyingine bila kibali cha wizara ya fedha.
- Nyongeza ya fedha za MMES ilitumika kufanya malipo ya kugushi ya Sh.724,633,829
- Hati za malipo zenye jumla yash. 1,973,200,811 hazikuwasilishwa kwa ukaguzi

7.1.13 Halmashauri ya Wilaya ya Bunda

Ukaguzi maalum ulifanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Muhtasari wa yaliyojitokeza ni kama ifuatavyo;

- Ununuzi wa viti kwa bei kubwa ya Sh.8,130,000 kutoka kwa M/S Kafumu Investment Co. Ltd
- Ununuzi wa mfumo wa sauti kutoka kwa mzabuni ambaye hakuidhinishwa.
- Halmashauri ilinunua meza kumi na tano (15) kwa ajili ya ukumbi wa halmashauri kwa bei iliyozidi kwa sh.100,000 kwa kila meza na kupelekea hasara ya Sh.1,500,000

7.1.14 Halmashauri ya Wilaya Mvomero

Ukaguzi maalum ulifanyika katika halmashauri ya Mvomero ambao ulihusu ujenzi wa jengo la utawala katika hospitali ya wilaya, ofisi ya mkurugenzi pamoja na nyumba ya kuishi mkurugenzi. Muhtasari wa matokeo muhimu ya ukaguzi ni kama ifuatavyo:

- i) **Ujenzi wa jengo la utawala hospitali ya wilaya**
 - Ongezeko la bei ya Sh.29,450,424 katika mkataba ambao haukupitishwa na bodi ya zabuni
 - Ongezeko la malipo ya Sh.16,739,081 kwa mkandarasi kutokana na nyongeza ya vipimo zaidi alivyopima

ukilinganisha na mchanganuo wa gharama ya kazi (BOQ) ya awali kwa

ii) Ujenzi wa nyumba ya kuishi mkurugenzi

- Malipo ya fedha yasiyostahili ya Sh.4,360,000 kwa mkandarasi kwakuwa hakumwaga zege kulingana na maelekezo ya gharama za kazi (BOQ) na matakwa ya maelekezo ya mchoro
- Kiasi cha ziada cha Sh.39,190,000 kililipwa kwa Mkandarasi kutokana na nyongeza ya vipimo zaidi ya viliyyopangwa katika mchanganuo wa gharama za kazi (BOQ) baada ya kupima jengo tena
- Hasara ya Sh.12,050,000 kutokana na gharama za awali katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa awamu mbalimbali

iii) Ujenzi wa jengo la ofisi

- Hasara ya Sh.17,339,000 ilipatikana kwa kulipa bei ya juu ikilinganishwa na bei ya soko kwa wakati huo
- Kiasi cha ziada cha Sh.41,186,616 kililipwa kwa Mkandarasi kwa vipimo vya ziada ukilinganisha na viliyyoonekana katika mchanganuo wa gharama za kazi (BOQ) baada ya kupima upya jengo
- Hasara ya Sh.72,630,000 kutokana na gharama za awali katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa awamu mbalimbali
- Hasara ya Sh.83,590,604 zinazotokana na ongezeko la ada za usimamizi na ushauri zinazochangiwa na ongezeko la bei za vifaa kutokana na utekelezaji wa ujenzi kwa awamu

Hata hivyo, kuna kaguzi maalum zingine zinazoendelea katika Halmashauri tano (5) ambazo ni Halmashauri za Wilaya ya Mpanda, Mufindi, Meru, Ileje na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala.

Ni matumaini yangu pia kuwa matokeo ya kaguzi maalum katika hizo Halmashauri tano (5) yatawasilishwa katika ripoti ya mwaka ujao pamoja na matokeo ya kaguzi nyingine zitakazofanyika ikiwa ni njia ya kuwezesha kuimarisha uwajibikaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ofisi ya Ukaguzi itaendelea kupokea maombi kutoka pande zote kwa kuzingatia sheria zilizopo, lakini ieleweke kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu hana wajibu na hatalazimika kuyakubali maombi yote lakini atazingatia kila ombi kulingana na uzito wake.

7.2 Mambo ya kujifunza katika Kaguzi Maalumu zilizofanyika mwaka huu

7.2.1 Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Jukumu la kuanzisha na kusimamia mfumo wa udhibiti wa ndani kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) 240 na Agizo 11 hadi 14 ya Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 2009 ni ya usimamizi wa uongozi husika wa Halmashauri.

Ni dhahiri kwamba, kuna udhaifu mkubwa wa usimamizi katika halmashauri juu ya usimamizi wa Mfumo thabiti wa udhibiti wa ndani.

Hali hii imesababisha menejimenti kushiriki kwa njia moja au nyingine kutawala mfumo wa udhibiti wa ndani, baadhi ya viashiria ni kama ifuatavyo:-

- Wizi ulikuwa unafanywa na watumishi wasio watiifu ambao walikuwa wanachukua mafuta kwa ajili ya magari ambayo yaliharibika lakini menejimenti haikuchukua hatua zozote za kisheria.
- Kuna ulegevu mkubwa wa menejimenti za halmashauri katika kupata na kulinda nyaraka zao muhimu. Hii ina madhara ya kikwazo katika mawanda ya ukaguzi.

- Hazina inawajibu wa kuhakikisha na kusimamia masuala yote yanayohusu fedha na udhibiti wake kama vile kusimamia idara ya fedha. Hali hii ilikuwa tofauti katika halmashauri zilizokaguliwa ambapo matukio yalibainisha kutokuwepo usimamizi na ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani, wizi wa mapato kupitia kughushit arakimu (carbon slipping), matumizi ya vitabu sambamba vya stakabadhi (carbon slipping), na makusanyo ya fedha kutopelekwa benki (mfano Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma)
- Kuna udhaifu mkubwa katika udhibiti wa mfumo wa ndani kuhusiana na usimamizi wa mikataba kwa mawakala ambao hukusanya mapato kwa niaba ya halmashauri, hali hii inasababisha kupotea kwa mapato kutokana na migongano inayotokana na kutofufa sheria na masharti yaliyoainishwa kwenye mikataba husika. (Mfano Halmashauri ya Manispaa ya Arusha na Halmashauri ya wilaya ya Kiteto)
- Wanasheria wa kila Halmashauri wana wajibu wa msingi wa kuhakikisha mikataba inatekelezeka, wajibu huu unatakiwa kupanuliwa ili kuhakikisha kesi zote zinazotokana na uvunjaji wa mikataba zinafikishwa mahakamani na kufuatiwa. Hali hii imekuwa tofauti kwa wanasheria wasio waaminifu kwa kushirikiana na wafanyakazi wengine wa halmashauri wamechangia katika kuongeza migogoro ya mikataba na mawakala wa kukusanya mapato kutokana na kushindwa kusimamia vizuri mikataba.

Hali hii inaonesha kushindwa kwa menejimenti kusimamia mfumo wa udhibiti wa ndani na kupelekea wizi wa mali za umma na kutofufa sheria na kanuni. Hizi ni sehemu muhimu sana ambazo zinatakiwa kushughulikiwa ipasavyo.

7.2.2 Menejimenti kutokuwa na ufanisi katika usimamizi wa miradi ya maendeleo

Ruzuku ya maendeleo katika serikali za mitaa inaweza kuleta faida inayotarajiwa iwapo itafuatiliwa na kusimamiwa vizuri. Miradi mingi ya maendeleo imekamilika katika halmashauri za vijiji na kata. Usimamizi na ufuutiliaji ni muhimu kwa sababu kuna upungufu au hakuna rasilimali watu na ujuzi wa kiufundi wa kusimamia miradi ya maendeleo kama vile ujenzi. Hata hivyo, Halmashauri inalazimika kutoa usimamizi wa karibu juu ya miradi ya maendeleo ili kupata tija, ufanisi, na ubora wa miradi.

Ukaguzi maalum uliofanywa katika halmashauri ya wilaya ya Songea na halmashauri ya Manispaa ya Dodoma umebaini kuwa, menejimenti za halmashauri hizo hazikuwa na ufanisi katika kutekeleza majukumu ya usimamizi wa miradi ya maendeleo inayotekelizwa katika ngazi za chini. Aidha, jamii haikuhimizwa kikamilifu katika utekelezaji wa miradi kwa ufanisi zaidi. Hakukuwa na ukaguzi kwa wakati wa miradi ya maendeleo na kusababisha kutokuwa na ubora na kuchelewa kukamilika kwa miradi husika.

Uzembe kama huu pia ultokea katika miradi inayoendeshwa na halmashauri ambazo zimeinga mikataba, mfano mzuri ni ukaguzi maalum uliofanyika katika halmashauri ya wilaya ya Morogoro amba ilipelekeea kucheleweshwa kwa ukamilikaji wa miradi ya maendeleo.

7.2.3 Kuwepo kwa Maofisa wanaokaimu nafasi za juu muda mrefu

Ukaguzi maalum uliofanyika Halmashauri ya Manispaa ya Arusha ulibaini kuwa kuna maofisa wanao kaimu nafasi za juu kwa muda mrefu. Mkuu wa kitengo cha ukaguzi wa ndani alikuwa anakaimu nafasi hiyo kwa kipindi kirefu

imepelekeea kutokuwa na utendaji mzuri katika kitengo cha ukaguzi wa ndani. Pia Idara ya fedha ilikuwa inaongozwa na kaimu Mweka hazina wa wilaya, pamoja na madhara mengine ni kutowasilishwa kwa mapato kutoka kwa mawakala wa ukusanyaji mapato. Hali hii pia imetokea katika halmashauri ya wilaya ya Songea.

7.2.4 Kuwepo kwa watumishi katika kituo kimoja cha kazi kwa muda mrefu

Hali ya kuwa na watumishi katika kituo kimoja kwa muda mrefu ilikuwa ikiripotiwa katika ripoti za ukaguzi tangu mwaka jana na bado inaendelea. Ukaguzi Maalum umebaini kuwa, kulikuwa na wafanyakazi katika idara ya fedha na idara nyingine ambao wamefanya kazi zaidi ya miaka 25. Hii ina madhara ya moja kwa moja kwenye uendeshaji wa halmashauri kwani inazuia ufanisi wa utendaji kazi. (Mfano ni halmashauri ya Manispaa ya Arusha, Dodoma na halmashauri ya wilaya ya Muheza)

Kutokana na kilichoonekana katika umiliki wa Kampuni ya Nyama Arusha, ni muhimu kwa halmashauri kuwa na mikakati sahihi juu ya uendeshaji wa miradi yake ya uwekezaji.

SURA YA NANE

8.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Kama ilivyoelezwa katika sura ya utangulizi kwamba, Ripoti hii ni muhtasari wa yale yaliyobainishwa katika ripoti za ukaguzi zilizotolewa kwa kila Halmashauri. Taarifa hizi zilizotolewa kwa Halmashauri pia zina mapendekezo juu ya kila suala lililobainishwa ambalo linahitaji maboresho. Maafisa Masuuli wa Serikali za Mitaa wanatakiwa kuandaa mipango ya utekelezaji juu ya kushughulikia na kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu na kuziwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa matakwa ya kifungu 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya mwaka 2008 na Kanuni 86 na 94 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009. Baada ya kuwasilisha mambo muhimu yaliyotokana na matokeo ya ukaguzi kwa mwaka 2011/2012 kwa hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika sura zilizotangulia, sasa niko katika nafasi ya kuja na hitimisho kwa ujumla pamoja na mapendekezo, ambayo kama yatakelezwa, yataimarisha usimamizi wa fedha katika uendeshaji wa Halmashauri.

8.1 Udhafu katika mikataba ya ukusanyaji wa mapato

Maboresho ya mapato ya Serikali za MitaayamesababishaSerikali za Mitaa kubinafsisha vyanzo zaidi vya mapato ya ndani.Hata hivyo,Serikali za Mitaa zimekutana na changamoto katikausimamiziwa makusanyo ya vyanzo vya mapato vilivyobinafsishwa ambazo zimetokana nasababuzifuatazo:

- **Ukosefu wampango thabiti kabla ya uamuza wa kubinafsisha vyanzo vya mapato**
Utafutaji wasoko la uhakika la ubinafsishaji haukufanyika kwa ufanisi kwenye Halmashauri.Hakuna ushahidi aukumbukumbu zinazoonesha kwamba, Halmashauri zilifanya utafiti wa upatikanaji wa mawakala wa

kukusanya mapato ambao watabeba majukumu ya Halmashauri katika ukusanyaji wa mapato. Pia, majukumu mapya ya msimamizi kwa ajili ya usimamiziwa mkataba kwa mawakala wa ukusanyaji mapato hayajawekwa bayana na uongozi wa Halmashauri. Aidha, upembuzi yakinifu haukufanyika kwa kina ili kuweka kiasi ambacho kinatarajiwa kukusanya kutoka kila chanzo cha mapato kama msingi wa ubinafsishaji.

- **Taratibu za kuwapata wakusanyaji mapato binafsi hazikufanyika kwa ufanisi**

Mawakala wa ukusanyaji wa mapato hawakupatikana kwa ufanisi kwa sababu ya ushindani mdogo kati ya wazabuni na ukosefu wa uwazi wa vigezo kwa ajili ya tathmini ya zabuni. Karibu nusu ya zabuni zilitangazwa katika mbao za matangazo za Halmashauri tu.

- **Mikataba hailindi maslahi ya Halmashauri**

Mikataba haikuandaliwa kwa nia yakulinda maslahi ya Halmashauri. Mkurugenzi wa Halmashauri hawezi kumshitaki wakala wa ukusanyaji mapato kwa kushindwa kuwasilisha kiasi chochote kinachozidi kiasi walichokubaliana. Kuna madhaifu katika kusimamia mikataba kwa baadhi ya Halmashauri.

- **Mapungufu katika kufuatilia utendaji wa mawakala wa kukusanya mapato**

Utendaji wa wakala wa ukusanyaji wa mapato haufuatiwi kwa ufanisi. Hii ni kwa sababu hakuna taarifa za uendeshaji zilizokuwa zikiandaliwa na mawakala hao wa ukusanyaji wa mapato na kuziwasilisha Halmashauri. Hakuna usuluuhishi wa taarifa uliokuwa ukifanywa na Halmashauri kati ya stakabadhi zilizotumiwa na mawakala na kiwango kilichowasilishwa Halmashauri. Uwasilishaji wa taarifa za uendeshaji na za vipindi haikuwa ni kigezo kilichotajwa kwenye mikataba

iliyosainiwa kati ya Halmashauri na mawakala wa ukusanyaji wa mapato.

- **Masharti ya mikataba ambayo hayajitoshelezi na hayafuatwi**

Masharti yaliyomo kwenye mikataba ya mawakala wa ukusanyaji wa mapato na masharti yaliyomo kwenye sheria ndogo ndogo za Halmashauri yanatekelezwa kwa nadra. Vilevile hakuna adhabu zinazotolewa kwa mawakala wa ukusanyaji mapato walioshidwa kuwasilisha kiasi walichokubaliana kwenye mkataba au wanaochelewa kuwasilisha mapato hayo. Kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, mapato ya kiasi cha Sh.4,466,028,478 yanayohusisha Halmashauri 56 hayakuwasilishwa na mawakala wa ukusanyaji mapato na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi yao. Kwa upande mwingine kumekuwepo na matukio ya ukiukwaji wa sheria zilizowekwa kwenye mikataba katika baadhi ya mawakala wa ukusanyaji mapato katika Halmashauri ambayo imepelekea mawakala hao kushtakiwa. Hata hivyo matokeo ya kesi hizo hupelekea Halmashauri kulipa fidia kubwa kuliko kiasi kilichokusanywa.

- **Vyanzo vya mapato vilivyobinafsishwa havikuwa vikifua tiliwa na mamlaka za juu**

Hakuna tathmini iliyofanywa na sehemu ya Fedha katika idara ya usimamizi wa huduma za Serikali za Mitaa (LGMSD) na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kuhusiana na taarifa za utekelezaji zilizowasilishwa na Halmashauri kila robo mwaka. LGMSD ilianda na kuchambua taarifa binafsi na taarifa jumuifu ambazo zimeonesha bajeti dhidi ya makusanyo halisi tu. Kuna haja ya OWM-TAMISEMI kutimiza wajibu wake wa usimamizi na udhibiti katika kuhakikisha kuwa, utendaji Halmashauri unakuwa wa viwango vya kukubalika.

Mapendekezo

Kulingana na matokeo ya ukaguzi na hitimisho, ninapendekeza yafuatayo:

- Mipango sahihi ifanywe kabla ya kufikia uamuzi juu ya kubinafsisha vyanzo vya mapato kwa mawakala binafsi ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa kina wa hali ya soko kwa ajili ya shughuli iliyotarajiwa. Upembusi yakinifu ufanywe kwa kina ili kuweka kiasi ambacho kinatarajiwa kukusanya kutoka kila chanzo cha mapato kama msingi wa kubinafsisha.
- Mchakato sahihi wa ununuzi ufuatwe ili kupata mzabuni sahihi kupitia ushindani. Hii ni pamoja na kutumia nyaraka za zabuni zenyenye viwango, utoaji wa muda wa kutosha kwa ajili ya wazabuni kuwasilisha zabuni zao, na mchakato sahihi wa tathmini ufanywe na wafanyakazi wenye utaalam.
- Mikataba kati ya Halmashauri na mawakala wa kukusanya mapato iandaliwe vema ili iweze kulinda maslahi ya halmashauri. Utendaji wa wakala wa ukusanyaji wa mapato ufuatiliwe kwa karibu ikiwa ni pamoja na mawakala kuwasilisha taarifa ya kila mwezi, robo na mwaka.
- Masharti ya mikataba yawekwekisheria na kutekelezwa.
- Kwa upande wa Serikali kuu na Ofisi ya Makatibu Tawala wa Mikoa (RAS), inapendekezwa kwamba, watoe msaada wa ushauri wa kitaalam na kiuongozi unaohitajika na Serikali za Mitaa juu ya masuala yanayohusiana na kubinafsisha vyanzo vya mapato.
- Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI inashauriwa kujenga uwezo kwa watumishi wa Halmashauri na madiwani ili kuwawezesha kusimamia vema ubinafsishaji wa vyanzo vya mapato. OWM-TAMISEMI pia inashauriwa kudai taarifa juu ya ukusanyaji wa mapato yanayotokana na vyanzo vya mapato vilivyobinafsishwa kutoka mamlaka za Serikali za Mitaa kwa nia ya kufuatilia vema na

kuwezesha kufanya tathmini ya utendaji Halmashauri kwa urahisi.

- Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) inashauriwa kuandaa nyaraka zazabuni zenyе viwango pamoja na mikataba ya ubinafsishaji wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.Hii italeta uthabiti katikashughuli za ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Kwa upande waWizara ya Fedha,inashauriwa kwamba isimamie vema mapato ya ndani ya Halmashauri na kutathminiripotiliyowasilishwa naOfisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI nakutoa maoni na mrejesho kwaHalmashauri.

8.2 Uboreshajiw makusanyo ya mapato ya Halmashauri kuitia vyanzo vya ndani

Kutoka miaka ya nyuma ilibainika kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa zina mikakati haba katika kuhakikisha kuwa makusanyo ya mapato ya kutosha yanapatikana kwa kuitia vyanzo vya ndani. Nimebaini kwamba, karibu Mamlaka za Serikali za Mitaa zote haziko makini katika kukusanya mapato yaliyopo katika himaya zao. Wala hazifuatilii fursa nyingine zilizopo katika kukusanya mapato ambayo yanaweza kuongeza wigo wao wa kifedha na kuongeza ukwasi na uhuru wa Halmashauri katika kujitegemea.

Katika mwaka huu wa ukaguzi, madhaifu mbalimbali yalibainika katika mfumo wa Serikali za Mitaa wa kukusanya mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani ikiwa ni pamoja na, vyanzo vichache vya mapato ya ndani, kutokuwepo kwa sheria ndogo ndogo kwa ajili ya baadhi ya vyanzomapato, Sheria ndogondogo za ukusanyaji wa mapato zilizopitwa na wakati kwa mfano baadhi ya sheria ndogondogo zimetungwa mwaka 1988, viwango vya mapato vinavyopaswa kukusanya ni vya chini sana na havijaboreshwa kulingana na mabadiliko ya

mazingira ya kiuchumi. Pia, kuna madhaifu katika usimamizi wa makusanyo ya mapato katika vyanzo vya mapato vilivyobinafsishwa kama vile, mikataba dhaifu iliyoandaliwa na halmashauri kwa ajili ya ubinafsishaji wa vyanzo vya ndani vya mapato, Upungufu wa ushindani wakati wa mchakato wa zabuni na mawakala wa mapato kutowasilisha kiasi cha mapato walichokubaliana. Aidha, udhaifu mwingine uliobainika unajumuisha, usimamizi dhaifu katika ukusanyaji wa kodi ya majengo uliofanywa na Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA), ufahamu mdogo wa walipa kodi, kukosekana kwa taarifa za kuaminika za walipa kodi na kwa ujumla ukosefu wa mikakati sahihi na usimamizi wa Halmashauri katika kuhakikisha kuwa ukusanyaji wa kiwango cha juu unafikiwa.

Pendekazo

Serikali Kuukupitia OWM-TAMISEMIlinapaswa kufanyatathmini ya kina yamfumo uliopowa kukusanya mapato ili kuhakikisha kwamba unazisaidia Halmashauri husika ili kuongeza mapato ya ndani ya kutosha. Halmashauri zinapaswa kupitisha sheria ndogo ndogo kwa ajili ya vyanzo vyote vya mapato ya ndani; hii itahakikisha kwamba kuna nguvu ya kisheria inayounga mkono ukusanyaji wa mapato na kwa ajili ya kuwadhibiti wale wanaokiuka. Halmashauri zinapaswa kufuatilia utekelezaji wa mikataba zilizoingia na mawakala wa ukusanyaji wa mapato. Viongozi wa kisiasa ni vema waelimishwe na mara nyingi wakumbushwe juu ya jukumu lao la kusaidia katika ukusanyaji wa mapato ya ndani.

8.3 Uchelewaji katika kuwasilisha taarifa za Utekelezaji wa Miradi

Pamoja na maelekezo yaliyotolewa na Katibu Mkuu wa OWM-TAMISEMI yaliyowataka Maafisa Masuuli wote kuandaa taarifa za utekelezaji wa miradi kwa kufuata

mfumo wa Kamati ya Bunge ya hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na kuziwasilisha pamoja na hesabu za mwisho kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa madhumuni ya ukaguzi kabla au tarehe 30 Septemba ya kila mwaka wa fedha, Halmashauri nyingi hazikutii maelekezo hayo.

Pendekazo

Maafisa Masuuli wote wanapaswa kuzingatia maelekezo yatakayowawezesha wakaguzi kukagua utendaji na utekelezaji wa miradi iliyopangwa kwa kipindi kinachokaguliwa na kuoanisha na taarifa nyingine za fedha; na kufanya ziara kwenye miradi husika ili kutathmini hali halisi ya miradi na mafanikio yaliyofikiwa. Hii itawasaidia wakaguzi katika kutathmini uwepo wa thamani ya fedha katika miradi iliyotekelawa na Halmashauri husika na kutoa taarifa juu ya matokeo ya tathmini hiyo.

8.4 Usimamizi wa Makatibu Tawala wa mikoa katika miradi ya maendeleo inayotekelawa na Halmashauri

Katika mwaka wa ukaguzi imebainika kuwa, moja ya Sekretarieti ya Mkoa ilifanya usimamizi wa miradi mara moja tu katika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2011/2012. Pia ilibainika zaidi kuwa Mhandisi wa Sekretarieti hakuwa sehemu ya timu ya usimamizi na ufuutiliaji. Zaidi ya hayo, tathmini ya taarifa za usimamizi wa miradi ilibaini mapungufu yafuatayo:

- Taarifa nyingi za usimamizi na ufuutiliaji hazioneishi ni miradi gani iliyotembelewa, udhaifu uliobainika na mapendekezo yaliyowasilishwa kwenye menejimenti za Halmashauri kuhusiana na miradi iliyotembelewa.
- Taarifa nyingi zinazotolewa zinajumuisha taarifa zilizotoka kwa Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika ambayo ina maana kwamba, usimamizi wa Mkoa unategemeana na kile walichokipata

kutoka kwa uongozi wa wilaya husika badala ya kuonesha mtizamo wao juu ya yale waliyoyabaini wakati wa kufanya ziara kwenye miradi iliyotekelozwa.

- Hakuna ushahidi kwamba, kuna ufuatiliaji unaofanywa juu ya utekelezaji wa maoni machache waliyoyatoa kwenye baadhi ya miradi.
- Hakuna ushahidi kwamba nyaraka zinazohusiana na miradi kama vile BOQ, MoU, Mkataba, taarifa za Bodi ya Zabuni, taarifa za tathmini na mambo kama hayo zinafanyiwa kazi wakati wa ziara ya kutembelea miradi iliyotekelozwa.
- Hakuna ushahidi wa kimaandishi kuthibitisha kuwa utekelezaji wa sheria ya manunuzi na kanuni katika miradi ikiwa ni pamoja na taratibu za zabuni, utoaji wa zabuni na malipo kwa makandarasi vilifanyiwa tathmini.
- Kutowashiriki kwa baadhi ya wajumbe wa timu kutoka Sekretarieti ya Mkoa katika ziara ya kutembelea miradi kunachangia mapungufu ya miradi inayotekelozwa katika ngazi ya Wilaya.
- Yaliyomo ndani ya taarifa zilizoandalisha hazikuthibitisha kuhalalisha thamani ya fedha zilizotumika katika usimamizi uliofanywa na Sekretarieti za Mikoa.
- Athari ya usimamizi unaofanywa na Sekretarieti za Mikoa kwa sekta zote inaweza isithibitike ikilinganishwa na fedha zilizotumika na hali halisi ya miradi iliyotekelozwa na Halmashauri zote.

Mapendekezo

Uongozi wa Sekretarieti ya Mkoa unapaswa kutunza orodha ya miradi yote iliyotekelozwa katika ngazi ya Halmashauri na kufanya usimamizi kwa kutembelea miradi itakayoichagua bila kuongozwa na viongozi wa Wilaya.

- Uongozi wa Sekretarieti ya Mkoa unapaswa kuhakikisha kwamba, nyaraka kuhusiana na miradi kama vile BOQ, MoU, nyaraka za Mikataba, taarifa za Bodi ya Zabuni, ripoti ya tathmini na mambo kama hayo, zinafanyiwa tathmini wakati wa zoezi la usimamizi na kama

inawezekana kuhudhuria baadhi ya mikutano ya kazi inayofanyika katika sehemu inapotekelezwa miradi.

- Ufuatiliaji wa kina wa mapendekezo yaliyotolewa ufanyike wakati wa usimamizi.
- Uongozi wa Sekretarieti ya Mkoa unapaswa kuhakikisha kwamba, usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hasa katika Halmashauri unafanywa angalau mara moja katika kila robo na Wahandisi wanapaswa kushiriki katika zoezi hilo.

8.5 Kuendelea kula njama kati ya watumishi wa Halmashauri na wafanyakazi wa Benki katika kufanya udanganyifu wa fedha za Halmashauri

Ukaguzi ulibaini kuwa, licha ya kutoa taarifa ya matumizi mabaya ya fedha za Umma kulikofanyika kwa njia ya kula njama kati ya watumishi wa Halmashauri wasio waaminifu na maafisa wa Benki katika ripoti zangu za miaka iliyopita, suala hilo limejirudia katika mwaka huu wa ukaguzi. Ukaguzi maalum ulibaini kwamba katika Halmashauri mbili tofauti (Halmashauri ya Manispaa Temeke na Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa) kwa kipindi cha ukaguzi, zimebainika kuwa na baadhi ya watumishi wa Halmashauri na Benki, huku wakijua, walivunja sheria kwa kula njama na kufanya ubadhirifu wa fedha za umma. Hii ni kinyume na taratibu zilizowekwa kati ya Benki na Halmashauri pamoja na miongozo mingine ya Taasisi za fedha kwa ujumla. Hali hii inaonesha kuwa, mbali na kuwa sehemu ya udhibiti wa matumizi mabaya ya fedha, Benki husika zimekuwa ni njia ya kufanikisha -udanganyifuwa watumishi wa Halmashauri wasio waaminifu.Ubadhirifu uliofanywa ungeweza kudhibitiwa kama zisingekuwepo njama za pamoja kati ya watumishi hao wa Halmashauri na Benki. Wakativitendo hivyo vikifanyika, wahusika hawakujulikana kwa muda mrefu. Hii ni ishara ya udhibiti dhaifu wa ndani juu ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaaa mbao hauwezi kutambua makosa na

vitendo vya ulaghai vinavyoendelea katika uendeshaji wa kawaida wa Halmashauri.

- **Mapendekezo**

Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na Serikali kwa jumla zinapaswa kuja na hatua muafakaza kukabiliana na tabia hii ya ubadhirifu wa fedha za umma kwa kushirikisha taasisi za kibenki ambazo zimekuwa zikiaminiwa kama sehemu ya udhibiti katika kulinda fedha za umma. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na Halmashauri wanapaswa kuweka mfumo imara wa kuwa chunguza watumishi wake.

- Matukio yanayojirudia ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa yanaashiria udhibiti dhaifu wa ndani. Kwahiy, inashauriwa kwamba Halmashauri kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI zinapaswa kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani katika usimamizi wa fedha za umma ikiwa ni pamoja na utendaji kazi wa ufanisi wa vitengo vya ukaguzi wa ndani.
- Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuhakikisha kwamba salio la benki la kila siku katika akaunti za kila Halmashauri zinajulikana kwa madhumuni ya kutambua muamala wowote ambao si wa kawaida uliofanyika katika akaunti husika. Aidha, usuluhihi sahihi wa benki uandaliwe kila mwezi na kutiwa saini na Afisa Masuuli.
- Hatua stahiki za kinidhamu na kisheria zinapaswa kuchukuliwa dhidi yawatumishi wote ambao kwa njia moja au nyingine, walihusika katika utovu wa nidhamu wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali.
- Taasisi za kibenki zimekuwa zikiaminiwa hasa katika kutunza fedha kwa niaba ya wadau wao ikiwa ni pamoja na Serikali za Mitaa. Hata hivyo, katika matukio hayo benki imechangia kwa hasara ya fedha za umma. Kwa hiyo Serikali inapaswa kutoa maelekezo kwa taasisi za kibenki ikiwataka kwamba wafanyakazi ambao

wamehusika katika udanganyifu huo wanapatikana na kuwachukulia hatua za kisheria .

8.6 Udmaifu katika mifumo ya Udhibiti wa ndani

Licha ya udhaifu uliokwisha bainika katika uhasibu na mifumo ya udhibiti wa ndani, kuna baadhi ya madhaifu ambayo yalibainishwa wakati wa ukaguzi ambayo yanaweza kuathiri umuhimu na kuaminika kwa taarifa za fedha zilizoandaliwa. Kama hayatazingatiwa, yanaweza kuharibu usahihi wa taarifa za fedha. Baadhi ya mapungufu ambayo yanahitaji usimamizi makini ni kama ifuatavyo:

- Vitabu vya kukusanya mapato ambavyo havikuwasilishwa kwa ukaguzi.

Kutowasilishwa kwa vitabu vya kukusanya mapato kwa ajili ya ukaguzi ni tatizo sugu katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kiutaratibu, wakusanyaji mapato wanatakiwa kuwasilisha kwa Mweka Hazina wa Halmashauri vitabu vya mapato vilivyotumika vikionesha stakabadhi zilizotumika na zile ambazo hazijatumika kabla ya kupokea vitabu vipyta. Katika hali halisi, utaratibu huu haukuwa ukifuatwa kikamilifu. Ni busara kuamini kuwa, vitabu vya kukusanya mapato ambavyo havikuwasilishwa kwa ukaguzi vilitumika kufanya ubadhirifu wamakusanyo ya mapato. Inawezekana kwamba, mapato yaliyokusanya hayakuwa yakiwasilishwa Halmashauri.

Kwa hiyo, kuna haja ya kuboresha taratibu za kutumika katika kukusanya mapato kwa kuanzisha udhibiti na michakato ya kufuatilia na ratiba za kuwasilisha vitabu vilivyotumika. Aidha,W akurugenziwa Halmashauri wanapaswa kufanya mafunzo mbalimbali kujenga uwezo wa watumishi wanaoshiriki katika ukusanyaji wa mapato hususan kwa Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji na mawakala wa kukusanya mapato.

- **Hati za malipo ambazo hazikuwasilishwa kwa ukaguzi**
Tatizo la Hati za malipo kutowasilishwa kwa ukaguzi ni moja ya kiashiria cha kukosa ufanisi kwa mfumo wa udhibiti wa ndani. Kwa kuwa hili limekuwa ni tatizo linaloendelea kujirudia katika Halmashauri nyingi kwa muda mrefu, napenda kuzikumbusha menejimenti za Mamlakaza Serikali za Mitaa juu ya wajibu wao wa msingi katika kuhakikisha kwamba, nyaraka muhimu za Halmashauri kama Hati za Malipo zinatunzwa vema.
- **Malipo ya Mishahara kwa watumishi hewa**
Malipo ya mishahara kwa watumishi waliokoma utumishi ni tatizo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Napendekeza kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutoza tozo kwa maafisa wale ambao kwa namna moja au nyingine wamechangia malipo ya mishahara kwa watumishi ambao utumishi wao umeshakoma.
- **Kamati za Ukaguzi**

Kutokana na utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya uhasibu katika sekta ya Umma, kulikuwa na mabadiliko muhimu katika masuala ya kutolewa taarifa kwenye taarifa za fedha. Kamati ya ukaguzi inapaswa kupewa fursa ya kutosha kuititia taarifa za fedha kabla ya kuwasilishwa kwa wakaguzi. Aidha, mafunzo juu ya mazingira na tafsiri ya taarifa za fedha yanapaswa kutolewa kwa wajumbe wa kamati za ukaguzi waliochaguliwa ilikuwawezesha kuelewa vema takwimu zilizowasilishwa.

Mapendekezo

Halmashauri kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani na Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala Mikoa na Serikali za Mitaa wanapaswa kuweka mpango kabambe wa kushughulikia masuala yanayohusiana na udhibiti wa

mfumo wa ndani na masuala ya utawala bora ambayo yameainishwa. Mpango huo uweke wazi malengo, hatua na makadirio ya muda kwa ajili ya utekelezaji.

8.7 Kuimarisha Usimamizi wa Rasilimali Watu

Rasilimali watu ni kipengele muhimu katika utendaji wa taasisi yoyote ikiwa ni pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Serikali za Mitaa zina sekta mbalimbali ambazo zinahusisha makundi mbalimbali ya rasilimali watu ikiwemo sekta ya elimu, afya na kilimo. Pamoja na mgawanyo huu, usimamizi bora wa rasilimali watu ni muhimu kwa ajili ya utoaji na ufanisi wa huduma. Hata hivyo ukaguzi uliainisha mapungufu kuhusiana na usimamizi wa rasilimali watu ikiwa ni pamoja na upungufu katika usimamizi wa mishahara kama vile malipo ya mishahara kwa watumishi hewa, watumishi kupokea chini ya moja ya tatu (1/3) ya mshahara, msongamano wa watumishi katika maeneo ya mijini, baadhi ya wafanyakazi kukaimu katika nafasi za juu kwa kipindi cha muda mrefu na uhamisho usiofaa kwa watumishi.

Mapendekezo

Serikali za Mitaa zishirikiane na Ofisi ya Rais -Utumishi wa Umma na Ofisi ya Waziri Mkuu- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kuwa kuna mfumo endelevu wa kufuatilia kiwango cha watumishi na kuchukua hatua mathubuti kwa wakati ili kujaza nafasi zilizo wazi ili kuboresha utoaji huduma katika sekta ya Umma. Imeonekana kuwa kubadilishwa mara kwa mara kwa watumishi wa Halmashauri kumechangia kupunguza uwajibikaji ambako kunaathiri utendaji kazi.

- Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inatakiwa kuhakikisha usawa wa mgawanyo wa watumishi unafanyika katika Halmashauri zote badala ya kuajiri watumishi wengi katika miji na Halmashauri za Manispaa. Hii itapunguza udhaifu katika utendaji

kazi kwa baadhi ya serikali za mitaa, na kuinua kiwango cha utoaji huduma kwa jamii.

- Kuwepo kwa watumishi wanaokaimu nafasi za juu katika Serikali za Mitaa kwa muda mrefu bila kuthibitishwa kunaonyesha udhaifu kwa menejimenti na hakuendani na kanuni za utawala bora. Menejimenti za Halmashauri zinapaswa kuangalia suluhu nzuri ili kupunguza tatizo hilo kwa kuwathibitisha watumishi ambao wamekuwa wakikaimu.
- Mbali na uvunjaji wa maagizo pia kuna kukosekana motisha kwa watumishi katika kufanya kazi kwa ufanisi kwa sababu ya kuwa na mikopo iliyokithiri inayopelekeea kushuka kwa kiwango cha utendaji kazi. Halmashauri zinatakiwa kuwaelimisha watumishi wake kuhusu matatizo ya mikopo iliyopindukia kutoka kwenye taasisi mbalimbali za fedha na kuhakikisha kuwa maombi ya mikopo yanapitia kwa Afisa Masuuli na maafisa Rasilimali watu kwa madhumuni ya kudhibiti. Serikali inapaswa kuja na mkakati wa kuwa na motisha kwa watumishi wake hasa wale wa kipato cha chini. Hii itasaidia kuepuka mikopo iliyokithiri kwa watumishi wa Halmashauri.

8.8 Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Sekta za Umma (IPSSAs)

Serikali kupitia kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilitoa mwongozo kupitia barua yenye kumbukumbu Na. CA: 26/307/01A/79 ya tarehe 28 Septemba, 2009 ikielekeza Mamlaka ya Serikali za Mitaa kote nchini kuandaa taarifa zao za fedha kwa kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Sekta za Umma (IPSSAs) kuanzia mwaka wa fedha 2008/2009. Ilibainika kuwa hadi tarehe 30 Juni, 2012 (mwaka mmoja kabla ya kutimia kipindi cha mpito cha miaka mitano (5) walichopewa ili kukamilisha

mabadiliko) kulikuwa na baadhi ya ofisi za Serikali za Mitaa ambazo hazikuonesha thamani ya Mali za kudumu inazomiliki, au thamani ya Mali za kudumu zilizoko chini ya Halmashauri hizo, hivyo hali hii imesababishia hesabu za Halmashauri hizo kutokuwa sahihi kwa kukosa kuonesha thamani ya Mali za kudumu.

Pia kuna mapungufu katika kupangilia na kuonesha orodha ya mali/vitu, madeni na mali tarajiwa kutoa taarifa kwa pande zinazohusiana na Halmashauri na Uharibifu wa mali kwa inavyotakiwa na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Sekta za Umma (IPSSAs) 12,14, 19, 20 na 21. Hali hii inabainisha kuwa hatua zilizochukuliwa na Serikali na Serikali za Mitaa husika kuhama na kuandaa taarifa za fedha kwa kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Sekta za Umma (IPSSAs) kwa kipindi cha mabadiliko hayo cha miaka mitano hazijatekelezwa ipasavyo.

Mapendekezo

Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali inatakiwa kuzijengea uwezo Serikali za Mitaa katika uandaaji wa Taarifa za fedha zinazofuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Sekta za Umma (IPSSAs) kwa njia ya mafunzo husika. Mbali na hayo Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali zinapaswa kuweka mfumo thabiti wa ufuatiliaji wa Serikali za Mitaa ili kuhakikisha na kujiridhisha kwamba Serikali za Mitaa kote nchini zinajunga katika mfumo mpya wa kuandaa taarifa za fedha kwa kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Sekta za Umma (IPSSAs) kabla ya kumalizika kwa muda wa mpito wa miaka mitano.

Serikali za mitaa zinapaswa kuboresha mfumo wa ndani wa uaandaaji wa taarifa za fedha hasa kwa kuendana na Mwongozo wa Kihasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 2009.

8.9 Udhifu Uliobainika Katika Kaguzi Maalum

Kutokana na kaguzi maalum, udhifu mkubwa ulionekana katika mfumo wa udhibiti wa ndani, kesi za wizi wa kukusudia na rushwa kwenye mikataba, manunuzi, mapato na uendeshaji wa Halmashauri ziliripotiwa.

Mapendekezo

Hivyo, kwa kuzingatia matokeo ya kaguzi maalum, napendekeza kwamba;

- Pamoja na kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani kama hatua ya kutatua udhifu uliobainika katika kaguzi maalum hatua za kisheria zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya maafisa ambao wamehusika katika taarifa hizo.
- Wanasheria wa halmashauri wana jukumu la msingi la kuhakikisha makubaliano ya mikataba yanazingatiwa na kufanyika ipasavyo. Wajibu huo ni kuhakikisha kwamba kesi zote zitokanazo na uvunjaji wa mikataba zinawasilishwa mahakamani na kusimamiwa.
- Maafisa Masuuli wanatakiwa kuteua wajumbe wa Bodi ya Zabuni ya Umma na Kanuni zake yanatakiwa yatolewe kwao kila mara. Kitengo cha Manunuzi kama wataalamu katika Manunuzi wanapaswa kuendelea kutoa ushauri kwa wajumbe wengine kwenye maswala ya kitaalamu wakati wa vikao vyta ya bodi ya zabuni badala ya kuwapotosha kama ambavyo imekuwa ikibainika katika baadhi ya kaguzi maalum.
- Ili kudumisha nidhamu katika maeneo ya kazi, napendekeza kwamba baadhi ya watumishi waliothibitika kuwa na utovu wa nidhamu pia waliohakikishwa kuwa na makosa kwenye utumishi wao wa umma, hatua madhubuti za kinidhamu

zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya maafisa husika badala ya kuwahamishia vituo vingine vyakazi.

- Wakuu wa Idara katika Halmashauri nyingi wanafanya kazi kwa kukaimu. Hii ni njia moja wapo inayoathiri utendaji kazi wao. Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa inapaswa kuhakikisha maafisa hao ambao wenye uwezo na ujuzi husika wathibitishwe katika nafasi hizo.
- Kitengo cha fedha ni sehemu muhimu katika utendaji wa Halmashauri hasa katika kubaini vyanzo muhimu vyamapato. Ili kuweza kubainisha na kukusanya mapato, halmashauri inahitaji kuwa na watumishi wenye sifa na uwezo, na kiwango kikubwa cha uadilifu. Hivyo napendekeza kwamba watumishi katika kitengo cha fedha ambao hawana sifa husika wasomeshwe ili kuwa na sifa zinazotakiwa.
- Ili kupunguza wizi wa makusanyo ya mapato ya ndani, napendekeza kwamba mapato yote yasiyokusanywa kwa njia ya mikataba, ambayo kiasi kinacholipwa kinafahamika, yalipwe kwa kutumia hundi zilizofungwa au yapelekwe moja kwa moja benki.
- Halmashauri zinapaswa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 na Kanuni zake. Kitengo cha manunuzi kitekeleze majukumu yake kwa kuzingatia sheria, sera na taratibu zilizowekwa.
- Halmashauri zinapaswa kuanzisha utaratibu wa kutoa mafunzo kwa maafisa wake wanaohusika katika kubaini na kukusanya mapato ya ndani ili kuboresha uwezo wao. Hii itapelekea kuwa na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Hata hivyo, haya ni sehemu tu ya mapendekezo ya jumla juu ya ukaguzi maalum, lakini sehemu kubwa ya masuala yaliyojitekeza wakati wa ukaguzi maalum yametolewa mapendekezo kama ilivyoainishwa hapo juu.

8.10 Udhaifu uliobainika katika Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo

Mfuko wa Maendeleo ya jimbo ulianzishwa na Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Na. 16 ya mwaka 2009 kwa ajili ya kuendeleza miradi katika kila jimbo. Mfuko huo unatoa rasilimali za kusaidia jamii katika maeneo yaliyopewa vipaumbele kama maji, elimu, afya, miundo mbinu na Kilimo. Mapitio ya utumiaji na uwajibikaji wa fedha za mfuko huo yalibaini mapungufu kama vile;

- Kulikuwa na kiasi kikubwa cha fedha ambazo hakikutumika katika mwaka wa ukaguzi. Hii inaonesha kuwa miradi mingi ya jamii haikutekelezwa kwa wakati.
- Hakukuwa na uandaaji na huwasilishwaji kumbukumbu za mapato na matumizi ya kila jimbo kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.
- Baadhi ya miradi haikuibuliwa na wanajamii, malipo yalikuwa yanafanyika kutoka kwenye mfuko bila kuidhinishwa na kamati ya mfuko, na kulikuwa na mabadiliko ya matumizi ya fedha ya mradi husika kwenda kwenye mradi mwingine kinyume na maelekezo ya mfuko huo.
- Baadhi ya Halmashauri hazikufungua akaunti mahususi kwa ajili ya fedha za mfuko wa jimbo, badala yake fedha zilikuwa zikitunzwa na kutumika katika akaunti ya maendeleo.
- Katika baadhi ya maeneo haikuweza kubainika kama manunuvi yaliyofanyika kuititia fedha za mfuko huo yalikuwa yakipitishwa na Bodi ya Zabuni ya Halmashauri.
- Wakati mwingine fedha za mfuko wa maendeleo ya jimbo zilitumika kununua jezi na mipira kwa ajili ya vikundi mbalimbali vyta michezo na kudhamini shughuli mbalimbali za kidini ambazo hazikuwa na uhusiano wa maendeleo ya umma kwa ujumla.

Mapendekezo

Menejimenti za halmashauri pamoja na kamati za mfuko zinapaswa kutumia fedha za mfuko kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Na. 16 ya mwaka 2009 na kuzingatia mfumo wa kisheria wa usimamizi wa rasilimali za umma.

8.11 Udhaifu katika utekelezaji wa bajeti

Bajetini nyenzo muhimu yamichakatoya fedha mipango, udhibitina tathmini ya Serikali za Mitaa. Kwa asiliyake, ni njia ya kugawa rasilimali ya kufikia malengo. Ni chombo cha usimamizi kwa ajili ya kupanga pamoja kama njia ya kudhibiti fedha kuhakikisha kwamba, kama inavyowezekana, malengo yaliyopangwa yanafikiwa.

Katika mwaka wa ukaguzi, mapungufu yaliyojitokeza katika ukaguzi wa bajeti ya Halmashaurini pamoja na yafuatayo:

- Bunge ilipitisha bajeti kwa baadhi ya vifungu vyta fedha za maendeleo vyenye jumla ya Sh.595,064,422,505 katika Halmashauri 113. Hata hivyo ni Sh. 345,568,067,477 tu ndizo zilizopokelewa na Halmashauri husika, na kufanya kuwepo upungufu wa Sh. 249,496,355,027 sawa 42%.
- Hadi mwisho wa mwaka kulikuwa na bakaa ya fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha Sh. 188,405,740,589 ambayo ni sawa na 35% ya kiasi cha fedha zilizokuwepo katika mwaka husika. Kiasi hicho cha fedha kimehusisha Halmashauri zipatazo 132.
- Pia fedha kwa ajili ya Matumizi ya kawaida zilitolewa pungufu kwa Sh.171,002,394,849 (sawa na 11%) katika Halmashauri 87. Bajeti iliyoidhinishwa ilikuwa Sh.1,618,877,128,175 wakati kiasi cha fedha kilichopokelewa na Halmashauri kilikuwa ni Sh.1,447,874,733,324 tu.

- Katika mwaka husika Sh.124,594,256,692 sawa na 5.4% ya fedha za matumizi ya kawaida zilizokuwepo hazikutumika.
- Jumla ya kiasi cha fedha Sh.1,688,848,579 katika Halmashauri 38 kimetumika nje ya Bajeti iliyoidhinishwa bila kupata kibali kutoka katika mamlaka husika kinyume na Kifungu 10(3) cha Sheria ya Fedha Na.9 ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000).
- Fedha zilizohamishwa kutoka Akaunti moja kwenda Akaunti nyingine kiasi cha Sh.2,673,964,170 hazikuweza kurejeshwa katika Akaunti husika katika Halmashauri 45.
- Kuchelewa kutolewa kwa fedhani sababu nyingine kubwa iliyochangia Halmashauri kwenda kinyume na bajeti na matumizi halisi ya maendeleo. Halmashauri hupokea fedha za maendeleo kutoka katika mfuko wa pamoja ambazo huletwa katika robo ya mwisho wa mwaka wa fedha. Uguzi ulibainisha kuwa fedha hizo hupelekwa mbele kwa mwaka wa fedha unaofuata. Uchelewashaji wa fedha na uharaka wa matumizi kufutia kipindi cha mwisho wa mwaka wa fedha hupelekea kutokuwepo ufanisi na hasara ya ubora katika matumizi.

Mapendekezo

Menejimenti ya Halmashauri inapaswa kufanya ufuatiliaji kwa Wizara ya Fedha ili kuhakikisha fedha inatolewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa na kama sio, basi warekebishe bajeti zao ziendane na ukweli. Aidha, Halmashauri na Serikali za Mitaa wanashauriwa kuhakikisha taratibu za matumizi ya ruzuku zinazingatiwa, kwa kuongeza uwezo wa upatikanaji wa ruzuku ambayo itaongeza kiwango cha utoaji huduma.

8.12 Uboreshaji wa Usimamzi wa Miradi

Matokeo juu ya usimamizi wa mradi unaonyesha kuwa usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi haukujitosheleza. Kulikuwa na usimamizi hafifu kwa baadhi ya miradi ambayo haikutekelezwa katika viwango, kuchelewa kukamilika kwa miradi ndani ya muda uliopangwa imepelekea kuwa na miradi mingi ambayo haikuishakwa wakati na kuhamishiwa mwaka mwingine wa fedha, na miradi mingine iliyomalizika kutowekwa katika matumizi. Usimamizi dhaifu na ufuatiliaji wa miradi unaweza kusababisha gharama kubwa za ziada.

Mapendeleko

- Menejimenti ya Halmashauri inapaswa kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa mara kwa mara na na uthamini wa mfumo ili kugundua na kukabiliana na changamoto zinazojitokeza na kuhakikisha mipango ya miradi ya maendeleo inatekelezwa kama ilivyopangwa.
- Fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri zinatakiwa ziendane na bajeti iliyoidhinishwa ili kutekeleza miradi ya maendeleo na hatimaye kuongeza kasi ya maendeleo katika jamii.

8.13 Kuhamia Mfumo funganifu wa Usimamizi wa Fedha(IFMS) kutoka Epicor7.3.5 kwenda Epicor9.05 iliyopitishwa na Serikali ya Tanzania

Katikamwaka wa fedha 2012/2013, Serikali ya Tanzania ilifanya mabadiliko makubwa katika mfumo wake wa kifedha wa kiuhasibu ambao unatakiwa kuongozwa na mfumo uliopo makao makuu kwa upande wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Mabadiliko hayo yanahusisha utumiaji watoleo jipya la mfumo uitwao Epicor9.05

ambao ni mfumo wa Fedha wa Kihasibu unaotumika kwa shughuli za kiuhasibu za kila siku kwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Uhamiaji huu unahusisha mabadiliko kwenye Miundombinu ya teknohama ya serikali ili ikiwezekana ukubaliane na mazingira ya uendeshaji wa mfumo wa Epicor9.05.

Uhamiaji huu wa kwenda mfumo mpya unahusisha Halmashauri zote na Wizara zote ilikufanya shughuli zao kwenye hifadhi taarifa ambazo zitakuwa katika Ofisi za TAMISEMI mkoa wa Dodoma na Ofisi za Mhasibu Mkuu (ACC-GEN) katika Wizara ya Fedha kupitia Mtandao wa “Wide Area Network” (WAN) ambao shughuli zote za kifedha zitahifadhiwa kwenye kihifadhi taarifa cha TAMISEMI na kwa kihifadhi taarifa cha Mhasibu Mkuu wa Serikali.

Uhamiaji huu, utaathiriwa na mpangilio wa kijiografia wa Halmashauri zilivyotawanyika Tanzania nzima, kwani sehemu nyingine hazina umeme na hazina huduma za mtandao wa kompyuta, wakati mfumo huu mpya unahitaji kusiwe na kikomo cha kuwepo mtandao; pia uundwaji wa kiunganishi hicho utakuwa mgumu hasa ukizingatia kihifadhi taarifa hicho kitakuwa kimewekwa TAMISEMI Dodoma na kutakiwa kisambaze taarifa kwenye Halmashauri zote. Inapaswa kuchukuliwa tahadhari ya kukabiliana na changamoto zitakazojitokeza wakati wa utekelezaji wa mfumo fonganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) Kutokana na ukweli kwamba mfumo wa uhasibu wa sehemu moja kwa Halmashauri zote zilizopo Tanzania nzima pamoja na miundombinu ya teknolojia ya habari bado ni mfumo mpya kwa Halmashauri za Tanzania, umakini unatakiwa kuzingatiwa katika changamoto

zinazoweza kujitokeza. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:

- Jiografia ya maeneo zilizoko Halmashauri ndani ya Tanzania;
- Teknolojia inayotumika kwa kuunganisha Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha IFMS(VSAT & fiber-Nzuri, ADSL&Radio- Mbaya);
- Uhaba wa rasilimali fedha;
- Miundo mbinu ya mawasiliano ya ndani ya kitekinologia (LAN) katika Halmashauri isiyo thabiti.
- Hofu ya Halmashauri zote kijiunga katika mfumo wa pamoja.
- Uhaba wa wataalamu kutoka TAMISEMI wa kusaida pale utendaji wa mfumo huo katika Halmashauri zetu.
- Changamoto ya kuwepo kwa umeme wa uhakika muda wote
- Uwezo katika ngazi ya uhasibu katika Serikali za Mitaa juu ya kutumia mfumo wa kiuhasibu wa Epicor9.05 na utayari wa kutumia mfumo huo wa pamoja nchini kote.

Pendekazo

Kutokana na mfumo huo wa kihasibu, ninatoa angalizo juu ya changamoto hizo zilizobainishwa ili kuimarisha na kuboresha uandaaji wa Taarifa za Fedha kutoka katika mfumo wa Epicor9.05 kwa wakati kuhusu taarifa ya matumizi ya fedha za Serikali za Mitaa. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI wanapaswa kufanya mafunzo ya mara kwa mara ili kuwajengea uwezo wafanyakazi wanaoshiriki kuandaa Taarifa za Fedha kutoka katika mfumo wa Epicor9.05 ambao kuna moduli nyingi kwa ajili ya kazi mbalimbali ndani yake.

VIAMBATISHO

Kiambatisho (i)

Makosa yaliyomo kwenye taarifa za fedha zilizowasilishwa katika mwaka 2011/2012

Na.	Halmashauri	Jumla ya matumizi	Jumla ya Makosa			
			Malipo pungufu	% ya Malipo pungufu	Malipo zaidi	% ya Malipo zaidi
1	H/M Arusha	34,784,318,000	306,510,866	0.9%	3,006,910,000	8.6%
2	H/W Karatu	18,935,692,938	242,593,184	1.3%	247,302,429	1.3%
3	H/W Monduli	16,422,811,550	28,126,484,383	171.3%	20,479,250	0.1%
4	H/W Ngorongoro	11,441,599,462	508,927,099	4.4%	127,920,060	1.1%
5	H/W Meru	26,007,088,049	233,127,379	0.9%	-	0.0%
6	H/W Longido	10,985,002,000	659,630,000	6.0%	1,359,761,578	12.4%
7	H/W Bagamoyo	23,681,421,718	979,693,325	4.1%	308,230,513	1.3%
8	H/W Kibaha	10,241,583,973	2,919,309,098	28.5%	1,124,087,658	11.0%
9	H/Mji Kibaha	13,219,584,792	-	0.0%	689,407,758	5.2%
10	H/W Mafia	18,141,703,472	35,591,187	0.2%	6,187,500	0.0%
11	H/W Rufiji/Utete	18,845,955,861	107,362,090	0.6%	728,713,949	3.9%
12	H/M Kinondoni	85,450,824,774	1,208,795,287	1.4%	46,884,306	0.1%

13	H/W Bahi	13,227,250,466	138,639,148	1.0%	4,538,216,702	34.3%
14	H/M Dodoma	27,737,333,179	546,710,071	2.0%	3,292,199,110	11.9%
15	H/W Kondoa	28,912,289,268	1,950,268,218	6.7%	2,441,138,757	8.4%
16	H/W Mpwapwa	18,936,969,607	2,377,400,790	12.6%	2,158,654,523	11.4%
17	H/W Bukoba	19,408,713,170	277,000,000	1.4%	-	0.0%
18	H/W Karagwe	19,599,050,182	393,131,640	2.0%	149,717,362	0.8%
19	H/W Muleba	23,176,957,849	181,949,510	0.8%	-	0.0%
20	H/W Ngara	18,812,821,787	1,042,729,866	5.5%	1,265,148,008	6.7%
21	H/W Missenyi	13,489,908,895	237,478,490	1.8%	-	0.0%
22	H/W Kasulu	27,161,183,946	14,897,234,996	54.8%	252,888,831	0.9%
23	H/W Kibondo	23,393,703,000	7,940,494,000	33.9%	2,303,651,000	9.8%
24	H/W Kigoma	25,470,347,000	204,917,533	0.8%	-	0.0%
25	H/M Kigoma/Ujiji	15,064,250,213	-	0.0%	71,034,213	0.5%
26	H/W Rombo	29,073,206,773	2,019,481,080	6.9%	-	0.0%
27	H/W Babati	18,872,394,000	4,457,756	0.0%	-	0.0%
28	H/W Hanang	15,898,541,000	730,777,491	4.6%	13,532,000	0.1%
29	H/W Kiteto	13,678,058,673	367,593,300	2.7%	101,246,853	0.7%
30	H/W Mbulu	22,586,477,732	-	0.0%	926,045,587	4.1%
31	H/W Simanjiro	8,984,970,565	258,245,652	2.9%	1,240,226,131	13.8%
32	H/Mji Babati	10,284,428,631	22,633,545	0.2%	-	0.0%
33	H/W Illeje	8,440,175,864	24,905,092	0.3%	7,500,000	0.1%

34	H/W Mbeya	9,744,546,854	14,053,148	0.1%	14,053,148	0.1%
35	H/W Rungwe	34,992,227,329	2,685,521,017	7.7%	2,253,467,152	6.4%
36	H/W Kilombero	26,863,545,224	888,509,778	3.3%	1,632,984,662	6.1%
37	H/W Kilosa	35,450,383,117	4,485,115,519	12.7%	1,275,029,867	3.6%
38	H/W Morogoro	18,267,072,206	2,286,651,484	12.5%	12,566,637,223	68.8%
39	H/M Morogoro	30,958,027,883	2,162,639,547	7.0%	3,607,128,490	11.7%
40	H/W Ulanga	18,801,728,240	758,216,999	4.0%	1,061,890,377	5.6%
41	H/W Mvomero	20,267,522,098	582,253,070	2.9%	2,728,355,675	13.5%
42	H/W Masasi	24,593,432,384	149,995,106	0.6%	510,019,394	2.1%
43	H/M Mtwara	20,279,329,000	73,500,000	0.4%	23,818,577	0.1%
44	H/W Newala	13,582,006,855	3,687,748,561	27.2%	1,082,633,249	8.0%
45	H/W Mpanda	35,335,408,000	29,721,000	0.1%	4,747,257,000	13.4%
46	H/Mji Mpanda	9,484,054,569	809,832,738	8.5%	809,832,744	8.5%
47	H/W Nkasi	12,124,370,083	9,595,480,828	79.1%	2,979,754,868	24.6%
48	H/W Sumbawanga	26,450,751,753	1,522,640,699	5.8%	6,347,700,047	24.0%
49	H/M Sumbawanga	14,607,773,873	394,181,291	2.7%	215,519,856	1.5%
50	H/M Mbinga	32,809,132,764	226,057,540	0.7%	592,375,000	1.8%
51	H/M Songea	16,793,514,623	85,728,587	0.5%	40,251,906	0.2%
52	H/W Songea	15,508,327,525	47,388,400	0.3%	744,215,182	4.8%
53	H/W Tunduru	19,422,286,817	9,747,364,622	50.2%	9,400,636,574	48.4%
54	H/W Namtumbo	12,695,331,694	2,166,759,206	17.1%	1,045,922,636	8.2%

55	H/W Iramba	23,411,172,000	2,133,227,332	9.1%	1,223,769,570	5.2%
56	H/W Manyoni	16,001,122,292	2,890,646,040	18.1%	-	0.0%
57	H/M Singida	10,107,255,906	421,592,686	4.2%	-	0.0%
58	H/W Handeni	17,855,615,763	416,203,418	2.3%	285,945,441	1.6%
59	H/W Korogwe	2,210,266,696	2,210,266,696	100.0%	3,228,448	0.1%
60	H/Mji Korogwe	7,727,649,697	303,860,597	3.9%	628,909	0.0%
61	H/W Lushoto	265,736,433	275,172,929	103.6%	275,172,929	103.6%
62	H/W Pangani	10,627,997,244	3,110,330,956	29.3%	11,220,638	0.1%
63	H/Jiji Tanga	24,649,915,769	1,872,619,156	7.6%	-	0.0%
64	H/W Kilindi	7,984,133,064	245,732,900	3.1%	2,483,704,739	31.1%
65	H/W Mkinga	12,119,727,343	430,807,386	3.6%	5,629,462	0.0%
66	H/W Sikonge	8,699,689,123	772,569,132	8.9%	291,655,617	3.4%
67	H/W Tabora	13,916,105,156	5,823,100	0.0%	174,888,301	1.3%
		1,294,973,777,766	126,432,283,544		84,862,411,758	

Kiambatisho (ii)

Mwelekeo wa Hati za Uguzi zilizotolewa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Miaka 2007/08, 2008/09, 2009/10, 2010/11 na 2011/2012

Mkoa	Halmashauri Husika	2007/08	2008/09	2009/10	2010/11	2011/12
ARUSHA						
1	H/W Arusha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
2	H/W Karatu	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
3	H/W Meru	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
4	H/W Longido	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
5	H/W Ngorongoro	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
6	H/M Arusha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha	Hati yenye shaka
7	H/W Monduli	Hati yenye shaka				
PWANI						
8	H/W	Hati	Hati yenye	Hati	Hati yenye	Hati

	Bagamoyo	inayoridhisha	shaka	inayoridhisha	shaka	inayoridhisha
9	H/W Kibaha	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
10	H/Mji Kibaha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
11	H/W Kisarawe	Hati inayoridhisha				
12	H/W Mafia	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
13	H/W Mkuranga	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
14	H/W Rufiji/Utete	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
DSM						
15	H/M Ilala	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
16	H/M Temeke	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
17	H/Jiji Dar es Salaam	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka
18	H/M Kinondoni	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka
DODOMA						
19	H/W Chamwino	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

20	H/W Kondoa	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
21	H/W Bahi	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka
22	H/W Kongwa	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
23	H/W Mpwapwa	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
24	H/M Dodoma	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka
IRINGA						
25	H/W Mufindi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
26	H/W Njombe	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
27	H/Mji Njombe	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
28	H/W Kilolo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
29	H/W Ludewa	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
30	H/W Iringa	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka
31	H/M Iringa	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
32	H/W Makete	Hati yenye				

		shaka	shaka	shaka	shaka	shaka
KAGERA						
33	H/W Biharamulo	Hati inayoridhisha				
34	H/W Ngara	Hati yeny shaka	Hati yeny shaka	Hati inayoridhisha	Hati yeny shaka	Hati inayoridhisha
35	H/W Missenyi	Hati inayoridhisha				
36	H/W Bukoba	Hati yeny shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
37	H/M Bukoba	Hati yeny shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
38	H/W Chato	Hati inayoridhisha	Hati yeny shaka	Hati yeny shaka	Hati yeny shaka	Hati inayoridhisha
39	H/W Muleba	Hati yeny shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
40	H/W Karagwe	Hati inayoridhisha	Hati yeny shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yeny shaka
KIGOMA						
41	H/W Kasulu	Hati yeny shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yeny shaka	Hati inayoridhisha
42	H/W Kibondo	Hati inayoridhisha	Hati yeny shaka	Hati inayoridhisha	Hati yeny shaka	Hati inayoridhisha
43	H/W Kigoma	Hati inayoridhisha	Hati yeny shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

44	H/M Kigoma/Ujiji	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka
KILIMANJARO						
45	H/M Moshi	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
46	H/W Hai	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
47	H/W Moshi	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
48	H/W Mwanga	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati isiyoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
49	H/W Rombo	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati isiyoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
50	H/W Same	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
51	H/W Siha	Hati inayoridhisha				
LINDI						
52	H/W Kilwa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati isiyoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
53	H/W Lindi	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
54	H/M Lindi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
55	H/W Liwale	Hati yenyeshaka	Hati	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati

		shaka	inayoridhisha	shaka	shaka	inayoridhisha
56	H/W Nachingwea	Hati inayoridhisha				
57	H/W Ruangwa	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
MANYARA						
58	H/W Babati	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
59	H/W Hanang'	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
60	H/Mji Babati	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
61	H/W Mbulu	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
62	H/W Simanjiro	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
63	H/W Kiteto	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka
MARA						
64	H/W Serengeti	Hati inayoridhisha				
65	H/W Musoma	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
66	H/W Bunda	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

67	H/M Musoma	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
68	H/W Rorya	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
69	H/W Tarime	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
MBEYA						
70	H/W Mbeya	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
71	H/W Rungwe	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
72	H/W Chunya	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka
73	H/Jiji Mbeya	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
74	H/W Mbozi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka
75	H/W Ileje	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
76	H/W Kyela	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
77	H/W Mbarali	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati Mbaya
MOROGORO						
78	H/W	Hati yenye	Hati yenye	Hati	Hati	Hati

	Kilombero	shaka	shaka	inayoridhisha	inayoridhisha	inayoridhisha
79	H/W Kilosa	Hati yenyeshaka	Hati isiyoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
80	H/W Ulanga	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
81	H/W Morogoro	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati isiyoridhisha	Hati inayoridhisha
82	H/M Morogoro	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
83	H/W Mvomero	Hati yenyeshaka				
MTWARA						
84	H/Mji Masasi	-	-	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
85	H/W Masasi	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
86	H/W Mtwara	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
87	H/W Newala	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
88	H/W Tandahimba	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
89	H/W Nanyumbu	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
90	H/M Mtwara	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

MWANZA						
91	H/W Kwimba	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
92	H/W Magu	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka
93	H/W Misungwi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati isiyoridhisha	Hati yenyeshaka
94	H/Jiji Mwanza	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
95	H/W Geita	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka
96	H/W Sengerema	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka
97	H/W Ukerewe	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
RUKWA						
98	H/W Sumbawanga	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
99	H/W Mpanda	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
100	H/M Sumbawanga	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
101	H/Mji Mpanda	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka

102	H/W Nkasi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka
RUVUMA						
103	H/M Songea	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
104	H/W Tunduru	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
105	H/W Namtumbo	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
106	H/W Mbinga	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
107	H/W Songea	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati isiyoridhisha	Hati yenye shaka
SHINYANGA						
108	H/W Meatu	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
109	H/W Bariadi	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
110	H/W Bukombe	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
111	H/W Kahama	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
112	H/W Shinyanga	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
113	H/M	Hati	Hati	Hati	Hati	Hati

	Shinyanga	inayoridhisha	inayoridhisha	inayoridhisha	inayoridhisha	inayoridhisha
114	H/W Kishapu	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati isiyoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
115	H/W Maswa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
SINGIDA						
116	H/W Iramba	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
117	H/W Manyoni	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
118	H/W Singida	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
119	H/M Singida	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
TANGA						
120	H/W Pangani	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
121	H/Jiji Tanga	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
122	H/W Mkinga	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
123	Lushoto H/W	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
124	H/W Muheza	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

125	H/W Handeni	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
126	H/W Korogwe	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
127	H/Mji Korogwe	Hati yenye shaka				
128	H/W Kilindi	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha	Hati inayoridhisha
TABORA						
129	H/W Igunga	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
130	H/W Urambo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
131	H/M Tabora	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati isiyoridhisha	Hati yenye shaka
132	H/W Nzega	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
133	H/W Sikonge	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka
134	H/W Tabora	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka

Kiambatisho (iii)

Idadi ya Halmashauri iliyopata Hati mbaya na ambazo zimepata Hati zenye shaka na sababu zilizopelekea kupata hati hiyo.

i) HATI MBAYA		
Mkoa	Halmashauri husika	Sababu zilizopelekea kupata hati mbaya
MBEYA		
1.	Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali	<ul style="list-style-type: none"> • Vitabu vya kukusanya maduhuli vipatavyo 2546 havikuonekana wakati wa ukaguzi. • Hati za Malipo hazikuonekana wakati wa ukaguzi Sh.1,030,765,405 • Malipo yenye nyaraka pungufu Sh. 21,646,300 • Maduhuli yamekusanywa lakini hayajapelekwa Benki Sh. 16,475,000
ii) HATI YENYE SHAKA		
Mkoa	Halmashauri husika	Sababu zilizopelekea kupata hati zenye mashaka
ARUSHA		
1.	Manispaa ya Arusha	<ul style="list-style-type: none"> • Malipo yenye nyaraka pungufu Sh.39,788,000. • Vitabu vya kukusanya maduhuli vipatavyo 15 havikuonekana wakati wa ukaguzi. • Hati za Malipo hazikuonekana wakati wa ukaguzi Sh.32,867,314.81 • Fedha ambazo zililipwa Bohari kuu ya Madawa kiasi cha Sh.17,965,500 lakini huduma haikutolewa pia hazikuoneshwa katika taarifa za fedha zilizoishia tarehe 30Juni 2012. • Wadaiwa wa Halmashauri wenye jumla ya Sh.192,000,000 hawakuoneshwa katika Taarifa za Fedha. • Taarifa ya Wadaiwa (Metro Merchandise) iliyooneshwa katika

		taarifa za fedha imepungua kwa kiasi cha Sh.209,910,880
2.	Halmashauri ya Wilaya ya Monduli	<ul style="list-style-type: none"> • Maduhuli ambayo hayakuingizwa katika daftari la fedha kiasi cha Sh. 2,822,000 • Maduhuli ambayo hayakupelekwa Benki kiasi cha Sh. 12,931,000 • Malipo yenye nyaraka pungufu yenye jumla ya Sh. 64,522,371 • Mafuta yaliyonunuliwa yenye thamani ya Sh.2,100,000 hayakupokelewa na Halmashauri. • Vitabu vya Maduhuli vipatavyo 34 havikuonekana wakati wa Ukaguzi.
DSM		
3.	Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam	<ul style="list-style-type: none"> • Malipo yenye jumla ya Sh. 175,968,667.51 ambayo yametumika kulipitia matumizi katika Miradi ya Maendeleo hayakuweza kuthibitishwa uhalali wake . • Wadaiwa wa Halmashauri ambao wanaidai Halmashauri kiasi cha Sh.19,249,700 hawakuweza kuthibitika. • Wadai wa Halmashauri ambao wanaidai Halmashauri kiasi cha Sh. 14,771,675,000 hawakuweza kuthibitika.
4.	Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni	<ul style="list-style-type: none"> • Vitabu vya Maduhuli vipatavyo 52 havikuonekana wakati wa Ukaguzi. • Malipo ya Sh.34,391,200 yaliyofanyika bila ya kuambatanishwa nyaraka husika. • Kukosekana kwa taarifa za kina za matumizi zikiwemo stakabadhi za kukiri mapokezi na taarifa za utekelezaji zenye thamani ya Sh. 832,134,594 katika malipo yaliyofanywa kwenye na Halmashauri kwenye kata mbali mbali kwa ajili ya kuwezesha shughuli za maendeleo.
DODOMA		
5.	Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma	<ul style="list-style-type: none"> • Malipo yaliyofanyika bila ya kuambatanishwa na nyaraka husika ya Sh. 58,701,905

